

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 8 Juni, 2015

(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

SPIKA: Ahsante Mchungaji Msigwa. Katibu!

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Maswali tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu; atakayeuliza swali la kwanza, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale.

Na. 160

Ujenzi wa Stendi na Barabara za Mji wa Mbalizi

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE aliuliza:-

Ujenzi wa stendi na barabara zake katika Mji Mdogo wa Mbalizi ulikuwa ni sehemu ya ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni za mwaka 2010:-

Je, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi hiyo?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu! Watu wote wamekwenda kutangaza nia hawapo humu. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, stendi ya mabasi iliyopo katika Mji Mdogo wa Mbalizi na inayotumika ina ukubwa wa mita za mraba 9,209 na inamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya. Kwa sasa inatumika kwa ajili ya mabasi madogo, daladala na mabasi yaendayo Mikoani. Aidha, Halmashauri ina barabara yenye urefu wa kilometa 1.3 iliyojengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, tayari Halmashauri imekamilisha michoro kwa ajili ya kujenga stendi pamoja na barabara. Tathmini iliyofanyika mwaka wa fedha 2010/2011, ili kuboresha miundombinu ya barabara na stendi hiyo ilionesha kuwa, ili stendi hiyo pamoja na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami viweze kukamilika, jumla ya shilingi bilioni 1.3 zilihitaajika. Kutokana na gharama za ujenzi kupanda, tathmini iliyofanyika katika mwaka wa fedha 2015/2016, inaonesha kuwa, jumla ya shilingi bilioni 1.6 zitatumika kukamilisha ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, Halmashauri katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, ilipokea jumla ya sh. 150,843,468/= kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya uboreshaji wa stendi hiyo, ambapo jumla ya mita za mraba 2,161.25 zilijengwa kwa kuzijengea tofali kati ya mita za mraba 6,117 za stendi hiyo. Aidha, ili ujenzi wa stendi hiyo uweze kukamilika kwa kuweka tofali jumla ya sh. 338,954,000/= zinahitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Halmashauri ilitenga fedha jumla ya shilingi milioni 525.7 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, ambapo jumla ya kilometa 1.3 zinaendelea kujengwa. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, jumla ya shilingi milioni 150 zimetengwa katika vyanzo vya mapato ya ndani, ili kujenga jumla ya mita za mraba 2,000 katika stendi hiyo na shilingi milioni 566.7 zimetengwa ili kukamilisha ujenzi wa barabara katika mji huo.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, mapato ya Halmashauri ya Mbeya Vijijini hayazidi bilioni mbili kwa mwaka na barabara hiyo, inakisiwa kwamba, itachukua shilingi bilioni 1.6; hamuoni kwamba, kama hela za ndani za Halmashauri zitatumika kujenga, basi ina maana maeneo mengine yote na barabara zingine zote hazitajengwa? Naomba Serikali iniambie kwamba, je, itakuwa tayari sasa kuisaidia Halmashauri kutenga hela kwa ajili ya kumaliza ujenzi wa stendi pamoja na barabara zake?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mbeya Vijijini ina vijiji 150 ambavyo vijiji hivi hutegemea misaada yote kutoka katika Halmashauri ambayo kama nilivyosema, fedha inayopatikana ni kidogo sana. Je, Serikali kwa sababu, ilianza kutoa hela shilingi milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa stendi na barabara, je, haiko tayari sasa kutoa fedha hiyo kumaliza ile stendi na barabara? Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, Serikali kwa utaratibu ambao tunao huwa tunatenga fedha kwa ajili ya kuendesha miradi ambayo inabuniwa kwenye Halmashauri, lakini Halmashauri zenyewe zinaweka kipaumbele kwa jambo ambalo halihitaji pamoja na kutenga fedha kupitia kwenye bajeti yake na bajeti ya mapato ya ndani hukadiriwa kutokana na makusanyo ya kila mwaka ambayo wanajua wanavyokusanya kiwango hicho na mipango yao ya kazi inaendana na makusanyo waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, ukusanyaji sasa tumeendelea kuuwekea mkazo na Halmashauri nyingi zimeonesha zinakusanya kwa zaidi ya 80%, tunayo matarajio kwamba, mchango ule wa Halmashauri wanaweza kufikia hatua, lakini watakaposhindwa tunao utaratibu wa barua maalum, maombi maalum kwa Wizara na kama Wizara tunakuwa na uwezo tunasaidia.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni pamoja na swali la pili ambalo linasema wingi wa vijiji na barabara zake; bado barabara hizi zilizoko kwenye Halmashauri zinazounganisha vijiji na vijiji zinakuwa ziko ndani ya Halmashauri yenyewe. Hata hivyo, tuna ule Mfuko wa Barabara ambao pia, kama Halmashauri imekidhi vigezo kwanza kuwa na *Engineer* ambaye amepata taaluma ya kutosha, lakini mbili, barabara hizo kuwa na mahitaji ya kujenga barabara mpya kwa maana ya kwa kiwango cha changarawe, tunaweza pia, kuona uwezekano wa kuangalia mapato ya ndani waliyotenga, Mfuko wa Barabara na mahitaji ambayo yanatakiwa yakamilishwe, ili kuweza kukamilisha barabara hizo zinazounganisha vijiji kwenye maeneo yote.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, litaulizwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, kwa niaba yake Mheshimiwa Ester Bulaya!

Na. 161

**Uhaba wa Walimu Shule za Sekondari
Mpanda Vijijini**

MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. MOSHI S. KAKOSO) aliuliza:-

Jimbo la Mpanda Vijijini lina shule za sekondari saba ambazo ziko katika Kata ya Karema, Ikola, Kabungu, Katuma, Mishamo na Mpanda Ndogo, lakini shule hizo zina upungufu mkubwa wa Walimu:-

- (a) Je, ni lini Serikali itapeleka Walimu wa kutosha katika shule hizo za Mpanda Vijijini?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa kutokuwa na Walimu kumesababisha kushuka kwa elimu na hivyo kuwafanya wanafunzi kufeli mitihani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeongeza idadi ya Vyuo vya Ualimu, Vyuo Vikuu na udahili katika kozi za ualimu pamoja na kuajiri Walimu kadiri wanavyofaulu. Mkakati huu umewezesha Serikali kwa mwaka huu wa 2015, kuajiri na kuwapanga katika shule za Sekondari Walimu 19,261. Kati ya hao Walimu 65 wamepangiwa Mpanda Vijijini na imewapanga katika shule za Kabungu Walimu watano, Mpanda Ndogo Walimu tisa, Katuma Ikoa Walimu 10, Mishamo Walimu 12, Mwese Walimu sita na Karema Walimu 10.
- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa elimu ya sekondari nchini kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, maarufu unajulikana kama MMES, ikiwemo kuhakikisha upatikanaji wa Walimu, vitabu, miundombinu na kuimarisha usimamizi. Mikakati hii imewezesha kuongeza kiwango cha ufaulu kutoka 43% mwaka 2012 hadi 69.7% mwaka 2014. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa Walimu, hususan wa masomo ya sayansi, wanapatikana wa kutosha katika shule zote na ifikapo mwaka 2016, Serikali itakuwa imekamilisha mradi wa ujenzi wa miundombinu kwa shule 528 zikiwemo shule za Ikola, Ilela, Utembe na Mamba.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Ester Bulaya, maswali ya nyongeza!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kupeleka Walimu ni jambo lingine, lakini kuhakikisha Walimu wanafika mashuleni na lenyewe ni jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa tuliyonayo ni miundombinu yani mazingira mabovu ya Walimu, kwa mfano kumekuwa na tatizo kubwa sana la nyumba za Walimu, usafiri na kiasi kwamba, mbali ya kwamba, tumewapeleka Walimu bado hawako tayari kwenda maeneo ya vijijini. Mwisho wa siku inabakia *figure* kwamba, Walimu wamekwenda, lakini tatizo la uhaba wa Walimu halimaliziki. Je, ni lini sasa Serikali mtahakikisha mnajenga nyumba za Walimu na kuboresha mazingira yao, ili wabaki kule mnakowapeleka, ili tatizo la Walimu liondoke katika Jimbo la Mheshimiwa Kakoso? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pia shule nyingi zimekuwa na uhaba wa Walimu wa kike ikiwepo shule ya msingi Kunzugu, Jimbo la Bunda. Ni lini sasa tatizo hilo litaondoka kwa kupeleka Walimu wa kike kwenye shule za msingi, ili kuna mambo ya wanafunzi wa kike ambao wanashindwa kuwashirikisha Walimu wanaume na mwisho wa siku wawe na Walimu wa kike ambao wanaweza kuwaambia matatizo yao ya kiuwanawake? Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, uko ukweli kwamba, ziko taratibu kadhaa zinaendeleza kuhakikisha kwamba, tunakuwa na nyumba za kutosha za Walimu wa sekondari na wa msingi. Lakini tunatambua kabisa kwamba, kada ambayo ina watumishi wengi kwenye utumishi wa umma ni Walimu na idadi ya Walimu ni zaidi ya 62% ya watumishi wote wa umma, ambao pia, Serikali iliamua watumishi wa kada ya elimu wawe na makazi yaliyoandaliwa na Serikali, kuwawezesha kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, bado hatujamudu kujenga nyumba ya kila Mwalimu, ili aweze kukaa kwenye nyumba yake, lakini iko mikakati kadhaa ambayo Serikali inaendelea nayo ili kupata nyumba moja kupitia mipango ya maendeleo ya sekta za elimu kwenye msingi na sekondari, ambayo ni MMEMna MMESkwa kutenga fedha ambazo pia, kwenye utengaji wa fedha hizo huwa tunatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu na taratibu hizo zinaendelea ingawa bado kuna mahitaji makubwa ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ambayo sasa tunayo kwa upande wa shule za sekondari kupitia mpango wa MMES, tumetenga fedha kujenga nyumba 183 ambazo zitajengwa katika Halmashauri 105 na mgawo wake wa fedha utaanza kutoka wakati wowote ule kwenda, ili kuweza kuongeza nyumba. Pamoja na mpango huu, lakini pia tunao mpango ambao tumeupanga wa kupelekea fedha milioni 500 kila Halmashauri na tulianza na Halmashauri 40, mpango wetu ni kuongeza Halmashauri nyingine 40 ili kujenga nyumba za Walimu kwa Kurugenzi zote mbili, Sekondari na Msingi.

Mheshimiwa Spika, lakini bado tuna mkakati ule ambao tumeuweka wa watumishi kuweza kujijengea nyumba, jambo ambalo pia tumetoa uhuru na tumeunda chombo kinaitwa *Watumishi Housing Company* ambayo mtumishi Mwalimu anaweza kukopa. Ndio watumishi wetu wa umma wakiwemo walimu anaweza kukopa na ina riba nafuu sana akajenga nyumba popote; kwa njia hii inaweza kusaidia pia, Walimu kuwa na makazi yao. Bado Wizara ya Ardhi nayo pia inatoa mikopo ya ujenzi wa nyumba na vifaa vya ujenzi ambavyo riba yake ni 3% ni kwa watumishi wote wakiwemo Walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa njia zote hizi huku Serikali tukijitahidi kujenga nyumba, tunaweza tukapata nyumba. Naomba niwathibitishie Walimu nchini kwamba, wale ambao tunawapangia kwenda kwenye maeneo ya vituo hivi vya kazi waende na Serikali itaendelea kupanga utaratibu wa kujenga nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili la upungufu wa Walimu wanawake; tunaendelea nalo, tunajua.

Msisitizo wa sasa wanafunzi kusoma na kwa jinsia zote unasaidia pia, kuwa na Walimu ambao wanajitokeza katika jinsia zote, wanaume na wanawake na msisitizo ambao tumeutoa tunapowapangia kwenye Halmashauri zetu, Maafisa Elimu wahakikishe kuwa, wanawapanga Walimu hawa kwa jinsia ili pia kila shule, angalau iwe na Mwalimu wa kike anayeweza kusaidia watoto wetu pale kwa yale ambayo yanapasa mwanafunzi akimbilie kwa Mwalimu wa kike.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kutoa majibu ya nyongeza kuhusu suala la Walimu wengi kutokupenda kwenda vijijini. Naomba nikiri kwamba, Walimu wengi wanafika mahali wanashindwa kwenda vijijini kwa sababu ya hali na pia kuna matatizo mengi kwenye ukaazi.

Mheshimiwa Spika, lakini ningepomba kutoa wito kwa Watanzania wote kwamba, kipindi hiki tumetoa Walimu wengi sana wa sekondari, ili tuondoe kabisa tatizo la Walimu upande wa sekondari. Kwa hivyo, niwasihi Watanzania wote wawapokee Walimu wale na kwa sababu, Walimu ni asilimia zaidi ya 62 ya watumishi, wajitahidi kuwapatia nyumba za kufikia wakati Serikali inatatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Same inafanya hivyo na Walimu wote waliokwenda Wilaya ya Same wamepata makazi.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, atauliza swali hilo!

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Awali ya yote kabla swali langu halijapatiwa majibu, nilikuwa nataka niongee yafuatayo...

SPIKA: Unauliza swali au...

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, nitauliza swali langu.

SPIKA: Sasa hakuna cha kuongea zaidi ya swali lako

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, haya nashukuru. Naomba sasa swali langu Namba 162 lipatiwe majibu.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

Na. 162

**Upasuaji wa Miamba Kwenye Madini Wakati
wa Ujenzi wa Barabara**

MHE. MOZA A. SAIDY aliuliza:-

Katika miradi ya ujenzi wa barabara, kampuni kutoka nje zimekuwa zikipasua miamba ambayo mingine ina madini:-

Je, Serikali huwa inafuatilia hatua kwa hatua kubaini madini hayo ili yaweze kunufaisha Serikali na wananchi kwa ujumla?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 na cha 18 cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010, kinatamka kila mtu anayejihusisha na shughuli za madini kuwa na leseni husika. Aidha, Serikali hutoa leseni za uchimbaji madini kulingana na madini yaliyoombwa kuchimbwa na mmiliki wa leseni anatakiwa kuzingatia kikamilifu masharti ya leseni wakati wa kuendesha shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, leseni nyingi za uchimbaji madini ya ujenzi kwa ajili ya miradi ya barabara hutolewa kwa Wakala wa Barabara yaani *TANROADS* ambao ndiyo wasimamizi wa miradi ya barabara. *TANROADS* huingia mikataba na Wakandarasi wa kujenga barabara ambao wanaweza kuwa wageni au wazawa.

Wakandarasi hao huchimba madini ya ujenzi kutoka katika viwanja vinavyomilikiwa na *TANROADS*. Madini yote yanayochimbwa kwa ajili ya miradi ya barabara hutumika kujengea barabara husika na si kusafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mmiliki wa leseni ya uchimbaji madini haruhusiwi kuchimba na kuuza madini ambayo yanaorodheshwa katika leseni anayomiliki. Aidha, ili kusafirisha madini nje ya nchi ni lazima mmiliki wa leseni apate kibali cha kusafirisha madini nje ya nchi yaani *export permit* kinachotolewa na Wizara, kibali hicho hutolewa baada ya wataalam wa Wizara kukagua na kuchukua vipimo ili kujiridhisha kuhusu aina na kiasi cha madini yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pia shughuli za uchimbaji wa madini ukaguliwa mara kwa mara na maafisa wa madini ili kuona utekelezaji wa masharti ya leseni za uchimbaji zilizotolewa. Katika kaguzi zinazofanywa haijawahi kubainika eneo linalochimbwa madini ya ujenzi, yaani mawe, kokoto, kifusi na mchanga kuwa na madini ya aina nyingine yanayoweza kuchimbwa kwa faida.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwa ujumla kutoa taarifa mara moja katika ofisi zetu za madini zilizopo sehemu mbalimbali nchini pindi wanapoona kampuni zinazojihusisha na miradi ya ujenzi wa barabara zinapasua miamba ambayo ina madini mengine tofauti na ya ujenzi ili ufuatiliaji ufanyike kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Moza maswali ya nyongeza!

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini napenda kumuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa barabara inayojengwa kutoka eneo la Mayamaya kuelekea eneo la Bonga, mpaka pale eneo la Humai, pana mkanda wa madini ya msufini yanaonekana kabisa na kuna madini ya dhahabu. Je, kama Serikali, mmechukua hatua gani za ufuatiliaji au kutoa wito gani kwa wananchi ambao hawana uelewa kama eneo lile kuna madini?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa madini ya ujenzi ambayo umeyasema ni changarawe, kokoto, kifusi, kinachimbwa katika maeneo husika. Je, wananchi wananufaika na madini hayo ya ujenzi wa barabara au ni kuwaharibia mazingira?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali lake la msingi kwamba, kama kuna dhahabu na madini mengine katika eneo hilo na watu hawana leseni, basi watu hao hawaruhusiwi kuchimba au kufanya biashara yoyote ya madini. Kinachotakiwa ni wananchi watoe taarifa na sisi kama kuna watu wenye nia ya kuendeleza eneo hilo basi tutawapa leseni kulingana na sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kunufaika kwa wananchi, la kwanza kabisa kwamba ile barabara inayopita pale itawanufaisha wananchi kwa kuwa na barabara iliyo nzuri na itawawezesha kusafirisha mazao yao. Vile vile kama kuna nafasi nyingine ya kibiashara itaonekana katika eneo hilo, basi watumie sheria zilizopo ili waweze kupata leseni zinazohusika ili waweze kupata faida kulingana na taratibu na kanuni tulizonazo.

SPIKA: Hili alilosema Moza Mheshimiwa Waziri, hayo aliyosema Moza kwamba kuna dhahabu, kuna nini huko siyo taarifa hiyo au ni nini? (Kicheko)
Haya Mheshimiwa Suzan Kiwanga!

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Wilaya ya Kilombero kuna barabara ambayo ilishatolewa ahadi na Serikali kwamba inajengwa kuanzia Kidatu mpaka Ifakara kilomita 80 na kuanzia Ifakara mpaka Mlimba mpaka Madeke kule Njombe. Mpaka leo hakuna dalili zozote za hiyo barabara kujengwa na katika bajeti ya Serikali haijazungumziwa kabisa. Wananchi wa Kilombero wengine wamewekewa X hawafanya maendeleo, je, ni lini sasa Serikali itakwenda kujenga hiyo barabara ili wananchi hao wapone na maisha yao ya kila siku?

SPIKA: Jamani hakuna madini kule, tafadhali hilo swali lingine kabisa wala halimhusu. Tunaendelea na swali linalofuata. Huyu anasema wanapojenga barabara kuna madini wewe unazungumza kujenga tu barabara? Basi tunaendelea Wizara ya Fedha, Mheshimiwa *Engineer* Mfutakamba, Mheshimiwa Ole-Medeye kwa niaba.

Na. 163

Uuzaji wa Petroli na Gesi Itakayopatikana Nchini

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE (K.n.y. MHE. ATHUMAN R. MTUTAKAMBA) aliuliza:-

Je, ni wapi patafaa duniani kwa ajili ya kuwekeza fedha za ziada (*sovereign wealth fund*) tutakapoanza kuuza petroli na gesi nchini na duniani ili uchumi wetu kuanzia mwaka 2020 usiyumbe?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Athumani Rashid Mfutakamba, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwekeza fedha za ziada (*Sovereign WealthFund*) zinazoambatanishwa na mapato yatokanayo na chanzo maalum, mara nyingi rasilimali kwa maana ya *resource based* umekuwa unatumika kwa muda wa zaidi ya miaka mia na kwa sasa nchi mbalimbali zinahifadhi fedha zao kwa utaratibu huu wa *Sovereign Wealth Fund* ambazo zimegawika katika zile zenye msingi wa bidhaa ya mafuta kwa maana ya *oil based* na zile zisizo za

vyanzo vya mafuta *non-oil resources*. Mifano iko mingi ya uzoefu wa usimamizi wa fedha hizi kupitia *Sovereign Wealth Fund* na matumizi na uwekezaji kupitia utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imefanya ugunduzi wa rasilimali ya gesi asilia na jitihada za utafiti zinaendelea. Rasilimali hiyo baada ya ugunduzi, kuna kazi kubwa, inayohitaji uwekezaji wa sekta binafsi na sekta ya umma ili kufikia matumizi ya gesi hiyo. Uwekezaji huo utafanywa kwa mujibu wa mikataba ambayo itaweka wazi mgao wa mapato yatokanayo na rasilimali ya gesi asilia. Kwa kutambua umuhimu wa kudhibiti maslahi ya Taifa yanayotokana na rasilimali, Serikali imemaliza kazi ya kuandaa sera na inaendelea na mchakato wa kuleta Bungeni Sheria ya Mapato na Matumizi ya Fedha Zitokanazo na Rasilimali ya Gesi Asilia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia sera na sheria itaweka utaratibu ulio wazi wa namna ya kufanya maamuzi kuhusu matumizi ya fedha hususan ikiwa ni pamoja na maamuzi ya uwekezaji wa *Sovereign Wealth Fund* na ni wapi na kwenye maeneo yapi na kwa wakati gani fedha zitaelekezwa kwenye matumizi, kwa mfano matumizi ya rasilimali kwa ajili ya manufaa ya vizazi vya baadaye vya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala hili na nawaomba Wabunge wote wajielimisha kuhusu masuala haya ya uwekezaji wa fedha za Taifa (*Sovereign Wealth Fund*) ili kuanza kujenga uelewa wa suala hili muhimu wakati Bunge lako litakapojadili utaratibu wa usimamizi wa mapato yatokanayo na rasilimali ya gesi asilia.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Medeye swali la nyongeza!

MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya swali la msingi. Serikali imeahidi kwamba italeta sheria ambayo itaweka utaratibu wa mapato na matumizi ya fedha hizo zitokanazo na gesi asilia. Utungaji wa sera umechukua muda mrefu sana, tulianza kulizungumza suala la sera tangu tulipoanza Bunge hili la Kumi na imechukua muda mrefu mpaka Sera hiyo kukamilika. Kwa msingi huo, ningepomba tujulishwe tarehe au Mkutano upi wa Bunge la Kumi na Moja tunatarajia Muswada wa Sheria hiyo utawasilishwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwanza nitangaze maslahi kwamba, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Maliasili, Kilimo na Chakula, na Miundombinu ya Jukwaa Mabunge ya SADC. Moja ya ushauri ambao tumetoa kwa Serikali za nchi za SADC ni kuwa na utaratibu unaoeleweka wa uanzishaji Mifuko hii ya *Sovereign Wealth* pamoja na kupanga namna ambayo itachangiwa na hao ambao tumewakabidhi dhamana ya kuchimba na kutumia rasilimali hizo kwa

maana ya wawekezaji kwa vile sehemu kubwa ya miradi hii haiendeshwi na Serikali zetu.

SPIKA: Swali sasa.

MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri atuambie, utaratibu ulio wazi kwenye sera wametamkaje kuhusu namna ambavyo kwamba wawekezaji walioko hivi sasa kwenye sekta ya gesi asili watachangiaje Mfuko huo wa *Sovereign Wealth*.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, hata Naibu Waziri wa Nishati naye yupo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Spika, nadhani hili la Sera, amesema imechukua muda mrefu, Sera imechukua muda mrefu, lakini ndiyo maandalizi ya sheria. Tumekuwa na Sera ya Gesi, Sera ya Petroli na sera ya vitu vingi. Sasa hii ni Sera maalum ya kuangalia, kwanza mapato yenyewe ya gesi yanaingiaje na mapato yenyewe yanatumikaje. Sasa tunasema hii utaratibu wa kuwa *Sovereign Wealth Fund* ni utaratibu mmoja tu katika namna nyingi ambazo tutagawa mapato ya fedha.

Mheshimiwa Spika, labda nimwambie Dkt. Medeye kwamba, katika hayo kuna maeneo mawili, moja ni kwamba, yale maeneo ya *Sovereign Wealth Fund* nchi nyingi zimetumia *Sovereign Wealth Fund* kwenye matumizi ya kawaida, *ordinary expenditure* na matokeo yake ni kwamba wame-deplete zile *Sovereign Wealth Fund* na malengo yake, sisi kwenye Sera yetu tumesema moja kwa moja kwamba mapato yatoanayo na gesi yanaingia kwenye Mfuko maalum ambayo yatakuwa na matumizi ya uwekezaji wa miundombinu. Sasa hiyo ni *standard format* ya *Sovereign Wealth Fund*.

Mheshimiwa Spika, upande wa pili, ni kwamba *Sovereign Wealth Fund* ile inatengewa kipande maalum ambacho hakiguswi mpaka muda fulani miaka 20 au 30 na lengo lake linakuwa kwa ajili ya kutumika kwa manufaa ya vizazi vya baadaye. Sasa hayo maeneo mawili yamo kwenye sera na sera imeshakamilika na sasa hivi tunaendelea na utaratibu wa kutengeneza sheria ambayo inafanywa na Wizara ya Fedha kwa sababu ni masuala ya mapato na matumizi.

Mheshimiwa Spika, ameuliza kuhusu tarehe ya lini sheria itakuja Bungeni, hilo ni suala la baina ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge na Ofisi yako kupanga tarehe ya lini sheria hiyo itakuja Bungeni.

SPIKA: Ahsante tunaendelea na swali linalofuata, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Suzan Lyimo anauliza swali hilo.

Na. 164

**Tume ya Kuangalia Matatizo ya Mikopo
ya Elimu ya Juu**

MHE. SUSAN A. J. LYIMO aliuliza:-

Suala la mikopo ya elimu limeendelea kuwa na changamoto kila mwaka, hali iliyopelekea kuundwa kwa Tume chini ya Uenyekiti wa Profesa Maboko:-

Je, matokeo ya Tume hiyo yakoje na ni kwa kiasi gani ilitatua changamoto hizo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo na Ufundi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anslem Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwaka 2011, Serikali iliunda Tume ya Kuchunguza Utendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu baada ya kutokea malalamiko dhidi ya Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya Tume hiyo yalibaini upungufu kadhaa kama vile mahusiano hafifu kati ya Bodi ya Mikopo, Tume ya Vyuo Vikuu, Taasisi ya Elimu ya Juu na Serikali ya Wanafunzi. Aidha, ucheleweshwaji wa fedha kutoka Hazina pamoja na Vyuo Vikuu kuchelewa kupeleka majina ya wanafunzi wanaoendelea na masomo kwenye Bodi ya Mikopo, kulichangia kwa kiasi kikubwa malalamiko dhidi ya Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mapendekezo ya Tume yamefanyiwa kazi na Serikali na kupata mafanikio makubwa pamoja na kuondosha migomo na maandamano dhidi ya Bodi ya Mikopo. Kila chuo kimeelekezwa kuajiri Afisa atakayeshughulikia masuala ya mikopo na kuwa kiungo kati ya wanafunzi, chuo na Bodi ya Mikopo. Aidha, fedha za mikopo ya wanafunzi zimekuwa *ring fenced* na hivyo kuwezesha fedha kuwafikia wanafunzi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mahusiano kati ya Tume ya Vyuo Vikuu na Bodi ya Mikopo yameboreshwa kwa kuwekwa mwakilishi wa Tume ya Vyuo Vikuu kama Mjumbe kwenye Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Aidha, Bodi ya Mikopo imeboreshwa kwa kuajiri watumishi wenye sifa stahiki na vitendea kazi vya kutosha. Vile vile Bodi ya Mikopo imeanzisha ofisi katika Kanda za Dodoma, Zanzibar na Mwanza ili kuwahudumia wadau kwa karibu.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, kwanza kwa masikitiko makubwa sana, ni wazi kwamba ama Naibu Waziri majibu haya hakuyafuatilia kwa kina au watendaji wamemdanganya.

Mheshimiwa Spika, majibu yanasema kwamba Serikali imepata mafanikio makubwa lakini vile vile fedha za wanafunzi zimekuwa *ringfenced*. Mheshimiwa Naibu Waziri anatambua kwamba, sasa hivi kuna wanafunzi wa vyuo vingi ambao bado hawajapata mikopo, kimojawapo ni Chuo Kikuu cha Dodoma ambapo wale wanafunzi wa *special diploma course* ya ualimu toka mwaka jana mwezi Novemba mpaka leo hawajapata fedha.

Mheshimiwa Spika, vile vile wanafunzi wa St. Joseph ya Dar es Salaam na Arusha hawajapata fedha. Vile vile hivi majuzi wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliandamana na ndani ya masaa kumi na mbili wakapata fedha. Sasa hayo mafanikio anayoyasema Mheshimiwa Naibu Waziri, ni yapi? Wakati yuko Tanzania hii hii na anaona mafadhaiko ya wanafunzi hao? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Naibu Waziri atakiri kwamba matatizo yanapotokea ni kwamba Serikali inashindwa kupeleka fedha kwa wakati, lakini mara zote wanafunzi ambao kimsingi asilimia mia ya fedha zao wanategemea mikopo, hawana mzazi anayewapelekea hasa wanaotoka katika mazingira magumu. Kwa hivyo, wanategemea fedha za mkopo asilimia mia kwa mia, lakini wanafunzi hao kama kweli mwanafunzi toka mwaka jana mwezi Novemba mpaka leo tunapoongea hajapata hata shilingi na Serikali imeshindwa kuwapelekea, lakini wanafunzi hao wanafukuzwa chuo kama ambavyo imetokea St. Joseph ya Dar es Salaam mwezi uliopita. Je, Serikali inasema nini pale ambapo ni haki ya mwanafunzi kupata fedha zake, lakini hajapata, matokeo yake wanafukuzwa lakini hatujasikia mtumishi wa Serikali amewajibishwa kwa kuchelewa kuwapelekea fedha zao? Naomba tamko la Serikali.

SPIKA: Maswali yenyewe marefu utafikiri hotuba ya bajeti. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba fedha zimechelewa na siyo kwa sababu hazijakuwa *ring fenced*, kwa sababu nadhani amechanganya mambo mawili; suala la kuwa *ring fenced* siyo kwa sababu ndiyo maana zimechelewa.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba, ni kweli pesa zimechelewa.

Tuna kama wiki mbili hivi, pesa zimekuwa zikitoka kwa utaratibu, kuna zingine zimetoka na hazitoki kwa sababu wanafunzi wamegoma, kwa sababu hata ukigoma kama hazipo haziwezi kutoka. Zimetoka kwenda kwa wanafunzi wa *University of Dar es Salaam*, zinatoka kwenda *UDOM* na tumeshawaambia *UDOM* kwamba wanafunzi ambao wana migogoro na Bodi ya Mikopo kwa pesa zao zile, sisi Wizara ya Fedha ndiyo tutachukua dhamana hiyo. Sasa wewe unamfukuza mwanafunzi wakati kweli anadai mkopo na sisi Serikali hatujatoa! Kwa hiyo, huo ni utaratibu tu na naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, kama kuna mgogoro sisi tunaotoa hela ndiyo tutawasilisha huko maelezo kwamba tafadhali, tafadhali pesa hizo zinakuja kama tulivyofanya *UDOM* kwa uongozi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tufahamu kwamba halina uhusiano na kuwa *ring fenced*, ni kwamba, pesa zenyewe kwenye makusanyo kulikuwa kuna kutetereka, lakini pesa zimeanza kutoka wamepewa Dar es Salaam, watapewa *UDOM* na wengine wote kadiri zitakavyopatikana na wanafunzi wasiondolewe hasa wale ambao *genuinely* wako kwenye orodha ambayo wanadai kupitia Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Waheshimiwa Wabunge tuwe wapenda haki. Tulikuwa na migomo mingi sana, lakini kuanzia 2011, baada ya Tume hii kuundwa, naomba Waheshimiwa Wabunge tukiri kwamba, migomo imepungua sana. Ifike mahali Waheshimiwa Wabunge tuwe tunaiona Serikali kwamba inafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu matatizo ya St. Joseph, Mheshimiwa Susan Lyimo ameongea sana kuhusu suala la St. Joseph. Juzi wakati nikichangia wakati wa Wizara ya Afya, niliomba Serikali tupewe muda, sisi ndiyo tulete ripoti humu ndani na siyo Kamati ya Mheshimiwa Mama Sitta. Kwa hiyo, narejea kwamba, naomba Serikali tulete majibu sahihi kuhusu matatizo ya St. Joseph pamoja na *KIU* na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Nimeagiza kabla ya tarehe 30 ripoti iletwe. Tunaendelea maana maswali yalikuwa marefu na majibu mazuri. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu.

Na. 165

Ahadi ya Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Igunga

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU aliuliza:-

Mwaka 2005 Serikali iliahidi kujenga Chuo cha Ufundi VETA katika Wilaya ya Igunga ili kuwapatia vijana mafunzo ambayo yatawasaidia kujijiri:-

Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali kujenga Chuo cha Ufundi Stadi Igunga iko pale pale kulingana na mpango wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa vyuo 27. Changamoto iliyopo ni kupata fedha za kuanza ujenzi wa vyuo hivyo, ambapo wastani wa ujenzi wa chuo kimoja ni kuanzia shilingi bilioni tatu na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, wakati juhudi za kutafuta fedha za ujenzi zikiendelea, Serikali imeanzisha mpango mbadala wa kuwapatia vijana mafunzo ya Ufundi Stadi kupitia Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi ili waweze kujijiri. Utekelezaji wa mpango mbadala ulianza Januari, 2013 kwa kutumia vyuo 25 kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tabora ni kati ya Mikoa yenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Nzega kilichopo karibu na Igunga. Chuo hiki ni mojawapo kati ya vyuo 25 vilivyoko katika awamu ya kwanza ambavyo vinatoa mafunzo ya ufundi stadi katika fani za ufundi umeme na magari sanjari na mafunzo ya maendeleo ya jamii chini ya usimamizi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Aidha, pamoja na Serikali kutumia mpango mbadala wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, inaendelea kutumia Chuo cha Ufundi Stadi cha Tabora (VETA). Hivyo, ipo fursa ya kutumia vyuo vyote hivi kuwapatia mafunzo vijana wa Igunga ili waweze kujijiri.

SPIKA: Mheshimiwa Doka Kafumu, swali la nyongeza!

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa tatizo la ajira kwa vijana siyo wa Igunga tu, lakini wa nchi nzima ni kubwa na kwa kuwa vijana hawa wamejitahidi sana kuanzisha kazi, kuanzisha shughuli za kujitolea ili kujiinua kiuchumi. Vijana hawa wanahitaji mitaji, wanahitaji *study* kama swali langu lilivyouliza. Serikali inawambia nini vijana wa Igunga kuhusu suala hili la kuwasaidia mitaji na *study* za kazi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa mwaka 2012 tuliwahasisha vijana wa Igunga waanzishe miradi na hasa vijana wasomi waliokuwa wametoka Chuo Kikuu na kwa kuwa Serikali baadaye iliwasaidia vijana hawa shilingi milioni tisini na tano. Bahati mbaya viongozi wa Wilaya baadhi yao walizibadili hizi fedha, je, Serikali inachukua hatua gani kuhusu watu hawa ambao wamechukua hela za vijana? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kuhusu wale ambao walizitumia vibaya pesa za hawa vijana, nadhani yeye mwenyewe anajua kwamba, baadhi yao tumewaondoa katika yale madaraka. Tumewavua na wengine tumewaachisha kazi kabisa. *(Makofi)*

SPIKA: Lile la kwanza mnatoaje mtaji bado hujajibu, bado ni TAMISEMI. Mitaji kwa vijana ambao wanatakiwa kujiajiri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana ambao wanapenda kujiajiri au tunawasaidiaje ili waweze kujiajiri. Tunao Mfuko wa Vijana, tunao Mfuko wa Wanawake na sasa hivi tumeziagiza Halmashauri pamoja na Waheshimiwa Madiwani na Wabunge kuhakikisha kwamba zile pesa asilimia ile inatoka na vijana wanapatiwa na pia kutenga maeneo ambayo vijana wataweza kufanyia shughuli zao ambazo zitawapatia ajira.

SPIKA: Mheshimiwa Lembeli, swali la nyongeza!

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wilaya ya Kahama ni Wilaya pekee hapa nchini ambayo ina migodi miwili mikubwa ya dhahabu inayotoa ajira zaidi ya vijana 10,000. Asilimia 98 ya ajira hizi zinatolewa kwa vijana wanaotoka nje ya Wilaya ya Kahama kwa sababu Kahama haina Chuo cha VETA. Swali, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga Chuo cha VETA, Wilaya ya Kahama ambako kinahitajika sana ili kuwapa vijana elimu stadi ya kuweza kufanya kazi katika migodi hii miwili ambayo iko katika Wilaya yao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, ni kweli ukiangalia hali halisi ya Kahama mahali ambapo nilifika, kulingana na hali ya uchumi upande wa madini tungehitaji kupata Chuo cha VETA. Naomba niseme kwamba ni uhaba tu fedha ndiyo unasababisha tusiweze kujenga Chuo cha VETA.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, tukitegemea Serikali ndiyo iweze kujenga hivi Vyuo vya VETA kwenye Wilaya zetu tutachelewa sana, ni vyema pia na ninyi pamoja tukishirikiana na Serikali tutafute wadau wa elimu ambao wako tayari kujenga vyuo hivi ili tuweze kutatua tatizo la ajira pamoja na matatizo kama yaliyopo Kahama. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Tuendeleo na Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa niaba yake Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o!

Na. 166

**Matumizi ya Dawa Zenye Madhara
kwa Binadamu**

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (K.n.y. MHE. MTUTURA A. MTUTURA) aliuliza:-

Mara nyingi Serikali imekuwa ikitangaza kupigwa marufuku kusambaza na kuuzwa baadhi ya dawa za binadamu zinazodaiwa kuwa na madhara ya kiafya licha ya kuwa dawa hizo zilipata kibali cha kutumika nchini miaka kadhaa huko nyuma.

- (a) Kwa nini Serikali isijiridhishe mapema kabla ya kuruhusu dawa hizo kutumika?
- (b) Je, Serikali imefanya utafiti kuona kama wananchi waliotumia dawa hizo kwa muda mrefu wamepata madhara yoyote?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru Kusini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia TFDA imeweka utaratibu wa kudhibiti dawa za binadamu unaojumuisha mambo yafuatayo:-

- (a) Kufanya tathimini juu ya ubora, usalama na ufanisi wa dawa;
- (b) Kufanya ukaguzi wa viwanda vinavyotengeneza dawa ndani na nje ya nchi;
- (c) Kuchukua sampuli za dawa kwenye soko na kuzipima kwenye maabara ya TFDA inayotambulika Kimataifa (*WHO prequalified and ISO accredited laboratory*); na
- (d) Kufanya utambuzi na ufuatiliaji wa madhara ya dawa zinazotumika nchini.

Mheshimiwa Spika, kupitia taratibu hizi, dawa kabla ya kuruhusiwa kutumika nchini, hutathiminiwa ubora, usalama na ufanisi wake na kiwanda kukaguliwa kama kinatengeneza dawa kwa kufuata vigezo vya utengenezaji bora wa dawa (*Good manufacturing Practices – GMP*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na dawa kuthibitishwa kwa matumizi ya binadamu, bado TFDA huendelea kufuatilia dawa hizo kwenye soko kama zinaleta madhara (*safety monitoring*) au zina matatizo ya ubora (*quality defects*) au hazitibu magonjwa (*ineffectiveness*). Hili hufanyika katika kipindi chote cha uwepo wa dawa yaani *pharmacological vigilance*. Mfumo huu hutumika duniani kote na kwa kuzingatia miongozo ya WHO.

(b) Mheshimiwa Spika, mfumo wa ufuatiliaji wa madhara ya dawa kwa binadamu hutumia fomu za njano na bluu (*yellow and blue forms*) ambazo zimeandaliwa na TFDA na kusambaza kwenye hospitali, vituo vya afya zahanati na maduka ya dawa nchini. Kupitia fomu hizi wataalam wa afya na wagonjwa hujaza taarifa za madhara yote yanayotokea na kuyatuma TFDA ambapo TFDA hufanya tathimini ya dawa na madhara hayo ambayo yamejitokeza pia kutumia Shirika la Afya Duniani ambapo tathimini ya jumla hufanyika na kufahamisha nchi wanachama wa WHO juu ya hatua za kuchukua. Hatua hizo ni pamoja na kufuta usajili wa dawa husika, kusimamisha usambazaji na kuondoa dawa kwenye soko, kubadili *label* za dawa ikiwa dawa husika bado ina manufaa kwa matumizi ya binadamu na kubadili matumizi ya dawa husika.

Mheshimiwa Spika, kupitia mfumo huu mwaka 2014, TFDA imefuta usajili wa dawa tatu (3); dawa ya malaria aina ya *Amodiaquine*, dawa ya kutibu fungus aina ya *Ketoconazole* na dawa za kikohozi zenye kiambata cha *Phenylpropanolamine*. Vile vile, imebadili matumizi ya dawa nne, dawa ya malaria aina ya *Sulphadoxine* na *Pyrimethamine(SP)* na dawa za kutibu bacteria aina ya *Kanamycin*, *Amikacin* na *levofloxacin*.

SPIKA: Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, swali la nyongeza!

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kwamba Wizara imekiri kwamba dawa zimeondolewa na kwamba tafiti mbalimbali zinafanyika. Je, Wizara imechukua hatua gani kwa watu ambao wamepata madhara ya hizo dawa? Je, Wizara iko tayari kuhudumia matibabu kwa wale ambao wamepata madhara ya hizo dawa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwamba ni hatua gani ambazo zinachukuliwa? Pale ambapo madhara yanajitokeza na fomu hizi ambazo nimeeleza hapa *yellow forms*, hatua ya kwanza kabisa ni kusimamisha matumizi ya dawa hiyo katika eneo la matumizi.

Mheshimiwa Spika, natoa maelekezo kwa watumiaji wote nchini wa dawa hizi, wasimamizi wa vituo hasa Waganga Wakuu wa Wilaya na Mikoa kuhakikisha kwamba fomu hizi za njano zinatumika na fomu hizi za *blue* kwa ajili ya utoaji wa taarifa hizo. Kwa hiyo, hatua ya kwanza kabisa ni kusimamisha hiyo dawa na baada ya hapo...

Mheshimiwa Spika, kwamba ni kitu gani au tayari ni hatua zipi ambazo zimechukuliwa kwa ajili ya kuwahudumia hawa wagonjwa. Pale ambapo imejitokeza unabadili dawa na napenda nitoe maelekezo nchi nzima, ni lazima kubadili hiyo dawa baada ya kuwa umesimamisha ili mgonjwa asipate madhara zaidi kwa tatizo analokuwa nalo. Hiyo ndiyo hatua inayotakiwa kufanyika kitaalam.

SPIKA: Mheshimiwa Msabaha, swali la nyongeza!

MHE. MARYAM S. MSABAHA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize Naibu Waziri suala dogo la nyongeza; kwa kuwa famasi nyingi hasa sehemu za vijijini wanauza dawa ambazo zimepitwa na wakati na dawa hizi zinaleta madhara kwa binadamu.

Je, Wizara yako inatambua suala hili na kama inatambua ni hatua gani mtachukua za mkakati kuhakikisha famasi za pembezeni zinapitiwa na kuhakiki dawa ambazo zinazwa ili zisilete madhara mengi kwa binadamu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, suala hili la dawa zile ambazo zimepitwa na wakati yaani *expired date*. Kazi hii inafanyika katika utaratibu wa kawaida wa mara kwa mara ikiwa ni pamoja na kuangalia *stock level* ikoje na kufanya *auditing* katika maeneo ya kazi na maeneo ya huduma kote nchini.

Mheshimiwa Spika, hivyo, napenda nitoe maelekezo na Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba, pia tunazo maabara saidizi ambazo zinahamishika 15 katika nchi ambazo zinasaidia ufuatiliaji wa ubora wa kazi na pia ubora wa dawa ukoje na pia matumizi ya dawa katika maeneo mbalimbali kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, kuna ufuatiliaji ambao unaitwa *pharmacological vigilance*, yaani muda wote ambao dawa inakuwa kwenye soko na inatumika kunakuwa na ufuatiliaji wa hali ya ubora wa dawa hizo mbali na Maabara Kuu ambayo tunayo pale Mabibo chini ya *TFDA*.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha atauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Njwayo!

Na. 167

Ujenzi wa Daraja katika Mto Momba

MHE. JUMA A. NJWAYO - (K.n.y. MHE. IGNAS A. MALOCHA) aliuliza:-

Kukosekana kwa daraja katika Mto Momba linalounganisha Wilaya ya Sumbawanga Vijijini na Wilaya ya Momba kati ya Vijiji Vya Kilyamatundu na Kamsamba ni tatizo sugu kwa wananchi wa maeneo hayo. Mwaka 2013/2014, Serikali ilitenga shilingi bilioni mbili na mwaka 2014/2015, ilitenga tena shilingi bilioni mbili, lakini hadi sasa ujenzi wa daraja hilo bado haujaanza:-

- (a) Je , ni hatua gani imefikiwa katika ujenzi wa daraja hilo?
- (b) Je, ni lini ujenzi huo utanza rasmi na kukamilika?
- (c) Je, ni kiasi gani cha fedha kinahitajika ili kukamilisha ujenzi wa daraja hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Momba umekamilika. Kwa sasa Serikali kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) inakamilisha maandalizi ili kutangaza zabuni ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Daraja la Mto Momba unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2015/2016 na ujenzi unatarajiwa kuchukua takribani miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, gharama zinazohitajika ili kukamilisha ujenzi wa Daraja la Momba zitajulikana baada ya zabuni ya ujenzi wa daraja kutangazwa na Mkandarasi kupatikana.

SPIKA: Mheshimiwa Njwayo, swali la nyongeza!

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri angalau katoa majibu ya matumaini, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, hii miradi ya barabara hasa madaraja madogo imekuwa ikichelewa sana kiasi cha kuwakatisha tamaa wananchi wetu kule. Je, Wizara au Serikali inachukua jitihada gani za makusudi kupunguza muda mwingi inaochukua, maana wananchi wanapata matumaini halafu baadaye yanakatika. Upo mpango wa haraka haraka kwenye haya madaraja madogo madogo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kati ya barabara ya kutoka Mtama kwenda Newala na Tandahimba kuna daraja pale linajengwa, limechukua muda mrefu kweli kweli kiasi kwamba yaani wala haileti ladha kuendelea kuona ucheleweshaji wa ujenzi ule unaofanywa pale. Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuambia na najua ni mdau anatoka Mkoa wa Lindi ambayo barabara hiyo iko. Jitihada gani za makusudi au usimamizi gani unachukuliwa na Serikali ili daraja lile limalizike haraka?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, ucheleweshwaji wa ujenzi wa madaraja, kwanza inatokana na viwango vya madaraja yenyewe kwa sababu madaraja yako yale madogo ambayo pia tumekabidhi shughuli hizi kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia Halmashauri na ndiyo wao wanaratibu ujenzi wa madaraja hayo.

Mheshimiwa Spika, pia yako madaraja makubwa ambayo pia yako kwenye ngazi ya barabara za Mikoa na ngazi za Kitaifa ambazo barabara zote hizi zinapokuwa na madaraja aina hiyo lazima yapitie kwenye taratibu za utoaji zabuni kwa kuanza kufanya upembuzi yakinifu, lakini pia kuwe na usanifu wa kina lakini na kutambua pia gharama halafu baadaye utangaze zabuni.

Mheshimiwa Spika, taratibu hizi ni za kisheria, kwa hiyo, huna namna nyingine ya kuharakisha zoezi hilo ni pale tu ambapo fedha ipo na taratibu zitambulike na baadaye sasa gharama zitafahamika baada ya kuwa tumepata Mkandarasi wa kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, taratibu hizi zitazingatiwa na pale ambapo panahitaji kupunguza muda tutasimamia muda upungue.

Mheshimiwa Spika, suala la daraja la Mtama, ni daraja lililoko kwenye barabara iliyoko chini ya Mamlaka ya Mkoa (TANROAD) na kwa hiyo basi, daraja hilo kwa kazi ambayo inaendelea sasa tutaendelea kuwasiliana na TANROAD, Mkoa wa Lindi na Mtwara ili kuona kuwa daraja hilo linajengwa kwa wakati na likamilikie ili kurahisisha usafirishaji wa abiria na mali kutoka Mkoa wa Lindi kwenda Mkoa wa Mtwara kwa Wilaya za Newala na Lindi Vijijini.

SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale, maswali ya nyongeza!

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa upembuzi na usanifu yakinifu umeshafanywa tayari kwa ajili ya daraja lile na hapa Serikali inatuambia kwamba gharama zitajulikana pale ambapo Mkandarasi atapatikana. Ili wananchi wawe na subira nzuri wajue kwamba Serikali imedhamiria kujenga daraja hili, je, hamwezi kuonesha ni kiasi gani cha gharama ambacho kitagharimu daraja hilo kwa sababu upembuzi unakwenda sambamba na kupanga bajeti na hiyo bajeti bila shaka itapangwa kufuatana na jinsi walivyofanya upembuzi wao? Je, Serikali haiwezi kuwaambia wananchi kwamba daraja lile gharama yake itakuwa ni kiasi kadhaa cha fedha? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI!

WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Naibu Waziri amesema kwamba, sasa hivi wapo katika mchakato wa zabuni, kwa hiyo, suala la kuwaambia wananchi kwamba daraja lile gharama yake ni kiasi hiki, ndiyo kusema unawaambia na wale ambao wataomba zabuni kwamba gharama ya hicho kitu ni kiasi gani. Kwa hiyo, itaathiri suala zima la ushindani katika utoaji wa hiyo zabuni. Kwa hiyo, kwa maana ya Serikali tunafahamu, lakini hatuwezi kutamka katika vyombo vya habari.

SPIKA: Ahsante. Maswali yamekwisha na muda wenyewe umekwisha. Waheshimiwa, naomba niwatambue baadhi ya wageni tulio nao.

Wako wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, ambao kwanza ni mke wake mpenzi, Bi. Germina Lukuvi. Ahsante. Huyu mke wake ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Wake za Viongozi iitwayo *Millennium Group*. Sasa *members* wa *Millennium Group* sijui kama wamefika, kama wamefika basi karibuni. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine wa Mheshimiwa William Lukuvi, ambao ni viongozi kutoka Wizarani. Hawa ni Katibu Mkuu, ndugu Alphayo Kidata. Yuko Naibu Katibu Mkuu Dkt. Selassie Mayunga. Yuko Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa, Mheshimiwa Nehemiah Mchechu. *(Makofi)*

Pia wapo Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, wapo Wakurugenzi na Maafisa wengine wa Wizara wakiongozwa na Bi. Tabu Aron, Mkurugenzi Utawala na Rasilimali Watu. Bi, Tabu Aron naomba asimame na wenzake. Ahsante, kumbe wote mko hapa, ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 10 wa Chuo cha Ardhi Tabora, wakiongozwa na ndugu Lazaro Masimami. Naomba na hao wanafunzi walipo wasimame, wako wapi, wamekosa nafasi, kama 10 tu wanaweza kukaribishwa kwa *Speaker's Gallery*. Ninyi mnaohusika kama wako 10 tu waingie kwenye *Speaker's Gallery*.

Halafu tuna viongozi wakuu wa CCM wa Jimbo la Ismani ambao ni Wenyeviti, Makatibu Wenezi na Fedha wa Kata zote. Wakiongozwa na ndugu Newton Mwongi. Ha hao wote wasimame walipo. Ahsante na karibuni sana, Waziri wenu anafanya kazi nzuri sana katika Wizara hiyo mpya. *(Makofi)*

Tuna wageni 20 wa Mheshimiwa Halima Mdee, Waziri Kivuli wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wakiongozwa na ndugu Hassan Athuman. Naomba hawa wageni 20 wasimame walipo, kama wapo hapa ndani. Nafikiri leo nafasi kidogo itapatikana baadaye mchana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa James Lembeli ambao ni wanafunzi 81 na Walimu wanne kutoka shule ya sekondari ya wasichana, inaitwa Malikia wa Familia, *Queen of the family*. Hawa nao *queens* hawa wasimame. Aaa, ni *ma-queen* kwelikweli hawa. Ahsanteni na karibuni sana, mnafanana na *ma-queen*, someni kwa bidii nyie *ma-queen*, *ma-queen* bila elimu hai-*fit*. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Ahmed Shabiby, ambao ni wanafunzi 30 na Walimu 11 kutoka shule inaitwa Shabiby Sekondari ya Gairo. Naomba wasimame wanafunzi kama wapo humu ndani, kama wapo wasimame. Basi na wao pia wamekosa nafasi.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Charles Kitwanga, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, ambao ni wanafunzi 75 na Walimu watano kutoka shule ya sekondari ya Bukumbi. Naomba wanafunzi wa Bukumbi wasimame kama wapo! Leo tuna wageni wengi, watakuja baadaye.

Tuna wageni 15 wa Mheshimiwa Khalfan Aeshi- kutoka Sumbawanga na hawa nao wasimame walipo kama wamepata nafasi, nao hawajapata nafasi.

Kuna wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wako watoto 30 na Walimu 10 kutoka Kanisa la Waadventista la Sabato la Ipagala Dodoma. Naomba watoto hawa wasimame kama wapo. Leo tumezidiwa hapa.

Tuna wanafunzi 45 kutoka Shule ya Msingi *Atlas Scout Group* Dar es Salaam. Kama wapo wasimame, *Atlas Scout Group*, okay wako pale wachache pale wadogo wadogo pale na wengine okay wako hapa. Tunaomba sana msome kwa bidii. (Makofi)

Halafu kuna wanafunzi 85 na Walimu 12 kutoka Shule ya Msingi Atlas ya Dar es Salaam, ni hao hao, hapana, basi simameni na wenyewe ni hao hao 85, nafikiri nao pia wamekosa, ndiyo hao wa kwanza eeh? Okay, ahsante sana mwalimu kwa kuwaleta watoto. (Makofi)

Tuna wanafunzi 30 na Walimu 20 kutoka Mikindani, Mtwara, kawa wapo wasimame. Leo nyumba imekuwa *overloaded*.

Tuna wanafunzi 65 kutoka shule ya sekondari ya *Don Bosco* Tanga, kama wapo wasimame, ahaa, ahsante sana, tunawatakiwa masome mema, mwendelee vizuri. (Makofi)

Tuna wanafunzi 61 kutoka Chuo Kikuu cha *Saint John* na hawa wasimame kama wapo ndani. Dalili haipo.

Tuna wanafunzi 46 kutoka Chuo Kikuu cha *Saint Joseph*, Tawi la Arusha, na wenyewe kama wapo wasimame. Wamekosa nafasi.

Kuna wageni 30 ambao ni Watawa Wamisionari Wa-*pasionist* kutoka Veyula Dodoma wakiongozwa na Padri Marcel Tarimo. Kama wapo na wenyewe wasimame. Karibuni sana na ahsanteni sana. (Makofi)

Halafu tuna ndugu Mohamed Bhailoo, Ndugu Reuben Thomas na Ndugu Eden Katininda. Hawa nao wasimame walipo, sijui wapi. Ahsanteni sana na karibuni, naona wengine wako huku nyuma. Bahati mbaya watu wengi wamesubiri siku za mwisho, nafasi imekuwa ndogo. Ahsanteni sana. (Makofi)

Wageni wengine wote ambao sikuwataja, mnakaribishwa. (Makofi)

Mheshimiwa Selasini!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68, kutokana na shida ambayo Walimu wapya wanaipata sasa hivi katika baadhi ya Halmashauri. Mwezi uliopita Serikali iliwapeleka Walimu wapya katika baadhi ya Halmashauri hapa nchini, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, lakini hadi sasa wale Walimu hawajapata fedha za kujikimu wala mshahara. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo hili linawapa matatizo makubwa, wamekuwa ombaomba, wengine wamekata tamaa na wanafikiria hata kuacha kazi na kurudi makwao. Ni kwa nini Serikali haiwaagizi Wakurugenzi au kama imeshawaagiza, ni kwa nini haiwachukulii hatua Wakurugenzi ambao hawataki kutekeleza agizo hili ili Walimu wetu wakafanya kazi zao kama vile ambavyo walitegemea kuzifanya?

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47, kuhusu kujadili suala la dharura, sijui unaruhusu nisome?

SPIKA: Unaeleza suala hilo linahusu nini!

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Naam.

SPIKA: Soma, kanuni naijua, sasa sema linahusu nini suala lako la dharura.

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Hilo suala linahusu watumishi wa TAZARA upande wa Tanzania, takribani wapatao 1600 na, ambapo ukijumuisha na familia zao, inakuwa takribani watu 6,000, kwa miezi mitano sasa mfululizo, hawajawahi kupata senti tano ya mshahara na wanahangaika na familia zao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili suala naona ni dharura na lina athari kwa umma, kwa sababu wanafunzi hawasomi, vyakula hawapati, wanavunjiwa haki za binadamu na mpaka sasa Wizara, Serikali haijatoa tamko lolote kuhusu wafanyakazi hao. (Makofi)

SPIKA: Hapana, litajadiliwa kwa utaratibu mwingine na siyo huo, lakini nimelipokea. Mheshimiwa Susan!

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimesimama niombe Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68. Juzi wakati tunajadili hoja ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, pamoja na mambo mengine kiti chako kilitamka wazi kwamba, Kamati ya Huduma za Jamii, ifuatilie kwa kina masuala ya vyuo vikuu hususan cha *Saint Joseph* na *KIU*, lakini leo kwa masikitiko makubwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu amesema kwamba yeye anataka Serikali ndiyo ilete ripoti na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba niliingia kwenye Kamati ya Huduma za Jamii na hili jambo lilijadiliwa kwa kirefu na Kamati Ndogo ikaundwa ya Serikali kwenda katika Chuo cha *Saint Joseph*, mwezi huu wa Mei mwishoni, lakini ripoti waliyoileta ilikuwa haikidhi kabisa na Waziri analijua hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba mtuambie, kiti chako kikishatoa maamuzi, inakuwaje Serikali inakuja inasema vinginevyo. Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Susan, wala halina tofauti kama tulivyokubaliana, halina tofauti. Sisi wote 357, hatuwezi kufikiria ripoti, ndiyo maana Serikali itapeleka ripoti yao kwenye Kamati, Kamati itajadili, ndiyo utaratibu ulivyo. Maana yake Kamati ni ndogo, inaweza kwenda kwa undani zaidi na kutuletea ripoti. Wote Serikali na Kamati watafanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Katibu! Aaa, Mheshimiwa sikukuona!

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE-: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba Mwongozo wako kufuatia taarifa ambazo tumekuwa tukitumiwa kwenye ujumbe mfupi wa simu kutoka Ofisi ya Bunge. Mara nyingi tumekuwa tukitumiwa ujumbe huu tuka-google ili tupate taarifa za Bunge zinazoendelea kila siku.

Mheshimiwa Spika, naomba tu Mwongozo wako kwamba, tuiombe Ofisi ya Bunge, kwa sababu si wote tuna simu za kupapasa, ama za ku-peruse ama za nini, wengine bado tuna simu zile za kizamani. Kwa hiyo, tunaomba ofisi yako watuletee taarifa pia kupita njia ile ya zamani tuliyokuwa tumeizoea. Ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kama mna simu za zamani mkanunue mpya. *(Kicheko/Makofi)*

Ndiyo, kwa sababu soon Bunge la 11 litaingia kwenye *e-Parliament*, sasa hamna namna, zile za zamani mziupe kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Katibu!

Mheshimiwa ulisema umekwishaelewa, ukishasema haujibiwi hapo hapo, vitu vingine vigumu kujibu.

Katibu ngoja kwanza. Mheshimiwa Selasini alikuwa amesimama, alifikiri atajibiwa hapa, nimesema, vitu vingine haviwezi kujibiwa na Spika, maana yake havijui. Ndiyo maana tuna-note hapa wanaohusika tutawapa kazi inayostahili. Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA WILLIAM V. LUKUVI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

SPIKA: Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwanza mniwie radhi kama mtakuta kuna upungufu, hii ni mara ya kwanza katika miaka 20 ya Ubunge wangu kusoma bajeti yangu mwenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mkikuta mambo hayajakaa vizuri, ingawa nimekuwa Waziri kwa miaka 15, lakini nilikuwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa miaka 10 na miaka mitano Mkuu wa Mkoa. Sasa hii ya kwangu ndiyo ya kwanza. Kwa hiyo, mkikuta kuna upungufu, mniwie radhi kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja, kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2014/2015 na malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nimewasilisha vitabu na viambatabnisho na majedwali ambayo yapo nyuma ya kitabu, yapo 18 kuanzia ukurasa wa 103 wa hotuba, ambayo mtagawiwa humu ndani mpaka ukurasa wa 192.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hiyo, nimeambatanisha pia vitabu ambavyo viko kwenye mabegi yetu.

- Kitabu cha kwanza, ni utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha mwaka 2014/2015. *(Makofi)*
- Halafu, kama mtakavyosikia kwenye hotuba yangu, ahadi niliyotoa ya kubadilisha viwango vya kodi, kuna kitabu cha mabadiliko ya viwango vya kodi na tozo zote mbalimbali. *(Makofi)*
- Halafu, kuna kitabu kingine cha kiongozi wa wanakijiji katika ushirikishwaji wa mpango wa usimamizi wa ardhi vijijini. *(Makofi)*
- Halafu kuna kitabu cha mpango wa Taifa wa matumizi ya ardhi mwaka 2013 mpaka 20133. *(Makofi)*
- Halafu kuna kitabu kipya cha maelezo kuhusu huduma za sekta ya ardhi. *(Makofi)*
- Pia, kwa kujua kwamba Wabunge ni Madiwani, nimewapa taarifa ili mjue ikama ya watumishi wote waliopo kila Halmashauri na upungufu wake kwenye kitabu hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa hizo, ndizo zilizowasilishwa na kuambatanishwa na hotuba hii na kuwekwa katika mikoba yenu mliyoipata. Naomba Bunge lipokee taarifa hizo na zijumuishwe kwenye *hansard*. Aidha, zipo taarifa nyingine nyingi ambazo zimeambatanishwa na hotuba yangu, lakini kutokana na *volume*, yaani ukubwa...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ulizosema wewe hizo, haziwezi kuingia kwenye *hansard*...

WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Basi hotuba yangu...

SPIKA: Kama zilitakiwa kuingia kwenye *hansard* ingekuwa *laid on the table!* Hiyo ni taarifa tu ya kwako, lakini *hansard* haiwezi kuweka.

WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, basi mtakavyoona.

SPIKA: Si umewagawia mifuko! (*Kicheko/ Makofi*)

Amewagawia mifuko, haya, tuendelee. Endelea Mheshimiwa!

WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Aidha zipo taarifa nyingine nyingi ambazo zimeambatanishwa na hotuba yangu, lakini kutokana na wingi wa taarifa, taarifa hizo hazikuweza kuingia katika mikoba yenu, nimeziweka kwenye tovuti ya Wizara, kwa anuani ya www.ardhi.go.tz.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa watu ambao hawapo ndani ya Bunge wakiingia ndani ya *website* hii, watapata hotuba na taarifa zote na sheria zote za Wizara tangu Wizara ile imeanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia, zinapatikana katika *mobile application* inaitwa *ardhi tza*. Sasa kwenye *App store*, uki-*google*, utapata *icon* inatokeza inaitwa *ardhi tza*, kwa hiyo, pale unaweza kupata taarifa zote. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenye *iPad* na simu pale nje kuna huduma watu ambao wanaweza kuwatolea ile *icon* kwenye simu yako ukasoma hotuba zote hizi zilizopo na taarifa nyingine ambazo hazipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kuingia katika Baraza la Mawaziri kufuatia mabadiliko aliyoyafanya mwezi Januari.

Vile vile nampongeza Mheshimiwa George Masaju, kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na Mheshimiwa Dkta Grace Kwahya Puja na Mheshimiwa Innocent Rwabushaija Sebba kwa kuteuliwa kuwa Wabunge. Nawatakia wote kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunitewa kuiongoza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, nampongeza yeye binafsi pamoja na Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa jitihada zao za kuiongoza, kusimamia na kuendeleza amani, utulivu na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa ambao unaniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa ya kuongoza sekta hii mtambuka na muhimu katika maendeleo ya Taifa letu.

Nawapongeza kwa dhati, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mbunge Kitope, kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, aliyeongoza Wizara kabla yangu, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye-, na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, waliokuwa Manaibu Mawaziri kwa kuweka misingi imara ya kusimamia sekta ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa hotuba yake iliyoeleza malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi ya Serikali kwa mwaka 2015/2016. Naahidi kwamba Wizara yangu itayafanyia kazi yale yote yanayoihusu sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe kwa kuongoza shughuli za Bunge kwa ushujaa na ufanisi ufanisi. Pia nampongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa na Naibu Spika wa Bunge letu, kwa utendaji mzuri katika uendeshaji wa Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza Wenyeviti wapya hawa wa Bunge ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiongoza shughuli za Bunge, Wenyeviti wote, akiwemo wa zamani Mheshimiwa Zungu na hawa wapya. Ni ukweli usiofichika kwamba wamemudu vyema jukumu hili la kuongoza Bunge lako Tukufu kwa ufanisi mkubwa. Mwenyezi Mungu aendeleo kuwaongoza na kuwapa nguvu, afya na hekima za kumudu zaidi majukumu yao, ikizingatiwa kwamba na Mheshimiwa Mng'ong'o ni Diwani wangu wa Iringa Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira inayoongozwa na jembe, Mwenyekiti James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Abdulkarim Hassan Shah, Mbunge wa Mafia, kwa ushirikiano mkubwa wa Kamati nzima na Wizara na ushauri wao ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ushauri wao utaendelea kuzingatwa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile natoa shukrani za pekee sana kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Angella Jasmin Kairuki. Bunge hili linamfahamu na wote tunajua kwamba hiki ni kifaa. Kama ingekuwa ni nguo ni ile ya kuweka chini ya kabati kila siku, kwa ushirikiano na msaada mkubwa anaonipatia wakati wa kutekeleza majukumu ya sekta ya ardhi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Katibu Mkuu, ndugu yangu Alphayo Kidata ambaye mmetambulishwa leo; Naibu Katibu Mkuu Dkt. Mayunga, Kamishna, Wakuu wa Idara, Makamishna Wasaidizi na Wakuu wote wa Idara katika Kanda na Makao Makuu na Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu pamoja na mashirika yote, pamoja na watumishi wote wa Sekta ya Ardhi kwa ngazi zote kwa kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Ismani ambao nimekuwa nao sasa kwa vipindi vinne. Nawapongeza sana Viongozi wangu wa Chama wa Kata zote ambao wameweza kuja leo na umewatambulisha hapa, nawapongeza sana lakini nawashukuru kwa kukubali kufika. Namshukuru mke wangu Germina Lukuvi ambaye leo amekuja na watoto wangu Norbert, Brown na Anifisye kwa uvumilivu wao na kunitia moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo za Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba, aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi na kifo cha Mheshimiwa Eugen Elishilinga Mwaiposa, aliyekuwa Mbunge wa Ukonga. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu ndugu na wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi na Ukonga pamoja na wale wote walioguswa na msiba huo.

Mheshimiwa Spika, kadhalika wako wananchi waliofariki katika maafa mbalimbali yaliyojitokeza nchini na ajali mbalimbali za barabarani na nyinginezo nchini na wengine kujeruhiwa. Nachukua fursa hii kutoa pole kwa wafiwa wote Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina. Aidha, nawatakia afya njema na kupona kwa haraka majeruhi wote.

Mheshimiwa Spika, sasa niangalie mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2014/2015 na Malengo ya Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Naomba nieleze kwa kifupi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 na malengo kwa mwaka 2015/2016. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa taarifa za utekelezaji zinaishia mwezi Aprili.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato; kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara ilipanga kukusanya Shilingi bilioni 61.32 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato yatokanayo na kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi Aprili 15, Wizara imekusanya Shilingi bilioni 47 sawa na asilimia 76.6 ya lengo na ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 3.8 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 43.2 zilizokusanywa mwaka 2013/2014. Aidha, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kuhimiza wamiliki wa ardhi kulipa kodi ya ardhi, ada na tozo mbalimbali kupitia benki. Hatua hii inalenga kuongeza ukusanyaji wa maduhuli na kudhibiti uvujaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, niliahidi kuhuisha viwango vya kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi ambavyo vinaonekana kuwa kikwazo kwa wananchi wanaohitaji huduma ya ardhi. Uhuishwaji huu wa viwango vya kodi, tozo na ada za ardhi umelenga kupata viwango vinavyopangika, kukubalika na kulipika. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi hiyo imekamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuhuisha viwango hivyo, wananchi wa kipato cha chini watamudu kulipa kodi, tozo na ada hizo. Kodi ya pango la ardhi imepungua kwa wastani wa asilimia 30 na viwango vingine vinavyomgusa mwananchi masikini wa kawaida vimepungua kwa asilimia 50 au zaidi. Kwa mfano, kodi ya mashamba yaliyopimwa na kumilikishwa, hasa ya wananchi vijijini imepunguzwa kwa asilimia 60. Kodi ya zamani ilikuwa ni Sh. 1000 kwa hekari, sasa imepunguzwa hadi kuwa Sh. 400 kwa hekari. Ya pili, kodi ya mashamba ya biashara imepunguzwa kwa asilimia 50 kutoka Sh. 10,000 hadi Sh. 5,000 kwa hekari.

Tatu, ada ya upimaji wa ardhi imepunguzwa. Watu wengi walikuwa hawawezi kupima ardhi zao kwa sababu gharama ilikuwa kubwa sana. Sasa tunawashawishi watu wapime kwa sababu kodi ya kupima sasa imepunguzwa kwa asilimia 62.5 kutoka ilivyokuwa Sh. 800,000 hadi Sh. 300,000 kwa hekta.

Mheshimiwa Spika, nyaraka za tahadhari na vizuizi *caviet* zimepunguzwa kwa asilimia 66.7 kutoka Sh. 120,000 hadi Sh. 40,000. Nyaraka za ubadilishaji wa majina *deed poll* zimepunguzwa kwa asilimia 62.5 kutoka Sh. 80,000 hadi Sh. 30,000. Usajili wa nyaraka nyinginezo zimepungua kwa asilimia 50 kutoka Sh. 80,000 hadi Sh. 40,000.

Mheshimiwa Spika, gharama za kupata nakala ya hukumu kwenye Mabaraza ya Ardhi ambazo zilikuwa Sh. 16,000 sasa zimepunguzwa hadi gharama yake kuwa Sh. 6,000 na zimepunguzwa kwa asilimia 62.5. Ada ya maombi ya kumiliki ardhi ambayo ilikuwa inatozwa Sh. 80,000 sasa imepunguzwa kwa asilimia 75, mwananchi atatakiwa kutoa Sh. 20,000 tu badala ya Sh. 80,000.

Ada ya maandalizi ya hati imepunguzwa kutoka Sh. 160,000 ilivyokuwa zamani hadi Sh. 50,000. Kwa hiyo, hii nayo ada ya maandalizi ya hati imepunguzwa kwa asilimia 68.8.

Mheshimiwa Spika, viwango hivi vitaanza kutumika tarehe 1 Julai na nimeshatia sahihi tayari na vipo katika kitabu cha kodi zote zilizomo kwenye kitabu hiki cheupe na wananchi wengine wote wanaweza kupata kwenye *website* ya Wizara. Ada na tozo mbalimbali za Sekta ya Ardhi ambazo kitabu hiki kimesambazwa na nyingine zinaonekana kwenye mtandao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwango vya tozo ya *premium* kuanzia mwaka wa fedha 2015 – 2019, tozo hii imepunguzwa kwa asilimia 50 kutoka asilimia 15 ya sasa hadi asilimia 7.5 ya thamani ya ardhi na kiwango hiki ndicho kitakacholipwa kwa mashamba na viwanja. Kama ilivyo kwa marejesho ya ada, kodi na tozo nyingine za Sekta ya Ardhi, asilimia 30 ya maduhuli yote yatakasanywa kutokana na tozo hii yatarudishwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na matumizi yake yataelekezwa katika kuboresha Sekta ya Ardhi. Kwa kuwa viwango vya kodi na ardhi sasa ni rafiki, natoa rai kwa wamiliki wote wa ardhi kulipa kodi kwa hiari na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya marekebisho ya viwango vya kodi kufanyika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi bilioni 70. Kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara yangu itaboresha ukusanyaji wa kodi, ada na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi kwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa ulipaji utakaotumia simu ya viganjani. Mfumo huu unatarajiwa kuanza kutumika tarehe 1 Julai, mwaka huu na utarahisisha ulipaji wa maduhuli, kupunguza adha ya msongamano wa kupoteza muda kwenye vituo vya malipo.

Mheshimiwa Spika, aidha huduma za ukadiraji wa pango la ardhi na uboreshaji wa taarifa za wamiliki wa viwanja na mashamba itapatikana kupitia simu ya kiganjani. Natoa wito kwa wananchi nchini kuupokea na kuutumia mfumo huu kulipa maduhuli yatoakanayo na ardhi kwa njia ya elektroniki.

Mheshimiwa Spika, matumizi; katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 85.74 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 11.54 zilitengwa kwa ajili ya Mishahara; shilingi bilioni 40.05 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 34.15 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha za miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 13.3 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 20.85 ni fedha za nje. Hadi Aprili, 2015, jumla ya shilingi bilioni 32.2 zilipokelewa, sawa na asilimia 37.6 ya fedha zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10.38 ni mishahara na shilingi bilioni 21.82 ni matumizi mengineyo, lakini fedha za miradi hatujapokea ila kazi hazikwami.

Mheshimiwa Spika, Utawala wa Ardhi; katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliahidi kuigawa Kanda ya Mashariki kuwa Kanda mbili, Kanda ya Dar es Salaam na Kanda ya Mashariki. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kanda ya Dar es Salaam imeanzishwa na inahudumia Manispaa za Temeke, Ilala na Kinondoni na Kanda ya Mashariki ambayo sasa nimeagiza makao yake yatakuwa Morogoro inahudumia Mikoa ya Pwani na Morogoro. Hadi sasa Wizara ina Ofisi za Kanda nane ambazo ni Dar es Salaam, Mashariki, Kati, Ziwa, Kaskazini, Kusini, Nyanda za Juu Kusini na Magharibi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu imeandaa rasimu ya mwongozo wa utaratibu wa kupanga, kuhakiki, kupima, kumilikisha na kusajili kila kipande cha ardhi. Hatua hii inalenga kuwaongezea watendaji wa sekta ya ardhi uelewa wa pamoja kuhusu masuala ya ardhi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Kazi hiyo itakamilika katika Mwaka huu wa Fedha 2014/2015. Aidha, Wizara imeandaa kitabu kwa lugha rahisi kinachoelezea hatua mbalimbali zinazopaswa kufuatwa na wananchi ili kupata huduma mbalimbali zinazotolewa na sekta ya ardhi, ambacho nimekigawa leo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imefanya uteuzi wa Wajumbe wa Kamati za Ugawaji Ardhi wa Halmashauri katika Halmashauri za Wilaya ya Mkuranga, Kibaha, Mlele, Uvinza, Musoma, Nzega, Ikungi, Mufindi, Kaliua, Busega, Kakonko, Biharamulo, Sikonge, Nsimbo na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

Mheshimiwa Spika, *Land Bank*; katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara imejiwekea lengo la kutambua maeneo ya ardhi yenye ukubwa wa ekari takriban 200,000 nchini na kuwa sehemu ya Hazina ya Ardhi kwa ajili ya uwekezaji na matumizi ya umma. Kwa kuzingatia mahitaji ya fidia kwa ajili ya utwaaji wa maeneo hayo, Serikali imetenga shilingi bilioni tano kwenye Mfuko wa Fidia ya Ardhi kwa ajili ya kulipa fidia ya maeneo yatakayotwaliwa. Hadi Aprili, 2015, Serikali imebatilisha milki za mashamba mawili (Ufyome katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati na *Fort Ikoma*, Mkoani Mara) na viwanja 67 nchini kote. Vile vile, uhakiki na ukaguzi wa mashamba pori yaliyotelekezwa na wamiliki utaendelea kufanyika ili kuitwaa na kubatilisha na kuihifadhi kwenye hazina ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Sheria ya Ardhi; Wizara inashughulikia utoaji wa Hati, Vyeti vya Ardhi ya Vijiji na Hati za Hakimiliki ya Kimila. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliahidi kutayarisha na kutoa Hati Miliki 40,000. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2015, Wizara iliandaa na kusaini Hati Miliki 20,189 sawa na asilimia 50.5.

Kanda iliyoongoza kuandaa hati nyingi zaidi ni Dar es Salaam (hati 4,491) ikifuatiwa na Kanda ya Kusini Magharibi (hati 3,516) Kanda iliyoandaa hati chache zaidi ni Kanda ya Kati (hati 680).

Mheshimiwa Spika, aidha, Halmashauri iliyoongoza kuandaa hati nyingi zaidi ni Temeke (hati 1,959). Hata hivyo, Halmashauri ambazo hazikuandaa hati au kuwamilikisha wananchi ardhi ni Iramba, Singida, Mkalama, Masasi, Lindi, Nyang'wale, Butiama, Mpanda, Nsimbo, Mlele, Kaliua, Ushetu, Msalala, Buhigwe, Kigoma, Kibondo, Kilindi, Momba na Busekelo, hawa hawakumilikisha hati hata moja.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, lengo la Wizara ni kuandaa na kutoa Hatimiliki 40,000. Napenda kurudia wito wangu kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinamilikisha viwanja vyote vilivyopimwa na kuandaa Hati ili wananchi waweze kuwa na milki salama za ardhi na kila mwaka ziwe zinaweka malengo makubwa ya upimaji na umilikishaji wa viwanja na mashamba nchini. Aidha, wananchi na viongozi wa Serikali za Mitaa wanahimizwa kuheshimu na kulinda miliki zilizotolewa kisheria na maeneo yaliyotengwa kwa matumizi ya umma. Hatua za kisheria zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya wavamizi wa maeneo ambayo yamemilikishwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilitoa ilani 3,823 za ubatilisho kwa wamiliki waliokiuka masharti wakiwemo wamiliki wa mashamba yasiyoendelezwa katika Mikoa ya Morogoro, Pwani na Rukwa. Kwa mwezi Mei pekee nafurahi kusema Mheshimiwa Rais, wili iliyopita ameridhia ufutwaji wa miliki ya mashamba pori makubwa 16 yaliyopo Wilaya ya Kibaha baada ya wamiliki kuvunja masharti ya umilikishwaji. Ardhi hii tunaifanyia utaratibu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kibaha na TAMISEMI ili angalau baadhi yake irudi kwenye Benki ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara itaendelea kushughulikia ubatilisho wa milki zote zinazokiuka masharti ya uendelezaji wa viwanja na mashamba. Mpaka sasa *notice* zimeshatolewa kwa ilani 3,823. Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatuma ilani za ubatilisho kwa wamiliki wote wa ardhi wa mashamba na viwanja ambao hawalipii kodi na hawaendelezi ili mashamba yao na viwanja vyao vifutwe wapewe watu wengine wenye nafasi ya kuendeleza sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Ardhi ya Vijiji; hadi kufikia Aprili, 2015, Wizara imetoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji 988. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Ofisi ya Rais kupitia Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge (MKURABITA) na wadau mbalimbali imeratibu na kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila 25,897 ikilinganishwa na lengo la kutoa Hatimiliki za Kimila 70,000.

Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya nchini pamoja na wadau mbalimbali kuhakikisha kwamba zoezi la utoaji wa Hatimiliki za Kimila linakuwa endelevu na linafanyika kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru taasisi za fedha ambazo zimetambua na kukubali kupokea hatimiliki za kimila kama dhamana ya kupata mikopo. Taasisi hizo ni pamoja na NMB, CRDB, PSPF, SIDO, Meru Community Bank na Agricultural Trust Fund Bank kwa kutoa mikopo ya jumla ya Shilingi bilioni 49.2 kwa mwaka huu wa fedha huu. Aidha, nahimiza benki na taasisi nyingine za fedha wazitambue na kuzikubali hati miliki za kimila kutumika kama dhamana ya kupatia mikopo kwa kuwa zina nguvu ya kisheria kama ilivyo kwa hati miliki za kawaida.

Mheshimiwa Spika, Udhhibiti wa Ardhi ya Vijiji; miaka ya hivi karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la uporaji wa ardhi vijijini. Hili linafanywa na watu wachache wenye uwezo wa fedha kwa kushirikiana na Viongozi wa Vijiji wasio waadilifu. Kwa kiasi kikubwa ardhi inayoporwa inaachwa bila kuendelezwa na nyingine kukopewa na nyingine kuhawilishwa, kupimwa na kuombewa hatimiliki za kawaida. Hali hii ikiachwa kuna hatari ya wananchi wa vijijini kugeuka wapangaji wa ardhi za vijiji vyao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, li kuhakikisha kuwa miamala ya ardhi vijijini inafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu, uhawilishaji wa ardhi ya vijiji, utafanyiwa tathmini kuanzia mwaka huu wa fedha ili kujua ukubwa wa tatizo na kuzuia mianya ya ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu, ikibidi kuweka ukomo wa kiasi cha ardhi (*land ceiling*) ambacho mtu mmoja anaweza kumiliki kijijini. Azma hii inalenga kuyalinda makundi mbalimbali ya jamii wakiwemo wakulima na wafugaji kumiliki ardhi. Aidha, Wizara imetoa Mwongozo sasa wa namna ambavyo vijiji vinaweza vikamilishwa ardhi kwa wananchi wanaotaka kuchukua ardhi ya vijiji na kuhawilishwa ili waweze kupata hati.

Mheshimiwa Spika, ili kusimamia kwa ufanisi ardhi ya vijiji iweze kuwanufaisha wananchi wote, napenda kutoa agizo kwa Watendaji wa Vijiji wote nchini kuandaa orodha ya walionunua ardhi katika vijiji vyao wakionesha majina na kiasi cha ardhi kilichonunuliwa. Taarifa hizi ziwafikishie Maafisa Ardhi Wateule katika Halmashauri husika kwa uhakiki na pia zinfikie mimi baada ya uhakiki. Vile vile natoa rai kwa wananchi wote waishio vijijini, kufuatilia kwa karibu uzaji wa ardhi ili kuhakikisha kuwa unafanywa kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka ya Mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, Udhhibiti wa Migogoro ya Matumizi ya Ardhi; baadhi ya hatua zilizochukuliwa za kupunguza migogoro ya ardhi katika Halmashauri nchini ni pamoja na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 1,560, kuandaa mipangokina ya miji na majiji na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu

sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo. Dawa pekee ya kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi nchini ni kupanga na kupima kila kipande cha ardhi na kuwamilikisha wananchi na taasisi kisheria kwa kuwapatia hatimiliki. Pamoja na jitihada za jumla, Wizara inaendelea kutafuta ufumbuzi wa migogoro mikubwa kwa kuwaita mezani pande husika na kukaa nao katika meza ya majadiliano ili kupata ufumbuzi na udhibiti wa migogoro.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kukaa mezani na pande husika zimeanza kuleta mafanikio na kupata ufumbuzi katika mgogoro wa mashamba kati ya Mwekezaji (*Tanzania Plantation Limited*) yale mashamba ya Arumeru ambayo yamekuwa kama dondandugu na wananchi wanaozunguka mashamba yake na mgogoro kati ya mwekezaji wa shamba la *Noor Farm* lililopo Oljoro katika Wilaya ya Arumeru.

Mheshimiwa Spika, kutokana na makubaliano na wawekezaji hao, Serikali imepata jumla ya ekari 7,236.5 kwa ajili ya wananchi wasio na ardhi ndani ya migogoro husika. Ardhi hii itagawiwa kwa Wilaya ya Arusha DC na Arumeru kwa wananchi ambao hawana ardhi kabisa kwa sababu ardhi hii sasa imechukuliwa na Serikali. Aidha, Wizara imeunda timu ikijumuisha wataalam kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na Meru ambayo inaendelea na kazi ya uhakiki wa wananchi wasio na ardhi.

Mheshimiwa Spika, narudia, kuhakiki wananchi wasio na ardhi, kwa sababu nimeona ikiachwa hivi hivi wakati mwingine inaishia kwa viongozi na watu wengine wenye ardhi nyingi. Kwa hiyo tutahakiki na kila mmoja asiye na ardhi atapewa kipande chake na tutampa na hati ya kumiliki ardhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kusesitiza kwamba, wakati wa ugawaji wa ardhi hii Halmashauri husika zizingatie mahitaji halisi ya wanakijiji na kutoa kipaumbele kwa kaya zilizo ndani ya kijiji ambazo hazina ardhi kabisa. Hati za umilikaji ardhi zitolewe mara tu mwanakijiji anapomilikishwa ardhi. Aidha, nawaasa wananchi wa maeneo husika ya Arumeru na Arusha DC kuwa watulivu na wenye subira ili zoezi hili likamilike kwa amani na mafanikio makubwa kwa sababu timu yangu iko huko inashirikiana na Viongozi wa Mkoa na Wilaya ili kuwatambua watu ambao hawana ardhi.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana Viongozi wa Mkoa wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa na Viongozi wa Halmashauri ya Arusha na Arumeru pamoja na Jiji la Arusha. Pia, nawashukuru sana Mheshimiwa Joshua Nassari, Mbunge wa Arumeru ambaye amesaidia sana katika kuwatuliza watu wake ili wasubiri utaratibu huu.

Vile vile namshukuru Mheshimiwa Ole-Medeye kwa ushirikiano wake, tumekuwa tunazungumza naye kila mara ili kuhakikisha watu wake wananufaika na watanufaika sana kwa sababu wao ndiyo watapata ardhi kubwa zaidi katika mashamba yote yaliyofutwa na Serikali, shamba 304 na 305. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imefanikiwa kumaliza mgogoro kati ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Vijiji vya Ayamango, Gedamar na Gijedabung, Wilayani Babati ambapo Mheshimiwa Rais amefuta Shamba la Ufyomi Galapo Estate. Kazi inayoendelea sasa ni kuhakiki, kupima na kumilikisha ardhi hiyo iliyofutwa na Rais ili wananchi wapatiwe ardhi katika shamba hilo. Aidha, Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili inaendelea na kazi ya uhakiki ya ufufuaji wa mipaka ya Hifadhi ya Tarangire na kuweka alama zenye kuonekana ili kuzuia kujitokeza migogoro mingine na kuondoa uwezekano wa mipaka ya hifadhi kukua na kujiongezea eneo katika ardhi za wanakijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgogoro wa Shamba la Malonje Mkoa wa Rukwa. Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga wameanza kuchukua hatua za kisheria kwa kutoa ilani ya siku 90 kwa mmiliki. Taratibu za sheria zinaendelea na zitafuatwa mara baada ya siku hizo kufikia tamati, kiambatanisho namba moja kinaonesha chimbuko la mgogoro wa ardhi nchini, aina ya migogoro na hatua zinazoendelea kujitokeza. Nawaomba wananchi wa Malonje na vijiji vinavyozunguka Malonje wawe watulivu, Halmashauri yao inashughulikia na baada ya kukamilisha hatua zao wataleta Wizarani na tutakamilisha kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba, Mheshimiwa Rais ameridhia ufutwaji wa shamba namba 86 kama nilivyoahidi Bunge lililopita na shamba la Utumani lililopo Halmashauri ya Mafia, lenye ekari 4,040, hivyo, shamba hilo la Mafia sasa limefutwa. Wizara kwa sasa inakamilisha taratibu zinazofuata kwa mujibu wa sheria. Hatua hii imefikiwa wakati nimeshachapa kitabu hiki cha hotuba. Kwa hiyo, maneno haya hamtayaona kitabuni, naomba marekebisho yafanyike katika ukurasa wa 22 *paragraph* ya 26 na ukurasa wa 30 *paragraph* ya 35 ya kitabu cha hotuba kuingiza taarifa hii ya kufutwa kwa shamba la Mafia.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba kero na malalamiko ya wananchi yasiposikilizwa na kupatiwa ufumbuzi husababisha migogoro. Wananchi huichukua Serikali yao na kutoitii sheria hivyo amani ya nchi kuwa hatarini kutoweka. Kwa kutambua hili, Wizara imedhamiria kuwa na utaratibu maalum wa kutembelea kila Halmashauri nchini ili kujadili kero na malalamiko mbalimbali ya wananchi na kuzipatia ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza azma hii, nimetembelea Halmashauri za Arusha, Meru, Jiji la Mwanza, Nyamagana, Ilemela Mjini Kahama, Manispaa ya Tabora, Manispaa ya Sumbawanga, Morogoro na Babati na kuzungumza na Viongozi wa Mikoa husika kuhusu migogoro ya ardhi, kero na malalamiko yanayohusu ardhi, kukusanya kero za wananchi na kuunda kikosi cha kushughulikia kero za malalamiko hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Mwanza nilipokea jumla ya malalamiko 280 ambayo 81 yametoka Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na 199 yalitoka Jiji Nyamagana. Malalamiko haya yaliwasilishwa kwa maandishi na Wenyeviti wa Mitaa kwa niaba ya wananchi na wananchi wenyewe mmoja mmoja pia walihudhuria. Kwa hiyo, jumla ya wananchi ambao wameleta malalamiko Mwanza walikuwa 395 na wengine walitoka Wilaya za jirani.

Mheshimiwa Spika, katika Manispaa ya Sumbawanga nilipokea malalamiko 91 likiwepo lalamiko kuu la vijiji vinavyoizunguka Malonje. Kahama nimepokea malalamiko 86, Babati nilipokea malalamiko 105, Jiji la Arusha, Halmashauri ya Arusha na Meru nilipokea malalamiko 102, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora nilipokea 215, Morogoro malalamiko 102 na Dar es Salaam nimeanzisha madawati maalum ya malalamiko yaliyofunguliwa Temeke, Ilala na Kinondoni na bado wanaendelea.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana katika wote hawa, mtu ambaye amefanya vizuri sana ni Mkurugenzi wa Babati, malalamiko yote, watu wote waliokuwa wanadai fidia ameshawapa *cheque* na wote waliokuwa wanadai viwanja wameshapewa viwanja na baadhi ya Kanda wanaendelea na kazi. Kwa hiyo, nawasihi Wakurugenzi wote na timu zangu wakamilishe kazi hii ili watu ambao wanadai fidia wapewe fidia yao kwa maandishi na barua iliyosainiwa na Mkurugenzi, lakini na fedha na viwanja vyao wapewe na watu ambao watathibitika kweli wana uhalali wa kupata fidia wapewe. Wilaya ya Babati imekamilisha na imefanya vizuri, nadhani na wengine wote wataiga mfano huo na watafanya vizuri ingawa wako kwenye hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonesha kuwa malalamiko mengi yanatokana na fidia kutolipwa au kuwa pungufu, kuchelewesha au ukadiriaji usiofuata utaratibu, uelewa mdogo wa kanuni, taratibu na sheria kwa watendaji na wananchi na uadilifu na utendaji usioridhisha kwa watumishi wa Sekta ya Ardhi. Napenda kutoa taarifa kwamba malalamiko haya yanashughulikiwa na zoezi hili ni endelevu, wananchi wawe watulivu, wananiletea meseji sana maana niliwapa kadi zangu, wawe watulivu kwani kazi hii inaendelea kuchambuliwa, kwa sababu uchambuzi unaendelea na wale wataalam wanawafikia mpaka kwenye *site* zao kupata ufafanuzi na majibu yatatolewa.

Mheshimiwa Spika, kila mwananchi aliyewasilisha malalamiko atajibiwa kwa maandishi na Mkurugenzi wa Halmashauri husika na nakala ya majibu italetwa kwangu kwa wakati na baadaye nitafanya tathmini juu ya majibu ya maeneo yote niliyotembelea na nitatembelea katika Mikoa mingine ya Mtwara, Mbeya, Kigoma na maeneo mengine ambayo nimesikia kuna malalamiko mengi.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa watendaji wasio waaminifu na wasio na maadili wanaosababisha kero na maumivu makubwa kwa wananchi. Kwa matapeli wa viwanja na wavamizi wa viwanja vya wanyonge hawatakuwa salama. Hatua kali zitachukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kuwavunja majengo yao kazi ambayo tayari tumeshaanza, wale ambao wamejenga kwenye viwanja vya maskini tunavunja majengo yao na tumeanza kuchukua hatua nyingine za kisheria kwa kushirikiana na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuanzisha dawati maalum la kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi yanayohusu masuala ya ardhi na kuwasilisha taarifa za utatuzi wa migogoro katika ofisi za Kanda kwa uchambuzi. Taarifa hizo ziwe zinawasilishwa Wizarani kila baada ya miezi mitatu kwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kufanyia kazi malalamiko ya wananchi wa Chasimba na Makongo Dar es Salaam ambayo yamekuwa sugu kwa muda mrefu. Lengo la Wizara ni kumaliza kabisa malalamiko hayo kwa kuweka mpango shirikishi utakaoridhiwa na wao wenyewe na Wizara. Natarajia kupata ufumbuzi wa kudumu katika kikao cha pamoja na wananchi kitakachofanyika Jumamosi kwa wananchi wa Chasimba na Jumapili kama walivyoomba wananchi wa Makongo. Hatoki mtu pale, tutamaliza kwa ushirikiano kama tulivyoanza na lazima tutamaliza migogoro yote miwili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie wananchi kwamba kazi ya utatuzi wa migogoro, malalamiko na kero ni endelevu na nitaendelea kupambana na matapeli na wahalifu wote wanaodhulumu ardhi za wanyonge walio nje na ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria; katika mwaka 2014/2015, Wizara ilikuwa na lengo la kusajili hati za kumiliki ardhi na nyaraka za kisheria zipatazo 87,000. Kati ya hizo hati za kumiliki ardhi ni 42,000 na nyaraka za kisheria ni 45,000. Hadi Aprili 2015, hati miliki na nyaraka za kisheria 69,063 zilisajiliwa sawa na 79.4% ya lengo lililokusudiwa. Kati ya hizo, hati 23,554, hati za sehemu ya jengo, eneo na *unit tittle* ni 1,005 na nyaraka 33,055 zilisajiliwa chini ya sheria ya usajili wa ardhi, Sura ya 334.

Aidha, nyaraka 9,937 zilishasajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura hiyo, pia rehani na mali zisizohamishika zipatazo 2,506 zilisajiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara inakusudia kusajili hati miliki na nyaraka za kisheria 88,000. Kati ya hizo hati miliki za ardhi ni 38,000 na hati za kumiliki sehemu ya jengo ni 2,000 na nyaraka za kisheria 48,000.

Mheshimiwa Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; Wizara yangu imeendelea kujenga, kuimarisha na kusimamia mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za ardhi. Mifumo hiyo ni; Mfumo wa kusimamia utawala wa kumbukumbu ya ardhi na mfumo wa kutunza kumbukumbu ya kukadiria kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliahidi ujenzi wa mfumo unganishi kuhifadhi kumbukumbu ya ardhi yaani *Integrated Land Management Information System* ambayo ni mfumo mpana zaidi ikilinganishwa na mifumo iliyopo. Kwenye kitabu changu wamejaribu kutoa picha ya kuangalia namna mfumo utakavyofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kazi ya ujenzi wa mfumo huo imeanza mwezi Mei na imekadiriwa kukamilika mwaka 2019/2020 kwa kufika kwenye Halmashauri.

Katika awamu hii ya mwanzo ambayo tumeanza, Serikali itakamilisha ujenzi wa mfumo ambao utafungwa katika Makao Makuu ya Wizara na Ofisi za Kanda nane, tutajenga na ofisi za Kanda nane na kuweka huo mfumo pamoja na Wizara. Awamu hiyo ya kwanza inatarajiwa kukamilishwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili itahusisha kufunga mfumo katika Ofisi ya Ardhi katika Halmashauri zote nchini. Baada ya mfumo huu kufungwa huduma za upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi zitakuwa zinatolewa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na hati zitakazotolewa zitakuwa na *Bar Code* ambayo itarahisisha uhakiki wa hati kwa kutumia *Bar Code Reader* ambayo inapatikana katika kila simu ya mkononi.

Mheshimiwa Spika, chini ya mfumo huu waombaji wa huduma hizo watakuwa na fursa ya kutuma maombi na kupata majibu kwa njia ya kielektroniki kupitia simu zao. Aidha, hatua hizo zitasaidia kurahisisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi, kurahisisha utoaji wa hati miliki, udhibiti wa makusanyo ya kodi ya ardhi, kudhibiti ugawaji wa miliki juu ya milki, kuzuia wizi, udanganyifu na ulaghai. Nashukuru kwamba Kamati inayoongozwa na Mheshimiwa Lembeli waliona mfano wa mambo haya katika nchi ya Uganda na Ethiopia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliahidi kusimamia kusimika mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu na kukadiria kodi ya ardhi katika Ofisi za Ardhi 30. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hadi kufikia 2015 mfumo huu umeunganishwa katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri 70 na kuzidi lengo zaidi ya mara mbili, hivyo kuwa na jumla ya ofisi 145 zilizounganishwa pamoja na CDA na hizo zilizobaki 23 zitaunganishwa kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa watendaji Sekta ya Ardhi katika Halmashauri zote kuingiza taarifa muhimu na sahihi na kikamilifu ili kuboresha utendaji wa kazi na hivyo kuongeza ukusanyaji wa kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeboresha mfumo wa kutunza kumbukumbu ya ardhi kuwa na uwezo wa kuhifadhi taarifa ya miamala inayofanyika katika Ofisi ya Ardhi ya Kanda na Msajili wa Ardhi. Kazi ya kufunga mfumo huu katika ofisi za Kanda inaendelea na itakamilika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Utunzaji wa Kumbukumbu nyingine za Sekta ya Ardhi; ili kuwawezesha wadau mbalimbali wa Sekta ya Ardhi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kupata taarifa mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ardhi, Wizara yangu imeziweka taarifa hizo katika mfumo wa kielektroniki, taarifa hizo zinapatikana kwenye *Mobile Application* inayoitwa *Ardhi TZA* ingawa sasa hivi watu wa *App Store Administrators* hawajatuunganisha, lakini eneo la nje kwa watu wenye *IPads* zao wanaweza kuunganishwa moja kwa moja, lakini baada ya muda mfupi kila mtu popote pale duniani anaweza kuona taarifa za kila siku za Wizara kwenye simu yake. Kwa sasa inapatikana kwenye *App Store* kwa anuani hiyo ya *Ardhi TZA*. Hatua hii itasaidia kupatikana kwa taarifa hizo kwa urahisi na mahali popote mhitaji atakapokuwepo ili mradi awe na *smart phone*.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa taarifa zilizowekwa katika mfumo huo ni pamoja na sera, sheria, kanuni, miongozo na machapisho mbalimbali yanayohusiana na Sekta ya Ardhi. Pia, Wizara imetayarisha mfumo unaowawezesha wananchi kupata taarifa za umiliki wa viwanja na mashamba yao kwa kutuma ujumbe mfupi kwa kutumia simu ya mkononi kwa kuandika neno *MoL* kwenda namba 15404. Azma hii inalenga kuwapa elimu ya kutosha wananchi kwa njia ya utandao.

Mheshimiwa Spika, uthamini wa mali; hadi mwaka 2015 Aprili, Wizara iliidhinisha taarifa 10,507 ya uthamini wa mali. Huduma hii ya uthamini iliyotolewa sawia na utozaji wa ada ya uthamini ambapo Sh. 637,114,010/= zilikusanywa. Aidha, katika mwaka wa fedha ujao Wizara imepanga kuandaa na kuidhinisha taarifa 12,000.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu, Wizara ilipanga kufanya na kuidhinisha taarifa za uthamini wa fidia kwa mali kwa wananchi 30,000 ambao mali zao zitaguswa na miradi ya maendeleo ya umma. Hadi Aprili mwaka 2015, Wizara iliidhinisha taarifa 138 za uthamini kwa ajili ya ulipaji wa fidia stahiki kwa wamiliki wa asili 23,107 wa ardhi. Mali zilizofanyiwa uthamini zilikuwa na thamani ya Shilingi bilioni 150.6.

Miradi ya uwekezaji iliyohusika ilikuwa ni ya migodi, miundombinu, kilimo, ujenzi wa barabara, upanuzi wa barabara, bandari, huduma za jamii, utekelezaji wa mipangomiji, upimaji wa viwanja kwa matumizi mbalimbali na katika mwaka ujao Wizara itafanya tathmini kwa mali na ulipaji fidia kwa wananchi 35,000.

Mheshimiwa Spika, Viwango vya Thamani; Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, inaelekeza kwamba hakuna mali ya mwananchi itakayochukuliwa bila fidia kulipwa. Kifungu cha 11(i) cha Sheria ya Utwaaji inaelekeza kuwa, pale ardhi inapotwaliwa mnufaikaji na utwaaji huo anawajibika kulipa fidia kwa mmiliki wa asili anayeondolewa kwenye ardhi hiyo. Aidha, kifungu cha 3(1)(g) cha Sheria ya Ardhi, Sura namba 113 na 114 kinaelekeza kulipa fidia hiyo ni lazima iwe kamilifu, ya haki na ilipwe kwa wakati ili kuhakikisha matakwa ya sheria hiyo husika yanazingatiwa kabla ya kutwaa eneo.

Mheshimiwa Spika, nimesaini waraka namba moja wa mwaka 2015 na nimeusambaza nchi nzima kwa wahusika wote tarehe 21 Mei. Mambo muhimu katika waraka ambao unatoa mwongozo wa masuala yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya uthamini kwa ajili ya kulipa fidia. Waraka huo umesambazwa kwa Wizara, Mikoa, Wilaya, Taasisi za Umma na binafsi, Mashirika ya Umma, Wakurugezi wa Majini, Manispaa na Halmashauri za Miji na Wilaya. Kwa sasa utaratibu ufuatao utapaswa kuzingatiwa:-

- (a) Wizara, Mamlaka za Mikoa, Wilaya, Taasisi za Umma, Taasisi Binafsi, Mashirika ya Umma, Mamlaka ya Halmashauri ya Miji na Wilaya inayohusika na ulipaji wa fidia inapaswa kuwasilisha uthibitisho wa uwepo wa fedha za kulipa fidia kwa mamlaka ya Halmashauri ambapo ardhi inatwaliwa na pia uthibitisho huo uwasilishwe kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kabla ya utwaaji wa ardhi yoyote kwa wananchi;
- (b) Zoezi la fidia lazima lizingatie ushirikishwaji wa kutosha wa wadau wote muhimu wakiwemo Viongozi wa Kata, Serikali za Mitaa na Vijiji na wananchi wenye mashamba yao.

- (c) Kuanzia sasa, Mthamini Mkuu wa Serikali hataidhinisha taarifa ya uthamini isiyokuwa na kiambatanisho cha uthibitisho wa uhakika wa uwepo wa fedha iliyotengwa kwa ajili ya kulipa fidia. (*Makofi*)
- (d) Zoezi la uthamini lifanyike kwa uwazi, uadilifu na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu na taaluma ya uthamini.
- (e) Wakati wa kufanya malipo ya fidia ni lazima kuwe na mwakilishi wa Mthamini Mkuu wa Serikali, maana yake ni kwamba, ardhi haichukuliwi bila mtu kulipwa.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa Halmashauri zote nchini na taasisi mbalimbali kutenga fedha za fidia kabla ya kutwaa maeneo ya watu.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi; hadi kufikia Aprili, 2015 jumla ya mashauri 13,338 yalifunguliwa katika Mabaraza ya Ardhi na hivyo kuwa na jumla ya mashauri 33,782. Kati ya mashauri hayo mashauri 13,749 yaliyamuriwa, mashauri 18,033 yalibaki na yataendelea kushughulikiwa kwa mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara itaendelea kuboresha Mabaraza yaliyopo kwa kuyapatia watumishi na vitendea kazi muhimu na kuanzisha mapya katika Wilaya za Kahama, Kilindi na Mbulu.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Upimaji wa Ramani; napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, Wizara imejenga na kuimarisha Kanzi za Wilaya nane katika Mikoa ya Shinyanga, Mwanza ambazo ni Shinyanga, Kahama, Kishapu, Kwimba, Magu, Ilemela, Ukerewe na Nyamagana. Katika mwaka wa fedha ujao Wizara itaendelea kukamilisha Kanzi za Wilaya nane za Kaliua, Urambo, Ikungi, Mkalama, Kalambo, Kasulu, Uvinza na Mbozi pamoja na kujenga Kanzi (*Database*) katika Mikoa ya Kigoma, Tabora na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2015 vijiji 133 vilihakikiwa na kupimwa katika Wilaya za Kiteto 45 na Bagamoyo 88. Katika mwaka wa fedha ujao Wizara yangu itaendelea na upimaji wa vijiji 100.

Mheshimiwa Spika, Mipaka ya Kimataifa. Uhakiki wa mpaka kati ya Tanzania na Burundi wenye urefu wa kilomita 450 ulipangwa kufanyika katika awamu tatu. Awamu ya kwanza imefanyika Wilaya ya Ngara ambapo kilomita 135.8 zilihakikiwa na alama za mipaka 365 zilisimikwa na kupimwa. Awamu ya pili na ya tatu zitafanyika katika Wilaya ya Kibondo na Kasulu Mkoani Kigoma katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Rais wa Jamhuri ya Burundi, Mheshimiwa Pierre Nkurunziza kwa pamoja walizindua rasmi uhakiki wa uimarishaji wa mpaka huo katika Kijiji cha Mugikomelo Wilayani Ngara mnamo tarehe 28 Agosti, 2014.

Mheshimiwa Spika, kazi ya upigaji picha na kutengeneza ramani za msingi katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji inaendelea. Kati ya kilomita 671, kilomita 51 ambazo ni sehemu ya nchi kavu zimeimarishwa na kupimwa. Kilomita 620 ambazo ni sehemu ya majini Mto Ruvuma zitafanyiwa kazi mara baada ya kukamilisha uandaaji wa Kanzi yaani *Database* na ramani za msingi sehemu ya nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa mazungumzo ya usuluhishi chini ya jopo la Marais wastaafu Joachim Chisano, Mwenyekiti, Thabo Mbeki na Mheshimiwa Faustine Mugae yanaendelea. Aidha, katika mwaka ujao wa fedha Wizara itaendelea na uhakiki wa uimarishaji wa mipaka kati ya Tanzania na Kenya na Tanzania na Zambia.

Mheshimiwa Spika, upimaji wa viwanja vya mashamba, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Aprili, mwaka huu ramani zenye viwanja 83,502 na mashamba 290 vimeidhinishwa. Katika mwaka wa fedha ujao, Wizara itaidhinisha ramani, zenye viwanja 90,000 na mashamba 300.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ili kurahisisha upimaji wa ardhi mijini, jumla ya alama za msingi 80 zimesimikwa katika Miji ya Kibaha 25, Bagamoyo 30 na Mkuranga 25. Kwa mwaka wa fedha ujao Wizara itaendelea kusimika na kupima alama za msingi 165 katika Miji 35.

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa huduma za upimaji kwenye Kanda; Wizara yangu imesogeza huduma za upimaji kwenye Kanda ili kuwezesha wananchi kupatiwa huduma za upimaji katika maeneo hayo. Aidha, Wizara itaanzisha vikosi maalum vya upimaji ardhi vitakavyokuwa na vifaa vyote vinavyohitajika pamoja na vyombo vya usafiri ili kufanikisha kazi ya upimaji katika Kanda. Aidha, hatua hii ni muhimu kwa kuwa migogoro ya mipaka ya wilaya na wilaya au kijiji kwa kijiji sasa itatatuliwa kwenye Kanda na hivyo kurahisisha na kuhakikisha utatuzi wa migogoro nchini.

Mheshimiwa Spika, vile vile upimaji wa ardhi za wananchi utakuwa rahisi na hivyo kuharakisha azma ya kupima kila kipande cha ardhi nchini na kuwa na kumbukumbu sahihi zinazohusu miliki. Ntoa wito kwa Halmashauri zote nchini kutumia huduma zitakazokuwa zinatolewa na vikosi hivi kwa ushirikiano na wapima wa TAMISEMI ili kuondoa migogoro.

Mheshimiwa Spika, Mipango Miji; uaandaji wa utekelezaji wa *Master Plan*; katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Halmashuri ya Jiji la Mwanza na Arusha pamoja na Halmashauri za Manispaa ya Ilemela na Wilaya za Arusha na Meru imeanza kuandaa mipango kambambe ya Halmashauri hizo kwa kutumia Watalaam Waelekezi kwa gharama za Wizara. Kazi hii imeanza mwezi Februari na itakamilika mwezi Septemba, 2016. Aidha, kazi ya kuandaa *Master Plan* ya Mtwara inaendelea vizuri. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini ambazo hazina mipango kabambe kutenga fedha za kuandaa mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni; katika mwaka wa 2014/2015, Wizara iliahidi kuendelea na uendelezaji wa Mji mpya wa Kigamboni chini ya usimamizi wa Wakala wa Uendelezaji mpya wa Kigamboni (*Kigamboni Development Agency*) hadi Aprili, mwaka huu, Serikali imefanya mapitio na kurekebisha matangazo ya Serikali kuhusiana na Mji Mpya wa Kigamboni ambapo eneo la Mpango limepunguzwa na limebaki kama lilivyokuwa kwenye Sheria kwa kuondoa Kata tatu za hekari 44,440,000 ambazo hazikuwemo katika mpango wa awali na hivyo kubaki na Kata sita zenye eneo la ukubwa wa hekta 6,494. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imefanya mikutano ya mashauriano na wadau mbalimbali wa Mji wa Kigamboni ili kuwa na uelewa wa pamoja juu ya dhana mpya ya uendelezaji wa Mji wa Kigamboni. Kwa mujibu wa dhana hii ambayo imetafsiriwa vizuri na wananchi, wananchi wa Kigamboni wana fursa ya kushiriki uendeshaji wa kutumia mojawapo ya njia zifuatazo:-

- (a) Wananchi wenyewe kuwa ni waendelezaji katika eneo lake kwa kuzingatia mpango;
- (b) Mwananchi kuingia ubia na mwekezaji kwa kutumia ardhi yake kama mtaji; na
- (c) Mwananchi kulipwa fidia au kuuza eneo lake mwenyewe bila ya kutumia dalali au Serikali kwa mwekezaji kwa hiari yake kwa kuzingatia bei ya soko.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2015/2016, Wizara kwa kupitia KDA itaendelea na kazi zifuatazo:-

- (a) Kuandaa mipango ya kina ya maeneo yaliyopo ndani ya eneo la mpango; na
- (b) Kuainisha maeneo ya matumizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hotuba yangu hii, Wizara itaanza kwenda kupima maeneo ya barabara, yajulikane, kufanya tathimini watu waliomo kwenye maeneo ya barabara na kuwalipa na barabara hizo tutaanza kuzitengeneza hivi sasa kabla ya mwaka mpya wa fedha. Dhana hii ya sasa siyo mpya ndivyo mpango ulivyotakiwa kuwa. Katika kutekeleza kikamilifu dhana hii nimefanya marekebisho yafuatayo:-

- (a) Nimerekebisha Tangazo la Serikali namba 229 la tarehe 24 Oktoba, 2008, lililotaja maeneo ya mpango ya kuwa ni Kigamboni, Vijibweni, Mji Mwema na Kibada kwa kuongeza Kata ya Ikungi na sehemu ya Kata ya Somangila katika Mitaa miwili ya Kizani na Mbwanaji ambazo hazikuwemo kwenye Tangazo la awali.
- (b) Nimerekebisha Tangazo la Serikali namba sita (6) la mwaka 2013, lililotaja eneo la mpango kuwa ni Kata tisa kwa kupunguza Kata ambazo hazikuwemo kwenye mpango na kubakiza Kata sita zilizokuwemo kwenye mpango.
- (c) Aidha nimeridhia marekebisho ya vipengele mbalimbali vilivyomo kwenye rasimu ya mpango kabambe kama yalivyowasilishwa na wataalam wangu na wataalam wa Mwanasheria Mkuu pamoja na Kamati ya Wadau wa Kigamboni.

Kwa ufupi Kigamboni itajengwa na Wanakigamboni wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mipango ya Matumizi ya Ardhi; kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara itaendelea kutekeleza mpango wa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya na vijiji hususan katika Ukanda wa SAGCOT hususan katika Wilaya za Kilombero na Ulanga. Wilaya hizi mbili zitatumika kama Wilaya za mfano katika kupanga, kupima na kumilikisha vipande vyote vya ardhi kupitia mpango wa *Land Tenure Support Program*. Aidha, Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika Ukanda wa Reli ya Uhuru, umefanyiwa mapitio kuuhisha katika Mikoa tisa ambayo ni Pwani, Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Dodoma ya Ukanda wa SAGCOT.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha ujao Wizara itachapisha na kusambaza mpango huo wa Ukanda wa SAGCOT, kutoa elimu kwa wadau na kuanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Mipango ya matumizi ya ardhi za vijiji; hadi mwezi Aprili, jumla ya vijiji 91 vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika wilaya mbalimbali.

Aidha, Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji na uhakiki wa maeneo ya uwekezaji umefanyika katika vijiji 38 kwa ukanda wa SAGCOT katika Halmashauri za Ulanga, Kilombero, Iringa, Njombe, Makete, Ludewa, Kibaha, Busokelo, Bagamoyo na Rufiji.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi hususani baina ya wakulima na wafugaji na Hifadhi, Wizara kwa kushirikiana na wadau imewezesha upangaji, upimaji na kuanza umilikishaji wa ardhi katika vijiji 60 vya Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero na vijiji 10 vya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto kipaumbele kimekuwa ni kuanza na Vijiji kumi vya Loltepes, Emart, Enguserodian, Kimana, Namelok, Kinua, Taigo, Krash, Ndirigish na Knati vinavyopakana na Pori la Hifadhi ya Emborley Murtangos, ambavyo vilikuwa ni kitovu cha migogoro katika eneo hilo. Pia kuna Tume ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ilikwenda huko na kuweka mipaka, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ameagiza ile taarifa ipitiwe kwanza na Halmashauri zinazohusika zote na Mikoa ili ichapishwe vizuri kwa maridhiano kwamba mikoa ipitie na kama kuna marekebisho yarekebishwe ili iwe taarifa ya kudumu ya kutatua mgogoro huu wa Kiteto.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Sekta ya Nyumba; napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mazingira mazuri ya kibiashara, kisheria na kimuundo yaliyowekwa kwa ushirikiano katika ya Wizara, Benki Kuu pamoja na Tanzania *Mortgaging Refinancing Company*, yamewezesha jumla ya Benki 20 kuanza kutoa mikopo ya nyumba. Hadi Desemba 14, Benki hizo zimetoa mikopo 3,598 yenye thamani ya shilingi bilioni 248.

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: We bado dakika ngapi? Mbona mlichukua muda wangu mwingi?

SPIKA: Endelea bado tano.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Nachukua fursa hii kuuzihimiza Benki ya Biashara ambazo hazijaanza kutoa mikopo ya nyumba Loh! Mheshimiwa Spika, nilichukuliwa muda wangu mwingi sana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha, Wizara iliratibu upatikanaji wa ardhi ya ujenzi wa nyumba za watumishi kupitia *Watumishi Housing* mtaiona kwenye Hotuba, uwezeshaji wa wananchi kumiliki nyumba, iko kwenye Hotuba na imeandikwa kwa kirefu zaidi, lakini ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kumiliki nyumba zenye ubora unaokubalika kijamii Wizara iliagiza Shirika la Nyumba na Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi kubuni mikakati ya kufanya utafiti kuwezesha upatikanaji wa nyumba zenye vyumba vitatu au zaidi kwa gharama isiyozidi shilingi milioni 35 bila VAT.

Mheshimiwa Spika, mazungumzo yanafanywa ndani ya Serikali ili nyumba zinazonunuliwa chini ya shilingi milioni 35 ziondolewe VAT. Uamuzi hajaufanywa, lakini tunaendelea kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, naomba radhi sana, basi itabidi maneno mengi yaliyopo hapa ya Shirika la Nyumba na Ujenzi wa Nyumba yote yaingizwe kwenye *Hansard* pamoja na ujenzi wa majengo ya kibiashara, uendelezaji wa...

SPIKA: Kwa sababu wewe mwisho katika Wizara tunakupa dakika kumi zaidi. (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, kutokana na kodi ya pango la nyumba, Shirika lilipata shilingi bilioni 71.15 ambayo ni 118% ya lengo kipindi husika. Kwa mwaka wa fedha ujao Shirika linatarajiwa kukusanya shilingi bilioni 82.2 kutokana na kodi na pango la nyumba. Pia vyanzo mbalimbali vya mapato viliwezesha Shirika kuchangia mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 18.66.

Mheshimiwa Spika, Wizara katika mwaka wa fedha ujao inapendekeza kutungwa Sheria mpya ya Usimamizi wa Mawakala ya Milki, Wabunge wengi wamekuwa wakilalamikia hili hasa Mheshimiwa Mbowe amekuwa akilalamika sana juu ya *Real Estate Agency* ambayo itashughulika na utoaji wa ardhi, Sheria inayosimamia Uanzishwaji wa Chuo cha Ardhi Tabora pamoja na Sheria ya Udhamini na Usimamizi wa Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Huduma za Wateja, katika mwaka wa fedha huu, Wizara ilianza kutoa huduma kupitia Kituo cha Huduma (*Customer Service Center*) kilichopo katika Makao Makuu ya Wizara, lengo la Kituo hiki ni kuboresha utoaji wa huduma kwa mpangilio na kwa uwazi unaosaidia kuleta ufanisi katika utendaji wa pamoja ambao unasaidia kupunguza mianya ya rushwa hadi kufikia mwezi Aprili, Kituo hiki kilikuwa kimepokea wateja zaidi ya 15,000.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Mteja kwa Njia ya Simu; Wizara yangu itaanzisha Kituo cha Huduma kwa Mteja kwa Njia ya Simu. Kupitia Kituo hiki wananchi wataweza kuuliza na kupata majibu ya maswali mbalimbali yanayohusu ardhi kupitia simu na kutuma ujumbe mfupi.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazokabili Wizara:-

- (a) Kutopatikana kwa taarifa sahihi za ardhi;
- (b) Migogoro ya matumizi ya ardhi nchini baina ya watumiaji wa ardhi;
- (c) Upungufu wa ardhi iliyopangwa na kupimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo uwekezaji;
- (d) Makundi mbalimbali yanayochukua ardhi ya wananchi kwa matumizi mbalimbali kutolipia fidia kwa mujibu wa Sheria;
- (e) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sekta ya ardhi pamoja na sheria zake, taratibu pamoja na miongozo iliyopo, haki zao na wajibu wao;
- (f) Uhaba wa wataalam na vitendea kazi vinavyohitajika ili kukidhi mahitaji; na
- (g) Kuweco kwa watumishi wa sekta ya ardhi wanaosababisha kero na wananchi hususani baadhi katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, shukrani; mafanikio ya Wizara yangu yamekuwepo kutokana na ushirikiano kati ya Serikali, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji na wadau wa maendeleo zikiwemo Taasisi za Fedha za Kimataifa, *Habitat*, Shirika la Maendeleo la Ujerumani, Serikali ya Denmark, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Marekani, Uchina na Norway.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, napenda kumshukuru sana tena Naibu Waziri wangu kwa kunisaidia, watendaji wote wa Wizara, Vitengo na Taasisi mbalimbali, lakini narudia tena kuishukuru sana Kamati yangu pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa muda mwingi wa miaka mitano mmekuwa mnachagiza akiwemo Waziri Kivuli Mheshimiwa Mdee. Najua leo atanisema sana, lakini sijui atanisemea nini, maana kero zake nyingi ziko humu ndani.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, ni wazi kwamba miongoni mwetu wako waliotangaza nia ya kugombea nafasi kubwa na wengine Ubunge. Niwatakie kila la heri kila mmoja wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara imeazimia kuendeleza mpango wake na katika mwaka huu ujao Wizara imejipanga kutayarisha mipango ya kuendeleza miji na vijiji na kusimamia na kupanga matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya Wizara; ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu niliyoyaeleza katika Hotuba hii katika kipindi cha mwaka 2015/2016, naomba kutoa hoja ya kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kama ifuatavyo:-

- (a) Mapato ya Serikali bilioni 70.5.
- (b) Matumizi ya kawaida sh. 69,584,347,000.
- (c) Matumizi ya maendeleo sh. 13,458,996,000.

Jumla ya matumizi ya mshahara na matumizi mengine na kila kitu ni sh. 83,043,343,000.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamalizia, ningepomba kutoa rai kama ifuatavyo:-

- (1) Ole wao watendaji wa sekta ya ardhi wanaoendesha kazi zao kwa dhuluma, kiburi na kunyanya watu.
- (2) Ole wao matapeli wanaojitajirisha kwa dhuluma, kupora na kunyang'anya ardhi ya wanyonge.
- (3) Ole wao wote wanaojilimbikizia ardhi na kuvunja masharti ya umilikishwaji, hawaendelezi na hawalipii kodi mashamba yao na viwanja vyao vitanyang'anywa. *(Makofi)*
- (4) Pia ole wao Viongozi wa Vijiji na Halmashauri wanaouza ardhi kubwa nje ya uwezo wao kisheria na wanatumia njia ya rushwa na udanganyifu kumilikisha ardhi ya kijiji bila ya kuwashirikisha wananchi.
- (5) Wizara yangu itaendeleza kasi ya kufuta miliki za watu wote wanaomilikishwa kinyume cha sheria na wale wote wanaomiliki kisheria, lakini wamevunja masharti ya umilikishwaji kwa viwanja na mashamba, nao watanyang'anywa kama ambavyo mmeona katika taarifa wiki hii Mheshimiwa Rais amefuta mashamba hayo yaliyoandikwa. *(Makofi)*

(6) Wizara yangu itawachukulia hatua kali za kinidhamu na kisheria watendaji wote wa ardhi wenye tabia ya wizi, dhuluma, utapeli na wasio waaminifu.

(7) Wizara yangu wakati wote itaendelea kuwatetea wanyonge wote wanaoonea, kuporwa, kutapeliwa au kudhulumiwa ardhi kwa namna yoyote ile.

Hatua kali zitachukuliwa kwa yoyote anayewadhulumu wananchi wanyonge bila kujali nafasi yake kifedha, madaraka au uaminifu. Naamini kwa ushirikiano wenu tutashinda.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, Kamati yangu, namshukuru mke wangu, nawashukuru pia viongozi wangu walio kuja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na wewe na sasa naomba kwa heshima yako na heshima ya Bunge nitoe hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Nafikiri kuna haja ya kuwahoji kama mnaafiki tuondoke siyo?

WABUNGE FULANI: Ndiyoooo.

SPIKA: Aah! Serious? Siyo utaratibu.

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI, MHESHIMIWA WILLIAM V. LUKUVI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA
FEDHA 2015/16 KAMA ILIVYOWASILISHWA
MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Ardhi, Nyumba

na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2014/15 na malengo ya Wizarakwa mwaka wa fedha 2015/16. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/16. Pamoja na hotuba hii nimewasilisha kitabu kinachoonisha taarifa ya utekelezaji wa kazi mbalimbali za Wizara pamoja na taasisi zake ikiwa ni sehemu ya hotuba yangu. Naomba Bunge lipokee taarifa hiyo na ijumuishwe kwenye Hansard.

2. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mhe. Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kuingia katika Baraza la Mawaziri kufuatia mabadiliko aliyoyafanya mwezi Januari, 2015. Mawaziri hao ni Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uhusiano na Uratibu; Mhe. Jenister Joakim Mhagama, (Mb.), Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge; Mhe. Christopher Kajoro Chiza (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwezeshaji na Uwekezaji; Mhe. Steven Masatu Wassira (Mb.), Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika; Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb.), Waziri wa Nishati na Madini; Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe, (Mb.), Waziri wa Afrika Mashariki na Mhe. Samuel John Sitta (Mb.), Waziri wa Uchukuzi. Aidha, nawapongeza Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb.), Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mhe. Steven Julius Masele (Mb.), Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais; Mhe. Charles John Mwijage (Mb.), Naibu Waziri, Nishati na Madini na Mhe. Anne Kilango Malecela (Mb.), Naibu Waziri, Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Vilevile, nampongeza Mhe. George Masaju kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mhe. Dkt. Grace Khwaya Puja na Mhe. Innocent Rwabushaija Sebba kwa kuteuliwa kuwa Wabunge. Nawatakia wote kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

3. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua kuiongoza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Aidha, nampongeza yeye binafsi pamoja na Mhe. Dkt. Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa jitihada zao za kuiongoza, kusimamia na kuendeleza amani, utulivu na maendeleo ya nchi yetu. Nawashukuru kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa ambao unaniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa ya kuiongoza sekta hii mtambuka na muhimu katika maendeleo ya Taifa letu. Nawapongeza kwa dhati Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na Mhe. Balozi Seif Ali Idd, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya

Mapinduzi Zanzibar na Mbunge wa Kitope, kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

4. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia kuwashukuru Mhe. Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka (Mb.), aliyeongoza Wizara kabla yangu; Mhe. Goodluck Ole Medeye (Mb.) na Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb.) waliokuwa Manaibu Waziri kwa kuweka misingi imara ya kusimamia sekta ya ardhi.

5. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa hotuba yake iliyoeleza malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/16. Naahidi kwamba Wizara yangu itayafanyia kazi yale yote yanayoihusu sekta ya ardhi.

6. **Mheshimiwa Spika**, nakupongeza wewe kwa kuongoza shughuli za Bunge wa ufanisi. Pia, nampongeza Mhe. Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa na Naibu Spika wa Bunge letu kwa utendaji mzuri katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiongoza shughuli za Bunge. Ni ukweli usiofichika kwamba wamemudu vema jukumu hili la kuongoza Bunge lako Tukufu kwa ufanisi mkubwa. Mwenyezi Mungu aendelee kuwaongoza na kuwapa nguvu, afya na hekima za kumudu zaidi majukumu yao.

7. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira inayoongozwa na Mwenyekiti Mhe. James Daudi Lembeli (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Abdulkarim Hassan Shah (Mb.) kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao unaiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ushauri wao utaendelea kuzingatiwa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Vilevile, natoa shukrani za pekee kwa Naibu Waziri, Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb.), kwa ushirikiano na msaada mkubwa anaonipatia wakati wa kutekeleza majukumu ya sekta ya ardhi. Pia, ninawashukuru Katibu Mkuu Bw. Alphayo Japani Kidata; Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Selassie David Mayunga; Wakuu wa Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu pamoja na watumishi wote wa sekta ya ardhi katika ngazi zote kwa kutekeleza majukumu yao.

8. **Mheshimiwa Spika**, nilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mhe. Kapteni John Damiano Komba aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu, ndugu na wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi pamoja na wale wote walioguswa na msiba huo.

Kadhalika, wapo wananchi waliofariki katika maafa na ajali mbalimbali nchini na wengine kujeruhiwa. Nachukua fursa hii kutoa pole kwa wafiwa wote Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina. Aidha, nawatakia afya njema waliojeruhiwa.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2014/15 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2015/16

9. **Mheshimiwa Spika**, naomba nieleze kwa kifupi utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/15 na malengo kwa mwaka wa fedha 2015/16. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa taarifa za utekelezaji zinaishia mwezi Aprili, 2015.

Ukusanyaji wa Mapato

10. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara ilipanga kukusanya **shilingi bilioni 61.32** kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato yanayotokana na kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi Aprili, 2015, Wizara imekusanya **shilingi bilioni 47.0** sawa na **asilimia 76.6** ya lengo na ikiwa ni ongezeko la **shilingi bilioni 3.8** ikilinganishwa na **shilingi bilioni 43.2** zilizokusanywa mwaka 2013/14. Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara iliendelea kuhimiza wamiliki wa ardhi kulipa kodi ya ardhi, ada na tozo mbalimbali kupitia benki. Hatua hii inalenga kuongeza ukusanyaji wa maduhuli na kudhibiti uvujaji wa mapato.

11. **Mheshimiwa Spika** katika mwaka wa fedha, 2014/15 Wizara iliahidi kuhuisha viwango vya kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi ambavyo vilionekana kuwa kikwazo kwa wananchi wanaohitaji huduma za ardhi. Uhuishaji huu wa viwango vya kodi, tozo na ada za ardhi umelenga kupata viwango vinavyopangika, kukubalika na kulipika. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi hiyo imekamilika.

12. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kuhuisha viwango hivyo, wananchi wa kipato cha chini watamudu kulipa kodi, tozo na ada hizo. Kodi ya pango la ardhi imepungua kwa wastani wa asilimia **30** na viwango vingine vinavyomgusa mwananchi wa kawaida vimepungua kwa **asilimia 50** au zaidi. Kwa mfano, kodi ya kupima mashamba imepunguzwa kwa **asilimia 60** kutoka **shilingi 1,000** hadi **shilingi 400** na mashamba ya biashara imepunguzwa kwa **asilimia 50** kutoka **shilingi 10,000** hadi **shilingi 5,000** kwa ekari; ada ya upimaji ardhi imepunguzwa kwa **asilimia 62.5** kutoka **shilingi 800,000** hadi **shilingi 300,000** kwa hekta; nyaraka za tahadhari na vizuizi (*Caveat*) vimepunguzwa kwa **asilimia 66.7** kutoka **shilingi 120,000** hadi **shilingi 40,000**, nyaraka za ubadilishaji wa majina (*Deed Poll*) zimepungua kwa **asilimia 62.5** kutoka **shilingi 80,000** hadi **shilingi 30,000**, usajili wa nyaraka nyinginezo zimepunguzwa kwa **asilimia 50**

kutoka **shilingi 80,000** hadi **shilingi 40,000**. Vilevile gharama za kupata nakala ya hukumu kwenye Mabaraza ya Ardhi zimepunguzwa kwa **asilimia 62.5** kutoka **shilingi 16,000** hadi **shilingi 6,000**, ada ya maombi ya kumiliki ardhi imepunguzwa kwa **asilimia 75** kutoka **shilingi 80,000** hadi **shilingi 20,000**, na ada za maandalizi ya hati imepunguzwa kwa **asilimia 68.8** kutoka **shilingi 160,000** hadi **shilingi 50,000**. Viwango hivi vitaanza kutumika tarehe **1 Julai, 2015** na vipo katika kitabu cha kodi, ada na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi ambacho kimesambazwa pamoja na hotuba hii.

13. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa viwango vya tozo ya mbele (premium), kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 tozo hii itapunguzwa kwa **asilimia 50** kutoka **asilimia 15** ya sasa hadi **asilimia 7.5** ya thamani ya ardhi na kiwango hiki ndicho kitakacholipwa kwa mashamba na viwanja wakati wa kumilikishwa. Kama ilivyo kwa marejesho ya ada, kodi na tozo nyingine za sekta ya ardhi, **asilimia 30** ya maduhuli yote yatakasanywa kutokana na tozo hii yatarudishwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na matumizi yake yataelekezwa katika kuboresha sekta ya ardhi. **Kwa kuwa viwango vya kodi za ardhi sasa ni rafiki, natoa rai kwa wamiliki wote wa ardhi kulipa kodi kwa hiari na kwa wakati.**

14. **Mheshimiwa Spika**, baada ya marekebisho ya viwango vya kodi kufanyika, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara inatarajia kukusanya **shilingi bilioni 70**. Lengo hili litafikiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- a) Kutumia njia ya kielektroniki kukusanya kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali;
- b) Wamiliki wa mashamba na viwanja kulipa kodi ya ardhi kupitia Benki;
- c) Kushirikiana na Wizara ya Fedha kurejesha asilimia 30 ya makusanyo kwa wakati kwenye Halmashauri kwa lengo la kuchochea ukusanyaji wa kodi ya ardhi;
- d) Kuhamasisha wamiliki wa ardhi kwa njia ya matangazo kwenye magazeti, redio, luninga na vipeperushi kulipa kodi kwa wakati; na
- e) Kufuta milki za wamiliki wanaokiuka masharti ya umiliki ikiwemo kutokulipa kodi ya ardhi kwa wakati.

15. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara yangu itaboresha ukusanyaji wa kodi, ada na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi kwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa ulipaji utakaotumia simu za viganjani. Mfumo huu unatarajiwa kuanza kutumika tarehe 1 Julai, 2015 na utarahisisha ulipaji wa maduhuli, kupungaza adha ya msongamano na kupoteza muda

kwenye vituo vya malipo. Aidha, huduma ya ukadiriaji wa pango la ardhi na uboreshaji wa taarifa za wamiliki wa viwanja na mashamba itapatikana kupitia simu ya kiganjani. **Natoa wito kwa wananchi nchini kuupokea na kuutumia mfumo huo wa kulipa maduhuli yatokanayo na sekta ya ardhi kwa njia ya kielektroniki.**

Matumizi

16. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 85.74** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 11.54** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara; **shilingi bilioni 40.05** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi bilioni 34.15** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za miradi ya maendeleo, **shilingi bilioni 13.3** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 20.85** ni fedha za nje. Hadi Aprili 2015, jumla ya **shilingi bilioni 32.2** zilipokelewa, sawa na asilimia **37.6** ya fedha zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2014/15. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 10.38** ni mishahara na **shilingi bilioni 21.82** ni matumizi mengineyo (OC). Aidha, hadi Aprili, 2015 Wizara haikupokea fedha za kutekeleza miradi (**Jedwali Na. 1**).

UTAWALA WA ARDHI

17. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania imejaliwa kuwa na ardhi kubwa na ya kutosha kwa kila mwananchi kuweza kumiliki kipande cha ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa ukubwa wa nchi unaokadiriwa kuwa kilomita za mraba **947,000**, kila Mtanzania anaweza kumiliki takribani ekari **tatu**. Ni jambo la kujivunia kuwa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 zinatoa haki sawa kwa raia wote kumiliki ardhi sehemu yoyote ya nchi bila kujali jinsia wala sehemu mwananchi alikozaliwa. Changamoto iliyopo ni kuhakikisha kuwa ardhi yote inapangwa, kupimwa na kumilikishwa kisheria. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali itaongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa wananchi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii na hivyo, kuongeza fursa za ajira, kupunguza umaskini na pia kukuza Pato la Taifa.

18. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inasimamia masuala ya ardhi nchini yanayohusisha mamlaka za Halmashauri za Vijiji, Halmashauri za Wilaya na Miji. Majukumu na mamlaka za usimamizi yameainishwa vema katika Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999. Lengo ni kuhakikisha kuwa wananchi wanashirikishwa ipasavyo katika suala zima la usimamizi wa rasilimali ardhi kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Taifa.

19. **Mheshimiwa Spika**, dhamira ya Serikali ni kuifanya ardhi kuwa kichocheo cha maendeleo na nyenzo muhimu katika kupambana na umaskini. Hivyo ni wajibu wetu kusogeza huduma za ardhi kwa wananchi na kutoa elimu kwa umma kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili wananchi waweze kuitumia ardhi ipasavyo kama mtaji hai kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

20. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kuigawa Kanda ya Mashariki kuwa kanda mbili, Kanda ya Dar es Salaam na Kanda ya Mashariki. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kanda ya Dar es Salaam imeanzishwa na inahudumia Manispaa za Temeke, Ilala na Kinondoni na Kanda ya Mashariki inahudumia mikoa ya Pwani na Morogoro. Hadi sasa Wizara ina Ofisi za Kanda nane ambazo ni Dar es Salaam, Mashariki, Kati, Ziwa, Kaskazini, Kusini, Nyanda za Juu Kusini na Magharibi.

21. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara yangu imeandaa rasimu ya mwongozo wa utaratibu wa kupanga, kuhakiki, kupima, kumilikisha na kusajili kila kipande cha ardhi. Hatua hii inalenga kuwaongezea watendaji wa sekta ya ardhi na wananchi kwa ujumla, uelewa wa pamoja kuhusu masuala ya ardhi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Aidha, Wizara imeandaa kitabu kwa lugha rahisi kinachoelezea hatua mbalimbali zinazopaswa kufuatwa na wananchi ili kupata huduma mbalimbali zinazotolewa na sekta ya ardhi.

22. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inalo jukumu la kuteua wajumbe wa Kamati za Ugawaji Ardhi kulingana na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 (Fungu 12) katika ngazi ya Taifa, Miji na Wilaya baada ya kupendekezwa na Halmashauri husika. Hadi sasa Halmashauri **119** kati ya Halmashauri **168** zina Kamati za Ugawaji Ardhi. Kamati hizi ni muhimu katika kushughulikia ugawaji ardhi nchini. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara imefanya uteuzi wa Wajumbe wa Kamati za Ugawaji Ardhi kwa Halmashauri za Wilaya zifuatazo: Mkuranga, Kibaha, Mlele, Uvinza, Musoma, Nzega, Ikungi, Mufindi, Kaliua, Busega, Kakonko, Biharamulo, Sikonge, Nsimbo na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani.

23. **Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi pamoja na majukumu mengine, inalo jukumu la kupitia maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Kamati hii ilipitia maombi 148 na kutoa ushauri wa kumilikisha viwanja 100 na mashamba 9 kwa ajili ya uwekezaji nchini. **Natoa rai kwa Halmashauri zote ziwe na Kamati za Kugawa Ardhi ili kuongeza uwazi katika kugawa ardhi.**

Hazina ya Ardhi (Land Bank)

24. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara imejiwekea lengo la kutambua maeneo ya ardhi yenye ukubwa wa ekari takriban **200,000** nchini na kuwa sehemu ya Hazina ya Ardhi kwa ajili ya uwekezaji na matumizi ya umma. Kwa kuzingatia mahitaji ya fidia kwa ajili ya utwaaji wa maeneo hayo, Serikali imetenga **shilingi bilioni 5** katika Mfuko wa Fidia ya Ardhi (*Land Compensation Fund*) kwa ajili ya kulipa fidia ya maeneo yatakayotwaliwa. Aidha, hadi Aprili 2015, Serikali imebatilisha milki za mashamba mawili (Ufyome katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati katika mkoa wa Manyara na Fort Ikoma mkoani Mara) na viwanja **67** nchini kote. Vilevile, uhakiki na ukaguzi wa mashamba pori yaliyotelekezwa na wamiliki utaendelea kufanyika ili kuitwaa au kubatilisha na kuihifadhi kwenye Hazina ya Ardhi.

Utekelezaji wa Sheria za Ardhi

25. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inashughulikia utoaji wa Hati, Vyeti vya Ardhi ya Vijiji na Hati za Hakimiliki ya Kimila. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kutayarisha na kutoa Hati Miliki **40,000**. Hadi kufikia Aprili 2015, Wizara iliandaa na kusaini Hati Miliki **20,189** sawa na **asilimia 50.5** ya lengo (**Jedwali Na. 2**). Kanda iliyoongoza kuandaa hati nyingi zaidi ni Dar es Salaam (**hati 4,491**) ikifuatiwa na Kanda ya Kusini Magharibi (**hati 3,516**). Kanda iliyoandaa hati chache zaidi ni Kati (**hati 680**). Aidha, Halmashauri iliyoongoza kuandaa hati nyingi zaidi ni Temeke (**hati 1,959**). Hata hivyo, Halmashauri ambazo hazikuandaa hati au kuwamilikisha wananchi ardhi ni Iramba, Singida (W), Mkalama, Masasi (W), Lindi (W), Nyang'wale, Butiama, Mpanda (W), Nsimbo, Mlele, Kaliua, Ushetu, Msalala, Buhigwe, Kigoma(W), Kibondo, Kilindi, Momba na Busokelo. Katika mwaka wa fedha 2015/16 lengo la Wizara ni kuandaa na kutoa Hati Miliki **40,000**. **Napenda kurudia wito wangu kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinamilikisha viwanja vyote vilivyopimwa na kuandaa Hati ili wananchi waweze kuwa na milki salama za ardhi na kila mwaka ziwe zinaweka malengo makubwa ya upimaji na umilikishaji wa viwanja na mashamba nchini. Aidha, wananchi na viongozi wa Serikali za Mitaa wanahimizwa kuheshimu na kulinda miliki zilizotolewa kisheria na maeneo yaliyotengwa kwa matumizi ya umma. Hatua za kisheria zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya wavamizi wa maeneo ambayo yamemilikishwa kisheria.**

26. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara iliahidi kushughulikia maombi ya kibali cha uhamisho wa milki **3,500**. Hadi kufikia Aprili 2015, maombi **4,540** yameshughulikiwa. Vilevile, Wizara itaendelea na jukumu lake la msingi la kusimamia masharti ya umiliki wa ardhi kwa kuhakikisha kuwa miliki zinaendelezwa ipasavyo. Ili kuhakikisha masharti ya uendelezaji ardhi yanazingatiwa, Wizara ilitoa ilani **3,823 (Jedwali Na. 2)** za ubatilisho kwa wamiliki waliokiuka masharti wakiwemo wamiliki wa mashamba yasiyoendelezwa katika mikoa ya Morogoro, Pwani na Rukwa.

Katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itaendelea kushughulikia ubatilisho wa milki zote zinazokuwa masharti ya uendelezaji wa viwanja na mashamba. **Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatuma Ilani za ubatilisho wa milki kabla ya kuwasilisha mapendekezo hayo Wizarani.**

Usimamizi wa Ardhi ya Vijiji

27. **Mheshimiwa Spika**, katika kuratibu usimamizi wa ardhi ya vijiji, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wananchi, kuhakiki mashamba, kuratibu utoaji vyeti vya ardhi ya kijiji na hati za hakimiliki ya kimila. Utoaji wa vyeti vya ardhi ya kijiji unaziwezesha Halmashauri za vijiji kutambua mipaka ya kijiji na kusimamia matumizi ya ardhi yao na hivyo kuepuka migogoro ya matumizi ya ardhi.

28. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2015 Wizara imetoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **988**. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Ofisi ya Rais kupitia Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na wadau mbalimbali imeratibu na kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila **25,897 (Jedwali Na. 2)** ikilinganishwa na lengo la kutoa Hatimilki za Kimila **70,000**. Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya nchini pamoja na wadau mbalimbali kuhakikisha kwamba zoezi la utoaji wa Hati za Hakimiliki ya Kimila linakuwa endelevu na linafanyika kwa kasi zaidi. Hatua hii inalenga kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutumia hati hizo kama dhamana kupata mikopo kwenye taasisi za fedha na pia kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi ambayo inaendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini.

29. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru taasisi za fedha ambazo zimetambua na kukubali kupokea hati milki za kimila kama dhamana ya kupata mikopo. Taasisi hizo ni pamoja na NMB, CRDB Bank, PSPF, SIDO, Meru Community Bank na Agricultural Trust Fund Bank kwa kutoa mikopo ya jumla ya **Shilingi bilioni 49.2** katika mwaka wa fedha 2014/15. Aidha, ninahimiza benki na taasisi zingine za fedha wazitambue na kuzikubali hatimiliki za kimila kutumika kama dhamana ya kupata mikopo kwa kuwa zina nguvu sawa ya kisheria kama ilivyo kwa hati miliki za kawaida.

Udhibiti wa Ardhi ya Vijiji

30. **Mheshimiwa Spika**, miaka ya hivi karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la uporaji wa ardhi vijijini. Hili linafanywa na watu wachache wenye uwezo kwa kushirikiana na viongozi wa vijiji wasio waadilifu. Kwa kiasi kikubwa ardhi inayoporwa inaachwa bila kuendelezwa na nyingine huhawilishwa, kupimwa na kuombewa hatimiliki za kawaida. Hali hii ikiachwa kuna hatari ya wananchi wa vijijini kugeuka wapangaji wa ardhi za vijiji vyao.

Ili kuhakikisha kuwa miamala ya ardhi vijijini inafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za uhawilishaji wa ardhi ya vijiji utafanyiwa tathmini kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 ili kujua ukubwa wa tatizo na kuzuia mianya ya ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu na ikibidi kuweka ukomo wa kiasi cha ardhi (*land ceiling*) ambacho mtu mmoja anaweza kumiliki kijijini. Azma hii inalenga kuyalinda makundi mbalimbali ya jamii wakiwemo wakulima na wafugaji kumiliki ardhi.

31. **Mheshimiwa Spika**, ili kusimamia kwa ufanisi ardhi ya vijiji iweze kuwanufaisha wananchi wote, napenda kutoa agizo kwa watendaji wa vijiji wote nchini kuandaa orodha ya walionunua ardhi katika vijiji vyao wakionesha majina na kiasi cha ardhi kilichonunuliwa. Taarifa hizi ziwasilishwe kwa Afisa Ardhi Mteule katika Halmashauri husika kwa uhakiki. **Vilevile natoa rai kwa wananchi wote waishio vijijini kufuatilia kwa karibu uuzaji wa ardhi kiholela ili kuhakikisha kuwa unafanywa kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999.**

Udhibiti wa Migogoro ya Matumizi ya Ardhi

32. **Mheshimiwa Spika**, karibu kila nchi duniani inakabiliwa na aina fulani ya migogoro ya matumizi ya ardhi. Nchini Tanzania kuna aina kuu tatu za migogoro ambayo ni kati ya wakulima na wafugaji; wakulima/wafugaji na hifadhi; na wanavijiji na wawekezaji. Wizara imedhamiria kudhibiti migogoro hiyo ambayo inasababisha uvunjifu wa amani na vifo katika baadhi ya maeneo yenye migogoro kwa kutekeleza Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria za Ardhi uliohuishwa mwaka 2013 (Strategic Plan for Implimentation of Land Laws - SPILL 2013), Mpango wa Matumizi ya Ardhi (2013- 2033) na Mpango Mkakati wa Wizara wa miaka mitano (2012/13 - 2016/17). Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ili kupunguza migogoro ya ardhi katika Halmashauri nchini ni pamoja na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **1,560**, kuandaa mipangokina ya miji na majiji na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo. Dawa pekee ya kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi nchini ni kupanga na kupima kila kipande cha ardhi na kuwamilikisha wananchi na taasisi kisheria kwa kuwapatia hatimiliki. Pamoja na jitihada za jumla, Wizara imeendelea kutafuta ufumbuzi wa mgogoro kwa mgogoro kwa kuwaita mezani pande husika na kukaa nao katika meza ya majadiliano ili kupata ufumbuzi na udhibiti wa migogoro.

33. **Mheshimiwa Spika**, hatua ya kukaa mezani na pande husika zimeanza kuleta mafanikio na kupata ufumbuzi katika mgogoro wa mashamba kati ya Mwekezaji (*Tanzania Plantation Ltd.*) na wananchi wanaozunguka mashamba yake na mgogoro kati ya mwekezaji wa shamba la *Noor Farm* lililopo Oljoro katika Wilaya ya Arumeru. Kutokana na makubaliano na wawekezaji.

Serikali imepata jumla ya ekari 7,236.5 kwa ajili ya wananchi wasio na ardhi ndani ya migogoro husika. Aidha, Wizara imeunda timu ikijumuisha wataalam kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na Meru ambayo inaendelea na kazi ya uhakiki wa wananchi wasio na ardhi katika eneo husika, uthamini, upimaji na umilikishaji wa ekari zilizopatikana. Mgawanyo huo utazingatia pia kipaumbele cha Serikali kuwa na akiba ya ardhi (*Land Bank*) kwa matumizi ya baadaye. Napenda kuisitiza kwamba, wakati wa ugawaji wa ardhi hii Halmashauri husika zizingatie mahitaji halisi ya wanakijiji na kuwapa kipaumbele kaya zilizo ndani ya kijiji ambazo hazina ardhi kabisa na kutoa hati za umilikaji ardhi mara tu mwanakijiji anapomilikishwa. Aidha, nawaasa wananchi wa maeneo husika kuwa watulivu na wenye subira ili zoezi liweze kukamilika kwa amani na mafanikio makubwa.

34. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia imefanikiwa kumaliza mgogoro kati ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na vijiji vya Ayamango, Gedamar na Gijedabung Wilayani Babati ambapo Mhe. Rais amefuta shamba la Ufyomi Galapo Estate. Kazi inayoendelea ni kuhakiki, kupima na kumilikisha ardhi ili wananchi walio katika hifadhi waweze kuhamishwa na kupatiwa ardhi katika shamba hilo. Vilevile, Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii inaendelea na uhakiki wa mipaka ya Hifadhi ya Tarangire na kuweka alama zenye kuonekana ili kuzuia kujitokeza migogoro mingine.

35. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu mgogoro wa shamba la Malonje, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga wameanza taratibu za kisheria za kufuta miliki ya shamba hilo kwa kutoa lani ya siku 90 kwa mmiliki. Taratibu za kisheria zitafuatwa mara baada ya siku hizo kufikia tamati. Kadhalika, shamba la Utumaini lililopo Halmashauri ya Mafia lipo katika hatua za mwisho za ufutaji. Kiambatisho Na.1 kinaonesha chimbuko la migogoro nchini, aina ya migogoro na hatua zilizotekelezwa/zinazotekelezwa na Wizara.

Utatuzi wa Kero na Malalamiko ya Wananchi Kuhusu Huduma ya Ardhi

36. **Mheshimiwa Spika**, ukweli ni kwamba kero na malalamiko ya wananchi yasiposikilizwa na kupatiwa ufumbuzi husababisha migogoro, wananchi kuichukia Serikali yao na kutotii sheria hivyo amani ya nchi huwa hatarini kutoweka. Kwa kutambua hili, Wizara imedhamiria kuwa na utaratibu maalum wa kutembelea kila Halmashauri nchini kujadili kero na malalamiko mbalimbali ya wananchi na kuzipatia ufumbuzi. Ili kutekeleza azma hii, nimetembelea Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Meru, Jiji la Mwanza (Nyamagana), Ilemela, Mji wa Kahama, Manispaa ya Tabora, Manispaa ya Sumbawanga na Morogoro kuzungumza na uongozi wa mikoa husika kuhusu migogoro ya ardhi, kukusanya kero za wananchi na kuunda kikosi cha kushughulikia kero na malalamiko hayo.

Kwa Mkoa wa Mwanza nilipokea jumla ya malalamiko 280 ambapo 81 yametoka Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na 199 kutoka Halmashauri ya Jiji la Mwanza(Nyamagana). Katika uchambuzi wa kina, masuala 395 yalijitokeza kama malalamiko zaidi ya yaliyokusanywa awali. Pia, katika Halmashauri ya Manipaa ya Sumbawanga nilikusanya malalamiko 91, Halmashauri ya Mji wa Kahama 86, Halmashauri ya Mji wa Babati na Halmashauri ya wilaya ya Babati 105, Halmashauri ya Jiji la Arusha pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na Meru malalamiko 102, na Halmashauri ya Manispaa ya Tabora 215. Kwa upande wa Dar es Salaam madawati ya malalamiko yamefunguliwa katika Manispaa ya Temeke, Ilala na Kinondoni. Uchambuzi umeonesha kuwa malalamiko mengi yanatokana na fidia kutolipwa, kuwa pungufu, kucheleweshwa au ukadiriaji usiofuata taratibu, yakifuatiwa na uelewa mdogo wa Kanuni, Taratibu na Sheria kwa watendaji na wananchi, na yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na uadilifu na utendaji usiyoridhisha wa watumishi wa sekta ya ardhi. Napenda kutoa taarifa kwamba malalamiko haya yanashughulikiwa na zoezi hili ni endelevu. Aidha, kila mwananchi aliyewasilisha malalamiko atajibiwa na asiyewasilisha atafikiwa na kusikilizwa. **Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuanzisha dawati maalum la kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi yanayohusu masuala ya ardhi na kuwasilisha taarifa za utatuzi wa migogoro katika ofisi za kanda kwa uchambuzi. Taarifa hizo ziwe zinawasilishwa Wizarani kila mwezi kwa hatua stahiki.**

Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria

37. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara ilikuwa na lengo la kusajili Hati za kumiliki ardhi na Nyaraka za Kisheria zipatazo **87,000**, kati ya hizo Hati za kumiliki ardhi ni **42,000** na Nyaraka za Kisheria ni **45,000**. Hadi Aprili 2015, Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **69,063** zilisajiliwa sawa na asilimia **79.4** ya lengo lililokusudiwa. Kati ya hizo Hatimiliki ni **23,554**, hati za sehemu ya jengo/eneo (*Unit Titles*) ni **1,005** na Nyaraka **33,058** zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi Sura 334 (**Jedwali Na. 3A**). Aidha, nyaraka **9,937** zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka Sura 117 (**Jedwali Na. 3B**). Pia, rehani ya mali zinazohamishika zipatazo **2,506** zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali Zinazohamishika Sura 210 (**Jedwali Na. 3C**).

38. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara inakusudia kusajili Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **88,000**. Kati ya hizi, Hati za kumiliki ardhi ni **38,000**, hati za kumiliki sehemu ya jengo/ eneo **2,000** na Nyaraka za Kisheria **48,000**.

39. **Mheshimiwa Spika**, katika kulinda haki za kumiliki ardhi, wadau wa Sekta ya Ardhi wanahimizwa kuzifahamu sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza Sekta hii.

Kila mdau akiwa na ufahamu huo na akitambua wajibu wake, kwa kiasi kikubwa utapeli wa ardhi na migogoro inaweza kupungua kwa kiasi kikubwa. Wananchi wanaofanya miamala mbalimbali ya ardhi wanashauriwa kupata taarifa sahihi za kiwanja au shamba kutoka ofisi za ardhi. **Nawahimiza wananchi/wadau wenye milki za ardhi kuhakikisha kuwa wanasajili miamala yao yote inayohusu milki zilizosajiliwa. Usajili wa miamala hii utawawezesha kuwa na kumbukumbu sahihi na usalama wa milki.**

TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

40. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kujenga, kuimarisha na kusimamia mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za ardhi. Mifumo hiyo ni: Mfumo wa Kusimamia Utawala wa Kumbukumbu za Ardhi (*Management of Land Information System- MOLIS*) na Mfumo wa Kutunza Kumbukumbu na Kukadiria Kodi ya Ardhi (*Land Rent Management System - LRMS*).

41. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kuanza ujenzi wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System - ILMIS*) ambao ni mfumo mpana zaidi ikilinganishwa na mifumo iliyopo. Napenda kuliariifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi ya ujenzi wa Mfumo huo imeanza Mei, 2015 na imekadiriwa kukamilika mwaka wa fedha 2019/20. Katika Awamu ya kwanza, Serikali itakamilisha ujenzi wa Mfumo ambao utafungwa katika Makao Makuu ya Wizara na katika Ofisi za Kanda nane. Awamu hiyo ya kwanza inatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2016/17. Awamu ya pili itahusisha kufunga Mfumo katika Ofisi za Ardhi katika Halmashauri zote nchini. **Baada ya mfumo huu kufungwa, huduma za Upangaji, Upimaji na Umilikishaji ardhi zitakuwa zinatolewa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.** Chini ya mfumo huu waombaji wa huduma hizo watakuwa na fursa ya kutuma maombi na kupata majibu kwa njia ya kielektroniki. Aidha, hatua hizo zitasaidia kurahisisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi, kurahisisha utoaji wa hatimiliki, udhibiti wa makusanyo ya kodi za ardhi, kudhibiti utoaji wa milki juu ya milki, kuzuia wizi, udanganyifu na ulaghai.

42. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kusimamia mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi Kumbukumbu na Kukadiria Kodi ya Ardhi katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri **30**. Napenda kuliariifu Bunge lako Tukufu kwamba, hadi kufikia Aprili, 2015, Mfumo huu umeunganishwa katika ofisi za ardhi za Halmashauri **70** na kuzidi lengo zaidi ya mara mbili hivyo kuwa na jumla ya ofisi za ardhi **145** pamoja na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) Dodoma zinazotumia mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu (**Jedwali Na. 4**), na Ofisi za Halmashauri **23** zilizobaki zitafungwa Mfumo huu kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2014/15.

Natoa wito kwa watendaji wa sekta ya ardhi katika Halmashauri zote kuingiza taarifa sahihi na kamilifu ili kuboresha utendaji wa kazi na hivyo kuongeza ukusanyaji wa kodi za ardhi.

43. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeboresha Mfumo wa Kutunza Kumbukumbu za Ardhi (*Management of Land Information System – MOLIS*) kuwa na uwezo wa kuhifadhi taarifa za miamala inayofanyika katika Ofisi za Ardhi za Kanda na Msajili wa Hati. Kazi ya kufunga mfumo huu katika Ofisi za Kanda inaendelea na itakamilika katika mwaka wa fedha 2015/16.

Utunzaji wa Kumbukumbu zingine za Sekta ya Ardhi

44. **Mheshimiwa Spika**, ili kuwawezesha wadau mbalimbali wa sekta ya ardhi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kupata taarifa mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi, Wizara yangu imeziweka taarifa hizo katika mfumo wa kielektroniki. Taarifa hizo zinapatikana kwenye **“app store”** inayoitwa **“ardhi tza”** inayopatikana kwenye programu za simu. Aidha, hatua hii itasadia kupatikana kwa taarifa hizo kwa urahisi na mahali popote mhitaji atakapokuwepo. Miongoni mwa taarifa zilizowekwa katika mfumo huu ni pamoja na Sera, Sheria, kanuni, miongozo na machapisho mbalimbali yanayohusiana na sekta ya ardhi. Pia, Wizara imetayarisha Mfumo unaowawezesha wananchi kupata taarifa za umiliki wa viwanja na mashamba yao kwa kutuma ujumbe mfupi kwa kutumia simu za mkononi kwa kuandika neno **MOL** kwenda namba **15404**. Azma hii inalenga kuwapa elimu ya kutosha wananchi kwa njia ya mtandao kuhusu sera na sheria zilizopo za ardhi na hivyo kutambua haki na wajibu wao hususan katika ulipaji wa kodi ya ardhi.

UTHAMINI WA MALI

45. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa huduma za uthamini wa mali. Huduma hii ina lengo la kuishauri Serikali na Taasisi zake kuhusu bei na fidia za miamala ya ardhi kama vile kuuza, kununua na kutwaa mali zisizohamishika. Aidha, Wizara iliendelea na jukumu la kukagua na kuidhinisha taarifa za uthamini zilizoandaliwa na kuwasilishwa na Wathamini wa Halmashauri mbalimbali nchini na Makampuni Binafsi ya Uthamini. Wizara pia inasimamia uthamini nchini kwa kutoa miongozo, kodi ya pango la ardhi na viwango ashiria vya thamani ya ardhi na mazao.

46. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara ilipanga kuandaa na kuidhinisha taarifa **10,000** za uthamini wa mali kwa matumizi mbalimbali. Matumizi haya ni pamoja na utozaji ada na ushuru wa Serikali unaotokana na miamala ya ardhi, vibali vya uhamisho wa milki za ardhi na utozaji malipo ya awali (*premium*) wakati wa utoaji milki mpya za ardhi, kuweka mali rehani, uhuishaji wa muda milki za ardhi na dhamana za mahakama.

Vilevile taarifa hizo hutumika katika mgawanyo wa mali za wanandoa, mirathi, kinga za bima, mizania na ushauri wa thamani katika kutatua migogoro ya ardhi.

47. **Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili, 2015, Wizara iliidhinisha taarifa **10,507** za uthamini wa mali. Huduma hii ya uthamini ilitolewa sawia na utozaji ada ya uthamini ambapo **shilingi 637,114,010** zilikusanywa (**Jedwali 5A**). Katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara imepanga kuandaa na kuidhinisha taarifa **12,000** za uthamini wa nyumba na mali.

48. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara ilipanga kufanya na kuidhinisha taarifa za uthamini wa fidia wa mali za wananchi **30,000** ambao mali zao zitaguswa na miradi ya maendeleo ya umma. Hadi Aprili, 2015 Wizara iliidhinisha taarifa **138** za uthamini kwa ajili ya ulipaji fidia stahiki kwa wamiliki wa asili **23,107** wa ardhi. Mali zilizofanyiwa uthamini zilikuwa na thamani ya jumla ya **shilingi bilioni 150.06**. Miradi ya uwekezaji iliyohusika ilikuwa ya migodi, miundombinu, kilimo, ujenzi wa barabara, upanuzi wa bandari, huduma za jamii na utekelezaji mipango ya miji na upimaji viwanja kwa matumizi mbalimbali (**Jedwali Na. 5B**). Katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itafanya uthamini wa mali kwa ajili ya ulipaji fidia kwa wananchi **35,000** katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Viwango vya Thamani

49. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhakikisha uwepo wa viwango sahihi vya ukadiraji thamani ya ardhi na mazao. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara ilihusha viwango vya thamani ya ardhi na mazao katika mikoa ya Mtwara na Lindi. Zoezi hili ni endelevu na hufanyika kila mwaka kwa vile thamani ya ardhi hubadilika kwa mujibu wa nguvu na mwenendo wa soko. Katika mwaka wa fedha 2015/16 kazi hii itaendelea katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Kigoma na Tabora.

50. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kusambaza miongozo kwa wataalam na wadau wa uthamini nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mwongozo wa Utaratibu wa Uthamini wa Fidia na Mwongozo wa Uchambuzi na uwekaji viwango vya thamani ya soko la ardhi, majengo na mazao imesambazwa.

51. **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaelekeza kwamba hakuna mali ya mwananchi itakayochukuliwa bila fidia. Kifungu cha 11(i) cha Sheria ya Utwaaji kinaelekeza kuwa pale ardhi inapotwaliwa mnufaika na utwaaji huo anawajibika kulipa fidia kwa mmiliki wa asili anayeondolewa kwenye ardhi hiyo.

Aidha, Kifungu cha 3(1)(g) cha Sheria za Ardhi (Sura 113) na (Sura 114) kinaelekeza kuwa fidia hiyo ni lazima iwe kamilifu, ya haki na ilipwe kwa wakati (*full, fair and prompt compensation*). Ili kuhakikisha matakwa ya Sheria husika yanazingatiwa kabla ya kutwaa eneo, tarehe 21 Mei, 2015 Wizara imetoa Waraka Na. 1 wa mwaka 2015 ambao unatoa mwongozo wa masuala yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya uthamini kwa ajili ya kulipa fidia. Waraka huo umesambazwa kwa Wizara, Mikoa, Wilaya, Taasisi za Umma na binafsi, Mashirika ya Umma, Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji na Wilaya kwa utekelezaji. Kwa sasa, utaratibu ufuatao unapaswa kuzingatiwa:-

- a) Wizara, Mamlaka za Mikoa, Wilaya, Taasisi za Umma, Taasisi Binafsi, Mashirika ya Umma, Mamlaka ya Halmashauri za Miji, Wilaya na Vijiji, inayohusika na kulipa fidia, itapaswa kuwasilisha uthibitisho wa uwepo wa fedha za kulipa fidia kwa mamlaka ya Halmshauri ambapo ardhi inatwaliwa na pia uthibitisho huo uwasilishwe kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kabla ya utwaaji wa ardhi ya mwananchi;
- b) Zoezi la fidia lazima lizingatie ushirikishwaji wa kutosha wa wadau wote muhimu wakiwemo Viongozi wa Kata, Serikali za Mitaa au Vijiji na Wananchi;
- c) Kuanzia sasa, Mthamini Mkuu wa Serikali hataidhinisha Taarifa ya Uthamini isiyokuwa na kiambatisho cha uthibitisho wa uhakika wa uwepo wa fedha iliyotengwa kwa ajili ya kulipa fidia;
- d) Zoezi la uthamini lifanyike kwa uwazi, uadilifu na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Taaluma ya Uthamini; na
- e) Wakati wa kufanya malipo ya fidia ni lazima kuwe na mwakilishi wa Mthamini Mkuu wa Serikali.

Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini na taasisi mbalimbali kutenga fedha za fidia kabla ya kutwaa maeneo.

MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA

52. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kuimarisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa kuyapatia vitendea kazi na kushughulikia mashauri **18,444** yaliyokuwepo hadi Aprili, 2014 na mengine yatakayofunguliwa. Napenda kuliariafu Bunge lako Tukufu kwamba Mabaraza matano (Mpanda, Kyela, Ngara, Karagwe, na Ngorongoro) yaliyoundwa mwaka 2013/14 yameanza kufanya kazi.

Hadi Aprili, 2015 jumla ya mashauri mapya **13,338** yalifunguliwa na hivyo kuwa na jumla ya mashauri **31,782**. Kati ya mashauri hayo, mashauri **13,749** yaliyamuliwa. Mashauri **18,033** yaliyobaki na yatakayofunguliwa yataendelea kushughulikiwa katika mwaka wa fedha 2015/16 (**Jedwali Na. 6**).

53. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekuwa ikiunda Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kutegemea upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara itaendelea kuboresha Mabaraza yaliyopo kwa kuyapatia watumishi na vitendea kazi muhimu na kuanzisha mapya katika wilaya za Kahama, Kilindi na Mbulu. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaendelea kutoa elimu kwa Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi katika Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata. Uimarishaji wa mabaraza hayo utapunguza mlundikano wa mashauri katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa kuwa migogoro isiyo ya lazima kwenda ngazi ya Wilaya itasuluhishwa katika ngazi ya Kijiji au Kata.

54. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara kwa kushirikiana na wadau itafanya tathmini ya miaka 12 ya Sheria ya Mahakama za Ardhi, Sura 216. Matokeo ya tathmini hiyo yatasaidia kupima utendaji kazi katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya pamoja na vyombo vingine vya utatuzi wa migogoro ya ardhi. Aidha, kutokana na matokeo hayo, Serikali itachukua hatua stahiki ili kuboresha utendaji kazi katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na mfumo wa utatuzi wa migogoro kwa ujumla.

HUDUMA ZA UPIMAJI NA RAMANI

55. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliendelea kusimamia upimaji ardhi na utayarishaji ramani za msingi kwa nchi nzima. Upimaji ardhi huwezesha kupata vipimo, ukubwa na mipaka ya vipande vya ardhi, taarifa na takwimu ambazo ni msingi wa usimamizi wa ardhi katika sekta zote. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara ilifanya kazi za kutayarisha ramani, kuhakiki mipaka ya ndani na ya kimataifa, kupima mipaka ya vijiji, kutafsiri Matangazo ya Serikali kuhusu mipaka ya hifadhi mbalimbali na kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja na mashamba.

Utayarishaji Ramani

56. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara ilipanga kujenga na kuimarisha kanzi ya taarifa za kijiografia (*geo-database*) katika wilaya **19**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2015, Wizara imejenga na kuimarisha kanzi za wilaya **8** katika mikoa ya Shinyanga na Mwanza ambazo ni Shinyanga, Kahama, Kishapu, Kwimba, Magu, Ilemela, Ukerewe na Nyamagana.

Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara itaendelea kukamilisha kanzi za wilaya **8** za Kaliua, Urambo, Ikungi, Mkalama, Kalambo, Kasulu, Uvinza na Mbozi, pamoja na kujenga kanzi katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Rukwa.

57. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kuchapa ramani za uwiano wa 1:2,500 za Jiji la Dar es Salaam, ramani elekezi ya Jiji la Dar es Salaam (*City Guide map*) pamoja na ramani za kuonesha maeneo ya utalii katika mbuga za wanyama za Serengeti na Mikumi.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hadi Aprili, 2015 ramani elekezi za Dar es Salaam za uwiano wa 1:2,500 zilichapishwa na kazi za uhakiki uwandani zinatarajia kukamilika Juni, 2015. Pia, uandaaji wa ramani zinazoonesha maeneo ya utalii kwenye mbuga za wanyama za Mikumi na Serengeti umekamilika. Kazi za uhakiki uwandani zitafanyika katika mwaka wa fedha 2015/16.

Mipaka ya Ndani ya Nchi

58. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kupima mipaka kati ya Hifadhi ya Serengeti na vijiji inavyopakana navyo pamoja na kutafsiri Tangazo la Serikali (*Government Notice*) Namba 358 la mwaka 1968. Aidha, Wizara iliahidi kuhakiki na kupima mipaka ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi za Wanyama za Taifa (TANAPA), wanavijiji na wadau wengine. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi ya upimaji na uhakiki wa mpaka wa Hifadhi ya Serengeti na vijiji inavyopakana haijakamilika kwa sababu ya kesi iliyofunguliwa Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza na vijiji vya Mbochugu, Bisarara, Nyambuli, Mbalibali, Nyamakendo, Machochwe na Merenga vilivyoko katika wilaya ya Serengeti. Kazi ya kuhakiki mpaka wa Hifadhi ya Serengeti katika vijiji visivyo husika na kesi hii inaendelea uwandani. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itaendelea kukamilisha uhakiki wa mipaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kushirikiana na wadau wengine iwapo yatakuwepo makubaliano kati ya Hifadhi na wananchi wanaopakana na Hifadhi hiyo.

59. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekuwa ikiendelea na upimaji wa mipaka ya vijiji vinavyoendelea kuanzishwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2015 jumla ya vijiji **133** vilihakikiwa na kupimwa katika wilaya za Kiteto (**45**) na Bagamoyo (**88**). Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara yangu itaendelea na upimaji wa vijiji **100**.

Mipaka ya Kimataifa

60. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kukamilisha upimaji wa mpaka kati ya Tanzania na nchi za Kenya, Burundi, Zambia, Msumbiji na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) pamoja na kuandaa kanzi ya mipaka hiyo. Uhakiki wa mpaka kati ya Tanzania na Burundi wenye urefu wa **kilomita 450** ulipangwa kufanyika katika awamu tatu. Awamu ya kwanza imefanyika katika Wilaya ya Ngara ambapo **kilomita 135.8** zilihakikiwa na alama za mpaka **365** zilisimikwa na kupimwa. Awamu ya pili na tatu zitafanyika katika Wilaya za Kibondo na Kasulu mkoani Kigoma katika mwaka wa fedha 2015/16. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Rais wa Jamhuri ya Burundi Mhe. Pierre Nkurunziza kwa pamoja walizindua rasmi uhakiki na uimarishaji wa mpaka huo katika kijiji cha Mugikomero wilayani Ngara mnamo tarehe 28 Agosti, 2014.

61. **Mheshimiwa Spika**, kazi ya upimaji picha ili kutengeneza ramani za msingi katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji inaendelea. Kati ya kilomita **671**, kilomita **51** ambazo ni sehemu ya nchi kavu zimeimarishwa na kupimwa. Kilomita **620** ambazo ni sehemu ya majini (Mto Ruvuma) zitafanyiwa kazi mara baada ya kukamilisha uandaaji wa kanzi (*database*) na ramani za msingi sehemu ya nchi kavu. Kuhusu mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa, mazungumzo ya usuluhishi chini ya jopo la Marais wastaafu Mhe. Joachim Chisano (Mwenyekiti), Mhe. Thabo Mbeki na Mhe. Festus Mogae yanaendelea. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itaendelea na uhakiki na uimarishaji wa mipaka kati ya Tanzania na Kenya, na Tanzania na Zambia.

Upimaji wa Viwanja na Mashamba

62. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara yangu iliahidi kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **70,000** na mashamba **500**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2015, ramani zenye viwanja **83,502** na mashamba **290** zimeidhinishwa (**Jedwali Na. 7**). Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara itaidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **90,000** na mashamba **300**.

63. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kukamilisha usimikaji wa alama za msingi (*Control Points*) **240** katika miji **38**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ili kurahisisha upimaji ardhi mijini, jumla ya alama za msingi **80** zimesimikwa katika miji ya Kibaha (**25**), Bagamoyo (**30**) na Mkuranga (**25**). Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara itaendelea kusimika na kupima alama za msingi **160** katika miji **35**.

Upelekaji Huduma za Upimaji Kwenye Kanda

64. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imesogeza huduma za upimaji ardhi kwenye kanda ili kuwezesha wananchi kupatiwa huduma za upimaji katika maeneo yao. Aidha, Wizara itaanzisha vikosi maalum vya upimaji ardhi vitakavyokuwa na vifaa vyote vinavyohitajika pamoja na vyombo vya usafiri ili kufanikisha kazi za upimaji. Hatua hii ni muhimu kwa kuwa migogoro ya mipaka kati ya wilaya na wilaya au kijiji na kijiji sasa itatatuliwa kwenye kanda na hivyo, kurahisisha na kuharakisha utatuzi wa migogoro nchini. Vilevile upimaji ardhi ya wananchi utakuwa rahisi na hivyo kuharakisha azma ya kupima kila kipande cha ardhi nchini na kuwa na kumbukumbu sahihi zinazohusu miliki. **Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kutumia huduma zitakazotolewa na vikosi hivi mara tu vitakavyokamilika ili kupunguza gharama za upimaji na pia kupunguza migogoro ya ardhi inayotokana na upimaji usiozingatia sheria.**

Upimaji wa Ardhi chini ya Maji

65. **Mheshimiwa Spika**, jukumu mojawapo la Wizara ni upimaji wa ardhi chini ya maji na kutayarisha ramani zinazoonesha umbile la ardhi chini ya maji hususan milima, mabonde, miinuko na kina cha maji. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara imepanga kukusanya taarifa za upimaji chini ya maji kutoka kwenye taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi ili kuandaa kanzi ya taarifa za umbile la ardhi chini ya maji.

MIPANGOMIJI NA VIJJI

66. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ina jukumu la kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji ili wananchi wawe na makazi yaliyopangwa. Majukumu hayo yanaratibiwa na kutekelezwa kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali na taratibu za uendelezaji Miji na Vijiji.

Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Jumla ya Uendelezaji Miji (Master Plans)

67. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kushirikiana na wadau mbalimbali kukamilisha Mipango ya Jumla ya Halmashauri za Manispaa ya Sumbawanga, Wilaya ya Mafia, Miji Midogo ya Bagamoyo na Bariadi. Rasimu ya Mipango ya Miji ya Bagamoyo na Kilindoni ilikamilika na itawasilishwa kwa wadau ili kupata ridhaa. Rasimu ya Mipango wa Manispaa ya Sumbawanga iko katika hatua ya kupata maoni na mapendekezo ya wadau.

68. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri iliahidi kuanza utayarishaji wa Mpango Kabambe wa Mji wa Mtwara ambao unajumuisha Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani na sehemu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara katika kata sita za Naumbu, Mbawala, Mayanga, Nanguruwe, Ziwani na Msangamkuu. Utekelezaji wa kazi hii uko katika hatua ya kukusanya na kuchambua takwimu na taarifa mbalimbali za kisékta. Mpango huu unaandaliwa na Mtaalam Mwelekezi na utakamilika katika mwaka wa fedha 2015/16. Aidha, maandalizi ya Mpango Kabambe wa Mji wa Lindi yapo katika hatua ya awali ya uhamasishaji na uelimishaji wadau.

69. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Mwanza na Arusha pamoja na Halmashauri za Manispaa ya Ilemela na Halmashauri za Arusha na Meru imeanza kuandaa Mipango Kabambe ya Halmashauri hizo kwa kutumia Mtaalam Mwelekezi. Kazi hii imeanza Februari 2015 na itakamilika Septemba, 2016.

70. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo Halmashauri za Manispaa za Iringa, Songea, Lindi, Shinyanga na Halmashauri ya Mji wa Geita ili kukamilisha Mipango ya Uendelezaji Miji. Kadhalika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo na Chuo Kikuu Ardhi zitaandaa Mipango Kabambe ya Miji midogo ya Chalinze na Msata. Taarifa kuhusu hali halisi ya mipango kabambe inayoendelea kuandaliwa nchini imeainishwa katika **Kiambatisho Na.2. Natao wito kwa Halmashauri zote nchini ambazo hazina Mipango Kabambe kutenga fedha za kuandaa Mipango hiyo.**

Uandaaji na Utekelezaji Mipangokina ya Uendelezaji Miji

71. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeendelea kutekeleza Mpango wa kuboresha makazi katika eneo la Makongo Juu kwa kufanya vikao vya maridhiano na wananchi/ wadau ili kupata uelewa wa pamoja wa kutekeleza mpango huo. Dhana mpya inayopendekezwa kutumika ni shirikishi ambapo wananchi kwa kushirikiana na wadau wengine watahusika katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa mpango. Aidha, Mpango wa Uendelezaji upya wa eneo la kati la Mji wa Njombe umekamilika na unasubiri ridhaa ya wadau. Hadi Aprili, 2015 jumla ya michoro **834** ilipokelewa, kukaguliwa na kuidhinishwa. Wizara inaendelea na kazi ya kuandaa miongozo ya namna ya kupanga matumizi ya ardhi katika miji midogo nchini.

Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni

72.**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara iliahidi kuendelea na uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni chini ya usimamizi wa Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni (*Kigamboni Development Agency-KDA*). Hadi Aprili, 2015 Serikali, imefanya mapitio na kurekebisha Matangazo ya Serikali kuhusiana na Mji Mpya wa Kigamboni ambapo eneo la Mpango limepunguzwa kwa kuondoa kata tatu ambazo ni Pembamazi, Kisarawe II na Kimbiji zenye ukubwa wa hekta **44,440** ambazo hazikuwemo katika mpango wa awali na hivyo kubaki na kata sita zenye eneo la ukubwa wa hekta **6,494**.

Aidha, Wizara imefanya mikutano ya mashauriano na wadau mbalimbali wa Mji Mpya wa Kigamboni ili kuwa na uelewa wa pamoja juu ya dhana mpya ya uendelezaji wa Mji wa Kigamboni. **Kwa mujibu wa dhana hii, wananchi wa Kigamboni wana fursa ya kushiriki katika uendelezaji kwa kutumia mojawapo ya njia zifuatazo: kwanza; mwananchi mwenyewe kuwa mwendelezaji katika eneo lake kwa kuzingatia Mpango; pili; mwananchi kulipwa fidia au kuuza eneo lake kwa mwekezaji kwa hiari yake kwa kuzingatia bei ya soko; na mwisho kuingia ubia na mwekezaji kwa kutumia ardhi yake kama mtaji.** Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara kupitia KDA itaendelea na kazi zifuatazo: kuandaa Mipango ya Kina (*Detailed Plans*) ya maeneo yaliyopo ndani ya eneo la Mpango kwa kuainisha maeneo ya matumizi mbalimbali; kuthamini, kulipa fidia na kupima maeneo ya miundombinu na huduma za jamii.

MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI

Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi

73.**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kukamilisha na kuchapisha Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi hii imekamilika na kusambazwa kwa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ambao wamegawiwa kama sehemu ya hotuba yangu. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara itaendelea kutekeleza Mpango kwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya na vijiji hususan katika ukanda wa SAGCOT katika wilaya za Kilombero na Ulanga. Wilaya hizi mbili zitatumika kama wilaya za mfano katika kupanga, kupima na kumilikisha vipande vyote vya ardhi kupitia mradi wa **'Land Tenure Support Programme.'** Aidha, mpango wa Matumizi ya Ardhi katika ukanda wa Reli ya Uhuru umefanyiwa mapitio na kuhuishwa katika mikoa tisa (Pwani, Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Katavi na Dodoma) ya ukanda wa SAGCOT. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara itachapisha na kusambaza mpango huu, kutoa elimu kwa wadau na kuanza utekelezaji wake.

74. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kukamilisha kuandaa Kanuni za Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 2007 pamoja na kutafsiri Mwongozo wa Upangaji na Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi Vijijini katika lugha ya Kiswahili. Pia Wizara iliahidi kuchapisha na kusambaza kwa wadau kitabu cha Kiongozi cha Mwanakijiji katika Upangaji na Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi Vijijini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba vitabu vya Kiongozi cha Mwanakijiji vimechapishwa na kusambazwa kwa wadau wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ambao wamegawiwa kama sehemu ya hotuba yangu. Kanuni za Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 2007 zimeandaliwa na tafsiri ya Mwongozo wa Upangaji na Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi Vijijini imekamilika. Kanuni na mwongozo huo vitachapishwa na kusambazwa kwa wadau katika mwaka 2015/16.

Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji

75. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kukamilisha kazi ya kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi katika Halmashauri za Wilaya za Tarime, Rorya, Newala na Geita pamoja na kutoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa Wilaya nne kuhusu Sheria za Ardhi na mbinu shirikishi za uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Rasimu za mwisho za taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi za Wilaya za Newala, Rorya, Muleba na Tarime zimekamilika na zitawasilishwa kwa wadau kwa maoni.

Aidha, ukusanyaji wa takwimu kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika Halmashauri za Wilaya za Geita, Mvomero, Ulanga na Kilombero umekamilika na kwa sasa zinaandaliwa rasimu za mipango hii; ambayo itawasilishwa kwa wadau ili kutoa maoni na kukamilika katika mwaka wa fedha 2015/16.

76. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliahidi kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **200** pamoja na kuendelea na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na Wilaya katika ukanda wa SAGCOT kwa kutenga maeneo ya matumizi mbalimbali ikiwemo uwekezaji. Hadi Aprili, 2015, jumla ya vijiji **91** vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika wilaya mbalimbali (**Jedwali Na. 8**). Aidha, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na uhakiki wa maeneo ya uwekezaji umefanyika katika vijiji **38** katika Halmashauri za Wilaya za Ulanga (6), Kilombero (4), Iringa (4), Njombe (2), Makete (2), Ludewa (2), Kibaha (2), Busokelo (4), Bagamoyo (4) na Rufiji (8).

77. **Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi, hususan baina ya wakulima, wafugaji na hifadhi; Wizara kwa kushirikiana na wadau imewezesha upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi katika vijiji **60** vya Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero na vijiji **10** vya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto kipaumbele kimekuwa kuanza na vijiji kumi (**10**) vya Loltepes, Emart, Enguserosidan, Kimana, Namelok, Kinua, Taigo, Krash, Ndirigish na Knati vinavyopakana na pori la hifadhi ya *Emboley Murtangos*; ambavyo vilikuwa kitovu cha migogoro katika eneo hili.

78. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itajenga uwezo na kuwezesha Halmashauri za Wilaya katika maeneo mbalimbali nchini kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **200**. **Natoa rai kwa Halmashauri za Wilaya kutenga fedha kwa ajili ya utayarishaji na utekelezaji wa mipango hii kwa kufuata miongozo inayotolewa na Wizara yangu.**

MAENDELEO YA SEKTA YA NYUMBA

79. **Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kusimamia sera na mikakati itakayowezesha kuwepo kwa ongezeko la nyumba bora zenye gharama nafuu, ushindani halali wa kibiashara, haki na uwazi kwenye sekta ya nyumba. Ukuaji wa sekta ya nyumba ni chachu ya kukuza ajira kwa vijana na kupunguza umaskini. Pia, sekta ya nyumba imekuwa ni miongoni mwa vichocheo vya ukuaji haraka wa sekta nyingine nchini.

80. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara iliahidi kutoa elimu kwa umma kuhusu utaratibu wa utoaji wa mikopo ya nyumba, ikiwa ni pamoja na haki na wajibu wa mkopaji na mkopeshaji kwa mujibu wa Sheria. Vilevile, Wizara iliahidi kuweka utaratibu utakaowezesha kupatikana kwa mikopo ya nyumba kwa masharti nafuu. Pia, Wizara iliahidi kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya nyumba ikiwemo sekta binafsi ili kujenga nyumba za kuuza na kupangisha.

81. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, kuwa mazingira mazuri ya kibiashara, kisheria na kimuundo yamewekwa kwa ushirikiano kati ya Wizara, Benki Kuu ya Tanzania na *Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC)* yamewezesha jumla ya benki **20** kuanza kutoa mikopo ya nyumba. Hadi Disemba, 2014 benki hizo zimetoa mikopo **3,598** yenye thamani ya **shilingi bilioni 248.35**.

82. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 utoaji wa mikopo ya nyumba uliongezeka kwa asilimia **59** ikilinganishwa na asilimia **23** kwa mwaka wa fedha 2013/14. Aidha, mikopo inatarajiwa kuongezeka katika mwaka wa fedha 2015/16 kutokana na Serikali kuiwezesha Kampuni ya TMRC kupata mtaji wa nyongeza wa Dola za Marekani **milioni 40. Nachukua fursa hii kuzihimiza benki za biashara ambazo hazijaanza kutoa mikopo ya nyumba zianze kufanya hivyo sasa kwa kupata mtaji kutoka Kampuni ya TMRC.**

83. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Serikali iliongeza mtaji wa Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba (*Housing Microfinance Fund-HMFF*) kutoka Dola za Marekani **milioni 3** mwaka wa fedha 2013/14 hadi **milioni 18** mwaka wa fedha 2014/15. Mfuko huu utakuwa ukizikopesha mtaji taasisi za fedha ambazo zinatoa mikopo midogo midogo ya nyumba kwa wananchi kwa masharti nafuu. Utekelezaji wake utanza mwaka wa fedha 2015/16 baada ya Mwongozo kuhusu sifa za taasisi za fedha zinazostahili kupata mikopo hiyo kukamilika.

84. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha, 2014/15 Wizara iliratibu upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma kupitia *Watumishi Housing Company*. Kampuni hiyo imepata ekari **741.3** katika mikoa **12** ambayo ni; Dar es Salaam (**36.3**), Arusha (**111**), Pwani (**262**), Tanga (**30**), Morogoro (**10**), Dodoma (**8**), Mwanza (**22**), Shinyanga (**10**), Lindi (**25**), Mbeya (**157**), Mtwara (**20**) na Kilimanjaro (**50**) kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ambazo zitauzwa kwa watumishi wa umma kwa bei nafuu.

Uwezesaji Wananchi Kumiliki Nyumba

85. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuwawezesha wananchi hususan wenye kipato kidogo kumiliki nyumba kwa kupata mikopo yenye gharama nafuu. Hata hivyo, tathmini iliyopo inaonesha kuwa wananchi walio wengi hawana uwezo wa kujenga nyumba kutokana na masharti magumu ya upatikanaji wa mikopo kutoka taasisi za fedha na mashirika yanayojenga na kuuza nyumba nchini. Aidha, wanaohitaji kumiliki nyumba binafsi wangependelea nyumba inayojitegemea (*detached*) yenye angalau vyumba vitatu vya kulala. Kwa bei za sasa, ujenzi wa nyumba ya aina hiyo isiyozidi eneo la meta za mraba **70** inagharimu **shilingi milioni 44**. Bei ya kununua nyumba kama hiyo ni **Shilingi milioni 59.71** ambazo ni pamoja na faida ya asilimia **15 (shilingi milioni 6.6)** na Kodi ya Ongezeko la Thamani-VAT asilimia **18 (Shilingi 9.11 milioni)**. Kwa kuzingatia wastani wa pato la Mtanzania ambalo ni kiasi cha Dola za Marekani **1,700 (shilingi milioni 3.4)** kwa mwaka, familia yenye wastani wa watu **watano** itapata mkopo wa nyumba usiozidi **shilingi milioni 37** iwapo itakopa kwa muda wa miaka **25** na kutozwa riba ya asilimia **15** kwa mwaka.

Ili kuwapa wananchi wengi fursa ya kumiliki nyumba binafsi zenye ubora unaokubalika kijamii, Wizara ililiagiza Shirika la Nyumba la Taifa na Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi kubuni mikakati na kufanya utafiti kuwezesha upatikanaji wa nyumba zenye vyumba vitatu au zaidi kwa gharama isiyozidi **shilingi milioni 35** bila VAT.

86. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Shirika la Nyumba la Taifa limejiwekea lengo la kujenga nyumba zenye gharama isiyozidi **shilingi milioni 25** bila tozo la VAT. Aidha, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi unaendelea na utafiti wa vifaa mbadala vya ujenzi wa kuta na paa ili kuwezesha kujenga nyumba yenye sifa zilizotajwa hapo juu itakayogharimu siyo zaidi ya **shilingi milioni 25**.

87. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutathmini njia mbalimbali zitakazowezesha kushuka kwa gharama za ujenzi na bei ya nyumba bila kuingilia mfumo wa soko huru ili wananchi walio wengi waweze kununua nyumba zinazojengwa na taasisi za umma kama vile, Shirika la Nyumba la Taifa, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Watumishi *Housing Company*. Maeneo ambayo Serikali inayafanyia tathmini ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kupunguza au kuondoa VAT kwa nyumba ambazo zitauzwa kwa bei isiyozidi **shilingi milioni 35**, kuzishirikisha taasisi zinazotoa huduma za miundombinu kuwekeza kwenye maeneo yanayoendelezwa ili kupunguza gharama za ujenzi na hatimaye kupungua kwa bei za nyumba. Aidha, Serikali pale inapowezekana itaendelea kuzipatia taasisi hizo ardhi kwa gharama nafuu pamoja na kuwapa masharti maalum ya uendelezaji wa ardhi kwenye maeneo wanayoyaendeleza.

88. **Mheshimiwa Spika**, katika miaka ya hivi karibuni sekta ya nyumba imekua kwa kasi na inachangia kukuza Pato la Taifa, kuongeza fursa za ajira na hivyo kupunguza umaskini. Aidha, takwimu za awali zinaonesha kuna waendelezaji wa nyumba (*Real Estate Developers*) zaidi ya **60** nchini ambao wanafanya kazi hizo bila kuwa na chombo cha kuwaratibu.

Ili kuwawezesha waendelezaji wa nyumba kuongeza kasi ya ujenzi wa nyumba, Serikali imemteua mtaalam mwelekezi atakayeshauri uanzishwaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Waendelezaji Milki (*Real Estate Regulatory Authority-RERA*) ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu uwekezaji katika milki, kusimamia haki za wapangaji, mapato ya serikali na ubora wa majengo pamoja na huduma zake. Katika kipindi cha mpito Wizara imeanzisha dawati la '*Housing and Real Estate Information Center*'. Azma hii inalenga kuongeza uwazi na upatikanaji wa takwimu sahihi za uwekezaji katika majengo na nyumba. Aidha, itasaidia kubainisha mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa na ajira.

Majukumu ya dawati hilo yatakuwa ni pamoja na kukusanya na kutunza taarifa za wadau wa sekta ya nyumba wakiwemo wajenzi, vyombo vya fedha vinavyotoa mikopo ya nyumba, kampuni zinazotoa huduma na ushauri mbalimbali kama vile madalali wa nyumba, viwanja na mashamba pamoja na taarifa za kodi za majengo na upangishaji.

Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi

89. **Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) una majukumu ya kutafiti, kukuza, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya utafiti na utaalumu wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu nchini. Kazi hizo zikifanyika kikamilifu zitaenua na kuboresha viwango vya nyumba zinazojengwa kwa kutumia vifaa vinavyopatikana hapa nchini na kuinua maisha ya wananchi wenye kipato cha chini. Aidha, Wakala umeeneza teknolojia ya ujenzi wa nyumba kwa kutumia malighafi zipatikanazo katika maeneo mbalimbali mijini na vijijini. Teknolojia hiyo hutumia nguvu kazi za vijana katika kuzalisha vifaa vya ujenzi na ujenzi wenyewe. Kupitia vikundi vya uzalishaji, vijana wanawezeshwa kupata ajira na hivyo kubadili hali yao ya maisha kwa kujiongeza kipato na kuchangia Pato la Taifa.

90. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara iliahidi kuhamasisha na kueneza teknolojia ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika wilaya za Nkasi, Kishapu, Chunya na Tandahimba. Aidha, iliahidi kujitangaza kupitia vyombo vya habari na kushiriki maonesho mbalimbali ya kitaifa. Hadi Aprili, 2015 semina za uhamasishaji wa ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu zilifanyika katika Kata za Chaume, Lukokoda na Lyenje katika Wilaya ya Tandahimba.

91. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wakala pia ulitoa mafunzo kwa vitendo katika Mikoa ya Shinyanga- Wilaya ya Kahama na Mbeya kwa kutumia vikundi vya SACCOS ya Muungano wa Vikoba (Mvita) na kikosi cha ujenzi “*Salen Group*” huko Mtwara. Vilevile, uhamasishaji wa ujenzi wa nyumba bora umefanyika kwa vikundi mbalimbali vya kijamii ambavyo ni “*Youth Technology Hub*” (Dar es Salaam) na Safina (Bagamoyo). Aidha, hadi Aprili, 2015, Wakala ulitengeneza mashine **210** za kufyatulia matofali ya kufungamana na kuziua kwa vikundi mbalimbali. Kadhalika, Wakala ulishiriki katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Mkoani Lindi, Kongamano la Wahandisi lilifanyika Mlimani City, Dar es Salaam na Maadhimisho ya Siku ya Makazi Duniani yalifanyika katika viwanja vya Makumbusho ya Taifa Dar es Salaam.

92. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wakala kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa pia uliendesha mafunzo katika Halmashauri za Wilaya zote **168** za Tanzania Bara. Jumla ya vijana **6,720** walishiriki mafunzo ambapo kulikuwa na washiriki **40** toka kila Halmashauri. Mafunzo haya yaliwezesha kuwa na ajira ya kudumu kwa washiriki. Pia kila Halmashauri ya Wilaya ilipewa mashine **nne** za kufyatulia matofali yanayofungamana ambapo jumla ya mashine **672** zilitolewa.

93. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wakala utaendelea kuhamasisha na kueneza teknolojia ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika Wilaya za Wanging'ombe, Bukombe, Nkasi na Nanyumbu. Aidha, Wakala utaendelea kufanya tafiti mbalimbali za kuendeleza teknolojia rahisi za uzalishaji wa vifaa vya ujenzi na utaandaa mwongozo wa usanifu na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Vilevile, Wakala utaendelea kufanya utafiti kuhusu matumizi ya nishati katika kutengeneza vifaa vya ujenzi na kulinda mazingira "*Energy for Low Income Housing Technology (ELITH)*". Kadhalika, Wakala utaendelea kujitangaza kwa kushiriki katika maonesho na makongamano ya wataalamu. Pia elimu kwa umma kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala itaendelea kutolewa kupitia semina za vikundi pamoja na kujenga nyumba za mfano kwa kutumia teknolojia ya vifaa vya gharama nafuu. Vilevile katika mwaka wa fedha 2015/16 semina za uhamasishaji wa ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu zitafanyika katika Wilaya za Nkasi, Kishapu na Chunya.

SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

Ujenzi wa Nyumba za Makazi

94. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Shirika lilipanga kukamilisha miradi **16** inayoendelea na kuanza miradi mingine mipya **26** ya nyumba za gharama nafuu, kati na juu. Miradi hii, inatekelezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara ambapo lengo ni kujenga nyumba **50** kwa kila mkoa. Hadi Aprili, 2015 Shirika limetekeleza miradi **51** yenye jumla ya nyumba **4,856 (Jedwali Na. 9A)**. Miradi hiyo, imeliwezesha Shirika kuifikia mikoa yote ya Tanzania Bara isipokuwa Kilimanjaro ambako bado ardhi haijapatikana. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Shirika litakamilisha baadhi ya miradi inayoendelea na kuanza ujenzi wa miradi mingine mipya. Jumla ya miradi itakayotekelezwa ni **73** yenye nyumba **7,628** yaani miradi **51** ya nyumba za gharama nafuu **2,175** na miradi **22** ya nyumba za gharama ya juu na kati **5,453**.

Upatikanaji wa Ardhi kwa ajili ya Ujenzi wa Nyumba

95. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa nyumba katika mikoa unategemea upatikanaji wa ardhi ya gharama nafuu. Hadi Aprili, 2015, Shirika lilionunua ardhi yenye ukubwa wa ekari **4,642.85 (Jedwali Na 9B)** katika Halmashauri mbalimbali nchini. Pia, Halmashauri **63** zilitenga jumla ya ekari **3,018.1** kwa ajili ya kuliwezesha Shirika kujenga nyumba. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Shirika litaendelea kushirikiana na Halmashauri ili kununua ardhi yenye gharama nafuu kwa ajili ya kuliwezesha kujenga nyumba.

Mauzo ya Nyumba za Makazi

96. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa kipindi cha 2010/11 – 2014/15, Shirika linatakiwa kuuza asilimia **70** na kupangisha asilimia **30** ya nyumba za makazi zinazojengwa. Hadi Aprili, 2015, Shirika limeuza jumla ya nyumba **959** kati ya **1,327** na kupata **Shilingi bilioni 80.23** kati ya **Shilingi bilioni 141.31** zilizotarajiwa sawa na asilimia **56.8**. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Shirika litaendelea kujenga na kuuza nyumba na matarajio ni kukusanya **Shilingi bilioni 160.2** zikijumuisha fedha ambazo hazijakusanywa kutoka kwa wanunuzi wa awali.

Ujenzi wa Majengo ya Biashara

97. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Shirika lilipanga kutekeleza miradi **30** ya majengo ya biashara. Hata hivyo, Shirika liliweza kutekeleza miradi **11**. Kati ya miradi hiyo miradi **sita** ni mipya na **mitano** ilikuwa inaendelea kutekelezwa. Hadi Aprili, 2015 Shirika lilikamilisha miradi **mitatu** kati ya ile iliyokuwa inaendelea kutekelezwa. Miradi hii, ipo katika barabara ya Ufukweni, Dar es Salaam; Mtaa wa Mkendo, Musoma; na Mtaa wa Kitope, Morogoro. Katika miradi mipya, Shirika lipo hatua za mwisho kukamilisha miradi miwili katika Mtaa wa Lupa Way, Mbeya na Barabara ya Old Dar es Salaam Manispaa ya Morogoro. Aidha, Shirika linaendelea na ujenzi wa miradi mitano iliyoko Mtaa wa Mkendo, Musoma (Awamu ya II); eneo la Paradise, Mpanda; Mtukula, Kagera; pamoja na Mitaa ya Boma na Lumumba katika Manispaa ya Singida. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Shirika litaendelea kukamilisha baadhi ya miradi inayoendelea kwa sasa na kuanza miradi mingine mipya **12** yenye jumla ya nyumba **674**.

Uendelezaji wa Vitovu vya Miji (Satellite Towns)

98. **Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Shirika kufanya kazi kwa ufanisi na tija, Serikali imelipa Shirika la Nyumba la Taifa mamlaka ya kuwa mwendelezaji ardhi mkubwa (*Master Estate Developer*) katika maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya kujenga vitovu vya miji (*Satellite Towns*) ikijumuisha kujenga nyumba nyingi kwa ajili ya kuuza au kupangisha kwa wananchi.

99. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Shirika lilipanga kukamilisha mipangokina (*detailed plans*) ya vitovu vya miji kwenye maeneo ya Luguruni (**ekari 156.53**), Kawe (**ekari 267.71**), Uvumba, Kigamboni (**ekari 202**), Usa River (**ekari 296**) na Burka/Matevesi (**ekari 579.2**). Hadi Aprili, 2015, Shirika lilikamilisha matayarisho ya mipangokina ya maeneo ya Burka/Matevesi, Usa River na Kawe. Ujenzi wa majengo mawili (**2**) yenye jumla ya nyumba za makazi na biashara **700** katika eneo la Kawe ulianza Desemba, 2014 na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu **300** katika eneo la Burka/Matevesi utanza mwezi Julai, 2015.

100. **Mheshimiwa Spika**, Shirika linaendelea kukamilisha matayarisho ya mipangokina ya maeneo ya Luguruni (Kwembe) na Uvumba (Kigamboni). Katika mwaka wa fedha 2015/16, Shirika kwa kushirikiana na waendelezaji mbalimbali litaendelea kuratibu na kujenga katika maeneo ya Kawe, Burka/Matevesi na Usa River na kuanza ujenzi katika maeneo ya miradi ya Luguruni (Kwembe) na Uvumba (Kigamboni) ambapo kupitia miradi hii jumla ya nyumba **15,000** za makazi na biashara zitajengwa.

Utafutaji wa Mitaji kwa ajili ya Miradi

101. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Shirika lilipanga kukopa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi na majengo ya biashara pamoja na kuwahamasisha wananchi kuchukua mikopo kwa ajili ya ununuzi wa nyumba zinazojengwa na Shirika. Hadi Aprili, 2015, Shirika limekopa jumla ya **Shilingi bilioni 242.4** toka benki **tisa**, ambapo mpaka sasa limetumia **Shilingi bilioni 192.1** kutekeleza miradi yake.

Mapato ya Shirika

102. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Shirika lilitarajia kupata **Shilingi bilioni 70.1** kutokana na kodi za pango la nyumba. Hadi Aprili, 2015, Shirika lilipata **Shilingi bilioni 71.15** ambayo ni asilimia **118** ya lengo la kipindi husika [**Jedwali Na 9C**]. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Shirika linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi bilioni 82.2** kutokana na kodi za pango la nyumba.

Mchango wa Shirika kwa Serikali

103. **Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili, 2015 Shirika limechangia mapato ya Serikali jumla ya **shilingi bilioni 18.66** kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani kama vile kodi ya pango la ardhi, kodi ya ongezeko la thamani, kodi ya majengo, kodi ya mapato, ushuru wa huduma za Halmashauri za Miji na Manispaa, kodi za mapato ya wafanyakazi, ushuru wa maendeleo ya taaluma na mchango wa pato ghafi kwa Serikali (**Jedwali Na.9D**).

Matengenezo ya Nyumba na Majengo

104. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Shirika lilipanga kutumia **Shilingi bilioni 6.1** kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa nyumba zake. Hadi Aprili, 2015, Shirika lilizifanyia matengenezo makubwa na ya kawaida nyumba **2,792** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 4.67**. Matengenezo hayo yameliwezesha Shirika kupunguza malalamiko kutoka kwa wapangaji. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Shirika litatenga kiasi cha **shilingi bilioni 7.5** kwa ajili ya matengenezo ya nyumba zake.

HUDUMA ZA KISHERIA

105. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara yangu iliahidi kukamilisha kazi ya uhuishaji wa sheria mbalimbali za ardhi zikiwemo Sheria ya Ardhi Sura 113, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura 114, Sheria ya Mahakama za Ardhi Sura 216 na Sheria ya Upimaji Sura 324. Wizara imepokea maoni ya wadau na inayafanyia kazi kwa ajili ya kuyawasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Wizara imewasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali marekebisho ya Sheria za Usajili wa Ardhi Sura 334, Sheria ya Usajili wa Nyaraka Sura 117, Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali zinazohamishika Sura 210, Sheria ya Mipangomiji Sura 355 pamoja na Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipangomiji Na.7 ya mwaka 2007 kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni.

106. **Mheshimiwa Spika**, Wizara katika mwaka wa fedha 2015/16 inapendekeza kutungwa kwa Sheria mpya ya Usimamizi wa Mawakala wa Ardhi (The Real Estate Agents Act), Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, Sheria itakayosimamia Uanzishwaji wa Chuo cha Ardhi – Tabora pamoja na Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini.

MAWASILIANO SERIKALINI

107. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 niliahidi kukamilisha kuhuisha mkakati wa mawasiliano wa Wizara, kuratibu mawasiliano kati ya Wizara na wadau wake; kuandaa na kurusha vipindi vya televisheni na redio na kuboresha mawasiliano. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imekamilisha kuhuisha mkakati wa mawasiliano ambao unawezesha namna bora ya kuwasiliana na wadau wa Sekta ya ardhi.

108. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliratibu uandaaji wa jumla ya vipindi **12** vya luninga ambavyo vilirushwa hewani na Televisheni ya Taifa.

Vipindi hivi vilielezea huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara. Aidha, taarifa mbalimbali kwa umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara zilitolewa kwenye vyombo vya habari kwa njia mbalimbali ikiwemo mikutano kati ya Wizara na wanahabari (*Press Conferences*) na kuchapisha nakala **5,000** za Jarida la Wizara la '**Ardhi ni Mtaji**' linalosaidia kuelimisha jamii kuhusu Sekta ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara itaendelea kuelimisha umma kuhusu Sera, Sheria, Kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya ardhi kwa kuratibu mawasiliano.

HUDUMA ZA UTAWALA NA RASILIMALI WATU

109. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliendelea kutoa huduma za utawala na usimamizi wa rasilimali watu kwa madhumuni ya kuboresha utendaji kazi unaolenga kuongeza tija na ufanisi hadi katika ngazi ya Halmashauri. Hatua hii itawezesha kazi za upimaji na upangaji kufanywa na wataalam waliopo katika ngazi ya kanda na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara itaendelea kupeleka watumishi wa sekta ya ardhi katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

110. **Mheshimiwa Spika**, Taifa limeshuhudia ongezeko la migogoro ya ardhi ambayo baadhi yake inasababishwa na watumishi wasio waadilifu. Katika maeneo ya mijini, malalamiko mengi ni yale yanayohusu kiwanja kimoja kutolewa kwa zaidi ya mmiliki mmoja, maeneo ya wazi kujengwa na wamiliki wengine kutozingatia matumizi ya ardhi yaliyoidhinishwa. Wizara imewachukulia hatua za kinidhamu watumishi waliobainika kujihusisha na migogoro hiyo. Hadi Aprili, 2015 watumishi sita wamefukuzwa kazi, tisa wamepewa onyo na wanne wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi. **Nawaagiza watumishi wote wa sekta ya ardhi kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu wa hali ya juu na kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ili kuwaondolea wananchi kero zisizo za lazima.**

Kituo cha Huduma kwa Mteja (*Customer Service Centre*)

111. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara ilianza kutoa huduma kupitia Kituo cha Huduma kwa Mteja (*Customer Service Centre*) katika Makao Makuu ya Wizara. Lengo la Kituo hiki ni kuboresha utoaji wa huduma kwa mpangilio na kwa uwazi unaosaidia kuleta ufanisi katika utendaji wa pamoja ambao unasaidia kupunguza mianya ya rushwa. Hadi kufikia Aprili 2015, Kituo kilipokea wateja takriban **80,000** na kushughulikia masuala mbalimbali yanayohusiana na umiliki wa ardhi. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara itaendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa kuweka mifumo inayorahisisha utendaji kazi.

Huduma kwa Mteja kwa Njia ya Simu (Customer Service Call Centre)

112. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara yangu itaanzisha Kituo cha Huduma kwa Mteja kwa Njia ya Simu. Kupitia Kituo hiki wananchi wataweza kuuliza na kupata majibu ya masuala mbalimbali yanayohusu ardhi kwa kupiga simu au kutuma ujumbe mfupi. Ili kutekeleza azma hii, Wizara itatoa namba maalum za simu kabla ya Septemba 2015 na hivyo, kuwawezesha wananchi kuuliza na kutoa taarifa zinazohusu masuala ya ardhi kwa kutumia simu za mkononi ambayo ni njia yenye gharama nafuu ambazo zitagharamiwa na Wizara.

113. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kuwawezesha watumishi kuhudhuria mafunzo ya aina mbalimbali nje na ndani ya nchi kwa ajili ya kuwajengea uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika mwaka wa fedha 2014/15 jumla ya Watumishi **58** walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi. Watumishi **22** wa taaluma mbalimbali walijiriwa, watumishi **watatu** walibadilishwa kazi baada ya kupata sifa na watumishi **sita** walithibitishwa katika vyeo vyao. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara inatarajia kuwapatia mafunzo watumishi **250** wa kada mbalimbali katika sekta ya ardhi. Kwa kutambua umuhimu wa michezo kwa ajili ya kuimarisha afya za watumishi, Wizara yangu ilishiriki katika mashindano ya SHIMIWI.

Vyuo vya Ardhi

114. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ina vyuo viwili vya Ardhi vilivyopo Tabora na Morogoro. Vyuo hivi vinatoa mafunzo ya Stashahada katika fani za Urasimu Ramani na Upimaji Ardhi, Cheti katika fani za Upimaji Ardhi, Umiliki Ardhi, Uthamini, Usajili na Uchapaji Ramani. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2014/15 Chuo cha Ardhi Tabora kimeanzisha Stashahada katika fani ya Umiliki, Uthamini na Usajili wa Ardhi ambayo itawapa wanachuo sifa ya kujiunga na Vyuo Vikuu. Aidha, Chuo cha Ardhi Tabora kimeboresha mitaala ili kutoa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko la wataalam wa sekta ya ardhi nchini.

115. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 idadi ya wahitimu katika vyuo vya ardhi vya Morogoro na Tabora ilikuwa ni **375**; kati yao wahitimu **204** ni wa Chuo cha Ardhi Morogoro na wahitimu **171** ni wa Chuo cha Ardhi Tabora (**Jedwali Na. 10**). Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara itaendelea kuviimarisha vyuo hivi ili viweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Udhibiti wa UKIMWI

116. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kuelimisha watumishi namna ya kujihadhari na janga la UKIMWI na kuwahamasisha watumishi kupima afya zao. Watumishi waliojitambulisha kuwa wanaishi na virusi vya UKIMWI wameendelea kupatiwa huduma na msaada wa fedha kwa ajili ya dawa na lishe. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara itaendelea kuhamasisha upimaji wa afya na kuendelea kutoa huduma stahiki.

C.CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA ARDHI

117. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi zinazoendelea kufanyika kusimamia sekta ya ardhi nchini, Wizara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- i) Kutopatikana kwa taarifa sahihi za ardhi;
- ii) Migogoro ya matumizi ya ardhi nchini baina ya watumiaji wa ardhi;
- iii) Upungufu wa ardhi iliyopangwa na kupimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo uwekezaji;
- iv) Makundi mbalimbali yanayochukua ardhi ya wananchi kwa ajili ya matumizi mbalimbali kutokulipa fidia kwa mujibu wa Sheria;
- v) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sekta ya ardhi pamoja na sheria zake, taratibu na miongozo iliyopo, haki zao na wajibu wao;
- vi) Uhaba wa wataalamu na vitendea kazi vinavyohitajika ili kukidhi mahitaji ya sekta ya ardhi; na
- vii) Kuwepo kwa watumishi wa sekta ya ardhi wanaosababisha kero kwa wananchi hususan kwenye baadhi ya Halmashauri.

118. **Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yangu nimeainisha mikakati mbalimbali itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/16 na hivyo, kukabiliana na changamoto hizo. Kuhusu changamoto ya migogoro ya matumizi ya ardhi nchini baina ya watumiaji, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kusogeza huduma za usimamizi wa ardhi karibu na wananchi kwa kuanzisha Ofisi 8 za Kanda.

Lengo la hatua hii ni kuongeza ufanisi na kasi ya upangaji, upimaji na utoaji wa hati miliki za ardhi kwa wananchi kama ufumbuzi wa kudumu wa kutatua migogoro ya ardhi nchini.

119. **Mheshimiwa Spika** kuhusu utatuzi wa migogoro inayosababishwa na ukiukwaji wa taratibu za upangaji na umilikishwaji wa ardhi, nilishatoa maagizo kwa Halmashauri zote nchini kuanzisha dawati la kushughulikia migogoro ya ardhi. Kwa wale waliobainika kukiuka masharti ya ajira zao na kusababisha

migogoro, hatua za kinidhamu zimeshaanza kuchukuliwa dhidi yao. Ili kudhibiti wavamizi wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya umma, Serikali itaendelea kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi iliyoidhinishwa na kuchukua hatua stahiki kwa wakiukaji. Kuhusu kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa taarifa sahihi za ardhi, nimeeleza katika hotuba yangu kuwa Serikali imeanza kujenga Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (ILMIS) ambao utatumika kutunza kumbukumbu zote za ardhi.

120. **Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na changamoto inayohusu ulipaji wa fidia, **natoa rai kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Wakala kutenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa mujibu wa Sheria, kabla ya kutwaa ardhi kwa matumizi mbalimbali.**

SHUKRANI

121. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio ya Wizara yangu yametokana na kuwepo kwa ushirikiano kati ya Serikali, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji na Wadau wa Maendeleo zikiwemo taasisi za fedha za kimataifa, nchi wahisani, taasisi zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini. Wadau hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-HABITAT), Shirika la Maendeleo la Ujerumani; na Serikali za Denmark, Sweden, Uholanzi na Uingereza, Marekani, China na Norway.

122. **Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki (Mb), kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia napenda kumshukuru Katibu Mkuu Bw. Alphayo Japani Kidata, na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Selassie David Mayunga kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. Namshukuru Kamishna wa Ardhi, Wakuu wa Idara na Vitengo, Makamishna Wasaidizi na Wasajili Wasaidizi wa Kanda, Wakurugenzi Wasaidizi na viongozi wa taasisi zilizo chini ya Wizara, watumishi na wataalamu wote wa sekta ya ardhi kwa kunisaidia katika kutimiza majukumu yangu kwa ufanisi. Naomba kila mmoja wetu aendelee kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

123. **Mheshimiwa Spika**, mwaka huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Ni wazi kwamba miongoni mwetu wapo waliotangaza kutogombea tena nafasi ya Ubunge. Kwa wale ambao wanatarajia kurudi kwa wananchi kuomba ridhaa yao ya kurudi tena Bungeni nawatakiwa kila la heri. Kipekee niwatakie kila la heri wale wote waliotangaza na wale watakaotangaza nia ya kupeperusha bendera za Vyama vyao katika nafasi ya Urais. Tukumbuke maneno ya Baba wa Taifa kwamba: Rais anaweza kutoka chama chochote, lakini Rais bora atatoka CCM.

C. HITIMISHO

124. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2015/16 Wizara imeazimia kuendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria za Ardhi uliohuishwa mwaka 2013 (*Strategic Plan for Implimentation of Land Laws - SPILL 2013*); na Mpango Mkakati wa Wizara wa miaka mitano (2012/13 - 2016/17) ili kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) na MKUKUTA II ambayo kwa pamoja yanalenga kufikia malengo makuu ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025.

125. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara imejipanga kutayarisha mipango ya kuendeleza miji na vijiji na kusimamia, kupanga matumizi ya ardhi, kupima ardhi, kuhakiki milki, kusajili na kutoa hati ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa milki. **Natoa rai kwa mamlaka na asasi mbalimbali kutoa ushirikiano unaotakiwa kuhakikisha kuwa ardhi inaziwezesha sekta zote ili kufikia malengo ya maisha bora kwa kila Mtanzania.**

D. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

126. **Mheshimiwa Spika**, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu niliyoyaeleza katika hotuba hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kama ifuatavyo:-

127. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii nimejumuisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na viambatisho mbalimbali. Naomba taarifa hiyo na viambatisho vichukuliwe kuwa ni vielelezo vya hoja hii. Aidha, hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Wizara kwa anuani ya **www.ardhi.go.tz** na kwenye **app store** inayoitwa **ardhi tza** inayopatikana kwenye programu za simu.

128. **Mheshimiwa Spika**, natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

129. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Wizara hii.

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/2016

KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana tarehe 19 Mei, 2015, Mjini Dodoma kupokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 na kupitia makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi akiwa na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Angellah Kairuki pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo alieleza Dira na Dhima ya Wizara na masuala yaliyotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho Kamati ilipitia taarifa zifuatazo:-

- (1) Utekelezaji wa kazi za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016;
- (2) Utekelezaji wa kazi za Shirika la Nyumba la Taifa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na mpango wa kazi za Shirika hilo kwa mwaka wa fedha 2015/2016;
- (3) Utekelezaji wa kazi za Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na vifaa vya ujenzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na mpango wa kazi wa mwaka 2015/2016; na
- (4) Utekelezaji wa kazi za Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na mpango wa kazi kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015; wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya ushauri umezingatiwa na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhishwa na hatua zilichokuliwa na Serikali kuondoa tatizo la kuchelewesha kulipa fidia pale Serikali inapotwaa ardhi ya wananchi. Kuanzia mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara imetoa mwongozo kwa mamlaka na Taasisi zote unaoelekeza ya kwamba, ninanukuu:

“Hakuna uthamini utakaoidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali kabla ya Halmashauri, mlipa fidia kuthibitisha uwepo wa fedha za kulipa fidia mwisho wa kununukuu.” Mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeanzisha Mfuko wa Fidia ambao kwa mwaka huu wa fedha umetengewa shilingi bilioni tano kwa ajili ya kulipa fidia pale Serikali inapotwaa ardhi kwa manufaa ya umma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati pamoja na Serikali kuchelewa kushughulikia uvunjaji wa jengo la ghorofa 16 lililoko katika Mtaa wa Indira Gandhi Jijini Dar es Salaam, ambalo Kamati iliitaka Serikali kulivunja mara moja ili kuepusha maafa yanayoweza kutokea endapo litapomromoka. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua stahiki ambazo imechukua na kwamba jengo hilo litavunjwa wakati wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhishwa na hatua za Serikali za kuandaa utaratibu wa kuondoa utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani kwa Mashirika yote ya Umma yatakayojenga nyumba ambazo kwa tafsiri itakayowekwa na Serikali zinahesabiwa kama nyumba za gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua za kumaliza sintofahamu kati yake na Wananchi wa Kigamboni kwa kuweka mazingira wezeshi, ambapo mmiliki wa ardhi katika eneo la Mradi wa ujenzi wa mji mpya Kigamboni atakuwa na fursa ama ya kuuza eneo lake, kukopa benki na kuliendeleza mwenyewe kulingana na *Master Plan* au kuingia ubia na mwekezaji na kwamba sasa mgogoro kati ya Wananchi wa Kigamboni na Serikali umekwisha. Tunaipongeza na kuihimiza Serikali kuharakisha uandaaji wa *Master Plan* ya Mji Mpya ili utekelezaji wa Mradi uanze mara moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kumaliza mgogoro wa muda mrefu uliokuwepo wa Mipaka halisi ya Msitu wa Hifadhi ya Kazimzumbwi na kwamba, uoto wa asili uliokuwa umetoweka baada ya hifadhi kuvamiwa umeanza kurejea. Aidha, Kamati inaihimiza Serikali kumaliza mgogoro wa Shamba la Utumaini lililoko Mafia kwa kulitwaa shamba hilo na kuwaacha Wananchi wa Mafia ambao wameishi katika shamba hilo kwa zaidi ya miaka 48, waendeleo kuishi na kufanya shughuli zao bila kubughudhiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliidhinishwa jumla ya shilingi 85,740,417,000/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 51,585,340,000/= zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 34,154,977,000/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mpaka kufikia mwezi Aprili 2015, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 32,200,205,372/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 21,824,542,602/= zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 10,375,662,770/= kwa ajili ya mishahara. Hakuna fedha zilizopokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na bajeti hiyo iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu, Wizara imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Ardhi na Nyumba; kuanzisha na kusimika mfumo wa pamoja wa kutunza kumbukumbu katika Ofisi za Makao Makuu na Ofisi za Kanda; kuunganisha na kusimika mfumo wa kutunza kumbukumbu na kukadiria kodi ya pango la ardhi na kutoa mafunzo kwa Halmashauri 85; na kuidhinisha ramani zenye viwanja 70,000 kutoka katika mikoa 25.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015. Changamoto hizo ni pamoja na kutokutolewa kabisa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo; uhaba wa Watumishi wa Sekta ya Ardhi kwa ujumla katika ngazi zote kuanzia Wizara, Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya; Watumishi waliopo hivi sasa ni asilimia 24 tu ya mahitaji halisi, hali ambayo inachangia ufanisi hafifu wa Wizara; ufinyu wa pesa zinazotengwa kila mwaka kwa Kitengo cha Mabaraza ya Nyumba, kutokana na ufinyu huu, kasi ya kufungua Mabaraza katika Wilaya mbalimbali imekwama; rushwa katika Vitengo mbalimbali vya Wizara; na mwisho, Nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba kuendelea kuwa ghali kutokana na kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kiasi cha shilingi 83,043,343,000/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 69,584,347,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 13,458,996,000/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi 13,458,996,000/= kinachoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, kinajumuisha fedha za ndani shilingi 10,000,000,000/= na shilingi 3,458,996,000/= kutoka kwa wadau wa maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuonesha juhudi za wazi katika kutenga fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kinachoombwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, kitatumika kutekeleza shughuli mbalimbali za Wizara hiyo ikiwa ni pamoja na kujenga mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi; kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mji mpya wa Kigamboni kupitia Wakala wa Mji mpya wa Kigamboni; na kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Bonde la Msimbazi kama Bustani ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali ya msingi na ya muhimu ambayo shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kimaendeleo, zinafanyika juu yake. Aidha, ardhi ni rasilimali adimu ambayo hushindaniwa na watu au shughuli mbalimbali na hivyo kuifanya iwe na thamani kubwa. Kwa sababu hiyo, ardhi inatakiwa kumilikiwa Kiserikali na Kimila kwa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazokubalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa asilimia 80 ya Wananchi wa Vijijini wanategemea ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi; na kwa kuwa mara nyingi viongozi wa Vijiji huingia Mikataba mibovu na wawekezaji; ni dhahiri kwamba Serikali isipokuwa makini katika suala la kumilikisha ardhi kwa wawekezaji na kutoa elimu kwa Viongozi wa Vijiji, Wananchi wataendelea kuwa maskini na watwana katika nchi yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Fungu 48, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa za Wizara hii ni kuongezeka kwa migogoro ya Mipaka ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Kwa mfano, migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji, Wawekezaji na Wanavijiji, Serikali na Wananchi. Migogoro hii inachangiwa na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutokupimwa kwa maeneo mengi ya makazi ya wananchi, upatikanaji mgumu wa hati miliki za kimila na ucheleweshwaji wa kulipa fidia pale ambapo wananchi wanatakiwa kuhama.

Mheshimiwa Spika, moja ya madhumuni ya kuanzisha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilikuwa ni kupanga matumizi ya ardhi ili kuondoa migogoro baina ya watumiaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa Tume hii, bado migogoro ya ardhi imeendelea kujitokeza katika sehemu mbalimbali nchini, ikichangiwa na kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kutokana na ufinyu wa bajeti, Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeshindwa kufanya tafiti kwa wingi kuhusu masuala ya ardhi hasa katika maeneo yenye migogoro. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Tume ilitengewa shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Tume kutoka bilioni 1.9 hadi bilioni 3.1, kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/16. Matumaini ya Kamati ni kwamba, sasa Tume ya Mipango na Matumizi ya Ardhi itaongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuanzisha utaratibu wa kuwa na ardhi huru kwa ajili ya matumizi ya Serikali na ardhi ya akiba kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na wa nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua inazochukua kuyatwaa mashamba makubwa hapa nchini yaliyotelekezwa. Aidha, Kamati inashauri Serikali isiachie Mamlaka za Halmashauri kuyagawa mashamba haya kwa Wananchi bali isimamie zoezi hilo. Uzoefu umeonyesha kuwa, baadhi ya mashamba yaliyotwaliwa na Serikali, wamegawana Viongozi wakubwa wa Halmashauri na Wilaya na kuwaacha wananchi ambao ndiyo walengwa wakiendelea kubaki na ardhi ndogo.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine wawekezaji wamepewa maeneo makubwa ambayo hawayaendelezi na hivyo kuzusha migogoro na wananchi wanaopakana na maeneo hayo kwani hawana ardhi ya kutosha. Mfano, ni wananchi wa Kijiji cha Lukenge, Wilaya ya Mvomero, ambapo ardhi iliyokuwa Shamba la Mifugo la Serikali imetwaliwa na kugawiwa kwa mwekezaji, yaani *Mtibwa Sugar Company* na kuwaacha Wanakijiji wa Lukenge bila ardhi; hivyo, kusababisha ugomvi kati ya Wafugaji na Wakulima katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, miji mingi hapa nchini imeendelea kukua kwa kasi kubwa bila ya kuwa na uwiano na taratibu za mipango miji. Ukuaji huu umechangia kuwepo kwa makazi yasiyo rasmi (*squatter settlements*) na ujenzi holela hasa katika maeneo ya mijini ambayo yamekuwa na wahamiaji wengi kutoka vijijini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya Mwaka 2008 na Sera ya Maendeleo ya Makazi (2000), zinasimamia ukuaji wa Miji na Majiji na zinatoa dira ya namna gani miji ipangwe kulingana na miundombinu ya eneo husika.

Hata hivyo, Halmashauri za Manispaa na Wilaya zimekuwa zikishindwa kuwapatia wakazi wake huduma mbalimbali zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na kupima viwanja kwa ajili ya makazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kusimamia na kutekeleza Sheria ya Mipango Miji kwani mbali na changamoto ya ukuaji wa kasi ya miji, kumekuwepo pia na ukaidi wa makusudi wa Wananchi kutotii sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha karibuni tumeshuhudia maendeleo makubwa katika ujenzi wa majengo ya ghorofa nchini kwa ajili ya makazi na Miradi mingine. Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 (Sura 191), inazitaka mamlaka zote zinazohusika na kutoa vibali vya ujenzi wa majengo ya ghorofa yatakayozidi ghorofa tano, zihakikishe majengo hayo yanafanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira ili kuepusha maafa yanayoweza kutokea endapo tathmini haitafanyika.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya Watu, Taasisi na Idara za Serikali ama kwa bahati mbaya au kwa makusudi, kupindisha Sheria ya Mipango Miji ni lazima vidhibitiwe kwa nguvu zote. Matukio kama ya ujenzi holela mijini na ujenzi usiozingatia sheria, mara nyingi umesababisha maafa makubwa ikiwa ni pamoja na kuporomoka kwa baadhi ya majengo na mafuriko yasiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Oktoba 2008, Serikali ilitoa tamko rasmi kupitia GN No. 229, kuhusu mpango wa kujenga Mji wa Kisasa eneo la Kigamboni, ambao unatarajiwa kuwa sehemu ya kitovu cha huduma za kijamii, kiuchumi na teknolojia cha Jiji la Dar es Salaam. Aidha, uendelezaji huu unatarajiwa kuuwezesha Mji mpya wa Kigamboni kushindana na Miji mingine duniani katika kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje.

Mheshimiwa Spika, toka mchakato wa kuendeleza Mji wa Kigamboni uanze, kumekuwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na malalamiko kutoka kwa wakazi wa eneo husika kwamba, mchakato wa uundaji wa Mpango Kabambe wa Mji Mpya haujazingatia Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya Mwaka 2007.

Kamati yangu ilitembelea nchi za Falme za Kiarabu hususan Dubai na Abu Dhabi na kujionea nchi hizo zilivyopiga hatua katika uendelezaji wa miji kwa kuandaa *Master Plan* na kuzisimamia kikamilifu. Aidha, nchi hizo zimefanikiwa sana kutokana na kupunguza urasimu katika umilikishaji wa ardhi na utoaji wa vibali vya ujenzi. Kamati inaishauri Serikali kuondoa urasimu usio wa lazima na kuleta tija katika uendelezaji wa miji yetu.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoielezwa hapo awali, katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Bunge lako Tukufu liliidhinisha shilingi 34,154,977,000/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 20,850,000,000/= zilikuwa fedha za ndani na shilingi 13,304,577,000/= fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Aprili 2015, hakuna fedha zozote za maendeleo zilizopokelewa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutotolewa kwa fedha za Miradi, ni wazi kwamba Miradi mingi haitaendelezwa kwa wakati kama ilivyopangwa na hivyo kuchelewesha faida ambazo nchi inatarajia kuzipata baada ya kukamilisha Miradi inayopangwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza jitihada za makusudi katika kuhakikisha fedha zinazotengwa zinapatikana kwa wakati ili kutekeleza Miradi kama hii yenye tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa lilianzishwa kwa Sheria Na. 2 ya Mwaka 1990, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005. Jukumu la msingi la Shirika hili ni kujenga na kuwezesha ujenzi wa nyumba za makazi na majengo ya biashara kwa ajili ya matumizi ya Wananchi na Serikali pia.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu lake la msingi, Shirika la Nyumba limeendelea na ujenzi wa Miradi saba yenye jumla ya nyumba 737 na kuanza matayarisho ya ujenzi wa Miradi 38 yenye nyumba 4,118 za gharama nafuu, za kati na za juu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za wazi za Shirika katika kujenga nyumba kwa ajili ya kuuza, bado nyumba hizo zinaonekana kuwa ghali kutokana na kuwekewa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Kwa mfano, kwa sasa nyumba za bei ya chini zinazwa shilingi milioni 46.9 kujumuisha na VAT, ambapo zingezwa shilingi milioni 39.8 bila VAT, ikiwa ni tofauti ya shilingi milioni 7.1.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba, Shirika limeweka lengo la kujenga nyumba 15,000 ifikapo mwaka huu, ili kuwawezesha wananchi wengi hasa wa kipato cha chini na kati kumiliki nyumba zinazojengwa na Shirika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha, ione umuhimu wa kusitisha utozaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Nyumba za Shirika zinazojengwa kwa ajili ya kuuzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuliondolea Shirika la Nyumba la Taifa ushuru wa forodha pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), kwa vifaa vya ujenzi vinavyoagizwa kutoka nje.

Aidha, Kamati inaendelea kuitaka Serikali kuzingatia agizo la Bunge la kutoruhusu kabisa, kuuza nyumba za Shirika la Nyumba za zamani kwa wanaodai wapangaji wa muda mrefu, ambazo nyingi ni nyumba zilizotaifishwa na badala yake Serikali kuhamasisha Wananchi na Wadau hao kununua nyumba mpya zilizojengwa hivi sasa na shirika hili.

Mheshimiwa Spika, kufuatia malalamiko ya Wadau wengi wa Shirika la Nyumba akiwemo Mbunge wa Ilala, Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Temeke, kuhusu ongezeko kubwa la kodi ya pango kwa nyumba za Shirika la Nyumba, Kamati inaishauri Serikali kutatua tatizo hili kwa mujibu wa sheria huku ikizingatia hasa wapangaji wazee na wastaafu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yapo masuala mengine ambapo Kamati inaishauri Serikali kuyafanyia kazi. Masuala hayo ni pamoja na Serikali ianzishe utaratibu wa kuhamisha ajira za Watumishi wa Sekta ya Ardhi katika Halmashauri zote nchini kuwa chini ya Serikali Kuu; Serikali iendelee kuwachukulia hatua kali za kinidhamu Maafisa wa Wizara wanaotuhumiwa kuvunja taratibu za kazi; Serikali iwekeze kwenye miundombinu katika maeneo yanayojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa ili kupunguza gharama za ujenzi na hivyo kuleta unafuu kwa wapangaji na wanunuzi wa nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea Miradi ya Utunzaji wa Kumbukumbu za Ardhi, yaani *Intergrated Land Information System* nchini Uganda na kujionea ufanisi wake na jinsi Uganda ilivyopiga hatua katika kupunguza migogoro ya ardhi na kuhakikisha kuwa, wananchi wa Uganda wanapatiwa hati za kumiliki ardhi bila usumbufu wala urasimu. Tunaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za kuanza kufanya majaribio ya Mradi huu katika Wilaya za Kilombero na Ulanga kama Wilaya za majaribio kabla ya kuusambaza nchi nzima. Matarajio ya Kamati ni kwamba, Mradi huu ukifanikiwa utaleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, nawapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu, kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge - Ndugu Charles Mloka na Katibu wa Kamati - Ndugu Gerald Magili, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii. Mheshimiwa Halima! *(Makofi)*

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI MHE. HALIMA JAMES MDEE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU BAJETI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI JUU YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa Mwaka wa Fedha 2015/16.

Mheshimiwa muhtasari wa mambo ambayo yatakuwepo kwenye hotuba yangu ni kama yafuatayo, lakini kwa sababu ya muda nitazugumzia machache:-

Kwanza, tathmini ya kazi za Upinzani katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa miaka mitano iliyopita.

Pili, Vigogo wa CCM wanavyohusika na uporoji wa ardhi.

Tatu, wimbi la unyakuzi wa ardhi ya Tanzania na mfano mahususi utatolewa kwa Wawekezaji wa Dongote na ukiukwaji wa Sheria za Ardhi.

Nne, migogoro ya ardhi inayoashiria kushindwa kwa Chama cha Mapinduzi.

Tano, mgogoro wa ardhi katika Kijiji cha Kifanya Halmashauri ya Mji wa Njombe, kwako Mheshimiwa na mimi nimekukumbuka mwaka huu.

Sita, mgogoro wa ardhi kati ya CDA na Wananchi wa Manispaa Dodoma. Hali kadhalika Msalato na Wizara ya Uchukuzi.

Saba, migogoro ya Ardhi baina ya wananchi na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Nane, jeshi linavyohusika na uporaji wa ardhi, mifano hapa itatolewa Kijiji cha Tondoroni Mkoa wa Pwani na Kijiji cha Ihumwa Dodoma.

Tisa, uvamizi wa ardhi ya TAZARA.

Kumi, wamiliki wa mashamba makubwa ambao hawalipi kodi ya ardhi.

Kumi na moja, kodi inayopotea kutokana na ukiukwaji wa Sheria za Ardhi.

Kumi na mbili, Soko la Nyumba na umuhimu wa nyumba katika kukuza uchumi.

Kumi na tatu, Master Plan ya Jiji la Mwanza na Arusha.

Kumi na nne, Serikali ya CCM ilivyoshindwa kusimamia Mipango Miji.

Kumi na tano, Serikali ya CCM ilivyoshindwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2010 - 2015.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Mabosi wangu na Wananchi wa Kawe, kwa imani kubwa waliyoonyesha kwangu na kwa ushirikiano mzuri wanaoendelea kunipa katika kazi zangu za Kibunge na Kijamii. Kupitia kwao, nimeingia katika ramani ya Tanzania na kupitia kwao pia nimeingia katika Ramani ya Dunia. Ombi langu kwenu na kwa Wananchi wote wa Dar es Salaam, mjitokeze kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Wapiga Kura pindi litakapopita, kwa kuwa Taifa zima linawategemea wananchi wa Dar es Salaam kuongoza mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya kazi za Upinzani katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa miaka yote mitano ya uhai wa Bunge hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itakumbukwa kwa kazi nzuri ya kutoa mawazo na fikra mbadala kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa majukumu yaliyopo chini ya Wizara hii. Ushauri ambao ulibezwa sana, lakini katika hali ya kushangaza ni ushauri huo huo uliobezwa ndiyo unaotumiwa sasa na wanaoitwa watia nia wa Urais wa CCM, eti na wao wana dhamira, nia na uthubutu wa kuyatekeleza. *(Makofi)*

Kwa uchache tulisema nini? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ilikemea na kulaani uporaji na ugawaji holela wa ardhi ya Watanzania kwa Mataifa ya nje chini ya usimamizi wa Serikali na kwa hila au kisingizio cha uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilikemea na kupinga ufisadi wa ardhi uliokuwa unafanywa na Viongozi wa Serikali na Chama cha Mapinduzi. Tuliwataja kwa majina na maeneo, lakini mpaka sasa japokuwa Mheshimiwa Lukuvi anajitahidi tahidi, lakini hajafika pale nilipotaka. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilifanya uchambuzi wa matukio ya ukiukwaji wa Sheria ya Ardhi Na. 4 na Na. 5 ya Mwaka 1999 kulikopelekea chimbuko la migogoro mingi ya ardhi. Kambi Rasmi ya Upinzani ilihoji vilevile juu ya Mradi wa viwanja 20,000; Mradi ambao ulitawaliwa na wizi, ufisadi na udanganyifu mkubwa na mpaka sasa hakuna taarifa yoyote juu ya Mradi husika, licha ya Kamati ya Bunge ya ardhi na Maliasili nayo kuhoji juu ya jambo hili. Kambi Rasmi ya Upinzani ilihoji juu ya migogoro isiyokwisha baina ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Wanavijiji wanaoishi pembezoni mwa Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, iliitaka Serikali kushughulikia migogoro mikubwa ya ardhi baina ya Wakulima na Wafugaji ambayo kwa nyakati tofauti imepelekea umwagaji damu. Hali kadhalika, Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka ushauri juu ya namna bora ya kuliboresha Shirika la Nyumba la Taifa ili liweze kutoa huduma bora kwa wananchi wa kada zote.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni vilevile, ilihoji juu kuendelea kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi, jambo ambalo limesababisha wananchi kuendelea kuishi katika mazingira duni na hivyo kuhatarisha usalama wao na kutweza utu wao. Tuliitaka Serikali kuanzisha Mamlaka ya Udhubiti wa Kodi za Nyumba (*Real Estate Regulatory Authority*), ili kuratibu, kuweka viwango na miongozo ya kodi za nyumba ili kuwaondolea wananchi wapangaji wa nyumba adha kubwa ya gharama kubwa za pango zisizo na viwango. Hali kadhalika, kuiongezea Serikali mapato makubwa kupitia Sekta ya Nyumba.

Mheshimiwa Spika, tulitaka ukaguzi ufanyike kwenye majengo yote yaliyojengwa na *Ladha Construction Limited*, aliyehusika na ujenzi wa jengo katika Mtaa Indira Gandhi – Dar es Salaam, lililoanguka na kuua watu wasiopungua 21. Tuliitaka pia Serikali ibomoe ghorofa pacha lililopo kwenye Kiwanja Namba 1662, Kitalu 75, Mtaa wa Indira Gandhi, miaka miwili imepita tunasubiri Watanzania wengine wafe ili tuchukue hatua. Sasa nasikia wanasema wanavunja, nataka ndani ya miezi hii, kabla haujaondoka kwenye wadhifa wako hilo jengo lidondoke.

Mheshimiwa Spika, Vigogo wa CCM wanavyohusika na uporaji wa ardhi: Kigogo anayehusika hapa ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Ndugu Leonidas Gama. Tumesema hivi, tutawataja kila siku mpaka mbadilishe tabia. Nilihakikishie Bunge hili, UKAWA ukiingia madarakani tutachukua hatua stahiki kurudisha ardhi ya umma.

Kigogo huyu anahusishwa na uporaji wa ardhi ya Wilaya ya Rombo, ambao fedha za Halmashauri shilingi milioni 168 zililipa fidia wananchi kwa madhumuni ya kupata eneo la uwekezaji. Katika hali ya kushangaza, ardhi ya umma iliyolipiwa fidia kwa fedha za umma, ilianzishwa kampuni binafsi ya *Jun Yu Investment International Company Limited*. Wanahisa katika kampuni husika wakiwa Raia wa China wawili wenye hisa 48,000 na mwingine 49,000, huku mtoto wa Mkuu wa Mkoa, Bwana Muyanga Leonidas Gama, akiwa na hisa 3,000.

Mheshimiwa Spika, habari tulizonazo ni kwamba, Mkuu wa Mkoa anamiliki hisa 20,000 kimya kimya ambazo zimefichwa kwenye hisa za Wachina hao katika Mkataba wa siri uliofichwa. Katika hali ya kushangaza, Halmashauri ya Rombo ambayo iliwekeza fedha zake shilingi milioni 168 haitambuliwi na wala haina hisa hata moja katika Kampuni hiyo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa za kiintelijensia ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, zinaonyesha kwamba wawekezaji hao wa Kichina walilipa shilingi milioni 500 kama fidia kwa wananchi katika ardhi hiyo, ambayo tunasema Halmashauri ya Rombo ilishalipa shilingi 168 milioni, fedha ambayo mpaka sasa haijulikani iko wapi! Kama hiyo haitoshi, Kigogo huyu pia anahusishwa na tuhuma za kutaka kufanya ufisadi katika eneo lililopo Kilacha. Hili eneo linagusa Jimbo la Vunjo kwa Mheshimiwa Mrema na Rombo, lenye ukubwa wa hekta 2700.

Kada huyu wa CCM anatajwa tena katika mgogoro wa ardhi unaofukuta, unaokihusisha kiwanja chenye Hati Namba C.T. 056035 Mawenzi - Moshi Manispaa, kilichokuwa chini ya miliki ya *The Registered Trustees of Mawenzi Sports Club*. Kiwanja hiki kilikuwa na hatimiliki ya miaka 33 iliyokwisha mwaka 1974.

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Mkoa huyu amekuwa akishirikiana na matapeli ama madalali ama wezi wa ardhi kama anavyowaita Mheshimiwa Lukuvi, wanaotambulika kwa majina ya Amratlal N. Pattn na Hittesh H. Solani, wanaojitambulisha kama wadhamini wapya, baada ya kikao cha makabidhiano kilichofanyika tarehe 5 Januari, 2008 mbele ya uwepo wa wadhamini wa awali, yaani Ndugu Devchad Nathu Shah na Mohamedali Sharriff.

Mheshimiwa Spika, taarifa za uhakika ambazo Kambi ya Upinzani inazo, Ndugu Devchad Nathu Shah alifariki dunia tangu mwaka 1979, wakati Ndugu Mohamed Shariff alifariki tangu mwaka 1998. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji inakuwaje wadhamini waliofariki mwaka 1979 na mwaka 1998 wakae tena kwenye kikao cha Januari 2008?

Kama hiyo haitoshi, matapeli haya yakijua wamiliki halali walishafariki toka mwaka 1979 na 1998 waliendelea kupeleka kumbukumbu za *Returns of Trustees* za miaka 2000 - 2008, zote zikiwa zimewasilishwa RITA kwa mkupuo mwaka 2012 zikiwa na saini za marehemu!

Mheshimiwa Lukuvi kama umeanza ngoma ndiyo kwanza mbichi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza mambo yafuatayo yafanyike:-

Moja, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, azuie haraka iwezekanavyo mchakato huu haramu kama bado hati haijatolewa na kama hati mpya imetolewa, tunamtaka Rais atumie mamlaka yake kubatilisha hati husika.

Mbili, Serikali ibatilishe michakato haramu inayoendelea katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo na Vunjo.

Tatu, Rais Jakaya Mrisho Kikwete amwajibishe mara moja Kiongozi huyu kwa kutumia madaraka yake vibaya na kujiingiza kwenye biashara chafu.

Nne, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imchunguze Kiongozi huyu sambamba na Watendaji wote wa Serikali waliohusika kwenye uporaji huu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wimbi la unyakuzi wa ardhi Tanzania, uwekezaji wa Dangote na Ukiukwaji wa Sheria ya Ardhi: Najua huyu ni kigogo tajiri namba moja msilogope.

Mheshimiwa Spika, suala la unyakuzi wa ardhi Barani Afrika na hususan Tanzania, ni suala ambalo limekuwa likizungumzwa na Kambi ya Upinzani kwa kipindi chote cha miaka mitano ya uhai wa Bunge hili.

Kudhihirisha umuhimu wa jambo hili, Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iliyowasilishwa hapa Bungeni mapema mwaka huu, ilieleza namna suala la unyakuzi wa ardhi linavyojadiliwa kwa kina katika Vikao vya Kamati na Bunge la Afrika na Bunge husika kuazimia Afrika kuwa na mikakati bora katika kushughulikia suala la ardhi kwa manufaa ya Waafrika. Vilevile nchi moja moja zilitakiwa ziweke mikakati ya kuboresha sheria na taratibu za ugawaji wa ardhi kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, wakati Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ikiyjadili haya, hivi karibuni tumeshuhudia bilionea namba moja Afrika, Alhaji Aliko Dangote, akikabidhiwa hekta 2,500 ama ekari 6,600, eneo la ufukwe wa Bahari ya Hindi na Mwenyekiti wa Kijiji cha Mgawo, Kata ya Maumbu, Wilaya ya Mtwara Vijijini, ili ajenge bandari itakayotumika kusafirisha saruji yake kutoka katika kiwanda chake cha saruji kilichoingwa katika Kijiji cha Msijute kwenda ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa Serikali kutoa ardhi kwa kubadilishana na ujenzi wa shule na hospitali. Hii haina tofauti na kubadilishana dhahabu na kipande cha kanga na haitofautiani na wale waliopokea vipande vichache vya kaniki wakawauza mababu zetu utumwani.

Hivi ni kweli Serikali imeshindwa kutoa huduma za jamii kwa Wananchi wake hivyo inagawa ardhi yetu ili iwezeshe na mgeni kutoa huduma hizo? Hii ni aibu na fedheha ya mwaka kwa Taifa!

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi imetoa ukomo wa mamlaka ya Halmashauri ya Kijiji kugawa ardhi. Ardhi inaweza kutolewa baada ya kuruhusiwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji na hata huo Mkutano Mkuu wa Kijiji hauna mamlaka ya kugawa zaidi ya ekari tano. Hata kama mmezima umeme tunasonga tu!

Nashukuru Mheshimiwa Lukuvi umeleta ...

SPIKA: Utaratibu wetu umeme ukizimika unaendelea humu ndani. Endelea!

MHE. HALIMA JAMES MDEE - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI JUU YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, sheria za nchi zinasema hata Mkutano Mkuu wa Kijiji ambao umepewa ruhusa ya kuruhusu watu walime kwenye maeneo yao, hauna mamlaka ya kugawa zaidi ya ekari mia tano. Kigogo huyu amepewa ekari 6,600, tena kwenye Wilaya ambayo anatoka Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili yafuatayo:-

- (i) Je, Waziri wa Ardhi anafahamu kinachoendelea Mtwara?
- (ii) Anadhani utaratibu uliotumika kumpatia ardhi ya ujenzi wa bandari ulizingatia matakwa ya kisheria au zile zilikuwa ni show za magazetini tu baina ya Mwenyekiti wa Kijiji na Bilionea huyo?

(iii) Je, kulikuwa na mahitaji halisi kutoa ya ekari 6,600 ya ardhi ya Wananchi kama hoja ilikuwa ni kujenga bandari?

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi na ishara ya kushindwa kwa Chama cha Mapinduzi. Kushindwa kwa Chama cha Mapinduzi kunatokana na ukweli kwamba, chanzo cha migogoro mingi kunatokana na kushindwa kufanya maamuzi kwa wakati. Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge ilibainisha kwamba, katika mapitio ya nyaraka mbalimbali waligundua kuna migogoro ambayo ilianza toka mwaka 1966 haijapatiwa ufumbuzi mpaka sasa; yaani miaka 49 iliyopita. Migogoro mingine ilianza miaka ya themanini haijatatuliwa mpaka sasa. Hata katika maeneo ambayo Wananchi wamekuwa wateja wazuri sana wa Chama cha Mapinduzi, mateso ni yale yale!

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tanga ambao kwa kipindi kirefu sana Wananchi wake wamekuwa waadilifu na wateja wazuri wa Chama cha Mapinduzi kwa kukipa ushindi unaoitwa wa kishindo katika chaguzi mbalimbali, imeshindwa kurejeshewa heshima husika kwa Chama hiki kushindwa kabisa kuyafanyia utekelezaji maamuzi yaliyofanyika mwaka 1985, yanayohusiana na ardhi yenye ukubwa wa hekta 15,612, ambayo yalikuwa yanahusisha Mashamba ya Mamlaka ya Mkonge ambayo yangenufaisha Wilaya za Muheza, Korogwe, Lushoto na Pangani.

Mheshimiwa Spika, ninapowasilisha hoja hii, baadhi ya Wanakijiji katika Vijiji vya Mgome, Mpapayu, Kigongomawe na Kwamnyefu, waliokuwa mstari wa mbele kupigania haki yao, wamebambikiziwa kesi za mauaji na wengine mpaka sasa wapo Gereza la Maweni.

Mheshimiwa Spika, tunashangaa mtia nia mmoja wa Urais kutoka Mkoa wa Tanga, ambaye hatujawahi kumsikia hata siku moja akitetea masuala ya ardhi ya mkoa wake na Tanzania kwa ujumla, anawahadaa Wananchi eti na yeye anaguswa na kero na migogoro ya ardhi atatua akiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri wa Ardhi alieleze Bunge hili Tukufu ni lini anatarajia kuimaliza migogoro hii sugu? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imetoa uamuzi gani kwa kufuatia adha kubwa na mateso wanayokumbana nayo wananchi wa Tarafa ya Olboloti Kibaya, Kiteto, ambapo wananchi wanalalamikia kamata kamata inayofanywa na Askari Polisi, inayokwenda sambamba na kuwachapa viboko na kuwalazimisha kutafuna mbegu za mahindi na alizeti na kuzimeza.

Nashukuru Mheshimiwa Waziri ametoa mwelekeo wa hapa, naamini hilo suala litapatiwa ufumbuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la Msitu wa Kazimzumbwi siyo geni. Kumbukumbu zinaonyesha kwamba, toka mwaka 1994, wananchi hawa wanahangaika bila mafanikio. Barua toka Ofisi ya Rais ya tarehe 10 Juni 2008, yenye kumbukumbu Na. CEA 110/302/IV/01 kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, juu ya malalamiko ya wakulima hao, pamoja na mambo mengine, inakiri kwamba, Hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi ilianzishwa na Gavana E. F. Twining, kwa Tangazo la Serikali Na. 306, lililochapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Septemba 1954. Tangazo husika liliweka Mipaka ya Hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi kwa kutaja vipimo vya maeneo ya Mipaka. Nakala ya tangazo imeambatanishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mbinu za kitapeli na uharamia dhidi ya Wananchi, Wizara ya Maliasili na Utalii imekuwa ikitumia GN. Na. 156 ya Mwaka 1997, iliyochapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 20 Mei 1997, ambayo inasema: *The Kazimzumbwi Forest Reserve (Removal of unlawful occupants and cessation of unlawful activities) Rules of 1997*, wakidai Wananchi hao wamevamia msitu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa amri hii kwa tafsiri tu, unawahusu wale wananchi walio ndani ya Hifadhi. Wizara ya Maliasili na Utalii inatumia ubabe wa amri hii pasipokuwa na ujasiri wowote wa kufanya rejea ya tangazo lililoweka mipaka ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ambazo Kambi ya Upinzani inazo ni kwamba, kuna mchezo mchafu uko nyuma ya pazia.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa heshima ya aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ukonga, Marehemu Eugene Mwaiposa, aliyepambana na hili suala mpaka umauti unamkuta, kuliangalia suala hili kwa jicho la ziada. Kuna upotoshwaji mkubwa sana unafanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii na mbaya zaidi hata Kamati yako ya Bunge, Ardhi na Maliasili inapotoshwa pia na Wizara.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Wizara ya Ardhi, ilitoa mapendekezo mazuri, lakini inaonekana kuna ukinzani kati ya Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepokea taarifa ya migogoro mbalimbali ya ardhi inayolihusu Jeshi kuvamia maeneo ya Wananchi. Kutokana na ufinyu wa muda, tutaongelea migogoro miwili; Kijiji cha Tondoloni – Kisarawe, Mkoa wa Pwani na Kijiji cha Ihumwa, Mkoa wa Dodoma ambayo inafukuta kwa sasa.

Meshimiwa Spika, ni matarajio yetu, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Wizara ya Ulinzi, itatumia busara ya hali ya juu kumaliza fukuto hili. Hatuwezi kuruhusu walinzi wetu wa amani ambao tunawategemea wawe chanzo cha uvunjifu wa amani katika nchi. Taarifa ya kina na viambatanisho vipo kwenye taarifa kuu na Wizara niliipatia hii taarifa mapema sana, nikiamini mtakuwa mnatoa mwelekeo leo pamoja na Wizara ya Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, wamiliki wa mashamba makubwa hawalipi kodi. Wakati migogoro ya ardhi ikifukuta nchi nzima kutokana uhaba wa ardhi kwa matumizi ya shughuli za kilimo na ufugaji, imebainika wamiliki wengi wa mashamba makubwa, wamekuwa wakiikosha Serikali mapato kwa kutolipa kodi ya ardhi kama matakwa ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 yanavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2013, kwa kutembelea mashamba 964 yenye ukubwa wa ekari milioni 3.7, umebainisha kwamba, wamiliki wa mashamba 642 kati ya mashamba 964 yaliyotembelewa walishindwa kuthibitisha kama wamelipa kodi ama la katika kipindi cha mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 33 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999, kinatamka kwamba, mwenye hati miliki anatakiwa pamoja na masharti ya vifungu vingine vya sheria, kulipa kodi ya mwaka kama inavyoelekezwa na Sheria ya Fedha za Umma (*Public Finance Act*). Kati ya shilingi bilioni 3.7 zilizotakiwa kukusanywa katika Mashamba hayo kama kodi, Serikali iliambulia milioni 130 tu, yaani asilimia 3.5 ya kodi yote iliyotakiwa kukusanywa. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kuwafuatilia wamiliki hawa wa mashamba makubwa ambao hawalipi kodi ya ardhi na kuchukua hatua stahiki za Kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kazi inayofanywa na Wizara ya Ardhi yenye madhumuni mema ya kuendeleza Jiji la Mwanza na Arusha. Hali kadhalika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba, Wizara ya Ardhi imeingia makubaliano na kampuni ya *Singapore Cooperation Services*, ambayo imepewa jukumu la kutoa ushauri wa kitaalam wa uendelezaji wa Jiji la Mwanza na Arusha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano ya awali, gharama za utengenezaji wa *Master Plan* ya Jiji la Mwanza ilikuwa Dola milioni 4.1, yaani shilingi bilioni 8.2 bila kujumuisha kodi, wakati Jiji la Mwanza makubaliano yalikuwa Dola milioni 4.5, yaani shilingi bilioni tisa bila kujumuisha kodi. Katika hali ya kushangaza, katika Jiji la Mwanza gharama zikaongezeka kufikia Dola milioni 4.4, ambayo ni bilioni 8.9, hali kadhalika Jiji la Arusha gharama zikaongezeka kufikia Dola milioni 4.9, yaani bilioni 9.8.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili Tukufu sababu ya ongezeko hilo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 4.1 cha makubaliano baina ya Wizara ya Ardhi na Mtaalam Mwelekezi kuhusiana na suala la kodi, ilikubalika kwamba, litakuwa ni jukumu la Mshauri Mwelekezi kulipa kodi na tozo kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za nchi.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kushangaza, *invoice* ya tarehe 18 Februari 2015 toka kwa Mshauri Mwelekezi kwenda Wizara ya Ardhi, inayodai malipo kwa ajili ya hatua ya kwanza ambayo ni asilimia 15 ya fedha kama walivyokubaliana kwenye mkataba, inaonyesha kwamba, kodi (*local taxes*), siyo tena jukumu la Mshauri Mtaalam huyo, bali ni jukumu la Serikali ya Tanzania!

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu kwa kinagaubaga ni lini na kwa mkataba upi jukumu la kodi lilihama kutoka kwa Mshauri Mtaalam kwenda kwa Serikali ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa pia kwamba, hata hiyo fedha asilimia 15 iliyolipwa, ililipwa kabla kazi ya hatua ya kwanza haijakamilika. Natarajia Mheshimiwa Waziri atakapokuja atatueleza kwa kina sakata hili, ili kuweza kuondoa sintofahamu ambayo ipo.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeshuhudia wanaojiita wafia nia kwa mbwembwe nyingi na kama kawaida yao wakiwaahidi Watanzania maziwa na asali! Cha kushangaza, wafia nia wote ambao wakiwa mbele ya Bunge lako Tukufu wamekuwa mstari wa mbele kutetea kile wanachokiita mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya CCM, wakati wanatangaza nia huko mitaani, wanageuka ghafla Wapinzani kwa kukosoa ufanisi wa utekelezaji wa kazi za Serikali hiyo hiyo wanayoiongoza! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ni kutapeliwa, Wananchi wa Tanzania wametapeliwa ile mbaya na Serikali hii ya CCM, kwa kuwa mambo waliyoahidi kwa Wananchi katika Sekta ya Ardhi na Makazi, ahadi nyingi zimekuwa ni ngonjera za utekelezaji tu! Hizi mbwembwe za Waziri leo ni joto la uchaguzi tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inawaonya wagombea Urais wa CCM, ambao walikuwa Serikalini na wakatamia nafasi zao kuwasababishia Watanzania umaskini uliokithiri na sasa wanaufanya umaskini wa Watanzania kama mtaji wao wa kisiasa. Hivi inaingia akilini; hivi mmewageuza Watanzania kuwa ni mazezeta kabisa kiasi cha kuwadanganya waziwazi namna hiyo?

Mheshimiwa Spika, ni kwa msingi huo, Kambi ya Upinzani Bungeni inawasihi wananchi, *in a very serious note*, wapime hoja za Upinzani kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya Awamu ya Nne, ili wajue ni nani kati ya UKAWA na ni nani kati ya hao wanaojipitishapitisha huko nje wanastahili kupewa ridhaa ya kuongoza Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na nakushukuru sana. (*Makofi*)

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI MHE. HALIMA JAMES MDEE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU BAJETI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda dhidi ya hila na mbinu za maadui zangu za kutaka kudhoofisha harakati zangu za ukombozi wa taifa hili, na kunipa nguvu na maarifa zaidi ya kusonga mbele. Pili napenda kuwashukuru Makamanda wote wa CHADEMA kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA Taifa (BAWACHA). Napenda kukiahidi chama changa CHADEMA, na wananchi wote wapenda mageuzi kwamba, nitaitumikia nafasi hii ya uenyekiti wa BAWACHA Taifa kwa uadilifu mkubwa na kwa moyo wangu wote.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wapiga kura wangu – wananchi wa Kawe kwa imani kubwa walioonesha kwangu na kwa ushirikiano mzuri wanaoendelea kunipa katika kazi zangu za kibunge na kijamii. Kupitia kwao nimeingia katika ramani ya Tanzania na kupitia kwao pia nimeingia katika ramani ya Dunia. Ni matumaini yangu kwamba iwapo chama changu kitaniteua kuwania tena Ubunge katika Jimbo hilo, hamtaniangusha. Ombi langu kwenu na kwa wananchi wote wa Dar es Salaam, mjitokeze kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Wapiga kura pindi litakapopita huko kwa kuwa Taifa zima linawategemea wananchi wa Dar es Salaam kuongoza mabadiliko. Hivyo makamanda wa Dare es Salaam, naomba tukaze buti tusije tukatia aibu katika uchaguzi wa Oktoba, 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uhai wa Bunge hili la Kumi unaelekea ukiongoni, hii itakuwa ni hotuba yangu ya mwisho katika Bunge hili nikiwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hata hivyo, namalizia muda wangu wa utumishi nikiwa na furaha kubwa kwani kwa muda wote wa miaka mitano ya uhai wa Bunge hili niliitendea haki nafasi yangu ya Waziri Kivuli wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nadhani watanzania waliona jinsi Kivuli changu kilivyomfunika aliyekuwa Waziri mwenye dhamana wakati huo Mhe. Profesa Anna Tibaijuka.

Mheshimiwa Spika, namalizia utangulizi wangu kwa kuwasih wananchi wote kutumia fursa hii ya maboresho ya Daftari la Wapiga Kura, kujiandikisha na kutumia haki yao ya kidemokrasia ipasavyo ili kuwachagua madiwani, wabunge na Rais watakaopendekezwa na UKAWA, ili kuuondoa utawala wa CCM ambao umewafanya watanzania kuwa masikini kwa miaka yote 53 ya uhuru.

2. TATHIMINI YA KAZI ZA UPINZANI KATIKA WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MIAKA MITANO ILIYOPITA (2010 – 2015).

Mheshimiwa Spika, Kwa miaka yote mitano ya uhai wa Bunge hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itakumbukwa kwa kazi nzuri ya kutoa mawazo na fikra mbadala kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa majukumu yaliyopo chini ya Wizara hii. Hata hivyo, kutokana na ugumu wa Serikali hii ya CCM wa kukiri udhaifu, ilibeza sana ushauri mzuri wa Kambi Rasmi ya Upinzani uliofanyiwa utafiti na hivyo kuacha mambo mengi kuendelea kuwa hovyoo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itakumbukwa kwa kuibua kasoro na matatizo mengi chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa lengo la kuitaka Serikali ambayo kimsingi ndiyo yenye dhamana na yenye mamlaka ya kukusanya kodi za watanzania itatue kasoro na matatizo hayo ili wananchi waweze kunufaika na rasilimali ardhi yao na kuishi kwenye nyumba zenye staha kwa mustakablali mwema wa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Kwa faida ya wananchi na wahanga wa migogoro ya ardhi, napenda kuchukua fursa hii kutaja baadhi ya masuala muhimu kuhusu ardhi nyumba na maendeleo ya makazi ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliyaiibua na kutaka yashughulikiwe na Serikali:

- i. Kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya awamu ya nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilikemea na kulaani uporaji na ugawaji holela wa ardhi ya watanzania kwa mataifa ya nje chini ya usimamizi wa Serikali kwa hila au kisingizio cha uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliibua jambo hili kutokana na taarifa za kitafiti zilizofanywa na taasisi ya hapa nchini ya HAKIARDHI ambayo pamoja na mambo mengine imeonyesha kwamba kati ya migogoro ya Ardhi, **1,825** iliyoripotiwa mwaka 2011, migogoro **1,095** ilikuwa inahusu wawekezaji wakubwa. Halikadhalika, tafiti zilizofanywa hivi karibuni na taasisi za kimataifa zikiongozwa na **'The International Land Coalition (ILC)'** zinazo-onyesha kwamba kuna mikataba mikubwa zaidi ya **1,217** ya utoaji ardhi kwa masuala ya kilimo takriban hekta milioni **83.2** imeridhiwa au iko katika mchakato wa kuridhiwa kati ya mwaka 2007-2012.

Mheshimiwa Spika, Bara la Afrikaambalo ndio mlengwa mkuu wa mkakati huu wa uporaji wa ardhi linaongoza kwa kuwa na "mikataba" **754** inayojumuisha eneo lenye ukubwa wa hekta milioni **56.6**, ikifuatiwa na Bara la Asia lenye hekta **17.7** milioni, huku Bara la Amerika ya kusini likishika nafasi ya tatu kwa kujumuisha ardhi yenye ukubwa wa hekta milioni **7**.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi 11 ambazo zinaongoza kwa kupokea maombi mengi zaidi ya 'wawekezaji'. Nchi nyingine ni Sudan, Ethiopia, Msumbiji, Madagascar, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Katika Bara la Asia nchi zinazoongoza ni Philippines, Indonesia na Laos.

Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo huo wa uporaji wa ardhi unaoendelea duniani na hapa nchini, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuchukua tahadhari mapema kuulinda Ardhi ya Tanzani isije ikachukuliwa na wageni na watanzania wakabaki kama watumwa ndani ya nchi yao. Katika kufanya hivyo, tunaitaka Serikali kurejea maneno ya Baba wa Taifa aliyesema mwaka 1958 kwamba: nanukuu, *"Nchi kama yetu, ambayo waafrika ni masikini na wageni ni matajiri, kuna uwezekano kwamba mwafrika akiruhusiwa kuiuza ardhi, katika miaka ya themanini au miaka ijayo, ardhi ya Tanganyika itamilikiwa na matajiri wageni, na wenyeji watakuwa watwana. Lakini hata kama wageni wasingekuwa matajiri, litaibuka tabaka la watanganyika matajiri wajanja.*

Tukiruhusu ardhi iuzwe kama kanzu, katika muda mchache, kutakuwa na kundi dogo waafrika watakaokuwa na ardhi na walio wengi watakuwa watwana” Tunaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imechukua hatua gani za kuzuia uuzaji wa ardhi kwa wageni kiholela?

- ii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilikemea na kupinga Ufisadi wa ardhi uliokuwa unafanywa na viongozi wa Serikali na Chama cha Mapinduzi. Tulienda mbele Zaidi kuwataja vigogo hawa kwa majina na nyadhifa zao! Kama ilivyo ada hakuna hatua zozote zilizochukuliwa!,hali inayopelekea mwendelezo wa kadhia hii kama itakavyobainishwa baadaye katika hotuba hii’.
- iii. **Mheshimiwa Spika**, kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii, Kambi Rasmi ya Upinzani pia ilibaini ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria namba 5 ya ardhi ya vijiji ambapo viongozi wa Serikali walikuwa wakigawa ardhi kiholela bila kuzingatia matakwa ya sheria hizo, jambo ambalo lilikuwa ni chimbuko la migogoro mingi ya ardhi katika vijiji vingi. ‘Hakuna hatua zilizochukuliwa, viongozi wa vijiji wanaendelea kugawa ardhi kwa wawekezaji kinyume na utaratibu kama ambavyo tutaainisha hapo baadaye’!
- iv. Kambi ya upinzani ilihoji juu ya mradi wa viwanja 20,000 , mradi ambao ulitawaliwa na wizi,ufisadi na udanganyifu mkubwa!(Mradi huu ulifanyika kipindi ambacho Mama Salome Sijaona alipokuwa katibu Mkuu wa wizara ya ardhi)Viwanja vingi viliishia kwa watu wachache!! (watumishi wa wizara waliopewa mamlaka ya kusimamia Mradi) na kuelekeza ukaguzi maalum(Special Audit)ufanyike ili kujua nani ni wamiliki halisi!, mpaka sasa hakuna taarifa yoyote juu ya ukaguzi wa mradi husika, licha ya Kamati ya Bunge ya ardhi na Maliasili nayo kuhoji juu ya jambo hili. !!
- v. Kambi rasmi ya upinzani ilihoji juu ya migogoro isiyo kwisha baina ya wizara ya maliasili na utalii na wanavijiji wanaoishi pembezoni mwa hifadhi. Hakuna hatua za maana zilizochukuliwa, tumeendelea kushuhudia malalamiko mazito ya wabunge wakati wakichangia hotuba ya maliasili na utalii.

- vi. Kambi ya upinzani ilihoji juu ya uporaji ardhi wilaya ya Mafia kwa kile kinachoitwa uwekezaji (Tumaini Plantation Ltd). Zaidi ya Kaya 2500 za wananchi wa vitongoji vya Mikongoni, Mkamba, Kipora, Kifinge, Mlundo, Gonge, Chunguruma, Baleni, Minaki vilivyopo katika vijiji vya Kirongwe, Baleni, Jojo, Gonge, Kifinge na Ndagoni, wilayani Mafia, mkoani Pwani, ziko katika **Msiba Mkuu** wakisubiri kufukuzwa majumbani mwao kutokana na serikali kutaka kukabidhi maeneo yao ya asili kwa mwekezaji.
- vii. Kwa miaka yote ya uhai wa Bunge hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, iliitaka Serikali kushugulikia migogoro mikubwa ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji ambayo kwa nyakati tofauti imepelekea umwagaji damu miongoni mwa wananchi. Wakati migogoro hii inachochewa na uhaba wa ardhi, kuna genge la watu wachache wanahodhi maeneo makubwa ya ardhi, ambayo hayajaendelezwa (Mashamba pori), huku serikali ikiwa haina ujasiri wa kuyarejesha ili yatumike kwa manufaa ya watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, bado wakulima na wafugaji wanaendelea kuuana, hakuna hatua zozote za maana zilizochukuliwa, licha ya Bunge lako tukufu, kupitia Kamati teule ya Bunge kutoa taarifa ya chimbuko la migogoro husika!

- viii. Kambi Rasmi ya Upinzani iliainisha matatizo makubwa katika tathmini ya malipo ya fidia kwa wananchi wanaotakiwa kuondoka katika maeneo yao kupisha matumizi mapya ya ardhi. Katika juhudi za kutatua tatizo hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka Serikali kulipa fidia stahiki kwa wananchi wanaotakiwa kuondoka katika maeneo yao kupisha matumizi mapya ya ardhi. Suala la fidia kwa wananchi bado ni donda ndugu!
- ix. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilihoji juu kuendelea kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi jambo ambalo limesababisha wananchi kuendelea kuishi katika makazi duni na hivyo kuhatarisha usalama wao na kutweza utu wao. Licha ya Mbwembwe za Katibu Mkuu wa CCM ndugu Kinana, kudandia hoja ya Kambi ya upinzani, na kuahidi kuelekeza serikali ya Chama chake kulifanyia kazi, hakuna

hatua za dhahiri zilizofanyika kuwapunguzia wananchi adha hii!

- x. Kambi Rasmi ya Upinzani pia ilikemea na kupinga tabia mbaya ya Serikali na taasisi zake kutolipa kodi za pango kwa wakati kwa Shirika la Nyumba la Taifa na hivyo kulirudhisha nyuma kimaendeleo.
- xi. Tuliitaka Serikali kubatilisha mkataba wa kifisadi kati Kampuni ya Uwindaji ya Game Frontiers of Tanzania Limited na Kampuni mbili za nje za uchimbaji madini za Uranium Resources PLC na Western Metals, kufanya utafiti wa uchimbaji wa madini ya Uranium kwenye kitalu cha uwindaji katika kijiji cha Mbarang'andu kinyume cha sharia na kujipatia kipato isivyo halali. 'Hakuna la maana lililofanyika Zaidi ya kulindana'
- xii. Tuliitaka Serikali kuanzisha Mamlaka ya Udhubiti wa Kodi za Nyumba (Real Estate Regulatory Authority) ili kuratibu, kuweka viwango na miongozo ya kodi za nyumba ili kuwaondolea wananchi wapangaji wa nyumba adha kubwa ya gharama kubwa za pango zisizo na viwango. Aidha, pendekezo hili lililenga pia kuipatia Serikali mapato makubwa kupitia sekta ya nyumba ambayo kwa sasa hayakusanywi ipasavyo.
- xiii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliishauri serikali kusitisha ugawaji wa ardhi kwa wageni (kwa muda) hadi tathmini ya kina ifanyike. Ili kuweza kuwa na mpango thabiti wa matumizi bora ya ardhi! Ushauri huu ulipuuzwa!
- xiv. Tulionesha pia jinsi Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba bora na Vifaa vya Ujenzi alivyoshindwa kuleta mabadiliko kutokana na kuongezeka kwa nyumba zisizo bora (kama vile nyumba za tembe, tope na nyasi) na kuongezeka kwa bei ya vifaa vya ujenzi.
- xv. Tuliitaka Serikali kuweka ukomo wa ardhi ya kilimo kwa wawekezaji.
- xvi. Kambi ya Upinzani ilihoji juu ya utekeleza wa Taarifa ya Kamati (ya Lukuvi)- alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ambayo iliundwa tarehe 18 Juni, 2010 ikiwa na jukumu la kuchunguza maeneo ya wazi yaliyomo katika Jiji

la Dar es salaam, ambayo yamevamiwa, kuendelezwa au kuuzwa kinyume na taratibu za mipango miji (Ripoti iko kwenye makabati imejaa vunmbi).

- xvii. Kambi ya upinzani iliitaka Serikali kuleta Bungeni Taarifa ya uchunguzi ya kuanguka kwa magorofa Dar es salaam ya mwaka 2006 na hatua zilizochukuliwa na baada ya ukaguzi !Na nyumba ngapi zilitakiwa kuvunjwa. Halikadhalika tulitaka Ukaguzi ufanyike kwenye majengo yote yaliyojengwa na Ladha Construction LTD (aliyehusuka na ujenzi wa jengo, katika Mtaa Indira Gandhi – Dar es Salaam, lililoanguka nakuua watu wasiopungua 21). Tuliambia Serikali kuwa kuna maghorofa aliyoyajenga yenye wapangaji ndani yake na ziko kwenye mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Spika, Mpaka sasa hakuna hatua zilizochukuliwa licha ya maagizo ya wizara ya ardhi kuitaka Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kubomoa (jengo la ghorofa 16) lililopo kwenye kiwanja Na 1662 kitalu 75 mtaa wa Idira Gandhi/Asia (Jengo pacha ya jengo lililoua watu wasiopungua 21) kupitia barua yenye kumbukumbu Na. C.A 174/333/05/107 ya tarehe 5/04/2013. kwa kukiuka Mpango wa uendelezaji .

Mheshimiwa Spika, Licha ya mbwembwe na matamko ya matambo ya viongozi wa Kitaifa, (Mkuu wa wilaya, Mkuu wa Mkoa , Waziri wa ardhi/ Ujenzi na hatimaye Rais wa Jamuhuri ya Muungano), leo ni mwaka wa '2' jengo hilo halijabomolewa, na wala Halmashauri haijatoa notisi ya kumtaka mwenye jengo abomoe!.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kwamba; moja ya sababu zinazotolewa na Halmashauri na Wizara ni kwamba "wanazingatia maelekezo ya Katibu Mkuu Kiongozi (Ndugu Ombeni Sefue) aliyotoa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi ambayo aliwaagiza waepuke kufanya jambo ambalo litaisababisha serikali kufikishwa mahakamani!(Barua imeambatanishwa). Hakika huu utawala wa CCM ni kama wa Kambale (yani baba, mama na watoto, - wote wana ndevu). Inakuwaje Rais anaagiza, Katibu Mkuu Kiongozi anazuia?!!

Mheshimiwa Spika, inaonekana serikali ya CCM inasubiri watanzania wengine wafe ndio waamke kutoka katika lindi la usingizi !!

Mheshimiwa Spika, masuala ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeyafanya kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii ni mengi na siwezi kuyataja yote hapa.

Utekelezaji wa ushauri na maoni ya Kambi ya upinzani umekuwa wa kiwango duni sana kwa kuwa waliopewa dhamana hawaoni umuhimu wa kuwajibika. Hali hii imepelekea marudio ya makosa yaleyale katika maeneo mengine ya nchi hii kwa kiwango kilekile.

3. VIGOGO WA CCM WANAVYOHUSIKA NA UPORAJI WAARDHI

Mheshimiwa Spika, Kama ambavyo imekuwa ada, kila mwaka katika hotuba ya bajeti tumekuwa tukiliambia hili Bunge na watanzania kwa ujumla, juu ya ushiriki wa vigogo wa CCM na serikali katika kuchochea au kuanzisha migogoro ya ardhi! (Rejea hotuba za kambi ya upinzani mwaka 2011/12, 2012/13 na 2014/15). Na kwa kuwa serikali hii ya CCM haina uthubutu wa kuchukua hatua, matukio mapya yanazidi kujitokeza na mwaka huu 2015/16 sakata la uporaji wa Ardhi linamhusisha Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, ndugu Leonidas Gama

Mheshimiwa Spika, Kiongozi huyu anaelezwa kuingia katika mkoa huo kwa mbwembwe nyingi akijipambanua kwamba anahitaji Halmashauri kutenga maeneo maalum ya uwekezaji! Halmashauri zikiamini kwamba kigogo huyu ana nia njema ya kuleta maendeleo zilipokea wito huo kwa mikono miwili! Moja kati ya Halmashauri hizo ni Halmashauri ya wilaya ya Rombo ambayo ilitwaa ardhi kutoka kwa wananchi na kuwalipa fidia ya jumla ya shilingi **milioni 168**.

Kada huyu wa CCM alikwenda China (kwa gharama za serikali) na kuja na watu wawili wanaoitwa 'wawekezaji' Katika hali ya kushangaza juu ya ardhi iliyolipwa fidia kwa fedha za umma ilianzishwa kampuni ya binafsi ya **JUN YU INVESTMENT INTERNATIONAL COMPANY LTD**. Wanhisa katika kampuni husika ni Wang Zhigang – raia wa China (hisa 48,000), Feng Hu - raia wa China (hisa 49,000), na Muyanga Leonidas Gama – raia wa Tanzania (hisa 3,000). Huyu Muyanga Leonidas Gama ni mtoto wa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, tumeambatanisha nakala ya Memorandum of Association (MOA) husika kama sehemu ya hotuba hii! **(Tazama kielelezo na.1 na 2)**

Mheshimiwa Spika, Habari tulizonazo ni kwamba Mkuu wa Mkoa anamiliki hisa 20, 000 ambazo ni hisa 10,000 zilizofichwa kwa mwanahisa wa kwanza na 10,000 nyingine kwa mwanahisa wa pili kwa mkataba wa 'siri uliofichwa'. **(Tazama kielelezo na. 3)** Katika hali ya kushangaza halmashauri ya Rombo ambayo iliwekeza fedha zake shilingi milioni 168 haitambuliwi na wala haina hisa hata moja katika Kampuni hiyo!

Mheshimiwa Spika, Taarifa za ki-inteligensia ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo; zinaonesha kwamba 'wawekezaji hao wa kichina' walilipa shilingi **milioni 500** kama fidia kwa wananchi katika ardhi hiyo hiyo (ambayo Halmashauri ya Rombo ilishalipa shilingi 168 milioni) - fedha ambayo mpaka sasa haijulikani iko wapi!!

Mheshimiwa Spika, Kama hiyo haitoshi; Kigogo huyu pia anahusishwa na tuhuma za kutaka kufanya ufisadi katika eneo lililopo Kilacha (linalogusa jimbo la Vunjo na Rombo) lenye ukubwa wa hekta 2700. Eneo hili lilikuwa mali ya ushirika uliokuwa ukifahamika kwa jina la LOCOLOVA. Wananchi wanaishi na kufanya shughuli zao za kila siku!! Eneo hili linanyemelewa kwa udi na uvumba na kigogo huyu kwa kisingizio cha uwekezaji! Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kwamba; mbinu alizozitumia katika uporaji wa ardhi ya Wananchi wa Rombo ndizo anazotarajia kuzitumia tena katika eneo hili!

Mheshimiwa Spika, Kada huyu wa CCM (ambaye ndiye mwakilishi wa Rais katika Mkoa huo) anatajwa tena katika mgogoro wa ardhi unaofukuta sasa hivi unaokihusisha kiwanja cha Mawenzi, chenye hati namba C.T 056035 kilichokuwa chini ya miliki ya **The Registered Trustees of Mawenzi Sports Club**. Kiwanja hiki kilikuwa na hatimiliki ya miaka 33 iliyokwisha mwaka 1974. Baada ya muda wa miliki ardhi kwisha kisheria, na kufuatia mipango ya serikali ya kuendeleza mji wa Moshi mwaka 1994, kupitia tangazo la serikali **No 606**, la 23/12/1994 - aliyekuwa waziri wa ardhi kipindi hicho Mhe. Edward Lowassa alitoa 'amri ya kutwaa' maeneo mbali mbali likiwemo eneo lenye mgogoro.

Mheshimiwa Spika,

Kufuatia utwaaji wa eneo tajwa tarehe 12/4/2001 aliyekuwa waziri wa ardhi, Mhe. G.A Cheyo 'alitoa amri ya kuendeleza' mji wa Moshi, amri iliyochapishwa na tangazo la serikali no 112 la 15/6/2001 (eneo lenye mgogoro likiwa sehemu ya eneo husika). Pamoja na mambo mengine kifungu na.3 kimeweka wazi fursa ya pingamizi (ndani ya miezi miwili baada ya Tangazo kutolewa) kwa yeyote mwenye maslahi katika eneo husika! Hakuna pingamizi lolote lililowekwa!

Mheshimiwa Spika, Eneo husika lilikuwa salama chini ya wakuu wa mikoa wote waliopita, lakini hali ilibadilika alipoletwa bwana Gama, ambaye amekuwa akitumia ofisi yake kushinikiza kiwanja husika kukabidhiwa kwa genge la matapeli, ambao wametengeneza nyaraka feki na kuziwasilisha Rita na kisha kujitambulisha kama 'wadhamini wapya - 'Trustees' baada ya kukabidhiwa jukumu hilo na 'wadhamini wa awali'.

Mheshimiwa Spika, Wakati 'matapeli' hawa wanaotambulika kwa majina 'Amratlal N. Pattn na Hittesh H.Solani wakionyesha kwamba kikao cha makabidhiano kilifanyika tarehe 5/1/2008 mbele ya uwepo wa 'wadhamini wa awali' ndugu Devchad Nathu Shah na Mohamedali Sharriff; taarifa za

uhakika ambazo Kambi ya upinzani inazo, Ndugu Devchad Nathu Shah alishafariki dunia tangu mwaka 1979 , wakati Mohamed Shariff alifariki tangu mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 26/11/2014 Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, akijibu dokezo lililowasilishwa kwake na Katibu Tawala Msaidizi kuhusiana na kiwanja tajwa hapo juu, anamwelekeza RAS aandike barua kwenda kwa Mkurugenzi wa Manispaa , na kumuonya asimzuie 'mwenye mali' kumiliki 'mali yake'!

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji:- inakuwaje wadhamini waliofariki mwaka 1979 na 1998 wakae tena kwenye kikao cha Januari, 2008? Ikumbukwe huyu ndio mwakilishi wa Rais Kilimajnaro...halikadhalika Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa (Polisi na idara za usalama wa Taifa za mkoa zote ziko chini yake)! Na kubwa Zaidi ni mjumbe wa Kamati ya siasa ya chama cha Mapinduzi ya Mkoa!! Na kama hiyo haitoshi matapeli haya yakijua 'wadhamini' walishafariki toka mwaka 1979 na 1998; waliendelea kupeleka kumbukumbu za 'Returns of Trustees' za miaka (2000-2008), zote zikiwa zimewasilishwa RITA kwa mkupuo mwaka 2012 zikiwa na saini za 'marehemu'!

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kazi njema iliyofanywa na Mkurugenzi Mkuu wa RITA aliyebatilisha uamuzi wake wa awali baada ya uongozi wa Moshi Manispaa kumpelekea nyaraka mbali mbali zilizoainisha udanganyifu husika,!! Hata hivyo tunatambua kuna mchakato unaoendelea wa kuwapatia 'matapeli'hawa hati mpya, na kwa kuwa kuna msukumo mkubwa wa Mkuu wa Mkoa 'ambaye anatuhumiwa kuvuta milioni 400' yawezekana mchakato husika ukafanikiwa au umeshafanikiwa!

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza mambo yafuatayo yafanyike:-

- 1) Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi azuie haraka iwezekanavyo mchakato huu haramu kama bado hati haijatolewa!! Na kama hati mpya imeshatolewa tunamtaka Rais atumie mamlaka yake kubatilisha hati husika!
- 2) Rais Jakaya Mrisho Kikwete amwajibishe mara moja kiongozi huyu kwa kutumia madaraka yake vibaya na kujiingiza kwenye biashara chafu!
- 3) Taasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imchunguze kiongozi huyu sambamba na watendaji wote wa serikali waliotumia vibaya madaraka yao kupotosha ukweli juu ya

uhalali wa Mawenzi Sports Club kupewa hati ya kumiliki kiwanja hicho!!

4. WIMBI LA UNYAKUZI WA ARDHI TANZANIA: UWEKEZAJI WA DANGOTE NA UKIUKWAJI WA SHERIA YA ARDHI

Mheshimiwa Spika, Suala la unyakuzi wa ardhi Barani Afrika, na hususan Tanzania, ni suala ambalo limekuwa likizungumzwa na Kambi ya Upinzani kwa kipindi chote cha miaka mitano ya uhai wa bunge hili. Na msingi wa hoja ya kuitaka Serikali kulinda ardhi yetu dhidi ya unyakuzi huo, unatokana na uhalisia kwamba; idadi ya watanzania inaongezeka na ardhi yenye rutuba inazidi kupungua. Aidha, mahitaji ya chakula yanaongezeka kwa kasi duniani. Kwa mujibu wa Taarifa Makisio ya Idadi ya Watu Duniani ya mwaka 2012, inatarajiwa kwamba iifikapo mwaka 2050, mahitaji ya chakula duniani yataongezeka kwa 70% kutokana na ongezeko la idadi ya watu duniani kutoka bilioni 7.2 mpaka bil 9.6.

Mheshimiwa Spika, Kudhihirisha umuhimu wa jambo hili, taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa juu ya utekelezaji wa shughuli za Chama Wabunge wa nchi wananchama wa Jumuiya ya Madola (CPA); katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai 2014 hadi 16 Januari 2015 (UK 21) ilieleza namna suala la unyakuzi wa ardhi linavyojadiliwa kwa kina katika vikao vya Kamati na Bunge la Afrika na kwamba Bunge la Afrika limesisitiza kwamba Umoja wa Afrika uweke mikakati bora katika kushughulikia suala la ardhi barani Afrika kwa manufaa ya waafrika na nchi moja moja iweke mikakati na kuboresha sheria na taratibu za ugawaji bora wa ardhi kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, Kuonyesha umakini wetu, kabla hata hoja hii haijaanza kujadiliwa katika ngazi ya CPA, miaka 5 iliyopita kambi ya upinzani tuliitaka serikali hii ya CCM, kufanya ukaguzi wa ardhi(land auditing)nchi nzima, ili kuliwezesha Taifa kujua kila kipande cha ardhi na matumizi yake!! ili tuweze kama Taifa kuweka mipango thabiti ya matumizi bora ya ardhi kwa manufaa ya Taifa na watu wake.

Mheshimiwa Spika, Wakati Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ikiyjadili haya, na wakati Kamati yako teule ya Bunge iliyopewa jukumu ya kufanya utafiti juu ya kasi ya migogoro baina ya wakulima na wafugaji, wananchi na wawekezaji na wananchi na hifadhi za Taifa wakiainisha uhaba wa ardhi na mipango mibovu ya matumizi ya ardhi kuwa ndio chanzo cha migogoro husika, hivi karibuni tumeshuhudia bilionea namba moja Afrika, Alhaji Aliko Dangote akikabidhiwa hekta 2,500 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ili ajenge bandari

itakayotumika kusafirisha saruji kutoka katika 'kiwanda chake' cha Saruji kwenda ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Bilionea huyu amekabidhiwa eneo la ufukwe wa bahari ya hindi, katika kijiji cha Mgao, Kata ya Maumbu, Tarafa ya Mayanga, Wilaya ya Mtwara vijijini, ambapo atajenga 'bandari yake' ya kisasa kwa ajili ya kusafirisha 'saruji yake' itakayozalishwa kwenye kiwanda chake kikubwa kinachojengwa katika kijiji cha Msijute.

Mheshimiwa Spika, Kwa taarifa ambazo zilizagaa kwenye vyombo vya habari (ambazo hazijakanushwa na chombo chochote cha serikali, akiwamo waziri mwenye dhamana katika masuala ya ardhi), Mwenyekiti wa Kijiji cha Mgao, ndugu Abrahaman Shaa ndiye aliyemkabidhi mfanyabiashara huyo ardhi. Mheshimiwa Spika, taarifa zinazidi kueleza kwamba ardhi hiyo - hekta 2500 (sawa na ekari 6,600/-) ilitolewa bure kwa mfanyabiashara huyo, kwa ahadi kwamba wanakijiji hao watajengewa shule na hospitali!

Mheshimiwa Spika, Ni aibu kwa Serikali kutoa ardhi yenye thamani kubwa...iliyopo ufukweni (prime area) bure kwa kubadilishana na 'ujenzi wa shule na hospitali. Hii haina tofauti na kubadilishana dhahabu na kipande cha kanga!! au haitofautiani na wale waliopokea vipande vichache vya kaniki wakawauza mababu zetu utumwani. Kweli karne hii ya 21 Serikali inafanya **barter trade**???! Ina maana sasa Serikali imeshindwa kutoa huduma za jamii kwa wananchi wake hivyo inagawa ardhi yetu ili iwezeshe na wageni kutoa huduma hizo? Kuna tofauti gani na kusema Serikali imewekwa mifukoni mwa wawekezaji?? Hii ni aibu na ni fedheha ya mwaka kwa Serikali.

5. UKIUKWAJI WA SHERIA YA ARDHI

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi ya Kijiji ya mwaka 1999 inatoa mamlaka kwa Halmashauri ya kijiji kusimamia ardhi yote ya Kijiji. Halmashauri ya Kijiji si mmiliki wa ardhi ya kijiji bali ni mdhamini aliyepewa wajibu wa kusimamia ardhi yote ya kijiji. Sheria ya Ardhi imetoa ukomo wa mamlaka ya Halmashauri ya kijiji kugawa ardhi. Na itagawa ardhi husika baada ya kuruhusiwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji ambao una mamlaka ya kupokea, kujadili na kuyafanyia maamuzi masuala kuhusu ugawaji wa ardhi. Hata huo Mkutano Mkuu wa Kijiji, una ukomo wa mamlaka wa kugawa ardhi. Baada ya kupokea maombi ya ardhi, kwa mujibu wa Sheria No.5 ya mwaka 1999, ina uwezo wa kugawa kati ya ekari 100-500 tu swa na (hekta 38- 190)tu!

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili yafuatayo:

- (i) Utaratibu uliotumika kumpatia Dangote ardhi ya uwekezaji ulikuwa ni wa kisheria au la?
- (ii) Je, kulikuwa na mahitaji halisi kutoa ya ekari 6,600 ya ardhi ya wananchi kama hoja ilikuwa ni kujenga bandari binafsi ya kumwezesha kusafirisha simenti toka kwenye kiwanda chake kwenda ndani na nje ya nchi? Msingi wa swali hili unatokana na ukweli kwamba eneo la ardhi lililochukuliwa ni kubwa mno ukilinganisha na mahitaji halisi ya eneo la ujenzi wa bandari.

6. MIGOGORO YA ARDHI: ISHARA YA KUSHINDWA KWA CHAMA CHA MAPINDUZI

Mheshimiwa Spika, kushindwa kwa Chama cha Mapinduzi kunatokana na ukweli kwamba migogoro baina ya wakulima , wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi imedumu kwa muda mrefu licha ya kwamba nchi yetu ina sera, mikakati na sheria kwa ajili ya kusimamia masuala ya ardhi .Uzembe huu ulibainishwa pia na taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa kuchunguza sababu za migogoro ya ardhi nchini (Taarifa ilitolewa 6/2/2015). Kamati hii ilibainisha kwamba katika mapitio ya nyaraka mbali mbali waligundua kwamba kuna migogoro ambayo ilianza toka mwaka 1966 (kijiji cha Mabwegere na majirani), haijapatiwa ufumbuzi mpaka sasa (Miaka 49 iliyopita).

Mheshimiwa Spika, usugu huu wa serikali ya CCM uliendelea kuthibitika kufuatia maelekezo yaliyotolewa na aliyekuwa waziri Mkuu na Makamu ya kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania , Ndugu, Joseph Sinde Warioba kwa barua ya tarehe 19/2/1986 iliyokuwa inamwelekeza Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Vijijini kushughulikia matatizo ya wakulima na wafugaji katika kijiji cha Kambala. Licha ya kupewa siku saba (7) kuanzia tarehe 22.2.1986 hadi 1.3.1986 za kutatua mgogoro husika, mpaka sasa (miaka 29) migogoro kati ya wakulima na wafugaji wa kijiji cha Kambala umeendelea kukua na kusababisha vifo, uharibifu wa mali ,uvunjifu wa amani na kuathiri uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, kushindwa kwa CCM kunaendelea kudhihirishwa na mateso wanayokumbana nayo wananchi wa mkoa wa Tanga,ambao kwa kipindi kirefu sana wamekuwa waadilifu na wateja wazuri wa CCM kwa kukipa 'ushindi' unaoitwa wa kishindo katika chaguzi mbali mbali! Mnamo tarehe 1/5/1985 katika sherehe ya wafanyakazi ya Mei Mosi iliyofanyika Tanga, Baba wa Taifa mwalimu Julius K. Nyerere alitoa agizo kwa mashamba ambayo yameshindwa kuendelezwa na hivyo kugeuka msitu wapewe wananchi wasio na ardhi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kauli ya baba wa Taifa, iliundwa kamati ndogo iliyowajumuisha Ndugu. Ibrahim J. Shemdoe, Ndugu Omari S.O Mduruma na Ndugu S. Saidi iliyopewa jukumu la kuzungukia mashamba yote yaliyotelekezwa na kutoa mapendekezo ya kiasi gani cha ardhi kitwaliwe kwa matumizi ya umma. Baada ya uchunguzi wake wa kina ilipendekezwa vijiji vyenye uhaba mkubwa wa ardhi vimegewe jumla ya **hekta 15,612** kutoka mashamba ya Mamlaka ya Mkonge Tanzania (MTT).Wilaya ambazo zilikuwa zinufaike na mchakato huu ni Muheza , Korogwe , Lushoto, na Pangani!

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada ya Serikali ya CCM, toka mwaka 1985, mpaka sasa mchakato huu haujafanyika kwa ufanisi. Mpaka sasa hivi kuna Mgogoro mkubwa sana unaofukuta katika wilaya ya Muheza! na waahanga wakuu ni wanavijiji wa Mgome, Mpapayu, Kigongomawe na Kwamnyefu. Mgogoro huu ni kati ya ndugu **Khamisi Kindoroko** 'mwekezaji' anayemiliki shamba la **KUMBURU Estate** ambalo liko chini ya **Silver General Distributors Ltd** na wananchi!

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mapendekezo ya Kamati ya wananchi iliyoundwa kipindi hicho shamba la Kumburu lenye ukubwa wa **hekta 2,904** lilitakiwa limegwe **hekta 904** ...mchakato ambao haujafanyika mpaka sasa!

Mheshimiwa Spika, licha ya aliyekuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Mhe. Ole Medeye kufanya ziara ya kikazi katika wilaya ya Muheza kwa lengo la kushughulikia maswala mbali mbali ya ardhi likiwemo shamba la Kumburu na kutoa maelekezo ya utatuzi kwa Mkuu wa wilaya kwa barua yenye kumbukumbu namba LD/1464 Vol. III ya tarehe 15/05/2012 kwa lengo la kuumaliza mgogoro husika, kama ilivyotokea kwa Mkuu wa wilaya katika tukio la mgogoro wa ardhi mwaka 1966 na 1986 chini ya CCM ndivyo ilivyotokea mwaka mwaka 2012! Kikubwa alichokifanya mwakilishi wa Rais, badala ya kutatua mgogoro alikwenda kuwaita wananchi MBWA!

Mheshimiwa Spika, ninapowasilisha hoja hii baadhi ya wanakijiji waliokuwa mstari wa mbele kupigania haki yao wamebambikiziwa kesi za mauaji ! wengine mpaka sasa wapo Geraza la Maweni! kama ilivyo kwa maelefu ya watanzania wengine wanaosota kwenye magereza kwa kesi za kubambikiwa na utawala wa CCM, bila kusikilizwa. Inasemekana jalada (P.I No. 4/2014) liko kwa mwanasheria mkuu wa serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya upinzani inamtaka Waziri wa ardhi alieleze Bunge hili tukufu, ni lini anatarajia kuimaliza migogoro hii sugu!!!

Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imetoa uamuzi gani kwa kufuatia adha kubwa na mateso wanayokumbana nayo wananchi wa **Tarafa ya Olboloti Kibaya, Kiteto**, ambapo wananchi wanalalamikia kamata kamata inayofanywa na Askari Polisi, inayokwenda sambamba na kuwachapa viboko na kuwalazimisha kutafuna mbegu za mahindi na alizeti na kuzimeza!!

Mheshimiwa Spika, wananchi wanapata adhabu hii kwa sababu tu ya kufanya shughuli za kilimo!!Shughuli ambazo wamekuwa wakizifanya toka mwaka 1998! Kambi ya upinzani inatambua kwamba iliundwa Tume ya maridhiano chini ya Ofisi ya waziri kuu kwa madhumuni ya kulitafutia ufumbuzi suala hili!!Na kwamba Tume husika imeshatoa taarifa kwa Waziri Mkuu! Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka majibu.

7. MGOGORO WA ARDHI KATI YA CDA NA WANACHI – MANISPAA YA DODOMA

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu sasa kati ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) ambapo wananchi siku zote wamekuwa ndio wahanga wakubwa na hakuna wa kuwasaidia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba mnamo tarehe 30 Machi, 2015 CDA ilitoa notisi ya kuvunjwa kwa nyumba tano za wananchi ili kupisha ujenzi wa kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, baada ya notisi hiyo, wananchi waliandika barua ya malalamiko kwa CDA ya kutaka kulipwa fidia kwa nyumba zao na maendeleo mengine waliyokuwa wameyafanya katika maeneo yao. Jambo la kushangaza ni kwamba wakati wananchi hao wanasubiri majibu ya barua zao, CDA iliendesha operesheni ya kubomoa nyumba zao mnamo tarehe 6 Mei, 2015 bila taarifa yoyote. Hadi muda huu ninaposoma hotuba hii, wananchi hao wanaishi chini ya miti na hawajui haki yao itapatikana wapi. Mpaka tarhe 1 Juni, 2015, Notisi nyingine za ubomoaji zimeendelea kutolewa na CDA kwa sababu za kupisha ujenzi wa huduma za jamii kama vile shule, hospitali na Barabara.

Mheshimiwa Spika, dhoruba hii ya kuvunjiwa nyumba bila fidia inayofanywa na CDA ilikuwakuba pia wakazi wa Eneo la Msangalalee ambapo, mwaka 2014 CDA ilitoa notisi ya kuvunja nyumba 35 katika eneo hilo bila fidia ili kupisha ujenzi wa barabara. Wananchi walifungua kesi mahakama kuu kanda ya Dodoma kupinga agizo hilo la CDA. Mahakama ikasikiliza na kutoa zuio kwa CDA kuvunja nyumba hizo hadi kesi ya msingi itakapomalizika. Chaajabu ni kwamba CDA ilivunja nyumba hizo bila kujali amri ya mahakama. Kuvunjwa kwa nyumba hizo kuwaliwaacha wananchi takriban 170 bila makazi.

Mheshimiwa Spika, Dhoruba hiyo iliendelea kuwakumba wananchi wa Eneo la Msalato ambapo zaidi ya wananchi 1000 walichukuliwa mashamba na nyumba zao na Serikali kwaajili ya kupisha ujenzi wa uwanja wa ndege. Tathimini ilifanyika tangu 2011, wananchi wamezuiwa kulima na/au kuendeleza maeneo yao kwa miaka yote bila kupata fidia wanayostahili kisheria. Watoto wameshindwa kwenda shule kwasababu ya kuvurugwa kwa mfumo wa uchumi wa familia hizi. Kuna watu ambao wamepoteza maisha kwa kukosa kipato kutokana na serikali kushikilia Ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu fidia kwa Wakazi wa Msalato ambao wanapisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege, aliyekuwa Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Harison Mwakyembe alishawaahidi wananchi hao kupitia barua yake kumb. Na. DE 20/230/01 ya tarehe 9 Mei, 2013 kwamba watalipwa fidia zao katika mwaka wa fedha 2014/15. Kwa mujibu wa barua hiyo, Mhe, Mwakyembe alisema Mthamini Mkuu wa Serikali ameshakamilisha zoezi la thathmini na kwamba kiasi cha takriban shilingi bilioni 3 zinahitajika kuwalipa wananchi 980 katika eneo la Msalato.

Mheshimiwa Spika, Mpaka sasa mwaka wa fedha 2014/15 unamalizi fidia hiyo haijalipwa kama Mhe. Mwakyembe alivyoahi. Kutokana na wananchi hao kumlalamikia Waziri Mkuu, juu ya ucheleweshwaji wa fidia hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu ilimwandikia Waziri wa Uchukuzi barua yenye Kumb. Na. PM/P//2/569/79 ya tarehe 21 Januari, 2015 ikiitaka Wizara ya Uchukuzi ilifanyie kazi zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi hao na kumpa taarifa Mhe. Waziri Mkuu juu ya utekelezaji wa zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri wa Ardhi alieleze Bunge hili amechukua hatua gani kuhakikisha kwamba Wizara ya Uchukuzi inalipa fidia hiyo. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri wa Ardhi alieleze Bunge hili kuhusu mambo yafuatayo:

- i. Ni sera ya Serikali hii ya CCM kuwabomolea wananchi nyumba zao bila kuwalipa fidia?
- ii. CDA ilivyowapa wananchi viwanja haikuwa na Master Plan kujua ni sehemu gani patajengwa shule, hospitali au barabara kiasi cha kuja kuwasababishia wananchi hasara na umasikini wa kudumu kiasi hiki?
- iii. CDA inatoa wapi kiburi cha kuwabomolea wananchi nyumba zao hovyohovyoy bila hata kutii amri ya Mahakama?
- iv. Serikali inatoa kauli gani juu ya wananchi waliobomolewa nyumba zao na CDA ambao mpaka sasa wanaishi chini ya miti?

- v. Ni lini Serikali itatoa fidia kwa wananchi waliovunjiwa nyumba zao katika Manispaa ya Dodoma kwa ajili ya kupisha miradi ya maendeleo?

8. MGOGORO WA ARDHI KATIKA KIJJI CHA KIFANYA HALMASHAURI YA MJI WA NJOMBE.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo kwa Mgogoro wa Ardhi katika kijiji cha Kifanya ndani ya Halmashauri ya Mji wa Njombe, ulionzishwa na kauli ya Mkuu wa Wilaya Bi. Sara Dumba tarehe 13/06/2014 wakati akifanya uzinduzi wa vitalu vya chai - Mawolo, Kijiji cha Kifanya. Kauli ya Mkuu wa Wilaya ilikuwa ni kwamba wananchi walime chai na Halmashauri za vijiji zigawe maeneo kwa wakulima wadogo. Kauli hii ilipelekea halmashauri ya kijiji kuvunja sheria ya ardhi na kanuni zake kwa kugawa ardhi pasipo kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Spika, ardhi iligawiwa pasipo kuwepo Mkutano Mkuu wa kijiji na kuhusisha wananchi kufanya maamuzi. Mkutano wa ugawaji ardhi ambao ulifanyika tar 15/06/2014 ambao ulihudhuriwa na wananchi 15 tu haukuonesha mahudhurio ya jamii ya wafugaji hata mmoja pamoja na kuwa na wajumbe wachache kutoka katika jamii ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, mnamo tar 31/11/2014 Halmashauri ya Kijiji iligawa Ardhi Jumla ya hekta 221. Baada ya eneo hilo kugawiwa kwa wananchi na wawekezaji kwa barua za Mwenyekiti wa Kijiji na nakala kupelekwa kwa Mkuu wa Wilaya ikisema.... **"nimetekeleza agizo lako la kugawa mashamba ya chai"** baada ya kufanyika zoei la ugawaji wa ardhi na shughuli za kilimo kuanza, yalijitokeza malalamiko ya wafugaji kudai maeneo yao yaligawiwa pasipo kuwahusisha wao kama wafugaji. Malalamiko hayo yalitolewa katika kikao cha wafugaji mnamo tar 28/02/2015 na kudai kuvunjiwa eneo lao la Igaba, Kuvunjiwa zizi la chanjo bila taarifa ambapo eneo hilo liligawiwa kwa wakulima, Kutishiwa amani na wakulima waliogawiwa eneo la wafugaji.

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa wilaya ambae alitoa agizo la utoaji ardhi ameshindwa kutatua mgogoro huu hadi sasa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Mkuu wa Wilaya anahusika pia kujipatia eneo kwa majina ya tofauti ili kuweza kujinufaisha yeye binafsi. Mkurugenzi wa Halmshauri ya Mji pia ameshindwa kutatua mgogoro huu kwa kuwa anamlinda Mkuu wa Wilaya. Matokeo yake, kuna uhasama mkubwa baina ya Wakulima na Wafugaji jambo ambalo limesababisha kutoweka kwa amani na utulivu kwa makundi haya ya jamii.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu hapa ili wananchi wa Njombe, Kijiji cha Kifanya chenye wakulima na wafugaji kujua nini hatma ya ardhi yao. Pili ni hatua gani stahiki zimechukuliwa baada ya malalamiko ya wananchi kupelekwa kwa Mkurugenzi chini ya kamati ya Uchunguzi ya Kijiji ambayo imeonesha uvunjifu wa sheria ya ardhi uliofanywa na mwenyekiti wa Kijiji Kifanya pamoja na Mkuu wa Wilaya?

9. MIGOGORO YA ARDHI BAINA YA WANANCHI NA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

Mheshimiwa Spika, Suala la migogoro ya ardhi baina ya wananchi na Wizara ya Maliasili na Utalii sio jipya katika Bunge lako tukufu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imelizungumzia mara kadhaa kama sauti ya wasio na sauti, na kamwe, Kambi ya Upinzani haitachoka kulizungumzia kutokana na vipigo mauaji, na uharibifu wa mali unaoendelea kuwakumba wananchi, huku Wizara ya Maliasili na utalii ikiratibu na kusimamia uhalifu huo dhidi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kumbu kumbu zinaonyesha kwamba toka mwaka 1994 wananchi hawa wanahangaika bila mafanikio! Hakuna ofisi ya serikali hii ya CCM yenye mamlaka ya kushughulikia suala hili ambayo hawajafika!! Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inajua (suala hili lilishughulikiwa na Ndugu George M. Masaju, (Mwanasheria Mkuu wa sasa, kipindi hicho akiwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali), Wizara ya Ardhi inajua, wananchi hawa walishafika mpaka hata ofisi ya Rais!!

Mheshimiwa Spika, wewe ni shuhuda wa malalamiko ya wabunge dhidi ya ukatili unaoanywa na wanaojijita maafisa wanyamapori na wahifadhi wa misitu!!

Mheshimiwa Spika, mawasiliano baina ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya tarehe 21/4/1994 yenye kumbukumbu namba MD/F.40/1/28 juu ya malalamiko ya kitongoji cha Nzansa, kijiji cha Chanika, wilaya ya Ilala kufukuzwa kwenye eneo linalopakana na hifadhi ya msitu wilaya ya Kisarawe, yanakiri kwamba wanakijiji walihamia hapo tangu mwaka 1954, wakati eneo la misitu lilikuja kupimwa mwaka 1993 na kwa kusimamiwa na Afisa Maliasili wa Mkoa wa Pwani, Ndugu Kessy.

Mheshimiwa Spika, barua toka ofisi ya Rais, ya tarehe 10/6/2008 yenye kumbukumbu namba CEA 110/302/IV/01 kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi juu ya malalamiko ya wakulima wa (Chanika-Nzasa), pamoja na mambo mengine, inakiri kwamba Hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi ilianzishwa na Gavana E.F Twining kwa tangazo la serikali Na. 306 lililochapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 septemba 1954.

Na kwamba Tangazo hilo liliweka Mipaka ya Hifadhi ya msitu wa Kazimzumbwi kwa kutaja vipimo vya maeneo ya Mipaka (Nakala ya tangazo imeambatanishwa).

Mheshimiwa Spika ukipitia ramani (Kama ilivyotolewa na Wizara ya Ardhi-wizara yenye dhamana ya kusimamia upimani na utayarishaji wa ramani nchini), ni ukweli ulio dhahiri kwamba wananchi hawa wako nje kabisa ya mpaka wa hifadhi!! Katika mbinu za kitapeli na uharamia dhidi ya wananchi wizara ya maliasili na utalii imekuwa ikitumia Government Notice No. 156/1997 iliyochapishwa katika Gazeti la serikali la tarehe 20 Mei 1997 (The Kazimzumbwi Forest Reserve (Removal of Unlawful Occupants and cessation of unlawful Activities) Rules 1997 wakidai wananchi hao wamevamia msitu!!

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa amri hii (kwa tafsiri) unawahusu tu wale wananchi walio ndani ya hifadhi! Wizara ya maliasili na utalii inatumia ubabe wa amri hii, pasipo kuwa na ujasiri wowote wa kufanya rejea ya Tangazo lililoweka mipaka ya hifadhi!. Cha kushangaza zaidi vijiji vya Vibura (Nzasa), Maguruwe na Vijibweni ambavyo viko ndani ya hifadhi havijaguswa!!

Mheshimiwa Spika, taarifa ambazo Kambi ya Upinzani inazo ni kwamba, kuna mchezo mchafu uko nyuma ya pazia. Nasema hivi kwa sababu wakati Wizara hii hii inafukuza na kuua wananchi kwa barua yake yenye kumb. Na. MTNREF/F/40/5/67 ya tarehe 30 Desemba 199, ilimjulisha Mwenyekiti wa Chama Cha Msaada wa Kisheria, Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwamba wananchi wa Nzasa wako nje ya Hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi na hivyo wananchi hao wasihofu kwa kuwa hawahusiki na zoezi la kuwaondoa wavamizi wa msitu!

Mheshimiwa Spika, Nikinukuu barua tajwa hapo juu, yenye kichwa cha habari **“Kazimzumbwi Forest Reserve Apprehension of Nzasa Villagers”**, kifungu cha pili kinasema, hivi: nanukuu,

“ It is true that the Government intends to evict encroachers from Kazimzumbwi Forest Reserve and wish to assure you that Nzasa Village is outside the Reserve, as such Nzasa Villagers have nothing to fear about the intended evictions” mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Suala la kujuliza: kama Nzasa Chanika ipo ndani ya eneo la hifadhi ya masitu (ambayo iko kisarawe, mkoa wa Pwani):

- i) Mbona ni kijiji kinachotambulika rasmi na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala (jimbo la Ukonga)?

- ii) Kama eneo la Kijiji cha Nzasa kimo katika hifadhi ya msitu mbona Kamishna wa madini amekuwa akitoa vibali vya machimbo ya mchanga katika eneo hilo?
- iii) Ikiwa eneo la kijiji cha Nzasa limo katika hifadhi ya misitu inakuwaje basi maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya huduma ya jamii katika kijiji hicho sasa hivi yanachukuliwa na watu wengine kwa ajili ya shughuli nyingine hatua ambayo imelalamikiwa na wakulima wa kijiji hicho cha Nzasa?
- iv) Na ikiwa kijiji cha Nzasa kimo katika eneo la hifadhi ya msitu, mbona wananchi wakulima wakazi wenyewe wa kijiji hicho ndio wako mstari wa mbele kutaka hatua zichukuliwe ili kuzuia uharibifu wa mazingira?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo kimsingi ndiyo yenye mamlaka ya usimamizi wa ardhi wa nchi hii kuliangalia suala hili kwa jicho la ziada. Wizara ya ardhi ina nyaraka zote zinazohusiana na mgogoro huu. Kama waziri kivuli niliwasilisha nyaraka nyingine kwa msisitizo!!Kuna upotoshwaji mkubwa sana unafanywa na wizara ya Maliasili na Utalii, na mbaya zaidi hata kamati yako ya Bunge ya ardhi na maliasili inapotoshwa na Wizara!.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima ya aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ukonga (ambaye naye alipambana sana bila mafanikio), Marehemu Eugene Mwaiposa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mhe. Waziri atoe kauli ya serikali hapa Bungeni juu ya mustakabali wa wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, nyaraka za migogoro ya Msitu wa Kazimzumbwi kati ya wananchi ha Wizara ya Maliasili na Utalii zimeambatanishwa katika hotuba hii katika **vielelezo na. 4,5,6,7 8,9,10 na 11.**

10. JESHI NA UPORAJI WA ARDHI KIJIKI CHA TONDOLONI (MKOA WA PWANI) NA KIJIKI CHA IHUMWA (DODOMA)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kazi nzuri inayofanywa na jeshi letu la kulinda mipaka ya nchi yetu. Halikadhalika, kazi nzuri inayofanywa katika kushiriki katika operation mbali mbali za kulinda Amani katikabara la Afrika na kwingineko duniani. Hata hivyo, Bunge lako tukufu limeshuhudia malalamiko ya wabunge kwa upande (kama wawakilishi wa wananchi kwa upande mmoja) na serikali (kupitia wizara ya ulinzi kwa upande mwingine), wabunge wakidai jeshi liinangia kwenye maeneo ya raia, serikali kwa upande mwingine ikidai wananchi ndio wanaovamia maeneo ya jeshi. Hoja zote mbili zina ukweli kwa namna Fulani.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepokea taarifa ya migogoro mbali mbali inayolihusu jeshi kuvamia maeneo ya wananchi, kutokana na ufinyu wa muda tutaongelea migogoro '2' (Kijiji cha Tondoloni-Kisarawe Mkoa wa Pwani na Kijiji cha Ihumwa, Mkoa wa Dodoma) ambayo inafukuta sana . Ni matarajio yetu, serikali kupitia wizara ya ardhi na wizara ya ulinzi, itatumia busara ya hali ya juu kumaliza fukuto hili!! Hatuwezi ruhusu walinzi wetu wa Amani ambao tunawategemea wawe chanzo cha uvunjifu wa amani nchini!.

Mheshimiwa spika, Kijiji hiki cha Tondoloni, kilianza mwaka 1960, wananchi walianza kuishi hapo kabla ya uhuru. Mwaka 1986 wanajeshi walikwenda kuomba kufanya tathmini ili kuwalipa fidia kwa madhumuni ya kuongeza eneo la jeshi. Tathmini ilifanywa ikiwahusisha **wanakijiji 1, 508**. Hakuna fidia yoyote waliyolipwa, baada ya malalamiko Wananchi walipokea barua toka ofisi ya ardhi na makazi ambayo ilielekeza wananchi walipwe ndani ya miezi mitatu na kwamba miezi mitatu ikipita haitambuliki tena. Tathmini husika ilikuwa tarehe 21/10/1992.

Mheshimiwa Spika, Hakuna fidia yoyote iliyolipwa, mpaka mwaka 1998 ambapo wanajeshi walikwenda kuharibu mazao ya wananchi na kukata miti ya kudumu. Taarifa ilitolewa kwa Mkuu wa mkoa kipindi hicho Prof. Philemon Sarungi. Mchakato wa utatuzi ulikwama baada ya Mkuu huyo wa Mkoa kuhamishwa kituo cha kazi. Mwaka 1999 barua iliyotoka ofisi ya afisa tawala mkoa ilielekeza kwamba endapo serikali ilikuwa inahitaji eneo la wananchi, lazima tathmini ifanyike upya. Kwa maelezo ya wananchi, hakuna tathmini yoyote iliyofanyika; ila kilichoendelea ni wananchi kupigwa, kuharibiwa mali zao na JWTZ kikosi No 83, wananchi wakipeleka malalamiko yao katika mamlaka mbali mbali za serikali ...hawasikilizwi!!

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa kuna mgogoro mkubwa, wananchi wanapigwa risasi (uthibitisho upo), nyumba zinavunjwa, mazao ya kudumu yanang'olewa...wananchi wanaishi katika ardhi yao kama wanyama! (Nyaraka zote zimeambatanishwa kama sehemu ya hotuba hii).

Mheshimiwa Spika, kadhia kama hii imekikumba pia kijiji cha Ihumwa, ambapo jeshi la wananchi JWTZ wamechukua mashamba ya wanakijiji na kuanza kujenga nyumba pasipo kuwalipa fidia. Kijiji hiki kilisajiliwa kwa sheria za ardhi na vijiji mwaka 1971, kikiwa na hati miliki Na. DO/KJ/IHM/353. Ikumbukwe kwamba Wananchi wa maeneo haya wanategemea kilimo kwa maisha yao hivyo kuchukua ardhi yao bila fidia ni kutaka kukatisha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kuthibitisha kwamba eneo husika halikuwa la jeshi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina barua toka Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ya tarehe 30/1/1987 na tarehe 1/1/1989, kwenda kwa mwenyekiti wa kijiji cha Ihumwa. Barua husika inaomba eneo la kijiji cha Ihumwa (kwa matumizi ya Muda) kwa ajili ya mafunzo ya askari waenda kwa miguu daraja la tatu katika eneo la kijiji kaskazini mwa barabara kuu iendayo Dar es salaam .(Barua husika zimeambatanishwa). Wanakijiji hawa wamehangaika bila mafanikio na hata walipowasilisha taarifa wizara ya ardhi, hakuna hatua zozote zilizochukuliwa, wanashangaa walipoandikia barua wizara kuikumbusha juu ya mgogoro husika, walijibiwa kwamba waliitwa kutoa ushahidi lakini hawakutokea (jambo ambalo sio kweli)!

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kinashangaza zaidi, ni kwamba; barua ya Wizara ya ardhi, ya tarehe 27 Novemba 2014 yenye kumbukumbu namba MLHSD-C/PODM/76, inaeleza kwamba jeshi la wananchi liliwasilisha Ramani iliyoidhinishwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani tarehe 30/05/1985. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji: Kama ramani ilishabadilishwa (kienyeji mwaka 1985 bila kukishirikisha kijiji) iweje basi jeshi hilo hilo, mwaka 1987 kupitia kwa Captain ALLY PSC (KNY Kamanda Rejimenti) na na mwaka 1989 kupitia Captain R.J. P.S.C waandike barua ya maombi ya ruhusa ya kufanya mafunzo? Utaombaje ruhusa kwenye eneo ambalo tayari ni la kwako?

Mheshimiwa Spika, kama kweli eneo husika lilishatwaliwa na jeshi toka mwaka 1985, (kama maelezo ya wizara ya ardhi yanavyoainisha, iweje basi mwezi Februari mwaka 2013, Brigedia Mndeme amteue Captain Manyiga na Coplo Halid na CP Kibonde kufanya uhakiki wa mashamba wakishirikiana na viongozi wa kijiji na wakulima kwa madhumuni ya kulipa fidia? Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, kwa migogoro ya ardhi kati ya jeshi na wananchi wa Tondoloni mkaoni Pwani na Ihumwa mkoani Dodoma, tazama **vielelezo na. 11, 12, 13 na 14.**

11. UVAMIZI WA ARDHI YA TAZARA

Mheshimiwa spika, wakati tukishuhudia wizi , udanganyifu na ufasadi katika zoezi la kuuza nyumba za TAZARA (Tanzania Zambia Railway Authority) kama ilivyobainishwa katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, katika Wizara ya Uchukuzi, Mhe. Mosses Machali, mali za serikali kugeuzwa shamba la bibi imeikumba pia ardhi ya Tazara ambayo imegawanywa vipande vipande.

Mheshimiwa Spika, Ardhi hii iliachwa wazi kwa ajili ya matumizi ya baadaye pale ambapo mamlaka ingepanuka kibiashara hivyo kuweka vitegauchumi vingine zaidi, halikadhalika kwa matumizi ya umma (masoko, parking, viwanja vya michezo na bustani).

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kawaida kwa serikali ya chama cha mapinduzi kushindwa kulinda mali ya umma. Uchunguzi uliofanywa katika eneo la Dar es salaam (Yombo – Kurasini) umegundua kwamba kuna nyumba zaidi ya 600 zimejengwa ndani ya ardhi ya mamlaka. Mgololo zaidi ya hektab 40 za ardhi imevamiwa na sasa limepandwa miti na kuna makazi ya watu pia. Uvamizi wa aina hii umeshamiri pia Makambako, Ifakara na maeneo mbali mbali ambayo yaliachwa mahsusi kwa malengo fulani. (Taarifa ya uchambuzi husika imeambatanishwa kama sehemu ya hotuba hii). Mheshimiwa Spika katika kudhihirisha kwamba wavamizi walikuwa wanajua wanachokifanya mawe yaliyokuwa yanaainisha mipaka (beacons) yameng'olewa ili kufuta ushahidi.

Mheshimiwa spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka waziri wa ardhi kuliambia Bunge hili tukufu, katika miezi 3 iliyobaki ya utawala wa CCM, atalishughulikiaje tatizo hili ili kuokoa ardhi hii muhumu.

12. WAMILIKI WA MASHAMBA MAKUBWA HAWALIPI KODI YA ARDHI

Mheshimiwa Spika, wakati migogoro ya ardhi ikifukuta nchi nzima kutokana uhaba wa ardhi kwa matumizi ya shughuli za kilimo na ufugaji, imebainika wamiliki wengi wa mashamba makubwa, wamekuwa wakiikosesha serikali mapato, kwa kutolipa kodi ya ardhi kama matakwa ya Sheria ya Ardhi No.4 ya mwaka 1999 inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu watafiti uliofanywa na Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2013 kwa kutembelea mashamba 964 yenye ukubwa wa takriban **ekari 3,706,757** umebainisha kwamba wamiliki wa mashamba 642 kati ya mashamba 964 yaliyotembelewa walishindwa kuthibitisha kama wamelipa kodi ama la katika kipindi cha mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, katika hali inayoonyesha ukosefu wa umakini kwa upande wa serikali, na hususan Wizara ya Ardhi utafiti umebainisha kwamba hakuna uwazi katika malipo ya kodi ya ardhi kutoka kwa wamiliki wa mashamba na kwamba kati ya hao wachache waliosema wamelipa kodi (wamiliki ma mashamba 322) zaidi ya 79% waliishindwa kutoa risiti kuthibitisha hilo, walioweza kutoa risiti ni 13% tu!

Mheshimiwa Spika, halikadhalika utafiti umegundua kwamba 43.47% ya wenye mashamba waliohojiwa walikiri kwamba hawajawahi kulipa kodi ya ardhi toka walipomilikishwa mashamba hayo!. Hii inaonyesha kwamba, hata wale watu ambao wanamiliki ardhi kihalali, uhalali wa umiliki wao una mashaka kutokana na kutokidhi takwa muhimu la kumiliki ardhi husika ambalo ni ulipaji wa kodi ya ardhi.

13. KODI INAYOPOTEA KUTOKANA NA UKIUKWAJI WA SHERIA YA ARDHI

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 33 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, kinatamka kwamba, mwenye hati miliki anatakiwa, pamoja na masharti ya vifungu vingine vya sheria hiyo, kulipa kodi ya mwaka kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Fedha za Umma (Public Finance Act).

Mheshimiwa Spika, kwa idadi pekee ya mashamba yaliyotembelewa, Serikali inapoteza zaidi ya shilingi **bilioni 3.7** kwa mwaka kutokana na kutokusanya kodi ya ardhi. Ikumbukwe kwamba wamiliki wa mashamba wanatakiwa kulipa kodi kiasi cha shilingi 1000tu kwa ekari 1 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, utafiti umeonyesha kwamba kwa mwaka 2012 kati ya shilingi **bilioni 3.7** zilizotakiwa kulipwa wenye mashamba walilipa shilingi **milioni 130 tu (3.5%)** ya kodi yote iliyotakiwa ilipwe! Utafiti huo pia unaonesha kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotoza kiasi kidogo sana cha kodi ya ardhi duniani.

Mheshimiwa Spika, Ukiukwaji huu wa sheria ni sababu tosha ya ya kuwafutia umiliki wenye mashamba ambao hawalipi kodi ya ardhi. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kuwafuatilia wamiliki hawa wa mashamba makubwa ambao hawalipi kodi ya ardhi na kuacha kuwakandamiza watu masikini wa Chasimba, Kapunga na Kigamboni. igamboni n.k.

14. SOKO LA NYUMBA NA UMUHIMU WA NYUMBA KATIKA KUKUZA UCHUMI

Mheshimiwa Spika, Sekta ya nyumba katika nchi zilizoendelea inachangia kati ya asilimia 50 mpaka 70 ya Pato la Taifa kwa mwaka. Tanzania inakabiliwa na changamoto ya uhaba mkubwa wa nyumba bora ambao unakadiriwa kufikia nyumba 3,000,000. Pengo la mahitaji ya nyumba linakadiriwa kukua kwa takriban nyumba laki 2 (200,000) kwa mwaka. Upungufu wa nyumba ni mkubwa zaidi sehemu za mjini ambako asilimia 37.5 ya watanzania ndiko wanakoishi. Shirika la nyumba la Taifa likiwa chombo cha serikali, lilitarajiwa kukabiliana na changaoto hii, hata hivyo mzigo wa kodi unakuwa kiwazo kikubwa cha ufanisi wa shirika hili, hali inayopelekea shirika kuhudumia watu wenye kipato cha juu na kipato cha kati.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa linakabiliwa na Mzigo wa kodi/makato mbalimbali kama ifuatavyo:

- i. 10% ya mapato yao ya mwaka - Mfuko mkuu wa hazina kushindwa kupeleka kunapelekea penalty ya 5%
- ii. Kodi ya makampuni ya asilimia 30%
- iii. Kulipa gawio la shilingi milioni 300,

- iv. Riba kwa mkopo wa ujenzi wa asilimia 16%
- v. Hakuna ruzuku ya aina yoyote toka Serikali kuu,
- vi. Kodi zingine kama vile; Kodi ya ongezeko la thamni-VAT, Kodi ya Ardhi (*Land rent*), Kodi ya Mengo (*Property Tax*), Kodi ya Zuo (*withholding Tax*), Kodi ya halmashauri (*City Service Levy*), na Kodi ya Veta (*Skills and development levy*).

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Bunge lako tukufu lilipitisha kodi ya zuio (*withholding tax*) ya 10% . Kodi hii ilianzishwa mahsusi kwa lengo la kuzitaka taasisi za umma, mashirika ya umma, wakala za serikali n.k kuchangia 10% ya mapato yao ya mwaka katika mfuko mkuu wa hazina. Kutokana na takwa hili la kisheria, Shirika la nyumba linalazimika kuazima fedha/kukopa fedha kuweza kutimiza takwa hilo la kisheria kwa sababu faida wanayoipata kwa mwaka ni pungufu ya kiasi cha fedha kinachohitajika.

Jedwali hapo chini linaonyesha hali halisi baada ya kuanzishwa kwa Kodi ya zuio

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2014 kutokana na mauzo ya nyumba shirika la nyumba linatarajia kupata mapato (*Gross Revenue*) ya **shilingi 176,875,348,298**. Hii inamaanisha watawajibika kuilipa serikali, **shilingi bilioni 17** kama **10%** ya mapato yao ya mwaka kwa kupitia mfuko mkuu wa hazina. Kutokana na ukweli kwamba Shirika la nyumba linakopa fedha za ujenzi kwa Riba ya 16% kwa mwaka, malipo haya ya shilingi bilioni 17 kwa serikali yanaipunguzia uwezo wake wa kukopa kwa shilingi **bilioni 110.5**.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kodi ya zuio kwa Shirika la Nyumba kumepunguza uwezo wake wa kujenga nyumba kwa 40% kwa mwaka. Kwa taarifa tu, kama Bunge lako tukufu lilikuwa halijui kwa malipo ya hizo shilingi bilioni 17, Shirika la nyumba linapoteza uwezo wa kujenga **nyumba 3,071** (kwa gharama ya shilingi 36 milioni kwa kila nyumba) kutokana na vikwazo katika mzunguko wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali ingeweza kupata mapato zaidi kama ingeiruhusu NHC kuwekeza kiasi hicho katika ujenzi wa nyumba. Kwa gharama ya shilingi milioni 36 kwa nyumba 3,071, serikali ingekuwa na uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi 26 bilioni kutoka kwenye kodi, achilia mbali faida za kijamii zitakazopatikana kutokana na ujenzi wa nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, Ni muhimu ikaeleweka kwamba mzigo huu wa kodi mbali unaathiri kwa kiwango kikubwa ufanisi wa shirika, una athari kubwa kwa mlaji, mtanzania wa kawaida anayetarajiwa kupanga au kununua nyumba za shirika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kufanya yafuatayo:

- 1) Kulisaidia shirika la nyumba kuweza kumiliki sehemu kubwa ya ardhi kwa gharama nafuu au kupewa bure, kwa kufanya hivyo itasaidia kupunguza gharama ya nyumba ambazo zinajengwa kwa ajili ya kuziua kwa wananchi wa kipato cha kawaida
- 2) Kuondoa/kupunguza kodi ya vifaa vya ujenzi ili kuwawezesha watazania kujenga /kununua nyumba bora kwa gharama nafuu.

15. MASTER PLAN JIJI LA MWANZA NA ARUSHA

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani inatambua kazi inayofanywa na wizara ya ardhi yenye madhumuni ya kuendeleza jiji la Mwanza na Arusha. Halikadhalika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba wizara ya ardhi imeingia makubaliano na kampuni ya Singapore Cooperation Services ambayo imepewa jukumu la kutoa ushauri wa kitaalam wa uendelezaji wa jiji la mwanza.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano ya awali gharama za utengenezaji wa Master Plan ya jiji la Mwanza zilikuwa \$ **4,131,010.00** (Bila ya kujumuisha Kodi) wakati jiji la Arusha makubaliano ya awali yalikuwa \$ **4,541,210.00** (Bila kujumuisha kodi). Katika hali ya kushangaza, katika jiji la Mwanza gharama zikaongezeka mpaka kufikia \$ **4,483,095** halikadhalika jiji la Arusha gharama zimeongezeka kufikia \$ **4,927,415**. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge sababu za ongezeko hilo.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa kifungu cha 4.1 cha makubaliano baina ya wizara ya ardhi na Mtaalam Mshauri kuhusiana na suala la Kodi (Clarification on tax liabilities issues) ilikubalika kwamba litakuwa jukumu la mtaalam mshauri (Consultant) 'kulipa kodi' na tozo kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi!

Mheshimiwa Spika, Katika hali ya kushangaza 'Invoice' (Invoice No: 20114088) ya tarehe 18/2/2015 toka kwa Mshauri Mtaalam (Consultant) kwenda wizara ya ardhi, inayodai malipo (kwa ajili Mwanza Master Plan) ya hatua ya kwanza ambayo ni 15% ya fedha kama walivyokubaliana kwenye 'mkataba' (15% of the Contract value (15% x 4,483,095) inaonyesha kwamba kodi (Local taxes) sio tena jukumu la Mshauri mtaalam huyo, bali jukumu la Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali ilieleze Bunge hili tukufu, kwa kinaga ubaga, ni lini na kwa mkataba upi jukumu la kodi lilihama kutoka kwa mshauri mtaalam kwenda kwa serikali ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika Kuna taarifa pia kwamba hata hiyo fedha iliyolipwa (15%), imelipwa kabla kazi katika hatua ya kwanza haijakamilika.

Makubaliano ya malipo yako katika hatua saba, katika mgawanyo wa (i) 15% (ii) 15% (iii) 25% (iv) 15% (v) 10% (vi) 5% (vii) 15%. Na katika kila hatua malipo yanafanyika baada kazi iliyotakiwa kufanyika katika hatua husika kukamilika. Makubaliano yanaelekeza kwamba: *“15% of the lumpsum amount shall be paid upon submission and approval of the inception report and Base Mapping.”*

Mheshimiwa Spika, Kwa taarifa ambazo Kambi ya Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, malipo yaliyofanyika kwa njia ya electronic ya tarehe 15/04/2015 (Legal Receipt number 048-048VC14003705 na 048-048VC14003615) ya jumla ya shilingi 1,118,857,334 yalifanyika kabla ya kuwasilishwa na kuthibitishwa kwa inception report na base mapping! Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka maelezo kuhusu jambo hili!

16. SERIKALI YA CCM NA MIPANGO MIJI

Mheshimiwa Spika, Idadi ya watu wanaoishi katika maeneo ya mijini kwa upande wa Tanzania bara imeongezeka kutoka kutoka 5.7% mwaka 1967 hadi 29.1% mwaka 2012 . Kiwango cha ukuaji wa miji kimekuwa ni kikubwa kuliko uwezo wa mamlaka husika kutoa huduma za viwanja vilivyopangwa kwa makazi na shughuli za maendeleo ya miji. Mheshimiwa Spika, katika jiji la Dar es salaam pekee linalokadiriwa kuwa na nyumba 500,000!. Tafiti zinaonyesha kwamba kati ya ‘hizo’ nyumba 400,000 zimeendelezwa katika maeneo yasiyopangiliwa au makazi yasiyo rasmi ambayo hayajapimwa!

Mheshimiwa Spika, Hali kama hii ipo pia katika majiji ya Mwanza na Arusha, hali hii imesababishwa na 88% ya waendelezaji katika maeneo ya kupata viwanja kutoka katika masoko ya ardhi yasiyo rasmi!!

Mheshimiwa Spika, Hali hii haijatokea kwa bahati mbaya!! kwani miaka 54 baaya ya uhuru 80% ya miji haina /haijawahi kuwa ‘General Planning Schemes’. Kati ya miji 148 iliyofanyiwa utafiti, miji 96 (65%) haijawahi kuandaa/kutayarisha Master Plan tokea ianzishwe, miji 52(35%) zina Master Plan lakini ambazo zimepitwa na wakati na hazijawahi kupitiwa upya!

Mheshimiwa Spika, Imegundulika kuwa ni 20% ya Planning Authority zilizogundulika kuwa na ‘planning scheme’ lakini utekelezaji wake umekwenda kinyume kabisa na kile walichokipanga! Kwa mfano, katika jiji la Dar es salaam ambapo Master Plan ya mwaka 1979 ilipanga eneo la Mwenge na Mbezi kama eneo la viwanda, wakati wa utekelezaji hali ikawa tofauti!

Mheshimiwa Spika, Ni dhahiri kabisa kwa usimamizi huu duni wa mipango miji, licha ya uwepo wa sheria ya Mipango miji Na. 8 ya 2007 na Uanzishwaji wa idara ya uendelezaji Miji ndani ya wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo ya makazi, Tamisemi na mamlaka ya serikali za Mitaa unaonyesha ni kwa kiwango

gani wizara ya ardhi na TAMISEMI zilivyoshindwa kusimamia kazi. Kuna ulazima mkubwa sasa , kama nchi kuangalia upya sheria, halikadhalika uwezo mamlaka za kupanga miji!

Mheshimiwa Spika, Katika Jiji tu la Dar es salaam tuna mamlaka za upangaji 4 tofauti za kupanga miji!, kila moja ina mamlaka ya kupanga halikadhalika mamlaka ya kubadilisha matumizi ya ardhi! . Haiwezekani katika karne hii kamati za mipango miji za halmashauri ambazo hazina utaalum wowote kupewa majukumu ya kitaalam ya upangaji wa mji. Lazima kuwe na mipaka!!

Mheshimiwa Spika, Ni lazima mamlaka zinazotoa huduma (Tanesco, TTCL, Dawasco, Tanroad etc) zishirikishwe katika michakato yote ya Mipango miji, katika kila hatua!kutokana na sheria za sasa kutokutambua ushirikishwaji wa vyombo vingine vinavyotoa huduma, katika kipindi cha mwaka mmoja, serikali (Tanroads) imepoteza shilingi **bilioni 28.53** kama gharama za ziada kwa malipo ya fidia na kuhamisha miundombinu. Hatuwezi kuendelea na utaratibu huu!!

17. ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI 2010-15 NA HILA ZA CCM

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeshuhudia wanaojiita 'watia nia' wa Chama Cha Mapinduzi wakitangaza nia , kwa mbwembwe nyingi na kama kawaida yao wakiwaahidi watanzania maziwa na asali! Cha kushangaza watia nia wote ambao wakiwa mbele ya Bunge lako tukufu wamekuwa mstari wa mbele kutetea kile wanachokiita 'mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya CCM', wakati wanatangaza nia huko mitaani, wanageuka ghafla wapinzani kwa kukosoa ufanisi wa utendaji kazi serikali hiyo hiyo wanayoiongoza!

Mheshimiwa Spika, Ili tuweze kupima ufanisi wa hiki chama...pamoja na wagombea wake ni muhimu basi tujiridhishe nini walichoahidi katika ilani na nini walichofanikiwa kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya CCM iliwaahidi watanzania kufanya yafuatayo:

- 1) Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi , wenye Program 12 ambazo ni progam ya kuimarisha TUME, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Mitu, Wanyamapori, Madini, Nishati , Miundombinu, Rasilimali maji, Utalii na uwanda/uoto asili kwa lengo la kukamilisha kazi ya upangaji wa matumizi bora ya ardhi nchi-
- 2) Kuandaa utaratibu wa kuwawezesha wananchi wasio na ardhi katika maeneo mengine ya nchi
- 3) Kuziwezesha Halmashauri za miji na wilaya zote nchini kuweka na kuutumia mfumo wa kutumia teknolojia ya kompyuta katika kutoa huduma za ardhi kwa kuimarisha na kuboresha utunzaji wa

kumbukumbu za upimaji ardhi na kuzibadilisha kutoka mfumo uliopo sasa kuwa wa keelektroniki,

- 4) Kushirikiana na Halmashauri za miji na wilaya kutambua ardhi kwa ajili ya kuanzisha Hazina ya ardhi (Land bank) kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi,
- 5) Kuzijengea uwezo Halmashauri za miji na wilaya ziweze kupima viwanja vingi na kuuza kwa wanaohitaji kwa kutumia mfuko wa mzunguko (Plot Development Revolving Fund),
- 6) Kuboresha utendaji kazi wa mabaraza ya wilaya ya ardhi na Nyumba 39 yaliyopo na kuanzisha mabaraza mapya 50 (wastani wa mabaraza 10 kwa kila mwaka) kwenye wilaya zenye migogoro mingi ya ardhi na nyumba -
- 7) Kuzijengea uwezo Halmashauri za wilaya , miji na majiji kuajiri wataalam wa kutosha wa sekta ya ardhi na kununua zana za kisasa za kupima ardhi na usanifu-

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Nyumba, Serikali hii ya CCM iliwaahdi wananchi:

- 1) Kushirikiana na wakala wa Taifa wa utafiti nyumba bora na vifaa vya ujenzi (NHBRA) katika kufanya tafiti mbali mbali za vifaa vya ujenzi wa nyumba bora kwa teknolojia rahisi na gharama nafuu na kufikisha matokeo ya utafiti huo kwa wananchi-
- 2) Kuhakikisha kwamba ujenzi wa nyumba na majengo yanayotumiwa na umma unazingatia mahitaji maalum hususan ya watu wenye ulemavu,
- 3) Kuhakikisha kuwa jumla ya nyumba 15,000 (kwa wastan nyumba 3000 kila mwaka) zinajengwa na shirika la nyumba la Taifa (NHC) kwa kushirikiana na sekta binafsi-
- 4) Kuhimiza uanzishwaji wa vyama vya ushirika wa nyumba, na pia vikosi vya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu katika ngazi ya wilaya na Kata ili kuwezesha wananchi wa kipato cha chini kufaidika na mikopo ya nyumba -
- 5) Kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa masharti nafuu, kuwahamasisha

wananchi kuzielewa sheria ili wazitumie kupata mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya kujenga au kununua nyumba na kuhamasisha mabenzi ya vyombo vingine vya fedha kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba ya muda mrefu yenye riba nafuu

- 6) Kulielekeza Shirika la Nyumba la Taifa kuwa mwendelezaji ardhi mkubwa (Master Estate Developer) na kujenga nyumba nyingi kwa ajili ya kuuza au kupangisha kwa wananchi wote na HASA WATU WA KIPATO CHA CHINI NA CHA KATI),
- 7) Kutunga sheria itakayowataka wote wanaojenga nyumba bora na majengo mbalimbali mijini na vijijini kujenga miundombinu ya kuvuna na kutumia maji ya mvua,
- 8) Kukamilisha utungaji wa sera ya Taifa ya nyumba (Housing Policy)-
- 9) Kuandaa mpango wa kampeni wa kitaifa katika kila wilaya kuhakikisha kuwa wananchi wanajijengea nyumba bora-
- 10) Kuweka mazingira yatakayoweza ujenzi wa nyumba wa gharama nafuu-

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Mipango Miji, Serikali ya CCM iliwaahidi watanzania:

1. Kuanzisha mji wa kisasa wa kigamboni,
2. Kulitafutia ufumbuzi tatizo la mpaka baina yetu na chini ya Malawi katika ziwa nyasa-
3. Kutekeleza mradi kambambe wa kuweka kituo cha kupokea picha za satellite (satellite Imagery Receiving Station) kitaakachorahisisha upimaji wa ardhi yote nchini na pia kitarahisisha utayarishaji wa ramani kwa ajili ya matumizi mbali mbali.-

18. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kama ni kutapeliwa, wananchi wa Tanzania wametapeliwa ile mbaya na Serikali hii ya CCM kwa kuwa mambo yote waliyoahidi kwa wananchi, katika sekta ya ardhi na makazi, ahadi nyingi zimebaki kuwa ngonjera, utekelezaji HAKUNA!

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu ya propaganda na upotoshaji mkubwa unaofanywa na wanaotangaza nia ya kugombea urais kupitia CCM kwamba watawaletea wananchi neema wakati walikuwa viongozi wakubwa Serikalini kwa miaka mingi na wakashindwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshtushwa sana kumsikia aliyekuwa Waziri Mkuu wa Zamani Edward Lowasa akiwaambia wananchi, wakati akitangaza nia ya kugombea urais kwamba: atapambana na ufisadi iwapo atakuwa rais wakati Serikali yake ilianguka kwa kashfa kubwa ya ufisadi katika sakata la Richmond. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepigwa butwaa kumsikia pia Waziri wa Kilimo akiwahadaa wananchi kwamba akiwa rais atahakikisha kwamba jembo la mkono litawekwa kwenye makumbusho akimaanisha atawapa wananchi matrekta ili waachane na jembe la mkono. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, kwanini asiwapatie wananchi matrekta hayo sasa tena ukizingatia ndiye waziri wa Kilimo? Tulinshangaa pia aliposema atapambana na rushwa nchini wakati yeye mwenyewe alishawahi kutiwa hatiani na mahakama kwa kutoa rushwa katika uchaguzi wa ubunge na hivyo kuvuliwa ubunge na kusimamishwa asigombe nafasi yoyote kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inawaonya wagombea urais wa CCM ambao walikuwa Serikalini na wakatimia nafasi zao kuwasababisha watanzania umasikini uliokithiri na sasa wanaufanya umasikini wa watanzania kama mtaji wao wa kisiasa. Tulinshangaa Mwigulu Nchemba akijigamba kwamba hakuusoma umasikini kwenye vitabu bali anaujua kwa kuzaliwa, lakini akiwa kama naibu waziri wa fedha halishauri taifa namna ya kuondokana na umasikini bali anasubiri kwanza awe rais ndio afanye hivyo. Inaingia akilini??! Hivi mmewageuza watanzania kuwa ni mazezeta kabisa kiasi cha kuwadanganya waziwazi namna hii?

Mheshimiwa Spika, ni kwa msingi huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawasihi wananchi, **in a very serious note** wapime hoja za upinzani kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya awamu ya nne ili wajue ni nani kati ya UKAWA na CCM wanastahili kupewa ridhaa ya kuongoza Serikali ya awamu ya tano.

MheshimiwaSpika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Halima James Mdee (Mb)
**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI NA WAZIRI KIVULI WA ARDHI,
NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

8 JUNI, 2015

SPIKA: Nawapa pole Watanzania kwa kupewa usanii wa kisiasa. (Kicheko/Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kuna wengine nitawaita mapema kwa sababu wana shughuli maalum wanatakiwa kusafiri sasa hivi. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Abdulkarim Shah, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul, halafu Mheshimiwa Henry Shekifu na Mheshimiwa Ndugulile wajiandae.

Mheshimiwa Shah halafu Mheshimiwa Gekul!

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, aliyeweza kutujalia sisi sote hapa leo kuwa na afya njema na kuweza kuja kutoa mawazo yetu kwa dakika hizi kumi ambazo tumejipangia wenyewe katika kuzungumzia mijadala ya Wizara mbalimbali na leo tuko katika Wizara hii ya Ardhi. Baada ya kumshukuru Mungu, nakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii kuwa mchangiaji wa kwanza katika kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ardhi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo ni Siku ya Kumbukumbu ya Azimio la Arusha. Toka mwaka 1967, leo mwaka 2015, miaka 48 baada ya kutangazwa Azimio la Arusha, Wanamafia wa Kijiji cha Gonge, Kijiji cha Ndagoni, Kijiji cha Chunguruma, Kijiji cha Kirongwe, Kijiji cha Jojo, Kijiji cha Baleni, Vitongoji vya Mkamba, Gonge A, Gonge B, Kipora, Sharaza, Nyamvula, Kidele, Mrundo na Kigomani, kuwa huru wa nafsi zao. Leo ni siku ya furaha na ninawaomba sana Wanamafia niliowataja, waliokuwa katika maeneo hayo, leo wajisikie huru na waone kazi tunazozifanya. Hatufanyi kazi kwa kulaghai watu na kutukana watu na kudhalilisha watu kwa shilingi 5,000/= au shilingi 10,000/=, kuwakusanya watu jioni, usiku na kuwahonga zile hela na kumtumia bepari aliyekuwa na yeye anawachangia wataka Ubunge wa kule kwenda kuwalaghai watu kwa kuwapa visenti tano tano, hela za haramu, wakati kila dini imetangaza rushwa ni haramu! (Makofi)

Sasa tunasema hayo ni ya kwao, sikiliza kazi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Msikilize Waziri Lukuvi, msikilize Naibu Waziri, bahati mbaya hamtomsikia Katibu Mkuu Kidata, Kamishna Mkuu wa Ardhi Kusiluka, Wakuu wa Idara zote, Makamishna wote, Mainjinia.

Mheshimiwa Lukuvi sina la kukwambia, sina la kukwambieni Wizara ya Ardhi, lakini nasema, Mwenyezi Mungu ndiye atakayekulipeni heri kwa niaba ya Wananchi wa Mafia. Ninawaomba Wanaisimani, hata kama ana mabaya gani aliyafanya Mheshimiwa Lukuvi katika Jimbo lake, lakini mfanyieni wema huu aliotusaidia sisi Wanamafia kuwa huru leo, basi mpeni heshima hii kwa kipindi

kijacho apate Ubunge na *Inshallah*, nakutabiria utapanda juu ya Wizara hiyo uliyoko na Mungu atakupa nafasi kubwa zaidi ya hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Shamba la Tumaini limetudhalilisha sana, tumetukanwa sana, nimedhalilishwa sana. Amedhalilishwa sana, namwonyesha kidole Mheshimiwa Lukuvi, ameambiwa eti alikuwa anataka kuhongwa na Muhindi mmoja bepari, nyang'au, dhalili, mwizi, jambazi wa ardhi, kuja kuwadhalilisha watu wakati eneo lile siyo la kwake! Sasa tunasema uhuru umepatikana na sasa leo Wanamafia tuko huru. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kutusikiliza na kusikia kilio chetu Watu wa Mafia. Mheshimiwa Rais, popote ulipo pokea shukrani zetu za Watu wa Mafia. Tunasema ahsanteni sana Wizara ya Ardhi na wote mlioshiriki katika kufanikisha kuwapa uhuru wana hawa wa vijiji hivi nilivyovitaja katika Wilaya ya Mafia.

Mheshimiwa Spika, sasa basi baada ya kutangaza leo shamba limefutwa, nisikilizeni vizuri Wanamafia; Waziri ameshatangaza, leo Shamba la Utumaini limefutwa, Hati imefutwa, Mali ya Serikali, liko chini ya Mheshimiwa Rais na Kamishna Mkuu wa Ardhi. Tusiwe na papara, kuweni na furaha. Ninachokuomba sasa Mheshimiwa Waziri, chomoka hapa tutoke hata kesho asubuhi twende Mafia tukawaambie Wananchi, ili isiwe sasa kila eneo wanalivamia. Kila mtu apate haki ya aneo aliloliendeleza na baada ya hapo na ninyi mtupangie mipango, ili maeneo yale ambayo wewe mwenyewe ulisema ya uwekezaji, yaweze kuchukuliwa na wawekezaji, wayaendeleze na kuleta tija katika maeneo ya vijiji hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, furaha niliyokuwanayo ni kubwa sana, eka 4,040 katika Kisiwa cha Mafia ni nyingi sana. Anakuja mtu anazichukua eti anajifanya yeye kapewa! Nilimwuliza wewe unaitwa nani? Ooh, mimi naitwa fulani! Mbona jina la Hati na hili tofauti? Ooh, mimi aliniuzia! Wapi? Ooh, mimi sijui, hakuna!

Mheshimiwa Waziri tunakushukuruni sana. Wanagonge na Vijiji vyote nilivyovitaja, nakuombeni sana, kazi mliyonituma, kazi tuliyoifanya tumemaliza. Sasa dhamira ya kwangu mnayo ninyi, kama mtaona zile shilingi elfu tano tano na kumi kumi za usiku ni bora, basi haya itakuwa Mungu kaandika, lakini kazi mliyonituma nimeifanya; Shamba limepatikana na hilo ni mali yenu na watapewa Watanzania na hakuna wa kubaguliwa. Maana pale walikuwa wanadhhalilishwa watu kwa makabila yao na ufukara wao, lakini leo uhuru umepatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, furaha niliyonayo ni kubwa sana. Sina la kusema, lakini tunamwomba sasa Mheshimiwa Waziri aje Mafia.

Tupangiye utaratibu mzuri wa kuja, wale wanaokaa wapate Hati Miliki hata hizi za kimila haraka iwezekanavyo, ili bughudha hii asije mtu mwingine akaanza kuja matajiri na kuanza kuja kuvamia na kuanza kuchukua na kujipimia. Hili jambo ni muhimu sana, naomba sana Mheshimiwa Waziri, lifanyike ili Wananchi hawa waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kusema, la kwangu lilikuwa hilo. Nasema Mheshimiwa nakushukuruni.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kwanza. Leo Wanamafia kazi mliyomituma, narejea tena, nimeifanya na sasa tuko huru, tutaishi kwa furaha na amani. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Hotuba hii, kwa asilimia zote 100 na kukutakieni kila la heri huko muendako na Mheshimiwa Angellah, Mungu atakujalia utafaulu tu katika uchaguzi huu, *Inshallah. (Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Pauline Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Henry Shekifu na Mheshimiwa Madabida!

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niseme machache katika Wizara hii. Namshukuru pia Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia afya njema tuendeleo kutekeleza wajibu wetu.

Nampongeza Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Halima Mdee, kwa Hotuba yake nzuri sana, ambayo amekuwa akigusia matatizo ya Watanzania popote pale walipo, hata kwenye vijiji amekuwa akiwasemea.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze katika Wizara hii. Kwa muda wa miaka mitano sasa, nimekuwa nikiongelea matatizo ya wananchi wa Babati na Wananchi wa Mkoa wangu wa Manyara. Kazi ya Mbunge yeyote ni kusema halafu Serikali watekeleze.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuwatia moyo wananchi wangu wa Mkoa wa Manyara kwamba, waendeleo kutuamini tuendeleo kuwawakilisha, tusemee matatizo yao, ili Serikali itende, kwa sababu Serikali inakusanya kodi, lakini pia ni wajibu wake. Waachane na wale Wabunge ambao wanasema Babati matatizo yamekwisha na niwahakikishie wananchi wangu wa Mkoa wa Manyara na wa Babati, kama nisingekuwa nawasemea Babati, basi Serikali isingejua Babati kuna nini. Kwa hiyo, tuwapuuze wale ambao wanasema Babati matatizo yamekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu nimeongelea matatizo ya ardhi Babati. Namshukuru Mheshimiwa Lukuvi, amenirudishia mashamba mengi sana. Nilikuwa nikizungumza matatizo ya mpaka katika Hifadhi ya Tarangire na Wananchi wa Gijedab Ayamango. Shamba la *UfyomiGalapo Estate* limerudishwa, Mheshimiwa Lukuvi ulifanya ziara pale. Kutoka moyoni mwangu, wananchi wale walikushukuru, wakasema tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu mpe cha kwake anachostahili; kwa muda mfupi Mheshimiwa Lukuvi amerudisha Shamba hili. Nilisema tukiwa kwenye Kikao cha RCC kwamba, Mheshimiwa Lukuvi, shamba ni eka 1,200, wale wananchi wanadai eka 17,000, Shamba halitoshi, nilimwambia na yeye anakumbuka, tulikaa kwenye Kikao cha RCC kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Mheshimiwa Lukuvi ukasema, Mheshimiwa Mbunge mlichoomba kwa Rais ni hiki, nimepigania kimerudi, lakini kama mna madai mengine na wale watu bado wanahitaji, maana yake tutaendelea kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili juzi tu ulivyosema tukae kwenye Kamati na Waziri, tukakaa na nakushukuru; tukazungumza na Mheshimiwa Nyalandu ameona tatizo la Babati kwa wale wananchi wa vile vijiji bado ni kubwa. Namwomba Mheshimiwa Lukuvi, aendeleo kwenda Babati asichoke, kwa sababu eka 17,000 hazijapatikana. Wizara ya Maliasili wamesema wako tayari kurudisha ule mpaka wa Tarangire urudi nyuma, kwa sababu ni kweli hawawezi kuwafidia eka 17,000 leo Babati watapata wapi?

Mheshimiwa Spika, eka 1,200 ulizotupatia mpaka sasa, zaidi ya eka 600 Wananchi walisha-occupy tangu zamani. Sasa unaona ni jinsi gani ambavyo tatizo hili bado ni kubwa sana. Naomba niendeleo kukuletea hili, kwa sababu nilishakwambia kwenye RCC na bado hujalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia Shamba la *RIVACU*, eka zaidi ya 4,300, kwa miaka mitano nimekuwa nikilisemea, hilo Shamba leo Mheshimiwa Waziri amemkabidhi Mkuu wa Mkoa, akamwambia wagawieni Wananchi ambao wana matatizo msigawane Viongozi. Shamba la Magugu eka 1,200, Mheshimiwa Lukuvi akaturejeshea amewapa Viongozi wa Mkoa, lakini mpaka leo Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya, hakuna chochote wanachokifanya! Wewe na Wizara yako mmefanya na nashukuru wananchi wote wanafahamu kwamba umewanyang'anya...

(Hapa kengele ililia)

MHE. PAULINE P. GEKUL: ...aah! ... kwamba, hilo Shamba sasa wakabidhiwe. Nikuombe Mheshimiwa Lukuvi, hebu mpigie Mkuu wa Mkoa umwulize ni kwa nini ulimwambia mwezi wa tano haya mashamba yawe yameshagawanywa kwa wananchi mpaka leo hawawapi? Wewe umefanya kazi yako.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Mheshimiwa Lukuvi, nilikueleza ufisadi unaofanyika kwenye Shamba la Katanini zaidi ya eka 4,000, ambalo tulirudishiwa. Wameuza viwanja na ninasikia umesema kwamba, Babati eti hakuna tatizo watu wanalipwa fidia! Waliolipwa ni akinamama wawili tu wanaopakana na *Police Barracks*, wananchi wengine wote mpaka leo hawajalipwa! Kinachotokea, Madiwani wanamtishia Mkurugenzi na juzi zile pesa za mauzo ya viwanja vya Shamba la Katanini, wamekwenda Dar es Salaam kuangalia lami inajengwaje!

Viongozi wa CCM pia, Mwenyekiti, Katibu na Katibu Mwenezi, wamekwenda Dar es Salaam, pesa za Katanini, wananchi hawalipwi fidia! Mheshimiwa Lukuvi nikakwambia kwamba, kuna ufisadi hapa na Kamati Ndogo ambayo uliagiza Mkuu wa Mkoa aunde na Halmashauri, walikwenda wakabaini viwanja 922 vimechakachuliwa!

Mheshimiwa Lukuvi ni kweli huku juu unafanya kazi, huku chini ambako Viongozi wapo hawatekelezi wajibu wao. Mwenyekiti wa Halmashauri na Madiwani wake wanamtishia Mkurugenzi, wameshaazimia zaidi ya mara mbili wamfukuze imeshindikana, kwa sababu Mkurugenzi mliyeteletea Babati anataka kutuletea maendeleo, Madiwani wa CCM na Viongozi wao hawataki. Viwanja 922 wanasema eti viko kwenye mashamba ya wananchi wa Kijiji cha Malangi, wananchi wa Malangi wanasema hakuna kitu kama hicho. Hivi Mheshimiwa Lukuvi, viwanja 922 wanagawana watu wa Halmashauri; inawezekana wapi?

Mimi nikuombe, nilikueleza kwamba kuna ufisadi na ninakuomba Babati uende tena umalize hilo, lakini kama siyo hilo tu Shamba la *Singu Estate* ambalo linapakana na Shamba la RIVACU, zaidi ya eka 3,000, wale wananchi na yule mwekezaji wa *Singu Estate* wana matatizo, hawajui watalimaje, hawajui watahunaje, kuna matatizo, mazao ya wananchi yanavurugwa kila siku wakipanda.

Mheshimiwa Spika, ni muda mfupi Mheshimiwa Lukuvi amefanya kazi. Naomba kwa sababu alisikia zaidi ya mashamba mengi amenirudishia hata yale ya Bonde la Kiru, zaidi ya mashamba matatu umerudisha. Umeandika hapa kwenye kitabu kwamba, wawekezaji walipwe waondoke wananchi wapewe mashamba. Mheshimiwa Lukuvi tunakushukuru, lakini urudi sasa umalize kwa sababu watu uliowaachia hawakufanya.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, kwa kweli kwa miaka mitano nimesemea haya, nisingekuwa nimeyasemea hata Lukuvi asingeyajua na pia wananchi wangu wasingetendewa haki. Niombe Mheshimiwa Lukuvi akamalizie kazi ambayo ameanza, kwa sababu wale kule chini wamekaa mkao wa kula wagawane pesa, mashamba na viwanja. Ukienda kuangalia, mwezi wa Tano umekwisha, kama hawajawakabidhi wananchi wafukuze. Wanafanya nini ofisini kama Wizara inasema huku halafu kule chini hawatekelezi!

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba, kauli yangu kwa miaka mitano haikuwa bure, matatizo ya wananchi wangu yamesikilizwa na pia yanafanyiwa kazi. Naomba nitoe nafasi ya mwisho kwa Mheshimiwa Waziri ili aje sasa atekeleze amaliziemalizie. (Makofi)

Viwanja viwili vya pale katikati ya mji ile Shule ya Miomboni, eka tisa umemnyang'anya mtu akapewa eneo la *National Housing*. Umeondoka tu, wakauza eneo la *National Housing* lile pale katikati ya Mji wa Babati!

Hivi hawa Watu wa Babati wana nani huku juu ambao kila siku wanauza maeneo ya wazi? Eneo la pale stendi ambalo Machinga walikuwa wanakaa, eneo lao leo ameuziwa mwekezaji mwenye duka la dawa pale Ikizu, siogopi kumtaja, anachukua eneo la shule ya msingi, tunamfukuza huku anakwenda anapewa eneo lingine. Haya yote anayafanya kwa sababu Madiwani wanachukua pesa kwa hawa matajiri wanauza maeneo ya wananchi na ndiyo maana wanamtishia Mkurugenzi. (Makofi)

Mheshimiwa Lukuvi ninakuomba, safari ya Babati inakuhusu kama siyo kesho ndani ya wiki ijayo na Wizara yako, nimwombe Dada Doroth, Kamishna wa Kanda, asisaini mabadiliko yale ya viwanja vya *National Housing*, ambavyo Madiwani wamegawana na wanawauzia watu wengine. Ukifanya hayo Mheshimiwa Lukuvi, naamini Mungu atakubariki. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Shekifu, atafuatiwa na Mheshimiwa Madabida na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile!

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya tatu. Namshukuru Mungu pia kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii.

Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitaanza kumshukuru sana Waziri na Watumishi wote wa Wizara ya Ardhi. Ni ukweli usiopingika kwamba, Waziri amekaa kwa muda mfupi sana, kazi aliyoifanya katika kipindi alichokaa pale ni kubwa sana. Nichukue nafasi hii, kumpongeza mzungumzaji wa sasa, anatoka Upinzani lakini ameelewa kumsifu mtu aliyefanya kazi vizuri. (Makofi)

Tuache siasa za kisanii, panapofanywa vizuri tuseme pamefanywa vizuri, palipofanywa vibaya tutamke pamefanywa vibaya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, wewe na msaidizi wako na watendaji wako, kwa muda mfupi mmebadilisha sura ya Wizara ya Ardhi na Makazi. Naomba pia ni-declare kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na nitamke wazi kwamba, nimeona mabadiliko makubwa. Nimeshakuwa Bungeni hapa hiki ni kipindi cha tatu, kwa mara ya kwanza nimepata Waziri ambaye anasema vitu kwa ukamilifu. Tumepata nakala na shajara la *National Housing*, tumekwenda tumeona, yaliyoandikwa katika kitabu hiki siyo ya uwongo, yametendeka, kasomeni na mtu akifanya kazi vizuri msifuni, siyo kutafuta tu ya kumlaumu. (Makofi)

Katika mambo ya hotuba yako Mheshimiwa Waziri, pengine kabla sijasahau, nianze na ombi la wananchi wa Lushoto, Jimbo langu. Tunakuomba sana, tulikwishaahidiwa Baraza la Ardhi la Wilaya, hivi sasa wananchi wanateseka kutoka Lushoto kwenda Korogwe, lakini Wilaya ya Lushoto ndiyo ya kwanza tangu tunapata Uhuru katika nchi hii ilikuwepo. Sasa watoto wanazaliwa wanapata haki kuliko baba, tunakuomba zawadi utakayotupa wananchi wangu wasihangaike, wape Baraza la Ardhi, hiyo ni ahadi yenu.

Sasa nije katika uchangiaji wa yale ambayo umeyasema. Kwanza, nikupongeze kwa kupunguza viwango vya tozo katika ardhi; hongera sana. Mtu yeyote anayejua historia, haijawahi kutokea, Waziri wa Ardhi ndiye anayetoa taarifa ya kupunguza tozo, tungetegemea sana Wizara ya Fedha, lakini wewe umekaa na wenzako umezungumzia sekta yako na umetoa marekebisho ambayo unataka kuboresha utendaji, lakini pia kuondoa kero kwa wananchi; hongera sana. (Makofi)

Utayarishaji wa hati, tumekwenda Uganda na tumepelekwa na Wizara yako kama Kamati, tuliyoyaona kule ni mambo ya kutia moyo sana, sisi ndiyo tulipaswa kuanza kwa taarifa tulizopata. Leo Uganda unataka kujua hati yako ni kubonyesha tu, unajua hati yangu inadaiwa hiki na hakuna ubabaishaji wa kutoa viwanja mara mbili, mara tatu. Sasa tekelezeni Mradi ule kwa haraka na utupe maelezo Mradi ule utamalizika lini, kwa sababu ndiyo ukombozi wa Serikali kupata mapato. Hivi sasa viwanja vingi havikupimwa na hatupati mapato, shughulikia hilo.

Lingine ambalo ningependa kuchangia ni uhuishaji wa miliki za ardhi, kupima ardhi yote na migogoro ya ardhi katika maeneo. Kwa upande wa Mkoa wa Tanga, migogoro ya mashamba ya ardhi, tunakushukuru mashamba sita tayari yamekwishatolewa idhini ya kufutwa. Tuna mashamba kumi nayo tunaomba yatolewe idhini, wananchi wapate na tunakuahidi sharti la Rais ni kwamba, tuyagawe vizuri, viongozi wasijinufaishe, tunakuhakikishia tutayagawa vizuri. Mimi ni Kiongozi wa Mkoa tutasimamia.

Mwisho kabisa, nimalizie kwa kuiomba Serikali hasa Wizara ya Fedha, *National Housing* ingeweza kujenga nyumba za bei nafuu zaidi na hasa hizi nyumba za bei nafuu punguzeni kodi. Kodi nyingine siyo za lazima hata VAT, hasa kwa zile nyumba ambazo ni za watu maskini, tufanye kama ilivyofanywa wakati shirika linaundwa, kuna nyumba za *National Housing* Magomeni pale maskini walikuwa wanapewa. Sasa haya yakiigwa, tutapata sifa. Nina uhakika Mheshimiwa Waziri una uwezo, tunakuomba sana usimamie. Tunaiomba Wizara ya Fedha ione umuhimu wa Mashirika haya ili kujenga *confidence* na mapenzi kwa wananchi. CCM itaendelea kutawala, niwahakikishie, huo ni ukweli usiopingika. (Makofi)

Kwa hiyo, tukiweza kuyatekeleza hayo, tunaongeza *cement* na kama ilivyosemwa, tuache usanii wa siasa. Tunaweza kutamka lolote, lakini ni ukweli kwamba ni usanii na msanii anakuja kwa sura tofauti; anavaa nguo hii, kesho anavaa ile, lakini atabaki ni huyo huyo msanii. Nawahakikishia nchi hii itaweza kuendelezwa chini ya Chama cha Mapinduzi, Viongozi wanatoka huko. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, namshukuru Waziri na niendeleo kumwomba na nitafanya la mwisho, siyo kitu cha kawaida, sasa hivi tuko kwenye mchakato wa kuomba uongozi wa nchi hii, naomba atakayeshika uongozi, wewe hukuchukua fomu Mheshimiwa Waziri, huyo atakayekuja nakuombea kazi akurudishe Wizara hii. Akurudishe Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, nina uhakika utafanya maajabu. Mungu akusaidie, ahsante sana. (Kicheko/Makofi)

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Madabida, halafu Mheshimiwa Dkt. Ndugulile!

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu. Nakuomba uniruhusu nikushukuru wewe binafsi, pamoja na Wabunge wote, kwa kutufariji sana katika msiba wa Mbunge wetu wa Dar es Salaam, Marehemu Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, tunasema ahsante sana kwa faraja mliyotupa, nashukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema mcheza kwao hutunzwa. Mheshimiwa Lukuvi amefanya kazi nzuri sana, namwomba nimpe salamu za Wana-Dar es Salaam, kwa kweli tunakushukuru sana, migogoro iliyokuwepo Kigamboni, Chasimba, Makongo na kote Dar es Salaam, kwa kweli umefanya kazi nzuri sana. Hii ndiyo sababu hata Mheshimiwa hapa Mbunge wa Dar es Salaam aliposimama, hakusema chochote kwa sababu umemaliza kazi Dar es Salaam, ahsante sana. Waziri Kivuli hakusema kitu, umemaliza kazi Dar es Salaam, tunasema ahsante sana.

Mheshimiwa Lukuvi tunakushukuru sana kwa kazi nzuri ambayo umeifanya Dar es Salaam. Sasa hivi tunaishi kwa amani kabisa na wewe ni jembe la Chama cha Mapinduzi. Tunajivunia wewe na siyo tu kutusaidia, lakini umewasaidia wananchi wote, Wananchi walikuwa wanalalamika kwa jinsi walivyokuwa wanadhulumiwa ardhi zao. Watu maskini walidhulumiwa na Mabwana Ardhi, walipokuwa wanapima na kuchukua bila kupata fidia. Kwa kweli Mwenyezi Mungu atakubariki sana, ahsante sana. (Makofi)

Mheshimiwa Lukuvi umefanya kazi nzuri sana, wakulima wadogo na wakubwa walikuwa wanalalamika sana kuhusu tozo mbalimbali za kodi za ardhi, hicho ni kilio cha watu wengi. Hapa hapa tayari nimepata meseji nyingi, maana na mimi ni mkulima, wanasema Mheshimiwa Lukuvi, mpe pongezi sana na salamu za pongezi nakupa hizi wewe na Naibu wako, mmefanya kazi nzuri sana. Siku zote watu walikuwa wanapiga kelele na kulalamika kwa sababu tozo zilikuwa kubwa sana. Tuendeleo kuziangalia, kwa sababu zikiwa kubwa sana matokeo yake ni watu kutokulipa, lakini umefanya hivyo, niwaombe Watanzania lipeni kodi kwa maendeleo ya nchi yetu, tunakwambia ahsante sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, umefanya kazi nzuri sana, umepunguza kodi katika majengo, majengo ya *National Housing*, vifaa, nasema endelea kupunguza, mtu haulizwi umekula nini, wanauliza anakaa wapi, amelala wapi. Punguza ili Watanzania waweze kumudu kuweka mabati, waondoe nyasi kwenye nyumba zao, wajenge nyumba badala ya tope waweke matofali. Mheshimiwa Lukuvi, hilo linaweza kupatikana kwa kuwapunguzia kodi katika vifaa. (Makofi)

Nami ninafikiri utakapopunguza kodi vitanunulika zaidi na Serikali pia itapata kupitia kodi kidogo lakini watu wengi watakuwa wamenunua. Kwa hiyo, tukuombe sana, hilo uliangalie, Watanzania tunaweza kabisa tukaishi maisha ya asali na maziwa kwa kupata nyumba bora za kuishi. (Makofi)

Niwaombe sana sana, ndugu zangu wa Jimbo la Mheshimiwa Lukuvi linaitwa nini?

MBUNGE FULANI: Isimani.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Isimani, mlioko hapa juu na mlioko huko, tunakuombeni mumrudishe Mheshimiwa Lukuvi, tena kwa kishindo bila kupingwa.

MBUNGE FULANI: Na Wapinzani wasiweke mtu.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Namwomba mdogo wangu Germina, tutunzie huyu baba amefanya kazi nzuri sana katika Tanzania. Atakayekuja yeyote mpigeni chini, kwa sababu kazi aliyoifanya ni kubwa na Mwenyezi Mungu atakubariki. Tunaomba, hatujasikia umechukua fomu kama alivyosema Mheshimiwa Shekifu, atakayekuja yeyote akuweke hapo, kinyume cha hapo akupandishe juu zaidi uweze kusimamia na sehemu nyingine tuweze kupata mafanikio hayo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Lukuvi, mimi leo kusema kweli nimesimama hapa nikiwa na furaha kubwa sana, kwa sababu umetutatulia matatizo makubwa sana. Nakuhakikishia, Dar es Salaam tunapeta nginjanganja, Wabunge, Madiwani na wote, mambo uliyotufanyia ni makubwa sana. Kuna visehemu vidogo dogo maliza kabisa, hakuna Chasimba, Makongo wala Kigamboni, kote maliza kabisa. Kule ulikosema waendeleo kukaa haondolewi mtu, haondolewi mtu, hicho ndiyo Chama cha Mapinduzi wananchi wa Dar es Salaam. Ahsante sana Mheshimiwa Lukuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana na jembe letu la Chama cha Mapinduzi, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, atafuatiwa na Mheshimiwa Naomi Kaihula!

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia. Kwa mara ya kwanza katika Ubunge wangu ndani ya miaka mitano, naunga mkono hoja ya Serikali. *(Makofi)*

Pongezi hizi naomba nizitoe kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara ya Ardhi, kwa mapinduzi makubwa ambayo wameyafanya ndani ya Wizara. Sasa hivi tofauti ni kubwa sana. Mwanzoni wananchi wa Kigamboni walikuwa wananusa kifo, sasa hivi wananchi wa Kigamboni wana uhai. *(Makofi)*

Niwapongeze Viongozi wangu wa Chama na wewe Mheshimiwa Spika, kwa ushirikiano ambao umeweza kutupa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam chini ya uongozi wa Mheshimiwa Abbas Mtemvu, tulitoa ushirikiano mkubwa sana, hili suala la Kigamboni lilikuwa letu kwa pamoja. Wajumbe wa Kamati ya Ardhi chini ya Mheshimiwa Lembeli, wamefanya kazi kubwa sana na nataka nitoe shukrani hizi kwa niaba ya wananchi wa Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapinduzi yaliyofanyika ndani ya Wizara ni makubwa sana, wenzangu wameyasema; punguzo la tozo, ada za ardhi, ni mambo mazuri, utaratibu mpya wa tathmini ambao mmekuja nao kwamba, sasa hivi tathmini zote zitafanyika pale fedha zitakapokuwa zimepatikana.

Hili ni jambo jema, mara nyingi migogoro mingi imekuwa ikitokea kwa sababu tathmini zinafanyika na fedha zinakuwa hazipo. Bado nina mgogoro mmoja, Wananchi wa Mbande kule eneo la Chamazi, ambao wanataka kufidiwa kwa ajili ya kupitisha Mradi wa Umeme, ni miaka zaidi ya mitano TANESCO, NSSF na Wizara ya Nishati na Madini wanasuasua.

Nami naomba niseme kwamba, kama haitawezekana kutoa fidia hiyo mwisho wa mwezi huu, naomba huo Mradi utupishe, wapitishwe hilo bomba sehemu nyingine ili wananchi hawa nao waweze kupata nafuu. Hamuwezi mkataka kuja kutaka uchumba, mmeleta na posa wakati uwezo wa kuo hamna, kama hamuwezi basi acheni ili huo Mradi mkafanye sehemu nyingine mtakapokuwa mmepata fedha.

Mheshimiwa Spika, bado kuna matatizo madogo na nataka niwaombe wenzangu wa Wizara ya Ardhi wasimamie, walituhidi hapa Bungeni kwamba, watachonga barabara katika Mradi wa Viwanja 20,000 Kibada. Najua tender imeshakamilika, mkandarasi ameshapatikana, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kusimama, atuambie ni lini huo Mradi utaanza ili wananchi ambao wameshajenga makazi kule waweze kupata barabara.

Vilevile kuna wananchi ambao walikuwa katika eneo la Dungu Farm ambao waliondolewa na baadhi yao wanadai fidia kama wananchi 52 hivi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, viwanja baadhi wameshapata, lakini bado tunahitaji wale ambao wanahitaji kulipwa fidia waweze kulipwa.

Nimalizie kwa kusema kuwa, hayo ukiweza kuyafanya kwa kiasi kikubwa na lingine moja, hivi karibuni watu wako wa Wizara ya Ardhi walikuja wakaweka mabango katika maeneo ya Tungi, barua tumeshakuandikia. Nitakuomba utupatie hatima ya hilo, kwa sababu kilichofanywa pale na Watendaji wako wa Wizara ya Ardhi hatuafikiani nao. Tunakuomba sana uwasimamie vizuri watendaji wako, yale mambo ambayo wanakuja kuyafanya Kigamboni, wafuate utaratibu na kuwashirikisha Viongozi wanaohusika pale.

Yangu ya leo ilikuwa ni kutoa pongezi kwa kurejesha heshima ya Wizara ya Ardhi, ambayo kwa miaka minne, mitano iliyopita, heshima hiyo ilikuwa imeshuka sana. Watendaji na Viongozi wa Wizara ya Ardhi walikuwa ndiyo chanzo cha migogoro na dhuluma kwa wanyonge. Kwa hili ambalo umeweza kulifanya ndani ya muda mfupi, tumefanikisha kwa kiasi kikubwa sana, tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wako. Sisi tuko tayari kukuunga mkono katika yale ambayo unaendelea kuyafanya na Mwenyezi Mungu akujalie, uweze kuchaguliwa tena na kurudi katika Wizara hii, ili kuendeleza yale mazuri ambayo umekuwa unayafanya. (Makofi)

Kwa kweli umekuwa mkombozi wa wanyonge na hili tunaomba tuliseme na sisi tunasema ulikwina? Ulikuwa wapi siku zote?

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru tena Serikali, kwa kutatua migogoro ya Kigamboni na kusema kwamba, ardhi ya Kigamboni itabaki kuwa mikononi mwa Wananchi wa Kigamboni, wataiendeleza wenyewe, wataingia ubia wenyewe na watauza wenyewe. Sasa wale makuwadi na madalali watatuchukia sana, lakini naomba niseme kwamba, kazi mliyomituma wananchi wa Kigamboni, nimeifanya na tumeifanya kwa ukamilifu. Tunachokiomba, *MasterPlan* ifanyiwe kazi kwa haraka, upimaji uharakishwe na utoaji wa hati ili Wananchi waweze kuendeleza ardhi zao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niendeleo kumaliza kwa kushukuru sana. Niliteuliwa katika Bunge hili nikiwa Mbunge pekee wa Chama cha Mapinduzi, lakini tulikuwa tunalisimamia hili. Nashukuru sana wananchi wa Kigamboni kwa kuniunga mkono katika jambo hili. Kazi waliyonituma wananchi wa Kigamboni nasema tumemaliza, nitarudi tena kuwaomba ridhaa yao ili sasa tuanze kazi ya kujenga Kigamboni mpya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nawashukuru sana, ahsanteni sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Sasa nilisema nitamwita Mheshimiwa Naomi Kaihula, atafuatiwa na Mheshimiwa Aeshi, Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Mngodo.

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nasikia furaha sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kufika wakati huu hata nami nikawa sehemu ya kutoa mawazo yangu katika jambo muhimu sana la ardhi na makazi.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Lukuvi, kwa kazi aliyofanya. Kweli katika muda mfupi amefanya kazi ambayo ilikuwa kama ni sugu vile imemshinda hata fisi kuula mfupa wake. Napenda pia nimkubushe mdogo wangu Mheshimiwa Lukuvi kwamba, mgema akisifiwa tembo hulitia maji, yaani asije sasa akabweteka, kwa sababu tumemsifu sana akasema basi nimemaliza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda niishukuru sana Kambi ya Upinzani yote, UKAWA na hasa kupitia CHADEMA. Napenda nimshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa umakini wake wa kupanga safu zake za Mawaziri Vivuli, kazi mmeiona, yaani tukichukua madaraka hakuna tatizo. Mambo yote haya yamefanyika kwa sababu ya umakini wa wale wanaowasimamia.

Mheshimiwa Halima Mdee ni jembe kabisa, yaani haya mambo hata mwenyewe Mheshimiwa Lukuvi alikiri kwamba, kuna mambo ambayo ameshirikiana ndiyo maana imetoka ile *sharp*. Ni kweli kabisa, lazima na yeye tumpe haki yake na tutambue mchango wake. Napenda na nafurahi sana kama mwanamke tena, kama vile ninavyojivunia wewe Spika Mwanamke, kuonyesha kazi nzuri, Halima anaonyesha kazi nzuri. (Makofi)

Suala la Kigamboni Halima amelishughulikia vizuri. Masuala ya ardhi Kimataifa na Kitaifa ameshughulikia vizuri. Kwa hiyo, kwa maneno mengine, lazima tukumbuke kwamba, ufanisi wa Chama cha Mapinduzi sasa ni kwa ajili ya wale wasimamiaji, tumekisimamia sisi Chama cha Mapinduzi mpaka hapa. Niwaambie hata alipokuwa anasifia mtu wa Mafia, hata hivi ninavyosema watu wa kule Mafia wanaelewa kimeendelea nini. Mtangaza nia wa kule wa CHADEMA, Mheshimiwa Kubenea, amefanya kazi nzuri ya kuwasimamia hawa watu wa Chama cha Mapinduzi. Amewasimamia akawabana sawasawa mpaka wakafikia kufanya kazi nzuri kama hiyo. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, lazima wananchi watambue kama tunavyosema, hata sasa hivi kwa sababu Chama au UKAWA una zile sera nzuri za utendaji siyo za maneno, wameweza kuwafanya hawa jamaa waache hata sera zao, sasa hivi wanatangaza Sera za UKAWA tu. Sera za elimu ni za UKAWA, Sera za Makazi ni za UKAWA, kila kitu. (Kicheko/Makofi)

Kwa hiyo, napenda niwapongeze sana Viongozi wa Upinzani mpaka humu ndani, kwa kazi nzuri. La muhimu, napenda niwaambie wananchi kwamba, wameona mfano mzuri wa kwamba, tunapokuwa na Upinzani ambao ni mzuri, nchi inapiga hatua. Mfano kamili wa hili ni huu hapa, yaani Upinzani ukiwa *constructive*, ukiwa unafanya kazi yake, ukiwa unaangalia masuala ya wananchi, unawafanya wale walioko kwenye Serikali na Chama kinachoongoza kufanya kazi. Kwa hiyo, nawaomba kufuatana na hili, mhakikishe sasa mnawapa wenyewe, wanaingia wanaongoza Serikali na Chama cha Mapinduzi kinakuwa *bench*, halafu mtaona mambo kwa sababu ni yao wenyewe wanatekeleza vizuri. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda niseme pia kidogo kuwa, namshukuru sana Mheshimiwa Lukuvi, kwa kweli amefanya kazi nzuri. Wakati huu naamini kwamba, atamalizia mambo mengine kama upande wa Dar es Salaam ni kweli amefanya vizuri kule Kigamboni, lakini upande wa *housing*, *National Housing* bado, bado, bado. (Kicheko)

Moja, *open space* nyingi bado hajazishughulikia, kiasi cha kufanya mpaka Jiji limeonekana kama vile *squatters* za ajabu sana. Hilo suala nafikiri kwa umahiri wake, tukisaidiana na Upinzani kumsukuma atalisimamia.

La pili katika *National Housing*, ni kweli kuna watu wanakaa katika *national housing*, lakini kuna suala moja ambalo hajalifanya vizuri, suala lenyewe ni la wastaafu wa Serikali walioko katika nyumba za *National Housing*. Kuna wale ambao walipendelewa wakapewa *National Housing* kwamba ni wastaafu hawajiwezi, lakini matumizi ya zile nyumba hawajafanya walivyoonewa huruma; wameuza vile viwanja na wakafanya majumba ya ajabu wakabadilisha hata matumizi ya zile nyumba. Tunapenda nalo alishughulie vizuri.

Sambamba na vile anavyosema kwamba, wale watu wa *National Housing* wanaokaa mle wakistaafu hawatawabadilishia mikataba yao, mimi ninaomba kama tulivyosema tumekwenda nchi nyingine tumeona. Tumekwenda kwa mfano The Hague, Uholanzi, Belgium na Indonesia, tumekuta hivi; ni lazima tuwe wabunifu, unaangalia nitakuwa na wastaafu wangapi, wa vyeo vipi na wakati upi, halafu unatayarisha majengo kwa ajili yao kwa kiwango chao watakachoweza kupima.

Inasikitisha sana jambo hili limenifanya niseme hapa. Kwa mfano, kuna Makanali wawili sitawataja majina, ambao wamedhalilishwa na Watendaji wa *National Housing* mpaka hata nilipokwenda kuangalia ule mshahara niliona aibu. Kanali ni Mheshimiwa, alitoa maisha yake kwa ajili yako wewe, sasa wewe unashindwa kumwachia nyumba hiyo akae hata kama ni bure hata nyumba ya aina gani inashindikana?

Napenda wapate busara hii na hekima hii, hilo jambo limetia doa, linadhaliisha, mtendaji kumwambia yule Kanali basi nitakupeleka kule wapi wanakoita mashenzini, siyo haki hata kidogo. Tulifikirie hili jambo. Nakuomba Mheshimiwa Lukuvi, pamoja na Msaidizi wake, ambaye pia ninapenda nimtambue na yeye amechangia vikubwa sana katika hili suala, Naibu wake, kwa hekima na busara na uelewa wa sheria, ametekeleza vizuri kiasi cha kwamba, mpaka wakatoka na Sera ambazo ni nzuri. Kwa hiyo, nawapongeza, naomba urudi upande ule. (*Makofi*)

Pale Upanga maghorofa yanajaa Wahindi, ondoeni matabaka. Baba wa Taifa aliondoa matabaka kwa kupeleka Waswahili, Waafrika, wakakae nao mle, lakini nyumba zile zote zimebadilishwa zimenunuliwa na wanjanja wamekwenda kuzifanya ni Uhindini wanaandika nyingine Ndogolabesh, mengine sijui Ina and China, mimi naomba hilo pia *intelligence* yetu ifanye hivyo. Msikubali kurudisha matabaka kule Uhindini, wapeni na wao kule *suburb*. Kwa nini kama ni Wananchi hawapendi kwenda kukaa kule kwenye *suburb*? Hili jambo nakwambia ni bora mlishughulikie mapema.

Yale maghorofa kodi tuziangalie wanalipa kiasi gani kwa sababu wameharibu mazingira, mifumo ya maji, maji taka na barabara. Sasa kama wao wamejenga maghorofa makubwa na wameongeza idadi ya watu kukaa pale viendane na kodi, watutengenezee hizo barabara na maji tupate. Nafikiri masuala kama hayo na sehemu za wazi tuzishughulikie na sehemu walizojenga walio wengi tushughulikie.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nakupenda. *(Makofi)*

SPIKA: Aah mwache tu siri yake anaijua yeye na mimi. Nilim-coach kuingia humu ndani pamoja na marehemu yule alikuwa anakaa pale. *(Kicheko/Makofi)*

Haya tuendeleo sasa na Mheshimiwa Aeshi Hilaly, atafuatiwa na Mheshimiwa Lulida, Mheshimiwa Rebecca Mngodo na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o.

MHE. KHALIFAN HILALY AESHI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, naomba nitoe shukrani zangu za dharti na pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina kila sababu na furaha ya kusimama hapa, kwa sababu nimeamini leo uongozi siyo lazima uwe Profesa. Mheshimiwa Lukuvi, umefanya kazi kubwa. Mheshimiwa Lukuvi, baada ya kuchaguliwa kuwa Waziri wa Wizara ya Ardhi, alikuja kututembelea Sumbawanga. Alilitembelea shamba lile, kwa kweli aliguswa na maumuvi makubwa waliyonayo Wananchi wa Jimbo langu la Sumbawanga Mjini. *(Makofi)*

Nikupongeze Mheshimiwa Lukuvi kwa sababu ulitoa kauli moja, ukasema utakuwa wa mwisho kuja Sumbawanga kama Waziri, hatokuja kiongozi yeyote tena isipokuwa wewe. Mheshimiwa Waziri, nilifarijika sana, lakini wapo waliotubeza wakiamini huwezi kuchukua hatua zozote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa sasa na leo nimemsikia Mheshimiwa Waziri, tumetoa *notice* ya siku 90, naamini toka imetolewa leo hii zimebaki siku 45 au siku 50, niwaombe tu wananchi wa vijiji vile kwenye Shamba la Malonje wawe wavumilivu, wasijichukulie sheria mkononi. Naamini kabisa, Serikali itatatua tatizo hili kwa sababu tumeteseka muda mrefu na hatua iliyobaki ni fupi sana na ni ya muda mfupi. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, ulishughulikie hili kwa kweli tutakuwa na faraja kubwa sana wananchi wa Jimbo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri ameongelea Shamba la Malonje, lakini pembeni yake kuna Shamba la Magereza, ambalo linahusiana na wananchi wa Malonje palepale. Magereza wana mashamba mawili na yote hayalimwi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri uongee na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ili aweze kutukubalia shamba lile ambalo halitumiwi na Magereza, basi wapewe wananchi waweze kuliendeleza, kwa sababu wananchi ni wetu na Serikali ni yetu. Naamini kabisa hatua hizi zitachukuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri amefanya mengi na mimi niseme sijui ulikuwa wapi, hii miezi sita uliyofanya wananchi wote Tanzania nzima wana imani na wewe. Tukuombe kwa Mwenyezi Mungu, wewe na Naibu Waziri wako, awape umri mrefu na muweze kurudi tena Bunge lijalo ili muendeleze yale yote ambayo mliahidi kuyatekeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nisiwe mchoyo wa fadhila, naomba niwashukuru sana *National Housing* na Viongozi wake wote, kwa sababu ndani ya Jimbo langu la Sumbawanga Mjini wamekuja kutujengea nyumba nzuri, za gharama nafuu, nawaomba wananchi wajitokeze kuzinunua nyumba zile.

Lingine Mheshimiwa Waziri, tuliwaahidi mlipokuja kutembelea Sumbawanga kuwapeni ardhi nyingine ili muweze kuja kuwekeza zaidi kwa sababu Sumbawanga inafunguka; Sumbawanga ya mwaka 2010 siyo Sumbawanga ya mwaka 2015. Kwa hiyo, naomba niwaambie Viongozi wa *National Housing* kwamba, nafasi ipo waje wapewe na wengine ambao wanataka kuja kuwekeza Sumbawanga, waje wawekeze; Sumbawanga imebadilika, Sumbawanga imekua, imekua Mji ambao ninaamini ndani ya miaka mitano ijayo tutakuwa pahali pazuri na tutakuwa tumeendelea kupita kiasi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Sumbawanga Mjini, kwa uvumilivu na ukarimu wao. Nimeongoza ndani ya miaka mitano, naomba sasa niwaombe tena kwa haya ambayo tumeyafanya sasa, watupe nafasi tena tuitoe Sumbawanga ilipo tuisogeze mbele. Nasema hivyo kwa sababu miaka mitano iliyopita wengine walitubeza kutuchagua, lakini tumeahidi, tumetekeleza na tunasonga mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mbali na ardhi ningependa kuishukuru tena Serikali, kwa asilimia 95 tumekamilisha llani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Mambo yote ya msingi ndani ya Jimbo la Sumbawanga Mjini yamekamilika. Ukimaliza tatizo la shamba, naamini kabisa Sumbawanga hatutakuwa na kero, japokuwa maendeleo ni sawasawa na gurudumu, tutakutana na mashimo mengine mbele, ambayo tunaamini tutayafukia kwa kasi tuliyokuwanayo kuanzia mwaka 2010. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nisipoteze muda sana, lengo langu kubwa lilikuwa ni shamba na Mheshimiwa Waziri ameliongelea. Niombe wananchi wa kwetu Sumbawanga kwamba, tumeshaogelea na mchanga tumeuona, sasa tusikate tamaa. Tuvumilie, tusivamie shamba lile, tsubiri hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Shamba hilo likirudi, Mheshimiwa Waziri utakuwa umekamilisha Kauli ya KILIMO KWANZA. Bila kilimo hakuna chochote na kilimo ndiyo uti wa mgongo, lakini tulikuja na Kaulimbiu ya Mwaka 2010 ya KILIMO KWANZA. Tumelima na kwa mara ya kwanza Tanzania haijaagiza chakula kutoka nje, sasa hivi tunauza chakula chetu kwenda nje. Miaka iliyopita tulikuwa tunaagiza vyakula kutoka South Africa, mahindi yanakuja mabovu, lakini kutokana na kaulimbiu ya Serikali ya KILIMO KWANZA, nasema naomba niwapongezeni sana, ongezeni juhudi, wananchi waweze kupata vifaa bora, wapate matrekta waweze kulima, wajikomboe kutoka katika dimbwi la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niwashukuru sana, tena sana, wananchi wa Sumbawanga, nawaambia bado nipo na nawapenda sana, wanipe nafasi tena ili niweze kuwaongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Ahsanteni sana, Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Riziki Lulida!

MBUNGE FULANI: Hayupo.

SPIKA: Hayupo? Basi atafuata Mheshimiwa Rebecca, atafuatiwa na Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, Mheshimiwa Mwatuka, Mheshimiwa Dkt. Mrema na Mheshimiwa Haji Khatibu Kai.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii ambayo ninaiona ni ya muhimu sana kwa nchi yetu. Kwanza, nimshukuru Mungu kwa ulinzi wake na kwa Jeshi kubwa la Malaika ambao amewaachia kunilinda mchana na usiku.

Kwa kuanzia ningependa kuzungumzia juu ya mipango miji ya nchi yetu. Kwa kweli katika karne tunayoishi ya 21, miaka 53 baada ya Uhuru, inasadikiwa kwamba, asilimia 70 ya miji yetu imejengwa kiholela. Pamoja na juhudi ambazo zimefanywa na Mawaziri wetu kwa muda mfupi ambao wamekuwepo katika nafasi zao, naona kuna umuhimu mkubwa kuona hatuendelei kuwa na miji ambayo imejengwa kiholela, kwa sababu tunakuwa kama tuko mbali na miji mingine ya ulimwengu.

Tunasafiri mara nyingi kwenda nchi zingine, tunaona miji ilivyojengwa vizuri, lakini tunaporudi nchini kwetu tunasikitika kuona haikujengwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusu migogoro ya ardhi. Nimeangalia Kitabu cha Waziri, ukurasa wa 106 umeorodhesha maeneo ambayo yana migogoro ya matumizi ya ardhi, lakini sikuiona Meru. Wilaya ya Meru ni Wilaya ambayo ina migogoro mingi hata kabla ya kupata Uhuru, hili linafahamika. Mtanzania wa kwanza kwenda *UNO* kudai haki ya ardhi, alitoka Wilaya hii ya Meru. Hapa mmeorodhesha maeneo mengi lakini Meru hamkuiweka, wakati inafahamika kabisa kule migogoro ni mingi. *(Makofi)*

Ninajua wengi wanaosababisha migogoro hiyo ni Mawaziri, nilishataja hapa sitaki kurudia kutaja na wengine ni Wabunge wamo humu ndani, leo sitawataja, lakini wanafahamika. Shamba la *Kalangai Estate Limited*, ambalo Mheshimiwa Mkapa alifuta umiliki wa mwekezaji, mpaka leo hii ninapozungumza Halmashauri ya Meru imeshindwa kuwarejeshea Wananchi wa maeneo yale ile ardhi, badala yake Vigogo wa Wizara mbalimbali wakiwemo Mawaziri hapa ambao sitawatawaja, wanawakodishia wananchi wa pale lile shamba kwa shilingi laki mbili na nusu. Naomba mfuatilie hilo jambo, kwa sababu ninasema habari ya kweli ambayo binafsi nimefika kule nikaona wanawake wanavyohangaika, wanavyolia kwamba, wanakodishiwa ardhi yao na Mawaziri na Wabunge wanafanya hivyo. Naomba Serikali ifuatilie jambo hili, kwa sababu Halmashauri imeshindwa na kama Halmashauri ya Meru imeshindwa ina maana inapewa chochote, inapewa percent!*(Makofi)*

Sawasawa na Shamba la Malula, hali kadhalika wananchi wamezuiwa wasiendelee ile ardhi na Halmashauri ya Meru, mpaka leo hakuna kinachoendelea, wananchi wanazidi kuhangaika, wanazidi kuteseka. Wewe ukisema kwamba, nisemeje? Na ninyi mkisema... *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala la kurasimisha ardhi ni la muhimu sana, najua kuna MKURABITA. Baadhi ya Maafisa wa MKURABITA, ili waje wapime ardhi yako lazima utoe rushwa, utoe chochote, hiyo inafahamika na mimi imenitokea. Ninazungumza mambo ninayoyajua kwa sababu imenitokea mimi. *(Makofi)*

Afisa anataka kwanza nimpe eneo dogo ili aweze kupima ardhi yangu! Hiyo ni aibu sana, nataka wananchi wasikie ya kwamba, tunaelekea uchaguzi, asilimia 80 ya Watanzania wako vijijini, ni asilimia kubwa zaidi wako vijijini na kama Serikali imeshindwa kuwapimia ardhi, hakuna haja ya kuendelea kuwachagua waendeleo kukaa madarakani na sisi tunaendelea kuteseka. Tunaweza kujandikisha, wakati huu ni wa kujandikisha wananchi wajiandikishe, kwa sababu watakapokuwa wamejiandikisha, wataweza kupiga kura na kumweka yule wanayemwona kwamba UKAWA tutaweza kuendeleza ile Sera, ambayo tulisema Wananchi wote warasimishiwe ardhi au wapimiwe ardhi yao.

Wananchi naomba mnisikilize hasa walioko kule Meru, kwa sababu ninajua ndiyo walioteseka zaidi na katika maeneo mengine ya nchi yetu. Kama ardhi ingepimwa, nina uhakika Watanzania wengi wangeweza kulipa kodi na kama wangelipia kodi ina maana ile fedha ingeweza tena kuwarudia wao kwa maendeleo yao, lakini Serikali imeshidwa kufanya hivyo.

Tumeletewa hapa taarifa nzuri sana, ni kweli inawezekana hayo mambo yamefanyika kwa muda mfupi, lakini katika Kitabu cha Kamati kinasema kwamba, fedha iliyotengwa mwaka jana shilingi bilioni 34, bilioni 13 za nje na 20.8 za ndani, mpaka kufikia Aprili 2015 hakuna fedha iliyokuwa imetolewa. Kwa hiyo, hata hiyo migogoro sijui iliyotatuliwa, hayo mafanikio mliyoyapata, nimeshindwa kujua mmefanyaje kwa sababu fedha ya maendeleo haikutoka hata shilingi moja? *(Makofi)*

Tunaomba fedha inapotengwa itolewe ili kazi ya maendeleo iweze kufanyika.

Nizungumzie kijitabu kidogo ambacho tumegawiwa kwenye mabegi mazuri tuliyopewa tulipokuwa tunaingia kuhusu hali ya Wataalam wa Sekta ya Ardhi hapa nchini. Kama kungekuwepo na Wataalam wa Ardhi, yaani wale wapima ardhi wangekuwepo, nachukulia mfano wa Mkoa wa Arusha; Mkoa wa Arusha katika hiki kitabu kidogo tulichopewa, naomba kunukuu: “Katika Jiji la Arusha kuna mpima ardhi, wanatakiwa 15 lakini ni zero, hakuna hata mmoja. Karatu wanatakiwa wapima ardhi watatu, lakini aliyepo ni mmoja. Halmashauri ya Meru wanatakiwa watatu, lakini waliopo zero, hakuna wapima ardhi, halafu mnatuambia mnataka kupima ardhi nchi nzima wakati hakuna wapima ardhi! *(Makofi)*

Wilaya ya Arusha wanatakiwa watatu, lakini ni zero, hakuna hata mmoja. Kule Longido bahati wao wanatakiwa watatu lakini kuna mmoja na ujue haya maeneo ni makubwa sana kijiografia, yanatakiwa yapewe wapima ardhi wa kutosha na siyo mmoja kama tunavyoona hapa watatu halafu ni zero, hawapo wa kufanya hiyo kazi. Kule Monduli, eneo la Monduli ambalo linasifika kwa wafugaji na wakulima na watia nia ya Urais wako kule, tunaona wanatakiwa wapima ardhi watatu lakini zero hakuna mpima ardhi; sasa hiyo ardhi itapimwa na nani jamani? *(Makofi)*

Tunataka Serikali iwe makini kabisa kwa suala hili la kupima ardhi, kwa sababu wananchi wengi wanateseka sana. Hatuhitaji kuendelea kuwa maskini namna hii na huku Mwenyezi Mungu ametupa ardhi nzuri, kubwa. Ukisafiri kwa gari utaona Tanzania ilivyo na ardhi nzuri, kubwa, lakini haijapimwa. Maafisa Ardhi hawapo, sijui hawasomeshwi au wanasomeshwa lakini hawapewi ajira sielewi?

Huu ni mwaka wa uchaguzi, Watanzania wote ni lazima tuijime Serikali iliyoko madarakani hasa walioko vijijini, msidanganyike safari hii kwa kupewa zawadi ndogondogo. Hakuna kupewa zawadi, hakuna kupokea zawadi ya mtu yeyote, hakuna kupokea rushwa kutoka kwa mtu yeyote. Tutumie haki yetu ya kupiga kura, tutumie vitambulisho vyetu vya kupiga kura vizuri, tusiviuze kwa watu wengine kwa ajili ya fedha kidogo, halafu kwa miaka mitano tutaendelea kuteseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kumaliza. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, atafuatiwa na Mheshimiwa Clara!

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja hii na ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kaka yangu Mheshimiwa William Lukuvi, kwa kazi nzuri aliyofanya na Mheshimiwa Angellah Kairuki, Naibu Waziri. Kwa kweli Rais pale alifanya asilimia 50 mwanaume na mwanamke na kazi imefanyika kwa uhakika kabisa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lukuvi, mahali popote alipopewa jukumu, hakuwahi kushindwa hata mara moja; amekuwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu na mabadiliko makubwa tumeyaona, amesimamia kila kazi aliyopewa, iwe ni maafa, iwe ni mapambano ya UKIMWI, iwe ni rushwa, ni mtu wa vitendo. Amepewa Ukuu wa Mkoa Dodoma, mabadiliko tuliyaona, taa ziliwaka mpaka Dodoma na aliondoka wanamlilia. Amepewa Ukuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ameifanya kazi kwa vitendo na ndiyo maana alipopewa hakuongozwa na mtu yeyote, watu wasiseme eti wamemwelekeza, aliyajua matatizo yalipo, kwa sababu alikuwa anashirikiana na watu. *(Makofi)*

Alianza kazi na Jimbo la Ismani, ambalo yeye ndiyo Mbunge wa kwanza, Jimbo lina mabadiliko makubwa kuzidi yaliyoko mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpeni sifa mtu anayotakiwa kupewa. Nasema hivyo nikiwa Diwani kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Leo tumetoa taarifa, yote mmesikia yaliyotolewa hapa, sasa tunampa taarifa Sosopi, aliyeko kwenye hilo Jimbo anahangaika, wote humu tumekiri kwamba, Jimbo hilo ni la CCM, hata wifu yangu Chiku Abwao ametulia kimya, anajua pale ubavu haupo, CCM inatamba. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, migogoro yote mmeiona imetatuliwa kila sehemu na wote tumekiri kwa umoja wetu, maana yake ni kwamba, wote UKAWA, CHADEMA, wamekiri kwamba pale ni jembe, hakuna anayefua dafu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, migogoro mingi tumesikia yote imetatuliwa na wote tumekiri. Sote tumepewa *documents*, hazikutosha kubeba mkononi, tumepewa na mabegi kwa sababu hata kwenye *pigeon hole* hazitoshi; ni kuonyesha jinsi alivyokuwa mtu wa vitendo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, masuala ya nyumba yote tumeona yanafanyiwa kazi, nampongeza kabisa Nehemia Mchechu, kwa kazi nzuri aliyofanya kwenye Shirika la Nyumba, kwa kuhakikisha kunakuwa na makazi bora na Watanzania wanapata makazi bora. Naipongeza Wizara kwa kupunguza tozo na gharama kwenye nyumba na hasa nyumba ambazo ni za chini ili Watanzania waweze kuzipata.

Naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Lukuvi, kwa kutatua mgogoro uliokuwepo kwa muda mrefu katika Gereza la Pawaga na Kijiji cha Kisananga, ambao umetatuliwa na wananchi wamefurahi na wanakupongeza sana kwa kazi nzuri uliyofanya. Umekwenda kila sehemu na tumekuona hata kwenye TV ukiitisha Mabaraza, unawasikiliza wanaume na wanawake, unawasikiliza wale wote waliopata matatizo ya kunyang'anywa viwanja vyao na umeyafanyia kazi wewe pamoja na timu yako. Songa mbele umepatia, hicho ndiyo Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nipongeze lingine la kuweka madawati ya kushughulikia matatizo ya nyumba na matatizo ya viwanja. Hii ni hatua nzuri sana, tunatakiwa sote tuipongeze na tuhakikishe haya madawati yanafika kila Halmashauri, ili wananchi waweze kuwa jirani, kero zao ziweze kutatuliwa. Naomba Wizara iongeze Wataalam wa Ardhi, kwa sababu wataalam kila Halmashauri ni wachache, tungependa tuone wataalam wanakuwepo mpaka vijijini.

Mheshimiwa Spika, wananchi vijijini wanajenga nyumba bila kufuata ramani. Tunaomba wasaidiwe kupata ramani ambazo ni za bei nafuu. Wataalam wawepo wawasaidie kuchora ramani ili waweze kujenga nyumba kwa kufuata vigezo vinavyotakiwa na kwa ramani ambazo zimepitishwa, lakini zipatikane kwenye Halmashauri zetu. Wanashindwa wazipate wapi ndiyo maana wanajenga nyumba vijijini, lakini kila mtu anajijengea yeye anavyoona. Tungependa wajenge kwa kufuata ramani ambazo zimetengenezwa na ambazo ni za bei ndogo na zipatikane kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, napongeza utoaji wa hati za kimila na kuweza kutambulika. Ningependa elimu itolewe zaidi ili wananchi wajue kuwa zinaweza kutumika pia kuweza kutoa kama dhamana kwa mikopo. Napenda pia wapimaji wa ardhi wahakikishe wanawake wanaendelea kupewa ardhi, badala ya kuendelea kumiliki ardhi ambazo ni za familia, baadaye wanapoachana wanakosa urithi. Kwa hiyo, naomba suala la kuhakikisha wanawake wanapewa ardhi vijijini nalo liendeleo kutiliwa mkazo. Napongeza katika Katiba inayopendekezwa haya yote yamewekwa na nina uhakika muda utakapofika tutaipigia Katiba hii Kura ya Ndiyo ili iweze kujibu matatizo yote yaliyokuwa kero kwa muda mrefu hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo natakiwa nilizungumzie ni la viwanja. Mara nyingi kiwanja kimoja wanapewa watu wawili au watatu, lakini Waziri amesema hili lote sasa linaangaliwa. Kwa vile tovuti itakuwepo, tunaomba hiyo tovuti iweze kufanya kazi haraka ili viwanja vyote viingizwe, kila mtu kiwanja chake aweze kujua kiko wapi na pia kujua gharama anazodaiwa. Nafikiri hilo ndiyo litakuwa suluhisho la kutatua tatizo la watu kusindwa kulipa kodi, kwa sababu hawakumbuki wanadiwa kiasi gani. Ikiwa kwenye mtandao, itakuwa ni rahisi kila mtu kujua anadaiwa kiasi gani na kuweza kulipa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni lile la kuondoa VAT kwenye vifaa vya ujenzi vinavyonunuliwa na *National Housing*. Hili ni jambo muhimu sana, ni jambo la kujivunia na wote tunatakiwa tuipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inayowasikiliza wananchi wake wakati wote. Haiambiwi na mtu na wala haielekezwi na mtu, inajua wananchi wake wanahitaji nini kwa sababu ndiyo iliyopewa dhamana ya kuwaongoza Watanzania. Kwa hiyo, itaendelea kusikiliza matatizo ya wananchi wa aina zote bila kujali inatolewa na chama gani na mtu gani, lakini yenyewe ndiyo yenye dhamana na yenyewe ndiyo yenye wajibu wa kujua tatizo ni lipi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nizungumzie suala la kuhakikisha miji yetu inapangwa na ni kweli miji mingi imejengwa bila kupangwa. Miji mipya inayoanzishwa na Wilaya mpya zinazoanzishwa, nafikiri hizo ndiyo tungeangalia zipangwe vizuri ili nazo zisije kujikuta zinakuwa kama ile miji ambayo ilianzishwa zamani. Kwa mtindo huu tunaokwenda nao, nina uhakika tunaweza tukafika mahala ambapo tumetarajia kufika.

Mheshimiwa Spika, naomba Watanzania waendeleo kujiandikisha walioko kwenye mikoa ambayo hawajajiandikisha. Mikoa yetu ambayo tumejiandikisha, tumejiandikisha kwa wingi ili tuhakikishe tunakipa Chama cha Mapinduzi kura za kishindo kuonyesha kazi ambayo imefanywa kwa miaka yote hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunampongeza pia Rais wetu, kwa kazi nzuri aliyofanya ya kutengua hati zote na kuhakikisha wananchi ambao walikuwa hawana ardhi sehemu mbalimbali hapa nchini wanapewa. Naomba katika huo mgawanyo wa ardhi na wanawake na vijana waendeleo kufikiriwa kupewa ardhi ili waweze kulima na kuweza kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie kuunga mkono hoja. Nirudie kumpongeza Waziri na tunamhakikishia wananchi wa Mkoa wa Iringa na hususan Jimbpo la Ismani kwamba, utaendelea kuwa palepale na kura zote ni zako. Ahsante sana kwa kunisikilza. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Clara Mwatuka, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mrema na baadaye Mheshimiwa Haji Khatib Kai!

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii.

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema na kufikia kuweza kusimama mahali hapa kwa nia ya kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijafika kwa Waziri, naomba nimpongeze Mheshimiwa Nehemia Mchechu, kwa kazi anayoifanya kwenye ujenzi wa nyumba. Kwa kweli sikutegemea Masasi kutakuwa miongoni mwa sehemu za yeye kwenda kupeleka ujenzi wa nyumba hizo. Namwomba Mungu azidi kumwongezea maarifa na juhudi aweze kuendelea na ujenzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawe pia nikushukuru kwa ujasiri ulionao kwa kazi unazofanya, kwa kweli unaongezeka siku hadi siku kiasi kwamba lile walilokuwa wamelisemea watu wengine kwamba ungefaa kuwa Rais na mimi ningekuunga. *(Makofi)*

Ningekuunga mkono tu, kwa hiyo, kachukue tu fomu, tupo wanawake wenzako tutakuchangia. *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Tutaondoka wote hapa Bungeni kuchukua fomu. *(Kicheko)*

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii ambayo ni ya muhimu sana, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu na jopo zima la Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, utakuwa shahidi, tangu miaka mitano hii ambayo tumekuwa hapa mimi nikiwepo, sijapata kuona siku yoyote ile, mwaka wowote ule ambapo Kamati imepigwa makofi wakati Waziri anasoma bajeti yake. Hii ni mara ya kwanza; kwa hiyo, Mheshimiwa Lukuvi hongera sana. *(Makofi)*

Nakupongeza hasa na inaonekana hii Wizara umeipenda sana, kwa sababu unaonekana umejiandaa, vitabu vyote hivi umejiandaa vya kutosha, ni kazi nzuri ambayo mmeifanya ukishirikiana na dada yako huyo Angellah Kairuki. Umenivutia zaidi kwenye kitabu hiki cha Kiongozi cha Wanakijiji Katika Ushirikishwaji wa Mipango na Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi Vijijini. Umeonyesha hata yule mwanakijiji akisoma kitabu hiki atafarijika. Umeeleza kila jambo, yaani mpango uliotimia; hongera sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nikuombe sasa, hali ya vijiji vingine ujengaji wake siyo mzuri. Nikitolea mfano pale nilipo, Kongowe Mzinga. Ujengaji wa pale hakuna upimaji, viwanja havikupimwa, watu wamejenga kiholela.

Nimewahi kuzungumzia hapa kwamba, pakitokea ajali nyumba za ndani ndani huko kama inaungua moto, hakuna nafasi ya kupitisha gari la zimamoto kwenda kuzima kule. Ikitokea kukawa na mgonjwa vijiji vya ndani, majumba yaliyopo huko, hakuna barabara ya kwenda kusaidia kumchukua mgonjwa kule kumpeleka hospitali. Kwa hiyo, naomba ufanyike utaratibu wa kupima, majumba yale yajengwe kwa utaratibu ambao ni wa hali ya kisasa, tupo kwenye hali ya zamani ya mwaka 1947, haipendezi.

Kulingana na utendaji wako wa kazi, nina imani kabisa kwamba, utalishughulikia hilo, maana kama umeweza kupita sehemu mbalimbali zenye ugomvi na hali iliyoshindikana, umeweza kutatua migogoro ile, hata hilo utaliweza kwa kuwa muda ni mchache, nitakutajia tu ni mambo gani uyatilie maanani uyashughulikie.

Mheshimiwa Spika, niende na hali ya mikopo, upatikanaji wa mikopo kwa kutegemea masharti ya kwamba mtu awe na hati miliki au awe na kitu cha thamani ambacho hakihamishiki, kwa mfano nyumba au mashamba. Hati miliki ya asili siyo rahisi kwa sehemu zingine, kwa sababu mashamba hayo tunategemea kupewa tu ya wazazi na sehemu pengine ndogo tu; kwa hiyo, hilo nalo lishughulikie. Vilevile hati miliki zenyewe sehemu zingine upatikanaji unakuwa mgumu. Samahani, nitolee mfano hati za viwanja; mtu anaweza akawa amelipia amemaliza anakaa miaka hajapata hati, ukienda wanakuzungusha mpaka utatoa hela.

Sasa hali hii inaonyesha kwamba, rushwa inakwenda kila sehemu. Lishughulikie hilo nalo, ukifanikisha hilo mambo yako yatakuwia mazuri tu. Kwa kuwa umeshaamua kujitoa muhanga kwa ajili ya hili, basi endelea ili na Mungu akushuhudie kwamba umedhamiria kweli.

Mheshimiwa Spika, nichukue mfano wa hati za viwanja, mtu anaweza akawa amemaliza kulipia, anakaa miaka hajakata hati, ukienda wanakuzungusha mpaka utatoa hela. Sasa hali hii rushwa inaonekana kwamba kila sehemu inakwenda. Lishughulikie hilo nalo, ukifanikisha hilo mambo yako yatakuwa mazuri tu; na kwa sababu umekwishaamua kujitoa muhanga kwa ajili ya hili, basi endelea ili na Mungu akushuhudie kwamba umedhamiria kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hali ya migogoro kwa wakulima na wafugaji sehemu kubwa tunachangia viongozi, kwa sababu utakuta Mkuu wa Wilaya amejimegea sehemu na yeye kule, au viongozi wengine. Wanashindwa kutatua matatizo yale, watafanyaje wakati na wenyewe wameshajimegea kule.

Mheshimiwa Spika, mwingine naye ndiye anakuwa chanzo, anashabikia upande ule ambao yeye mwenyewe ana maslahi nao. Kwa mfano, wafugaji wengine wanatozwa ng'ombe, sasa akishapata ng'ombe atawasimamia wale wafugaji kwamba, wavuruge tu waende wakachungie hata kwenye mashamba ya watu. Nimesikitishwa jana, juzi nimesikia kwenye vyombo vya habari kwamba wafugaji wamekwenda wakakata mazao kwenye mashamba ya wakulima eti kwa sababu wao wanatetewa na mkuu aliyepo pale. Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa Lukuvi jaribu au fanya bidii ya kwenda kusuluhisha sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka juzi ulitoa kazi kwa Kamati hii ya Maliasili, Ardhi na Mazingira kwenda sehemu nyingine zile kwa ajili ya hii migogoro. Naomba hilo nalo litazamwe ili Kamati iende pale ipunguze walau kama sio kumaliza, lakini isaidie kutatua migogoro ile.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi, niliwahi kuzungumzia kwamba wengine wanaopewa kwa kuwa hakuna elimu iliyotolewa, sasa tuangalie, kama kutakuwa na uwezekano awamu hii ya Mheshimiwa Lukuvi awape elimu, hata hizo za vijijini sio za kwamba wapelekwe shuleni lakini humo humo kwenye kata wapate elimu kidogo waweze kuongoza watu hawa, wawahukumu watu kadri ya Mungu anavyopenda. Kwa sababu, hivi sasa inaonekana wapo zaidi kwenye mambo ya rushwa, anayetoa pesa ndiye atakayepata haki hata kama eneo lilikuwa la kwake kisheria, atanyang'anywa tu kwa sababu ya kukosa pesa. Hivyo, wakipata elimu, pengine itasaidia kupunguza matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile wakati huo ilikuwa kwamba, Mabaraza haya ilikuwa mpaka uende mkoani ndipo ukapate kule, nilishukuru kidogo niliposikia kwamba mpaka wilayani sasa watahughulikia, basi litiliwe maanani hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mengi ya kusema nilikuwa nayo, lakini ameninyang'anya Mheshimiwa Lukuvi kwa jinsi anavyofanya kazi hii na kwamba kila mmoja ameshuhudia humu ndani, maana haijatokea kwamba mpaka sisi Wapinzani huku tunashangilia anaposema, tunapiga makofi, yaani ni kwamba ametumaliza. Kwa jinsi hiyo, naomba aendelee na hali hii, apate afya njema na ikiwezekana sio vibaya akirudi na kama atabahatika, kama hatapata Jimboni, basi Rais atakayepata nafasi amteue awe Mbunge na akifika hapa apewe nafasi hii azidi kuendeleza, maana sikuona yule aliyekuwepo nyuma alifanya kazi, lakini ameondoka na kesi ametuachia huko vijijini, lakini yeye anapita kufufua mle ambamo kulikuwa na matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mheshimiwa Lukuvi anastahili pongezi sana, aendelee na mimi nitakuwa nyuma yake, yaani sehemu zile ambazo atashindwa kufika kama ni upande wa kwetu, nitajaribu kusaidia kwa kweli kumwitia kwamba njoo ushughulikie hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Haya, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Khatib Kai na Mheshimiwa Herbert Mtangi ajiandae!

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Lukuvi na dada yangu Mheshimiwa Angela Kairuki kwa kazi nzuri, kazi takatifu wanayoifanya. Nimpongeze na Rais Jakaya Kikwete na Waziri Mkuu, hasa kuhusu tatizo la Lokolova kule Vunjo.

Mheshimiwa Spika, pia, niungane na Mheshimiwa Halima Mdee kwamba, kule Kilimanjaro hatuna Mkuu wa Mkoa, tuna dalali wa ardhi. Hatumsingizii, kwa sababu wakati Rais amekuja, baada ya ile biashara ya mpakani, tukakubaliana tutafute Soko la Kimataifa.

Wale wanaushirika wa Lokolova, kwa upendo, kwa ukarimu, bila kulipwa hata mia, wakakubali kugawa ardhi yao ya ufugaji na kilimo eka 140, bure.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mchakato wa kuanza kujenga soko pale ndipo ukaanza, eneo lingine likabaki, lakini, kwa hila za Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Leonidas Gama, huyo kada wenu, alichokifanya, kwanza ni kwenda kufuta ile hati ya ushirika, ule Ushirika wa Wakulima na Wafugaji kwa hila bila kuwashirikisha wahusika.

Wale wanaushirika wamehangaika mpaka kwa Waziri Mkuu, wengine tumekwenda mpaka kwa Rais. Nakushukuru Mheshimiwa Lukuvi na mwenzako hapo, ule Ushirika sasa umerudishwa rasmi kwamba wataendelea na Ushirika wa Wakulima na Wafugaji.

Mheshimiwa Spika, sasa zile eka 140 ndizo walikuwa wametoa, zikabaki kama eka 2400. Sasa zile 400 wakawadanganya kwamba mtaendelea nazo na Serikali itachukua eka 2000 kwa ajili ya kujenga mji wa kisasa. Gama akaenda huko China kwenda kutafuta hao Wachina wake, akaniacha mimi Mbunge wa Jimbo la Vunjo, akatafuta watu wake wamekwenda kwa ajili ya kujenga mji wa kisasa, wale wananchi wa pale, wafugaji na wakulima wala hawakushirikishwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachotaka kusema, Mheshimiwa Lukuvi uliichofanya Kigamboni na ufanye kule Lokolova, kwamba wale wananchi, ardhi ile eka 2,600 ni za kwao, watatafuta wawekezaji wenyewe, watanunua hisa wenyewe na kama ni kushirikiana na mtu yeyote duniani, tena wana vijana wao maprofa wa chuo kikuu, wameshawaandikia *write up*. Sisi hatutaki Mkuu wa Mkoa na hilo genge lake wanaunda kampuni yao ya kuja kumiliki Lokolova, hakipatikani kitu pale! Hilo la kwanza. Kwa hiyo, Mheshimiwa nakushukuru sana, uliyoyafanya Kigamboni uyafanye kule Lokolova.

Mheshimiwa Spika, la pili, nilikuandikia barua kuhusu tatizo la Himo. Barua yenyewe iko hapa, nikakufafanulia. Matajiri wa Himo wanaotutesa na wanaotaka tuondoke kwenye madaraka waweke watu wao, mashamba wamepora, wamejamilikisha kwa kutumia hawa maafisa wako hapo kwenye *gallery*. Kwa sababu huwezi, *general land* unampa mtu eka 11.7 eti kwa ajili ya kituo cha redio, sio kiwanda cha redio. Watu waliokufa mnawagawia ardhi, nimeorodhesha watu wote hapa na sisi hatuwezi kukubali na wananchi wamezingira lile eneo, hakitoki kitu pale na mambo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa najua kazi hiyo ni ngumu sana, Mheshimiwa Lukuvi unafanya kazi niliyokuwa nafanya lakini ni kazi rahisi ni kazi takatifu, kazi ya Mwenyezi Mungu. Yale maeneo ambayo ni *open space* waliyoenda kujenga, ukayabomoe usiogope na mimi nilikuwa nafanya kazi kwa ujasiri kama unavyofanya. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, juzi nime tembelea huyu Mwadhama Kardinali Polycarp Pengo, kwa sababu watu wanaviamia kule Vunjo, hawanitaki, wananchi changia kama mpira wa kona, CCM na UKAWA, nikataka kwenda kujua...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanamwingilia mzungumzaji bila utaratibu)

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Ndiyo, hasa UKAWA ninyi siyo watu wema sana. *(Makofi/ Vicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, na yeye aweke kwenye kumbukumbu zake, awe jasiri na Mheshimiwa Angela pia. Maneno aliyoyasema Polycarp Pengo, ukitaka ile sauti yake, *WhatsApp* yangu ni 0712261229, nitakurushia usikie sauti. Anasema hivi, anamwambia nini Mrema kwa watu wema waadilifu, wacha Mungu:

“Mawazo yako daima nimekubaliana nayo hata kama umeingia Chama cha Upinzani hujawa mtu wa kuzusha vurugu kwa sisi wala kwa watu wengine. Umeongelea daima vitu ambavyo vinalinda haki, na hatuwezi tukapikwa katika chungu kimoja sisi na CCM, kuwe na nafasi ya vyama vingine sawa tutachangia mawazo, lakini hatuna sababu ya kukatana shingo sababu eti huyu ni chama kingine na ndani hakuna tofauti yoyote.”

Mheshimiwa Spika, akaendelea kusema: “...kwa hiyo mimi daima nimekuwa nakuheshimu sana”. Huyo ni Pengo, nimemrekodi ndiyo sababu nikakupa na *WhatsApp* nikurushie. “Nakuheshimu sana, sijawahi kuwa na kitu nikasema niitieni Augustino niije kumueleza kwamba hiki kibaya na kama ningekiona ningekuwa nimekwishakuita, nisingekuwa na hofu ya kukwambia hiki unachosema ni kibaya. Daima nimekuwa nikisema ni mawazo ambayo lazima yaruhusiwe na hayana madhara yoyote.

Kwa hiyo, nakushukuru pia, kwa historia yako na mchango wako, watu wanaweza wakasema lolote wanalotaka, lakini naona kuna umuhimu wa mchango wako katika nchi yetu ya Tanzania na hilo nalitamka, na sio mimi tu, bali nalitamka kwa niaba ya waumini wote kwamba umekuwa mchango mkubwa katika historia ya Tanzania, watu wengine wanaweza kuwa na mawazo tofauti, lakini kwa mchango wako ni wale tu wenye uovu wanaoweza kuukataa.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninao waovu kule kwangu ndio wanaonichangia kama mpira wa kona na kwa ushahidi, hii ni picha niliyopiga na Mwadhama Pengo. Naomba Kamera mpeleke kule Vunjo. Angalia baraka napewa na Pengo, hii hapa! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Lukuvi, aendelee, asiogope. Nataka aitengeneze Vunjo iwe kama Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Kwaheri ya kuonana! *(Makofi/Kicheko)*

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba mbingu na ardhi kwa kuweza kuniamsha salama siku ya leo nikiwa na afya tele na kuweza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu kuweza kutoa mchango wangu kwenye hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, Sheria za Ardhi Namba 4 na Namba 5 za mwaka 1999 zinatoa miongozo muhimu ya umiliki wa ardhi Tanzania. Sheria hizi zinatoa fursa ya kuhakikisha...

SPIKA: Huwa hatusomi!

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Sheria hizi zinatoa fursa kwamba ardhi yote Tanzania inafaa kumilikiwa kisheria. Wananchi wengi waliomba kupatiwa hatimiliki za ardhi Tanzania. Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilifanya safari ya ziara ya kwenda nchini Uganda kwa ajili ya mafunzo ya kujifunza ni namna gani wenzetu, majirani zetu Uganda wamefanikiwa katika mfumo mzima wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, mwananchi wa Uganda anapotaka kuomba hatimiliki ya ardhi imekuwa ni rahisi tofauti na kwetu Tanzania. Kwa mfano, hapa kwetu Tanzania mwananchi anapotaka kuomba hatimiliki anaanza kwenye kijiji, anaenda tarafa, anakwenda wilaya. Kwa kufuata mtiririko wa wenzetu Uganda, ndani ya wiki moja anakuwa amepatiwa hatimiliki ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, niishauri Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, mwananchi anapomba hatimiliki iwe ni sawa sawa na utaratibu wanaotumia wenzetu Uganda kwani itasaidia kwa mwananchi huyu kuweza kujikwamua kimaisha na kuendelea na shughuli zake za kawaida.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu vilevile ilifanya ziara nchini Dubai kwa ajili ya kujifunza ni namna gani wenzetu Dubai wameweza kufanikiwa kupiga hatua ya kuweza kufanikisha Shirika la *National Housing* la nchini Dubai. Kitu ambacho nilibaini au Kamati ilibaini, ni kwamba, wakati tunakwenda nchini Dubai tulijua kwamba Kamati inakwenda kujifunza kwa watu wa Dubai, lakini kitu cha kusikitisha ni kwamba, wakati Kamati imefika Dubai ilikutana na wahusika wa Shirika la Nyumba la Dubai, lakini wakati huo huo tunaangalia na tunakutana na Mtanzania ambaye ameweza kuliongoza Shirika la Nyumba la Dubai (*National Housing*).

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni kitu cha kushangaza na ni kitu cha ajabu na naweza kusema kwamba ni aibu. Ni aibu kwa sababu sisi Watanzania tunaondoka tunakwenda kujifunza kwa wenzetu Dubai, lakini tunakwenda kujifunza kwa wale wale Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli binafsi jambo hili sikulifurahia hata kidogo kwa sababu Mkurugenzi Mkuu wa *National Housing Dubai* ametuambia maneno yafuatayo:- Kwamba, anaona aibu kusema kwamba yeye ni Mtanzania. Anaona aibu kwa sababu yeye Mtanzania, lakini wamekuja Watanzania kujifunza katika *National Housing* ya Dubai, yaani ni vipi Tanzania inaweza kujifunza kwa Mtanzania! Kwa kweli jambo hili sio jambo zuri, ni aibu kwa Tanzania, ni aibu kwa Watanzania pia.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi Mkuu wa *National Housing Dubai* anasema pia kwamba, lolote ninalotaka kufanyiwa nafanyiwa na anafanyiwa kwa sababu ikiwa jambo lile litakuwa lina faida kwa *National Housing Dubai*, basi jambo lile halikaliwi kwenye Baraza la Mawaziri kujadiliwa, linaamuliwa na linafanywa hapo hapo.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, *National Housing* haiwezi kupiga hatua mbele, wala hatuwezi kufanikiwa katika Shirika letu la *National Housing* tunaposema kwamba, *National Housing* inataka kujenga nyumba za gharama nafuu, hatuwezi kupata nyumba za gharama nafuu iwapo tozo zote za ushuru hazitoondolewa. Ni kweli kwamba Serikali imekubali, lakini kama ni kweli imekubali, ni vyema basi ianze sasa ili Watanzania waweze kufaidika na Shirika la Nyumba la Taifa ili waweze kupata hizo nyumba za gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *National Housing* ni Shirika ambalo lina uwezo mkubwa na Mkurugenzi huyu Mkuu wa *National Housing Dubai* alikiri kwamba *National Housing Tanzania* ina uwezo mkubwa na ina wataalam wakubwa, lakini kitu kinachoshangaza na kitu ambacho kinafanywa na *National Housing* hawafanyi vizuri, hata sisi Kamati ya Ardhi Maliasili tumeshawahi kushauri kwamba, Shirika hili lipewe mamlaka kamili, liweze kujitegemea. Kwa hiyo, ni kweli kwamba Shirika la *National Housing* lina uwezo mkubwa wa kujiendesha lenyewe ili kuweza kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa *National Housing Dubai* amekiri, hatuoni sababu ni kwa nini sasa *National Housing* haiwi ni taasisi ambayo inajitegemea, ni taasisi ambayo inajendesha ili iweze kufikia hilo lengo ambalo tunalitarajia au tunalolitaka kwa Tanzania!

Mheshimiwa Spika, ikiwa ni hivyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi alivyoanza na jinsi alivyoanza na Naibu Waziri wake, tuone kwamba sasa analitetea Shirika la *National Housing* ili liweze kupata mamlaka yake na kujiendesha ili kuweza kupiga hatua mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nakushukuru.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Nilidhani sitapata nafasi, lakini nashukuru.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri Lukuvi pamoja na Naibu wake na watendaji wake. Hii ni historia, kwa muda mfupi tu ambao mabadiliko haya yamefanyika na ameingia katika Wizara hii tunashuhudia mabadiliko makubwa sana. Hii ni dhahiri kwamba huko tunakokwenda Mwenyezi Mungu awajaalie ili muweze kusaidia nchi hii na wengine waige mfano wenu, maana wako wengi, lakini tunasema waige mfano kutoka kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imekuwa na mtatizo makubwa sana huko ilikotoka, ni imani yangu kwamba kwa kadri Mwenyezi Mungu alivyokujaalia Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wamebadilika, ni wazi kwamba huduma za Wizara hii zitabadilika. Kwa hiyo, tunawaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahi kama wengine kwa viambatanisho ambavyo wametupatia, lakini, natoa ushauri kidogo kwamba, katika kiambatanisho kinachoonyesha Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi, kitu ambacho mmekionyesha pale ni tathmini ya kuonyesha kwamba idadi ya watu imeongezeka nafikiri kwa 2.7%. Hata hivyo, ni vizuri mkaweka takwimu, wapo wenye uwezo wa kuelewa maana ya 2.7%, lakini tulio wengi tunapenda kuangalia takwimu.

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo tu nimewapa, idadi ya watu Tanzania huko tulikotoka ilikuwa 8,000,000, lakini leo tunavyozungumza tumefikia 45,000,000 mpaka karibu 48,000,000. Sasa ukizungumzia takwimu za namna hiyo ndiyo unasema kama tuko 45,000,000 na tunasema zaidi ya 60% ya watu wa Tanzania wako huko vijijini, maana yake ni nini, mahitaji ya ardhi kwa ongezeko hili la watu kwa eka ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, sasa ukichukua 60% ya idadi ya watu 45,000,000, utaona 60% inakwenda kuwa ni ongezeko la watu 37,000,000. Sasa watu 37,000,000 ukisema 60 kwa 100 ya watu hao wapo vijijini, tupe *figure!* 60 kwa 100 ni watu 22,000,200, hao wameongezeka. Ardhi ya Tanzania huko tulipotoka, hivi kweli imeongezeka! Hapana, lakini watu wameongezeka. Sasa tujue watu wameongezeka kwa kiasi gani!

Mheshimiwa Spika, ukisema wakulima kwa asilimia hiyo utawapa ekari mbili mbili tu, watu 22,000,000, maana yake unahitaji eka 48,000,400. Sasa ukiwa na takwimu za namna hiyo zinatusaidia kupata picha nzuri ya kujua kwamba alah, kumbe ndiyo sababu kuna migogoro mikubwa ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji na wakulima na watu wengine kwa sababu ya ongezeko la idadi ya watu kwa hesabu za taslimu kwa namba kama nilivyotoa.

Mheshimiwa Spika, nikija katika maeneno mengine, nitaelezea, kwanza nina furaha kwamba, Mheshimiwa Rais amekubali kuridhia kufuta hati za mashamba zaidi ya nane ya Mkonge katika Wilaya ya Muheza peke yake na katika Mkoa wa Tanga ni sisi na Handeni tunaongoza.

Hata hivyo, nasema Rais ametusaidia, tumefuta hati za hayo mashamba, lakini kazi kubwa ameomba tuanze ugawaji wa ardhi hiyo. Nashukuru nimeomba utaratibu, Mheshimiwa Naibu amenipa tathmini ya muundo wa Kamati. Nashukuru sana, tunaufanyia kazi na nina imani Kamati yako iko kule inawasaidia ndugu zangu.

Mheshimiwa Spika, kubwa ni kwamba tutajitahidi kwa shamba hili la Kibaranga kuhakikisha ardhi inapatikana kwa wananchi. Wenzetu wengine ambao walianza kugawa shamba hilo kabla hati haijafutwa, wakaanza kujigawia wao wenyewe tena watu ambao ni wa kutoka nje ya Wilaya ya Muheza eka 500, eka 100 na kuendelea. Waligawa kinyume cha utaratibu nje ya utaratibu kabla hati haijapewa utaratibu wa kuifuta. Kwa hiyo, nasema tutakaa tutajadiliana ili kuhakikisha hilo linafanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo moja kubwa ambalo namwomba alifanyie kazi, nimelizungumza miaka na nilisema na ndani ya Bunge hili kwa maandishi kabisa kwamba yanayofanyika katika shamba la Kumburu yataleta matatizo na watu watauana, niliandika kwa maandishi na Wizara ya Ardhi wakati huo walijibu na wakaomba mkoa walifuatilie.

Mheshimiwa Spika, leo nataka nikwambie kwamba niliyoyasema miaka 10 iliyopita, leo yametokea katika shamba hilo la Kumburu, kama nilivyosema watu watapoteza maisha, watu wameshaanza kuuana, kwa sababu gani, walifuta hati ya shamba la Kumburu kwanza hawakufuata utaratibu, wapo watu ambao kisheria walikaa katika lile eneo la shamba ambalo lilikuwa haliendelezwi kwa zaidi ya miaka 12. Watu waliingia wakakaa na wamekaa kwa zaidi ya miaka 25. Ukijumlisha hiyo 25 na 15 unapata miaka mingapi, mpaka wamefika mahali lile eneo likatambuliwa kama kijiji na kijiji kikaandikishwa kipo kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kumbe kimeandikishwa kijiji, hati ya shamba imefutwa na huyo aliyekwenda kufuta hati tulimwambia tumia hekima na busara, unapofuta hati basi toa lile eneo ambalo tayari watu wamekaa kwa miaka mingi, hawakufanya hivyo, matokeo yake watu wanauana sasa kwa kutotumia busara tu. Kwa sababu angeondoa lile eneo tu ambalo wananchi walikuwa tayari wameshaka kwa zaidi ya miaka 40, leo huo mgogoro usingekuwepo, lakini, tumeachia hayo yote yanayotokea.

Mheshimiwa Spika, nilisema ndani ya Bunge kwamba, utaratibu haukufuatwa, waliokuwepo kwenye Wizara hiyo walinihidi kwamba watafuatilia, lakini nasema mpaka leo hakuna kitu. Nitakupa nakala zote za maandishi yote ambayo pia nilikabidhi kwa Waziri aliyekuwa anahusika kwa wakati huo na Mheshimiwa Waziri Mkuu nilimkabidhi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba tusaaidiane kushawishiana namna gani ya kuondoa migogoro hiyo, ni kukaa na mwekezaji yule ambaye mpaka sasa hivi hilo shamba hajamaliza kuliendeleza, anaendelea kwenda katika maeneo ambayo watu wamekaa, wamepanda mazao ya kudumu, huko eti ndiyo wanakokwenda kuendeleza kwa kukata mimea yao, lakini eneo la pori kubwa bado limebaki, hajaliendeleza. Huo ni utaratibu gani katika maisha ya nchi hii ya Tanzania? Hivi kweli tunataka kujenga amani au tunajenga chuki zisizokuwa na sababu?

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, niseme nawaunga mkono *National Housing* kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nina imani kabisa kwamba kama hawataingiliwa, kwa sababu najua wewe upo utasimamia, *National Housing* wataonyesha kitu ambacho hakijawahi kutokea katika Taifa letu na maisha ya wananchi wa Tanzania yatapata nafasi nzuri na fursa ya kuboresha nyumba na maisha yao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, najua muda umekwisha, naomba niishie hapo. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii kama Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii tena katika Bunge lako Tukufu, lakini pia nikushukuru wewe.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu wamesema vizuri sana juu ya sifa za Mheshimiwa Waziri na nitaonekana wa ajabu nisipomsifu kwa sababu ni kweli kafanya kazi nzuri.

Ukisikia kila Mbunge anayesimama anazungumzia mashamba yaliyokuwa yameachwa, mashamba pori Rais amefuta, migogoro imerekebishwa. Kwa kweli ni kazi nzuri. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na Makatibu Wakuu wako. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niko na jirani yangu Mheshimiwa Abuu, amefurahi sana kusikia kwamba mashamba pori ya kule Soga na kwingine yamefutwa. Kwa kweli ni jambo zuri, tunakushukuru sana na tunaomba uendelee kufanya kazi hiyo ili wananchi siyo wa Kibaha tu, bali na wananchi wa sehemu zote waweze kufurahia kazi yako. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufanya kazi hii nzuri ya kumaliza migogoro mingi iliyotajwa katika maeneo mengi, sipendi kuyarudia maeneo ya Babati, Malonje, mashamba ya Sumbawanga na sehemu nyingine, lakini bado kuna matatizo makubwa sana ya shughuli za ugawaji wa viwanja katika halmashauri zetu. Mfano ni Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, viongozi na wataalamu wa ardhi wanajilimbikizia viwanja, wanachukua viwanja vitatu vitatu, wanadhulumu wananchi, mwananchi anafika ana kiwanja chake, wanachukua wanamnyima kiwanja, wanauza kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri sasa aelekeze nguvu zako kwenye halmashauri huko. Kuna hawa *Assistant Commissioners* uliowaanzisha kwenye Kanda, hebu wape nguvu watutembelee ili waweze kushughulikia haya mambo, kwa sababu wananchi wetu wanalalamika kweli. Kuna wakati nilitaka hata nije nikuombe tuwe na ziara ya kwenda Igunga ukasikilize tu wananchi wanavyosema, kwa kweli kuna taabu. Najua hata halmashauri nyingine ni hivyo hivyo kuna shida kweli viongozi wetu hao na wataalamu wetu wa ardhi wanafanya mambo ya ajabu kweli.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba muda umebaki mfupi bado ataendelea mpaka Oktoba, katika kipindi hicho, najua bado utakuwa Waziri, ufanye hii kazi ili tutakapokwenda kumaliza tuwe tumerekebisha na haya mambo ya ugawaji wa viwanja katika halmashauri zetu, kwa kweli ni tabu kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo kuhusu mambo ya nyumba. Tunalipongeza sana Shirika la Nyumba kwa kazi nzuri linalofanya. Naomba pia Serikali ifikirie kwamba nyumba zinazojengwa ni za gharama nafuu, lakini siyo nafuu sana na Wabunge wengi wamesema hapa, ni kwa sababu ya kodi na VAT, lakini bado hata tukipunguza VAT, tukipunguza kodi, bado nyumba zitakuwa haziwezi kuwafikia wananchi wa kawaida kwa gharama nafuu. Gharama nafuu kwa wananchi wa kawaida wale tunaowaondoa kwenye maeneo ya *squatters*, bado tukijenga nyumba hawawezi kupanga wala kuzinunua.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, tulikwenda kutembelea nchi ya Ethiopia na South Africa. Kwa kweli wenzetu pamoja na kuwa na mashirika kama Shirika la Nyumba linalofanya biashara ya *Real Estate*, wao Serikali ina utaratibu tofauti wa kuwajengea wananchi makazi ya gharama nafuu.

Kwa hiyo, Shirika la Nyumba liendeleo, basi mnaweza mkaanzisha na utaratibu mwingine, Serikali itoe fedha makusudi ili kuwajengea watu wa kawaida na watafutwi utaratibu wa kuingia kwenye hizo nyumba. Wananunua vifaa vya ujenzi, wanachukua maeneo, wanajenga na wananchi wa kawaida wanakwenda.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia Mzee Karume alivyoanza, alijenga nyumba, sijui mkoa gani ule? Hivi hatuwezi kufanya hilo jambo kweli wananchi wetu wakaingia kwenye nyumba hizo, kwa namna fulani, wanavyolima walipe kidogo kidogo hata kama ni miaka 100 basi warudishe gharama. Tukiishia tu kwenye Shirika la Nyumba, kwa kweli wananchi wa kawaida wengine hatuwezi kuwafikia.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri, tulishazungumza kwenye vikao vyetu vya Kamati tukakuomba, fikirieni kama Serikali kuanzisha shirika au hata idara huko kwenye Serikali, muanzishe kitu ambacho kitawafikia wananchi wa kawaida, vinginevyo tutawaacha wananchi hawa hawana nyumba.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, napenda kurudia tena kusema kuhusu suala la wafugaji na wakulima wanavyogombana. Katika Jimbo la Igunga, eneo la Wembele ni eneo la ufugaji lakini pia kuna kilimo kimeanza, lakini lilikuwa bado linaonekana ni eneo la hifadhi. Sasa tumemwomba Waziri wa Maliasili na Utalii ali-*categorise* eneo hili tuweze kupanga matumizi ili liwe ni eneo la kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanywa hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi alete mradi wa kupima maeneo hayo yawe ni maeneo kwa ajili ya kilimo na ufugaji, kama alivyofanya Kiteto, kama mnavyofanya Mvomero, basi *next* iwe Igunga, wananchi waweze kupangiwa maeneo haya. Huu ugomvi wa kuuana, ugomvi wa kupigana kwa ajili ya matumizi mabaya ya ardhi umalizike, tunaomba sana.

MBUNGE FULANI: Hata Kibaha!

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Yako maeneo mengi, jirani yangu anasema Kibaha.

MBUNGE FULANI: Na Bunda!

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Bunda pia na sehemu nyingine nyingi, naomba sana Mheshimiwa Waziri mlete huu mradi kwa ajili ya kuwapimia wananchi ili wawe na matumizi salama ya kilimo na ufugaji ili wasigombane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mngekuwa mmeniruhusu, tungeingia vifungu asubuhi kabisa, maana naona mmefurahi. Ni kweli hata mimi kukaa kwangu miaka yote hii, ni mara ya kwanza Wizara ya Ardhi watu wanapigiwa makofi wanapoingia. Kwa hiyo, nadhani ni kazi nzuri, kilichobaki ni kuombeana tu ili tufanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Tutakaporudi saa kumi, nawataja wachangiaji wafuatao ili kusudi wawahi: Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro, Mheshimiwa Esther Bulaya, Mheshimiwa Abuu Jumaa na Mheshimiwa na bado nitawataja Waheshimiwa wengine na Mheshimiwa Chomboh pia awe tayari.

Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli mpaka saa kumi.

(Saa 7.50 Mchana Bunge lilisitishwa Hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuahirisha kikao nilikuwa nimewataja ambao watachangia sasa hivi. Sasa namuona Mheshimiwa Abbas Mtemvu!

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wabunge wa Dar es Salaam na wananchi wa Dar es Salaam, tunakushukuru sana wewe na Wabunge kwa kutufariji kwenye msiba wa mpendwa wetu Mheshimiwa Mwaiposa. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema.

Mheshimiwa Spika, nijikite sasa kwenye masuala ya msingi. Huu ni mwaka wangu wa tisa na miezi sita na toka nimeingia kwenye Bunge hili nimekuwa siungi mkono hoja ya Wizara hii, lakini leo natamka kwamba naunga mkono na napongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tuna tatizo kubwa sana Kurasini, lakini Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri toka wameingia; na Katibu Mkuu wa sasa Ndugu Kidata, nampongeza sana, wamefanya kazi kubwa sana na hivi ninavyokuambia watu waliobaki wako katika matayarisho ya kulipwa. Nina uhakika miezi miwili ijayo mtaa ule mmoja wa Kurasini uliobaki nao utakuwa umelipwa kwa sababu Katibu Mkuu amefanya kazi kubwa sana sana ya kuhakikisha wanalipwa wananchi wa Mtaa wa Kurasini.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imetufilisi maneno, kwa sababu leo tulikuwa tuna hoja mbili kubwa; tulikuwa na hoja ya wapangaji juu ya kodi zilivyopandishwa mara tatu, lakini tunashukuru, mimi na Mheshimiwa Zungu tulikutana na Kamati na tukazungumza na Kamati, Kamati imetuelewa na kuna taarifa nzuri tu. Tunaamini Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho ataizungumzia. Tunashukuru sana na tunaishukuru sana Kamati kwa kuona umuhimu wa kodi kupandishwa mara tatu zaidi na wao kutuunga mkono, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na suala la Keko Maghorofani, kuna maghorofa manne pale, kuna wananchi karibu 64, nao nimekuwa nikilalamika, bajeti iliyopita nilileta picha zao hapa, lakini nikapuuzwa, nao walikuwa katika mpango wa kuhamishwa, ndiyo ilikuwa hoja yangu kali sana mchana huu. Hata hivyo, nashukuru wakati wa mapumziko, chini ya Waziri tumeongea na Mkurugenzi Mkuu wa *National Housing*, Ndugu Mchechu, tumeelewana na tumekubaliana kuwa tarehe 20, kamati ya wale wananchi pamoja na yeye DG na kamati yake na mimi Mbunge tutakutana ili hili suala tulizungumze na limepata baraka za Waziri.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, tulikuwa na mgogoro mkali sana wa Chasimba, lakini Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yake wameushughulikia, tunashukuru sana. Nampongeza sana pia kwa kutatua matatizo ya Makongo, nakupongeza sana kwa kutatua tatizo kubwa la Kigamboni, Mheshimiwa Mbunge kasema pale kuwa lilikuwa ni kero, lilikuwa linamfanya Mbunge anakosa amani Bungeni na Jimboni, lakini pia lilimfedhesha Mbunge wakati anatetea haki za wananchi wa Kigamboni, alitolewa nje kama mkimbizi katika nchi hii. Kwa hiyo, tunamshukuru sana sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nisingependa kupoteza muda kwa sababu natarajia wakati wa majumuisho, yale masuala mawili yatakata majibu. Suala lile la akinamama Mfuko, tumeishaongea, tarehe 20 tutakutana na DG, na namshukuru sana Ndugu Mchechu anafanya kazi nzuri sana. Mimi nilimwambia Mzee ninyi mmetokea Temeke ndiyo Makao Makuu, basi na Temeke muwakumbuke, msitusahau! Kwa hiyo, namshukuru, tumeongea vizuri na tumeelewana. Natarajia lile la kodi, Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho, basi tutapata jawabu hilo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia siku hii ya leo bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, sina tofauti na wenzangu, kwa miaka yote sijawahi kuunga mkono hotuba ya Wizara ya Ardhi. Kwa mara ya kwanza niunge mkono hotuba hii. Watu wanasema mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wameonyesha kwa muda mfupi mbali ya kwamba kuna changamoto kubwa sana; na wote tungekuwa na uwezo wa kusema tuendeleo kuwafanya wawepo, tunaamini kabisa kuwa wangeweza kufanya mambo mengi mazuri na kutatua migogoro na hatimaye kumaliza matatizo makubwa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Lukuvi, *Youth League* wa zamani, kazi yako inaonekana pamoja na Mheshimiwa Angella Kairuki. Pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii, kaka yangu Kidata, ni mzalendo, niseme wazi, anatokea Bunda na hiyo inaonyesha ni jinsi gani Bunda ni hazina ya viongozi na watu waadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa namna ya pekee, mbali ya mbwembwe za siasa na *allergy* ya Chama cha Mapinduzi kwenye hotuba zao, nichukue fursa hii kumpongeza rafiki yangu Mheshimiwa Halma Mdee, kuna mambo ya msingi ambayo ameyaweka katika hotuba yake na naamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaendelea kuyafanyia kazi kama ambavyo Mheshimiwa Lukuvi, Mjumbe wa Kamati Kuu ameanza kuyafanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie migogoro ya ardhi. Wakati tuko kwenye Kamati nilimwambia Mheshimiwa Lukuvi kuwa kwenye Jimbo la Bunda, Kijiji cha Mikomalilo kuna tatizo kubwa, nadhani ulishasikia kwenye vyombo vya habari kulikuwa na tatizo la mgogoro wa ardhi kati ya Wilaya ya Bunda na Serengeti mpaka kuna baadhi ya watu walipoteza maisha.

Niliitwa na Wazee wa kule, wakanipa malalamiko yao, wanamwomba Mheshimiwa Waziri atatue migogoro huu. Inavyoonekana GN ya zamani ya Mkoa wa Mara katika eneo hili imebadilishwa kinyemela. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Lukuvi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna migogoro ya ardhi katika eneo la Salawe, eneo la Mikomalilo nimeshasema, la Mgeta kote huku kumekuwa na matatizo ya migogoro ya ardhi. Sasa naomba unapozunguka katika ziara zako, ujue pia matatizo kama haya Bunda yapo. Pia, nilishazungumzia matatizo ya migogoro ya ardhi kwenye Hifadhi ya Kawangwa pamoja na wananchi wa Kawangwa, Kijiji cha Kawangwa, Unayali, Maliwanda, Muhale, Nyamatoke na Kunzugu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Mheshimiwa Waziri akayapatia ufumbuzi haya mambo yote. Mawaziri waliopita wakiwepo wa Ardhi na Maliasili walishindwa kuyafanyia kazi. Kumekuwa na unyanyasaji mkubwa sana kwa wananchi ambao wanazunguka kule. Inasemekana kuwa hata katika kubadilisha matumizi ya ardhi wananchi hawakushirikishwa. Wananchi hawana tatizo hilo, kinachotakiwa ni ushirikishwaji kwa sababu maeneo mengine ambayo yamechukuliwa kulikuwa kuna makaburi na katika mila zetu watu wanapenda kwenda kuhani katika maeneo ambayo wamewapumzisha ndugu zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Lukuvi atakapokuwa anaendelea na ziara zake, kwa kuwa siyo mtu wa kukaa ofisini, basi naomba atukumbuke na nyumbani kwetu Bunda na kwenyewe kuna matatizo ya migogoro ya ardhi ya Wilaya ya Bunda na Serengeti, lakini pia katika migogoro ya ardhi kwenye Hifadhi. Kwa hiyo, na hilo pia naomba sana liendelee kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, ni kwa nini leo hii kila mtu anaposimama hapa anampongeza Mheshimiwa Waziri? Jambo la kwanza, hivi tunavyoongea isingekuwa ni jitihada zake, tungekosa mradi wa bure ambao tumepewa fedha na *World Bank* wa kuhakikisha kuwa ardhi yetu inapimwa kisasa na hati zinatoka ndani ya muda wa siku mbili au tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua changamoto kubwa leo hii ya kupata hati, unaweza kupata kiwanja, lakini hati inaweza kuchukua zaidi ya mwaka mmoja. Ule mradi tulipewa tangu mwaka 2006, lakini inawezekana haikuwa ni kipaumbele kwa Waziri aliyekuwepo, tunamshukuru kwa hilo. Tunachoomba ni mradi huu uanze mapema ili Watanzania wapimiwe viwanja. Unapokuwa na hati, una uwezo wa kwenda kukopa benki na ukaondokana na umaskini.

Kwa hiyo, tunaomba zoezi hili lianze haraka ili wananchi wanufaike na ardhi yao wakiwemo akinamama, wakiwemo na vijana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ningependa kuzungumzia uchache wa Maafisa Ardhi au wataalamu wa ardhi, wakati tunataka kuanza zoezi hili ni lazima kuhakikisha Wizara ya Ardhi inashirikiana na Chuo cha Ardhi mnachukua wataalamu wa kutosha na kuhakikisha wanakwenda kwenye maeneo yetu katika halmashauri, wapo vijana ambao wanamaliza Chuo cha Ardhi hawana kazi, lakini bado Serikali ina upungufu wa wataalamu wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia suala la *National Housing*, Kamati tumekuwa tukilizungumzia kwamba mhakikishe mnawaondolea kodi ili ile dhana ambayo pia Mheshimiwa Rais anaipigia kelele ya Watanzania kupata nyumba bora iwe na maana. Kama hatutafanya hivyo, watakuwa wanajenga nyumba, wenye uwezo wa kununua watakuwa wananunua kwa milioni 200, lakini hawa wafanyakazi wa kada ya kati, Walimu na Manesi hawataweza kunufaika na nyumba hizi, lakini chanzo ni kodi zisizokuwa na lazima.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Lukuvi, agizo la Kamati la kubomoa jengo lililopo pale Mtaa wa Indira Gandhi lifanyiwe kazi. Jengo lile ni hatari, limeua watu na hatuitarajii tena Watanzania wengine wafe ndipo hatua zichukuliwe. Kingine, tunakuomba kuwa kabla jengo halijajengwa, ufanyike utafiti wa kina kushirikiana na Wizara ya Mazingira ili kuona eneo hilo linakidhi kuwepo jengo la ghorofa ngapi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunavyoongea, pia angalia katika nchi nzima na Mkoa wa Dar es Salaam, kuna maghorofa ya aina ile mengi. Ukienda Sinza, mengine yanabomoka, yanaua watu, lakini bado yapo katika baadhi ya maeneo maghorofa yanajengwa bila kiwango na yanaibuka kama uyoga hata Kariakoo, lakini, kwa muda ambao umefanya, tuna imani mambo haya yote utakuwa na uwezi wa kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, nina uhakika mkibomoa majengo matatu, manne hakutakuwa na mtu yeyote mwenye kiburi atakayeonyesha kama ana uwezo wa kuiweka Serikali mfukoni, anapewa *order* ya kutokujenga na akaendelea kujenga. Kwa hiyo, naomba sana kwa maslahi ya maisha ya wananchi wa pale, kuna msikiti, kuna watoto pale wanasoma madrasa. Kwa habari nilizonazo kuna baadhi ya watu wengine wanaozunguka eneo lile wameamua kuhama kwa ajili ya hofu ya jengo lile lingine pacha kudondoka.

Tunajua kuwa unahitaji utaalumu wa kutosha katika kulivunja lile jengo lakini naamini kabisa kwa sababu una dhamira na ukiamua lile jengo liondoke mapema naamini kabisa kuwa linaweza kuondoka ili liondoe hofu ya Watanzania na wengine ambao wameondoka yale maeneo ukizingatia kuwa

ni maeneo ya kibiashara tunaweza kabisa kuhakikisha kuwa lile jengo linaondoka na wananchi wakaendelea kubaki salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba zoezi la upimaji liendeleo, naomba ule mpango wa kujenga Kituo cha *Satellite* Dodoma ambao unaweza kupima viwanja vingi kwa kanda hii yote ya Dodoma na Singida, hilo jambo linahitaji bilioni sita tu. Naamini kabisa kwa huu mchakamchaka ulioanza wa kuhakikisha Wizara yako inakusanya kodi, hizo fedha zitakuwa kidogo na Kituo cha *Satellite* kitajengwa, Watanzania watahakikisha wanamiliki viwanja vyao kwa uhalali na wanaweza wakatumia hati zao kwa ajili ya kuzikopea.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha *Satellite* ni muhimu, mbali na ule mpango mwingine tuliouona Uganda, lakini hiki Kituo cha *Satellite* kwenye hii kanda kitarahisisha upande mwingine wakati maeneo mengine yanaendelea kupimwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nikupongeze wewe, lakini pia nimpongeze na dada yangu, yeye asingekuwa anakutunza vizuri, kazi hizi usingekuwa unazifanya. Pia na Mheshimiwa Angela, Mheshimiwa Balozi Mbelwa asingekuwa anakutunza vizuri, nadhani hizi kazi pia zisingekuwa zinafanywa. Mheshimiwa Mdee pia, shemeji yangu yule asingekuwa anakutunza vizuri, hizi nondo usingekuwa unazitoa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mimi sijui wanatunzaje kupiga nondo! Mheshimiwa Mohammed Chomboh akifuatiwa na Mheshimiwa Abuu Jumaa. *(Kicheko)*

MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Spika, nami naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na kusimama jioni hii kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Ardhi. Pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kama walivyotangulia wenzangu.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpa pongezi yeye, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, watendaji wote kwa maana ya Makamishina, Maafisa Mipango Miji, lakini pia kwa sifa za pekee *National Housing*, Mtendaji Mkuu na timu yake wanastahili kila hongera kwa bidii yao na kwa utendaji wao wenye ufanisi mkubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi leo ambalo mimi nilitaka kuchangia ni kwa wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi kubadilisha *mindset* zao sasa. Ule uzoefu wa kufanya kazi kama walivyozoea huko nyuma wajue sasa hivi ile hali imelshabadilika. Wajue pia kwamba kati ya vitu muhimu duniani, hakuna kitu kikubwa kuliko ardhi.

Mheshimiwa Spika, ardhi ndiyo ila kitu, sisi sote tuko juu ya ardhi na kila tunachokifanya tunakifanya juu ya ardhi; na kingine chochote tunachokifanya hata kama kikiondoka hapa kwenda angani ni lazima kiondoke juu ya ardhi. Sasa wajue umuhimu huu ya kwamba ardhi ni kila kitu; na hata mwisho wa safari yetu sisi tunarudi ndani ya ardhi. Kwa hiyo, wajue umuhimu huo kwamba wana dhamana kubwa sana kwa watu wa Tanzania, wamepewa dhamana na wana wajibu wa kila linalowezekana watimize wajibu wao kwa mujibu wa taratibu za sheria za kazi zinavyowaruhusu au zinavyowataka. Mtindo ule wa kuichezea ardhi kwa maslahi yao waache kabisa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri ameanza kazi nzuri, Waheshimiwa Wabunge wamempongeza sana, nimeona siri kubwa aliyokuwa anafanya yeye ni *transparency* (uwazi), hakuna kuficha wala hakuna kubabaisha.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, nimebahatika kukaa kipindi kifupi na Mheshimiwa Waziri huyu tofauti na Mawaziri waliopita, tofauti nimeiona ya kwamba huyu Waziri yuko wazi kabisa na yale mambo, nimeshawahi kwenda mara mbili/tatu, ukimshtakia kitu, palepale anamuita afisa, njoo unieleze hiki kiko wapi, hapo hapo, hakuna kesho wala keshokutwa. Hali kadhalika Katibu Mkuu naye pia, hata Naibu Waziri, ni kwamba sasa hivi ile Wizara ina watu ambao ndiyo hasa wanaoweza kuiendesha Wizara.

Mheshimiwa Spika, wenzangu walitangulia kutoa baraka au kutoa mapendekezo ya kwamba Serikali ijayo kwa Rais ajaye, kwa sababu huyu bwana tumemuona kwa miezi sita tu, basi afikirie huyu jamaa kumuweka tena ili aendelee kwa sababu ya maslahi ya nchi, lakini pia kwa maslahi ya Taifa letu kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kupunguza tozo mbalimbali katika majengo, ardhi na kila kitu. Hii ni kutaka kuwafanya kwamba kila mmoja awe na uwezo wa kuweza kulipa tozo zile, jambo ambalo uking'ng'ana na bei kubwa utapata kidogo, kuliko kuweka bei ndogo utapata kwa wingi, ni muhimu zaidi kufanya *collection* ya *revenue* ya Wizara ya Ardhi, ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, pia, tozo hizo zilikuwa zinakosekana kwa sababu ya mtu mmoja, au watu wawili kupewa ardhi mara mbili ama mara tatu, nani alipe nini na haeleweki! Sasa ndugu zangu watendaji mliokuwa na mtindo huo, mmetupeleka mahali pabaya sana kiasi ambacho Wizara inakosa mapato kwa sababu ya *double location*, lakini pia bei kubwa kiasi kwamba mtu akitaka kulipa anashindwa, “anasepa”, kwa hiyo, tunapoteza mapato kila siku.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri alivyoanza kuwa wazi pamoja na timu yake, *transparency* peke yake, uwazi ndio unaweza kuweka kila kitu bayana na tukajua uwezo uko wapi. Tumemsikia hapa hata Waziri Kivuli, cha msingi usiogope kivuli chako. Anaogopa kivuli chake, punguani huyo. Wewe usiogope kivuli chako, hicho kivuli chako! Kwa hiyo, fanya nacho kazi na uzuri wake kwamba naye, kiasi fulani sisi hata kama...

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati, tunapokwenda kupata elimu ya mambo ya ardhi anahakikisha kwamba na Waziri Kivuli anakuwepo, ili aone na yeye elimu hiyo anaipata. Kwa kweli huo ni mpango mzuri, hata kama kuna Kamati zingine hazifanyi hivyo, basi ni vizuri wale Mawaziri vivuli nao washirikishwe katika sekta fulani. Kwa sababu wakati mwingine wanaweza wakazungumza kitu ambacho hakipo. Hata hivyo, leo alipokuwa anazungumza yote hakumgusa sana Waziri akijua kwamba elimu anayo na majibu anayo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa maana ya Waziri kivuli kwa ile elimu aliyoipata na akaeleza hapa bayana kwamba..., pamoja na ndugu zangu wengine wa Kambi ya Upinzani wamei-*support* hotuba yako Mheshimiwa Waziri kwa mara ya kwanza, lakini nakuomba na nakusihi hakikisha kwamba wafanyakazi wako hawatakuangusha, baadhi sio wote. Sasa yale “matogatoga” ya baadhi hakikisha kwamba unaweka sawa. Najua wengi sana ni wazuri, lakini wale wachache wasije wakaharibu sifa yenu nzuri mliyoondoka nayo sasa hivi. (Makofi)

National Housing hongereni sana. Yaani mimi sitaki niongeze lolote kwa sababu naweza nikaharibu ule utamu ambao kila mmoja anaujua hapa. Kwa hiyo, endeleeni, mpo chini ya Waziri madhubuti, na nyinyi Mungu atawasaidia kufika yale malengo yaliyokusudiwa na nchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. (Makofi)

MHE. ABUU HAMAD JUMAA: Mheshimiwa Spika, kwanza kama ilivyokuwa desturi, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia kusimama hapa leo katika Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa mchango wangu katika mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, la pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii muhimu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Pia nichukue fursa hii ya kipekee kama wenzangu wote walivyochukua jukumu lao la kumpongeza Mheshimiwa Waziri, niseme tu mengi yamesemwa nisingependa kuyarudia sana, lakini kwa kweli Mheshimiwa Waziri Lukuvi pamoja na Naibu wake, kazi ambazo mmezifanya kwa muda mfupi zimeweza kututoa matongotongo kwa sisi tunaosema wana CCM, kumbe wakati mwingine tunaweza tukawa na wasiwasi na mambo fulani, lakini kumbe wasiwasi huo unaweza kuondokana kwa kupata viongozi wazuri wenye kujituma, kutafakari mambo na kuwa na huruma na wananchi wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna wakati fulani tulikuwa tunakaa tunasema, nchi yetu yako baadhi ya mambo hayaendi, tukawa tunasema kwa nini! Kila mtu analalamika, wakati mwingine Wabunge wanalalamika, wananchi wanalalamika, lakini suluhu haipatikani, lakini, kumbe majawabu yapo, wakipatikana viongozi wazuri wenye moyo wa kufanya kazi kama Mheshimiwa Waziri Lukuvi, tukipata watu kama hao kumi katika Serikali yetu, tunaweza kupunguza matatizo kwa kiasi kikubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini sio peke yake tu na hii yote inaonesha ushirikiano baina ya Waziri na Naibu Waziri, lakini na watendaji wake kwa ujumla. Yupo Katibu Mkuu pale, Wakurugenzi mbalimbali, ushirikiano mzuri ambao umepelekea kupunguza kero kubwa kwa wananchi. Leo kwa muda mfupi, Wizara hii imeweza kupunguza migogoro takribani 50.

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro kule Arumeru, kuna mgogoro Kigamboni na hasa suala hili la Kigamboni, nimeshangaa sana na bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati, lakini Mheshimiwa Lukuvi ameingia kwa muda mfupi, tatizo hili la Kigamboni tumelizungumza kwa miaka mingi, muda mwingi tunalizungumza na tulikuwa tunaona jambo hili kama tumebeba mawe mazito kichwani. Hata hivyo, bwana mkubwa huyu alivyoingia kwa muda mfupi ni sawasawa na kubeba kijiti cha chelewa, ameweza kuliondoa tatizo hili kwa muda mfupi sana na wananchi kule wameridhika, mambo yanakwenda vizuri, hatukuamini kwa jinsi jambo hili alivyoweza kulichukulia kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni kero kubwa sana kwenye Kamati, mara kwa mara tunazungumzia tatizo hili, lakini, kiongozi umelifanyia kazi. Mheshimiwa Lukuvi, tunakushukuru, tunakupongeza na tunakuombea Mwenyezi Mungu akujalie. Siku moja nilikwambia kwenye Kamati yetu ile, ningekuwa nagombea urais, basi ningekuteua moja kwa moja kabla ya ushindi, lakini kwa bahati mbaya mpango wangu wa kugombea urais bado, labda 2025.

Mheshimiwa Spika, vilevile iko migogoro mingine; Makongo kule, Chasimba, migogoro hii yote ameweza kupunguza kwa haraka zaidi. Nilikuwa namwona kwenye TV mara kwa mara katika ziara zile anajituma, wakati mwingine tunaingia kwenye Kamati, lakini anatoka kwenda kutatua migogoro na ziara hizi zimeweza kusaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza migogoro katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, yako mambo ya msingi ambayo napenda niyaseme kidogo, upande wa Shirika. Kwanza, upande wa Wizara, mchanganyiko huu umekuwa mzuri kwa sababu ukienda Shirika la Nyumba pale vilevile kazi zinazofanywa ni kazi nzuri, Mji wetu wa Dar es Salaam leo umebadilika na maeneo mbalimbali. Miaka ya nyuma huko watu walikuwa hawaitambui *National Housing*, lakini sasa hivi yamekuja mabadiliko makubwa, ukifika Dar es Salaam unashangaa, miradi mikubwa mikubwa, majengo marefu, majengo mazuri yenye kuvutia na yenye kubadilisha mji wetu, lakini vilevile itasaidia kuongeza kodi na vilevile mji wetu umepangika vizuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue fursa hii nizungumzie suala zima la kodi. Kodi ambayo imepunguzwa italeti faida kubwa kwa wananchi na watakuwa na imani.

Mheshimiwa Spika, zamani nilikuwa natambua kuna kitu kimoja kinaitwa Tume ya Bei, lakini nilikuwa naiita Tume ya Kupandisha Bei, kwa sababu Tume ya Bei wakati mwingine inakaa inafikiria kupunguza bei, lakini Tume iliyokuwepo ile kila siku inapandisha bei. Sasa leo nafarijika kuona kwamba Serikali tunakwenda na wakati ambao unatakiwa, inafikia mahali kuona kwamba wananchi wanaoathirika katika eneo moja au lingine ni kuwapunguzia kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kidogo tu, kwa ndugu yangu Mchechu, najua kazi anayoifanya ni nzuri, amebadilisha *National Housing*, mambo yanakwenda vizuri. Yapo malalamiko kidogo tu, nashauri tu, katika kodi wananchi wengi sasa hivi wanalalamika katika upandishaji wa kodi, kodi inapanda sana na kiwango kinakuwa kikubwa sana cha kupandisha kodi. Sasa tulikuwa tunaangalia, katika zile nyumba mpya ni vizuri tukapandisha kodi, lakini kuna nyumba ambazo ni za majengo yale ya zamani, sasa leo tunapandisha kodi wananchi kwa kweli wanalalamika sana.

Naamini Mheshimiwa Waziri mkikaa vizuri na eneo hili mnaweza mkaliangalia kwamba, zile nyumba za zamani mjaribu kidogo kodi ziweze kushuka ili wawe na matumaini makubwa, lakini vilevile Serikali iangalie, iwezeshe *National Housing* waweze kupunguziwa kodi mbalimbali, zifutwe ili waweze kujenga nyumba zingine.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, nichukue fursa hii ya kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kufuta hati za mashamba pori nyingi katika Mkoa wa Pwani na hasa Kibaha kule kwangu. Kulikuwa na migogoro mingi vilevile, lakini karibuni mashamba 19 yameweza kufutwa. Niombe tu yapo maeneo machache tu ambayo namuomba Mheshimiwa Waziri na kama kawaida yake akisema mambo yanakwenda vizuri tu.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo moja kwenye Jimbo langu, Kata ya Ruvu na Kata ya Kwara kuna migogoro hii ya muda mrefu sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili mnisaidie tuweze kumaliza tatizo hili. Vilevile kama kawaida yake Mheshimiwa Waziri, najua jambo hili anaweza kulimaliza mapema, tukaweza kuwaweka wananchi wetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, tumetembea nchi mbalimbali, tunaona wenzetu wanajenga majengo mazuri sana na sehemu nyingine wanasema siasa ni nyumba. Yako maeneo tumetembea wanasema siasa ni nyumba. Sasa na sisi vilevile tunaweza kufanya mambo, wako wasemaji mbalimbali wamezungumza hapa, akina Dkt. Kafumu, wamesema kama Mzee Karume aliweza kufanya mambo hayo, sisi tunashindwa nini!

Mheshimiwa Spika, leo tumeambiwa katika Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, pale Kibaha wanategemea kujenga barabara ya njia sita na barabara zile kubwa (*highways*). Sasa, tukipata barabara zile miji itakuwa mikubwa, ni vizuri tukajiandaa, tukaanza sasa kupima viwanja vyetu vizuri, tujiandae na wimbi kubwa ambalo limejaa Dar es Salaam, watu waanze kupungua wakimbilie maeneo ya Kibaha. Tukiufanya haya yatatusaidia na wananchi wetu kule wanaweza kuishi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nimwombe ndugu yangu Mchechu, miradi mingi imekwenda katika mikoa mbalimbali, lakini Mkoa wetu wa Pwani na hasa pale Kibaha kwangu na uzingatie Mzee mimi ni Mjumbe wa Kamati, uniangalie angalie kidogo. Ukileta miradi hiyo itasaidia, kwa sababu tuna wakazi wengi pale, lakini tuna watumishi mbalimbali. Viwanja vipo na tulishawahi kuwaambia tunayo maeneo pale, tunaweza tukawapa maeneo mkajenga nyumba ili watu wetu waweze kupata nyumba hizo zivasaidie katika kupunguza makali ya maisha. Wote tunafahamu sasa hivi kodi zimepungua na zikipungua kodi maana yake upungufu wa gharama zile za kujenga nyumba zitapungua na wananchi wakipata nyumba zinaweza kuwasaidia katika kusukuma maisha yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Nawashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza, mwaka 2025 nategemea kugombea urais. (*Kicheko*)

SPIKA: Unatangaza nia mapema kabla. Sasa namwita Mheshimiwa Michael Laizer kwa sababu sijasikia mfugaji kabisa hapa. Mheshimiwa Benedict Ole-Nangore hayupo! Halafu kwa upendeleo maalum namuita Mheshimiwa Halima Mdee. *(Kicheko)*

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie Wizara hii ya ardhi. Kwanza kabisa, nitangulize kuunga mkono hoja na niwapongeze sana Waziri pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kati ya Mawaziri wote waliopita katika Wizara hii namkumbuka Waziri aliyekuwepo zamani Gideon Cheyo alikuwa ni Waziri ambaye kila bajeti yake anapongezwa inapita kilaini, ni makofi tu. Sasa Waziri huyu amenikumbusha enzi za Gideon Cheyo kwamba, naye aliiweza Wizara hii vizuri sana, sasa amepatikana Waziri mwingine ambaye ameweza Wizara hii. Wizara hii ni ngumu kwa sababu ardhi ndiyo uhai na ndiyo yenye migogoro kuliko kila kitu. Kwa hiyo, nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa sababu amekuja kutatua matatizo, migogoro sugu ya muda mrefu. Migogoro iliyokuwepo kati ya hifadhi na vijiji, mashamba na wafugaji yalikuwa ni mengi sana. Kwa kipindi kifupi ametatua migogoro ambayo imeshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakumbuka zamani ulikuwa Mwenyekiti wa Kamati hii na tulikuwa wote kwenye Kamati hii. Kuna migogoro ya wakati ule mpaka sasa ndiyo imekuja kutatuliwa wakati huu. Kwa hiyo, nampongeza sana Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Kigamboni tulikuwa tunaambiwa kulikuwa na sheria, sijui hizo sheria zimepita wapi, kwa sababu tulikuwa tunasomewa sheria, kanuni, Rais amesema, yaani ikawa ni vurugu kila siku. Waziri akienda Kigamboni ni vita, akija kwenye Kamati ni vita! Sasa hii imekuja kutatuliwa kirahisi.

Mheshimiwa Spika, nashindwa kujua kwamba zile kanuni zimepita wapi, zile sheria zimepita wapi, yale matamko ya Rais amesema yamepita wapi, mbona Rais ni yule yule? Kwa hiyo, nakushukuru sana kwa sababu umekuja kurahisisha mambo ambayo yalikuwa ni magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa tena na jambo alilolisema Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 27. Anasema dawa pekee ya kudhibiti migogoro na matumizi ya ardhi nchini, ni kupanga na kupima kila kipande cha ardhi na kuwamilikisha wananchi na taasisi kisheria kwa kuwapa hati miliki. Kilichokosekana katika maeneo na kusababisha migogoro ni hiyo. Kwa hiyo, naomba hiyo ikamilike na najua unaiweza.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba, Mheshimiwa Waziri, kuna mgogoro uliopo kati ya Arumeru na Monduli na kati ya Arumeru na Wilaya ya Longido. Wakazi wa maeneo ya Wilaya hizo zote tatu ni ndugu, kwa hiyo, unashangaa ndugu wakigombana kwa ajili ya mipaka ya wilaya. Naomba Serikali iende kutatua migogoro hiyo kwa sababu ni rahisi kabisa, ni kwamba, watu wanalazimisha tu kuhamisha mipaka iliyopo. Tunaomba Serikali iingilie kati kabla watu hawajauwana katika maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ni mgogoro ambao unafahamu, mwekezaji aliyepo kati ya Siha na Longido. Mwekezaji huyu ana mgogoro na vijiji vinne, vijiji viwili vya Wilaya ya Longido na viwili vya Wilaya ya Siha.

Mheshimiwa Spika, eneo lile halijawahi kuwa matumizi ya mashamba, wala halijawahi kuwa la matumizi ya aina yoyote. Lilikuwa ni eneo la mifugo na wafugaji wanafugia enzi na enzi na enzi! Sasa mwekezaji kuja kulifanya kwamba ni eneo la wanyama, bado ni tatizo kubwa sana ambalo wananchi wa vijiji hivyo wanapambana na huyo mwekezaji na mwekezaji amefanya eneo la malisho kuwa ni *National Park* ya kwake. Wafugaji wanasema kamwe, huyo mwekezaji hatachukua eneo lile, kama ni kuwauwa hawa wafugaji, wapo tayari na hawataondoka katika eneo lile. Tumejaribu kusuluhisha hilo jambo, limeshindikana na nashukuru wafugaji wamekuja kukuona.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nalifurahia sana ni fidia. Umekuja kuweka wazi jambo la fidia, kwamba ni lazima kila eneo ambalo litachukuliwa, iwe na Serikali, iwe na mwekezaji ama na nani, wananchi walipwe fidia. Nakupongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni agizo alilotoa. Naomba hili agizo alilotoa leo, kwamba ole wao! Haya maagizo yote naomba yafike kwenye halmashauri, kwa sababu watu ambao wanawanyanganya wananchi viwanja ni watu wa halmashauri zote, wala siyo Halmashauri ya Longido tu ni halmashauri zote, wanapima viwanja na kuficha na kuja kuuza hivyo viwanja kwa watu wengine, wamefanya kwamba ni miradi yao. Naomba hili jambo litatuliwe katika halmashauri zote, kwa sababu wapimaji ni wao na wanatumia sheria ambazo siyo wazi. Naomba hili aliweke katika maagizo yake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nakupongeza sana kuhusu jambo la Emborey Murtangosi pale Kiteto, nadhani Mbunge wa Kiteto hayupo leo, naomba sana hili jambo litatuliwe, kila mwananchi, mkulima ajue hili ni eneo lake, mfugaji ajue kwamba hili ni eneo lake.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hili limekuwa ni mgogoro wa muda mrefu na bado linaleta shida, naomba wakulima na wafugaji waweze kukaa vizuri, wakaishi, wakafuga na wakalima bila mgogoro.

Mheshimiwa Spika, katika ukanda wetu siyo kwamba sisi hatuna wakulima, tuna wakulima wengi. West Kilimanjaro katika Jimbo langu wote ni wakulima, lakini kuna wafugaji huko kwenye maeneo hayo, wanaheshimiana ndiyo maana husikii mgogoro kati ya wafugaji na wakulima katika Mkoa mzima wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, tatizo letu ni wawekezaji, hawa wawekezaji wanaopewa maeneo kwamba eneo hili ni wazi, siyo wazi kwetu, eneo hilo mndlosema kwamba ni wazi ndilo eneo la malisho na sisi tumetenga malisho tunaheshimu, huwezi kuweka makazi ndani ya malisho. Sasa kama sisi hatuwezi kuweka makazi ndani ya malisho, kwa nini mnawaleta wawekezaji kuweka ndani ya malisho na kuja kufanya kwamba ni hifadhi yao? Ndivyo alivyofanya huyu mwekezaji. Mnasema kwamba ameuziwa na *Breweries...*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee, una haraka! (*Kicheko*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Kwanza, Mheshimiwa Waziri, Wabunge wamekusifia sifia, lakini ujue kwamba kazi uliyoifanya ni kidogo sana ukilinganisha na ukubwa wa tatizo. Kwa hiyo, usije ukavimba kichwa ukajua kwamba umemaliza, kazi ni ndefu sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa dhati kabisa, nitambue kazi ambayo imefanywa Jimboni kwangu, Chasimba, Makongo. Najua wananchi wa Chasimba wananiangalia, wananchi wa Makongo wananiangalia, yale mapambano ambayo tuliyaanza sasa yanaonekana kufika mwisho na haondoki mtu. Kikubwa ni kwamba ni wajibu wa Serikali kwenda kukutana na wananchi, kukubaliana na wananchi, kwenda hatua kwa hatua na kwa uwazi, Watanzania hawana matatizo, matatizo tunayo sisi viongozi kwa vificho, ubadhirifu na tamaa, lakini, ukiwaambia nini kinachotakiwa kufanywa watakupa ushirikiano wa dhati sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nilipogeukwa mwaka jana kwa sababu wananchi walikuwa wameshakata tamaa kabisa, wakasema hatutoki, Serikali ikaja ikasema Mbunge utusaidie tuwalipe fidia, wananchi wakasema kwa kuwa Mbunge umesema ngoja tuangalie tutaendaje. Tukafika katikati ya njia tukatapeliwa!

Mheshimiwa Spika, sasa nashukuru kwamba kile kilio cha wananchi tokea mwanzo sasa kimesikika. Nitakuwa sina shukrani kwa niaba ya wananchi wangu ambao walikuwa na hatihati sana ya kupelekwa Pwani huko, sasa hivi kuna uhakika wa kubaki. Kwa hiyo, vikao vyetu basi tuiendeshe kwa kuzingatia kwamba kwenye maeneo tunayokwenda tuna wananchi wa kipato cha chini kabisa, kipato cha kati na kipato cha juu. Kwa hiyo, kwa maamuzi yoyote tutakayofanya, ambayo yatahitaji ushiriki wa wananchi, ni lazima tuzingatie hivyo vitu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kawe, tunafahamu *Tanganyika Packers* kwa kipindi kirefu sana lile eneo lilikuwa chini ya mikono ya wachache, lilikuwa halieleweki eleweki. Katika kipindi changu cha miaka mitano nashukuru kwa kweli Shirika la Nyumba pamoja na Serikali kwa kiwango fulani walisaidia, lile eneo sasa hivi wamepewa Shirika la Nyumba, kinajengwa kitu kinachoitwa Kawe *Satellite City*, inawezekana watu wengine mkawa mnakuja kujifunza Kawe jinsi miji inavyopangwa. Kwa hiyo, hayo ni matunda ya kuwa na Wawakilishi wanaosema, lakini vilevile Wawakilishi ambao wanatoka kwenye maeneo ambayo yako *very prime*, hata *National Housing* wanajua wakija kuwekeza biashara italipa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa wananchi wa *Tanganyika Packers*, ile *project* ikikamilika, thamani ya ardhi ya wananchi wa Kawe pale itaongezeka kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, tuuchukulie huo mradi kama sehemu ya kutusaidia sisi. Naamini Shirika la Nyumba kwa sababu pale kuna viwanja vya michezo na tulizungumza nao, tukaafikiana kwamba, hata kama kuna mji unajengwa pale, lazima kuwe kuna utaratibu, yale maeneo ambayo yalikuwa ni ya kiutamaduni ya michezo, yaboreshwe kisasa ili wananchi wa pale wa asili, lakini vilevile wananchi wengine ambao ni wageni watakaokuja waweze kufaidi matunda ya mji huo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kodi ya ardhi; Ni kweli Mheshimiwa Waziri na timu yako mmekubali ama mmefikiria suala la busara ni kupunguza kodi. Kuna kodi nyingi mmezipunguza nakubaliana na ninyi. Hata hivyo, naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize, linapokuja suala la kodi ya ardhi ambayo kwa tafiti tu Tanzania ni kati ya nchi ambazo inatoza kodi ya ardhi kidogo sana, sizungumzii kodi ya kupima ama nini, siyo hizo, hizo kwa kweli ilikuwa ni kero sana. Ekari moja mtu analipa shilingi elfu moja.

Ni kweli kwamba makusanyo yalikuwa hayafanyiki, lakini naamini makusanyo yalikuwa hayafanyiki kwa sababu tulikuwa hatuna takwimu sahihi za wenye mashamba makubwa. Kwa hiyo, ni kweli mnafanya maboresho, lakini lazima kwa hawa wawekezaji wakubwa tuliangalie upya.

Mheshimiwa Spika, ni makosa makubwa sana kama nchi, thamani ya kiwango cha kodi ikalingana maeneo yote. Haiwezekani mtu ambaye yupo karibu na maji thamani yake ikalinganishwa na mtu ambaye yuko katikati huko kukame. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie kama nchi, kwamba kunakuwa na viwango tofauti vya kodi kutokana na thamani ya ardhi. Naomba hilo mlifanyie kazi. Vilevile tukitoza kodi tuta-encourage watu wafanye maendelezo, kodi ikiwa kidogo mtu ana uhakika atalipa mia mbili mia mbili, maeneo yanakuwa mapori.

Mheshimiwa Spika, suala la Msalato, Dodoma, hapa jirani, nimeandika kwenye hotuba yangu. Wananchi tokea mwaka 2003 na mwaka 2011 wamefanyiwa tathmini kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege. Mwaka 2013 Mei, Mheshimiwa Mwakyembe akawaambia kwamba pesa yao ipo kwenye bajeti ya 2014/2015. Bajeti imekwisha bila bila, wananchi hawajalipwa fedha, wameambiwa wasiendeleze maeneo yao huu ni mwaka wa kumi, hii siyo sahihi! Naomba kama Waziri mwenye dhamana atoe majibu.

Mheshimiwa Spika, viwanja 20,000 ulikuwa ni mradi wa Wizara, ule mradi haujakamilika. Juzi mafuriko yalipotokea Dar es Salaam, wananchi walilala nje. Kwa hiyo, natarajia ukija kunipa majibu, kwa kuwa wananchi walinunua viwanja kwa thamani kubwa, mtuambie mnaendaje kuboresha miundombinu kwenye hii miradi ya viwanja 20,000 na Mbweni *specifically* ikiwa mojawapo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile tumesema kulikuwa kuna uchafu na wewe unajua kulikuwa kuna uchafu, ndiyo maana tunakuwa na watu hawalipi kodi, kwa sababu kuna maeneo ni mapori, mwenye kiwanja hajulikani, Serikali inakosa mapato. Tunaomba tufanye *audit* ya ule mradi. Hatuna nongwa na mtu, tunataka uwazi upatikane tuweze kukusanya kodi vizuri, lakini vilevile wananchi waweze kupata ardhi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, CDA; Najua Mheshimiwa Waziri ni mdau mkubwa wa CDA, lakini naomba awe na utu, awe na roho ya huruma. Najua sasa ni nani, huyo huyo, yeye ni wa Ardhi, yupo Mheshimiwa Jenista ni Mwenyekiti kwa sababu yeye ni Waziri anayeshughulika na masuala ya Uratibu ni kweli, lakini wanafanya kazi kama timu, ndiyo maana yeye ni Mwenyekiti, lakini kwenye Bodi kuna Mawaziri kutoka Wizara nyingine ambazo zinahusiana. Naomba hili suala waliangalie. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wananchi wanabomolewa nyumba zao, *notice* ni fupi, wanabomolewa nyumba zao, wanapewa viwanja, wakienda kwenye kiwanja, kiwanja kina mtu ameshajenga nyumba yake. CDA wawe na utu, Kisasa, maeneo ya Njedengwa na maeneo yote ambayo CDA inafanya kazi zake, kuna kazi nzuri inafanya, lakini tunapofanya kazi zinazohusiana na binadamu, wananchi maskini wanaojikongoja kujenga kibanda chao, hata kama kuna makosa yamefanyika, basi tuwe na utu wa kuangalia sheria za nchi, Sheria ya Ardhi Na. 4, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 inazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu migogoro ya ardhi bado ni changamoto. Kamati Teule ya Bunge imetoa mifano mingi, imetoa ushauri wa kutosha, lazima tuanze kuchukua hatua. Kila mwaka kwa makusudi kabisa tunatoa taarifa za viongozi ambao kwa nyadhifa zao wanatumia kunyanyasa wananchi ama kuvunja sheria za nchi. Hatuhitaji majina yao kwa sababu tuna nongwa, tunataja majina yao kwa sababu tunataka tuanze kutengeneza nidhamu ili kila kiongozi ambaye anafanya mambo ya giza giza huku, hatusemi viongozi wasimiliki mali, hatusemi viongozi wasimiliki mashamba, hatusemi tunakataa wawekezaji, tunahitaji wote, lakini, tunahitaji kila tunachokifanya tukifanye kwa uwazi, tufuate sheria, tukifanya vyote hivyo, utakuwa na kumbukumbu, utaweza kudai kodi, nchi itasogea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: *I see!* Leo umeongea kama Mbunge, siyo kama mgomvi. *(Kicheko)*

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami ili nieleze machache niliyonayo katika Wizara hii ya Ardhi na migogoro yake.

Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata uzima na nguvu ya kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu na nikishukuru Chama changu, Chama cha Wananchi kwa kunirejesha tena katika ulingo huu, kunipatia nafasi. Najua tuna safari ndefu, lakini na wenzangu na ninyi mtabarikiwa.

Mheshimiwa Spika, leo Waziri amesifiwa sana na iko haki kidogo ya kusifiwa kwa sababu ukweli ni vizuri kusemwa. Wapinzani siku zote huwa panapo ukweli tunakubali ule ukweli, lakini panapo makosa pia tunajaribu kukosoa Chama Tawala au Serikali iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kupunguzwa tozo kimesaidia wanyonge na wao sasa kuweza kumiliki viwanja. Kwa hiyo, hizo ni pongezi kwa Mheshimiwa Waziri.

Naomba, mbali ya baadhi ya tozo hizo zilizopunguzwa, lakini pia ufikirie vilevile na utizame uwezekano wa VAT katika nyumba za *National Housing* na nyumba zingine za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari na kufikiria eneo hilo, nafikiri unaweza ukawasaidia sana wananchi na hasa wafanyakazi wa Serikali ambao mzigo wa kodi na hizi nyumba ni mkubwa sana kwao na hata pale ambapo wale wanaotamani kununua zile nyumba inakuwa mzigo mkubwa ukiingiza na VAT. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri eneo hilo alitazame kwa umakini ili liongeze sifa ambazo umeshazipata kwa miezi michache. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo linakwenda kwa sifa za Waziri, lakini sifa hizi nitazipa maelezo kidogo, kwamba, mara tu baada ya kukalia kiti, wewe mwenyewe inaonekana uliingia kwenye *database* na ukagundua mambo mengi sana ya watu au miongoni mwao ni viongozi ambao hawajalipa kodi mbalimbali za ardhi. Pia, wewe ni shahidi umeweza kugundua watu ambao wana viwanja kumi kumi, ishirini ishirini na wao ni wakubwa wakati wanyonge wapo wanahitaji hivi viwanja hawavipati.

Mheshimiwa Spika, sasa, haiwezekani mtu mmoja anamiliki viwanja kumi, ishirini, thelathini wakati wapo wengine wanyonge wanahitaji viwanja vile hawavipati. Mheshimiwa Waziri, pamoja na sifa ulizozipata, hili tunaomba ulifanyie masahihisho. Huu ni aina ya mgogoro kwamba, walionacho wanazidi kuwa nacho na wasiokuwa nacho wanazidi kukosa hiyo nafasi. Hii siyo haki na kama yupo katika kiti hicho kutenda haki, wote pamoja na Naibu Waziri wake naomba jambo hili walipatie ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo kitendo cha Mheshimiwa Waziri kuingia kwenye *database* kimesaidia sana kuona au kugundua matapeli. Yeye ni shahidi, kuna Wabunge wengi wamepeva viwanja toka mwaka 2009 nikiwemo mimi, lakini hati yenyewe sijaipata mpaka leo! Baada ya kufuatilia, baada ya kuingia kwenye *database*, akaniletea kodi au akatuletea kodi zinazodaiwa na tukaenda tukalipa hizo kodi, tulipoenda kuangalia hivyo viwanja vyenyewe, tunakuta tayari vina picha za watu na wamepeva hati. Huu ni utapeli mkubwa na unafanywa kwenye ofisi yako, jambo hili linahitaji marekebisho makubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, siyo marekebisho tu, wale wote waliopewa viwanja kwa kutumia majina ya viongozi na hati *fake fake*, wachukuliwe hatua zinazofaa *immediately*. Wizara yako inahusika na wapo watu ndani ya Wizara wanahusika na utapeli wa aina hii na kuwapa watu viwanja ambao hawahusiki kwa kutumia majina ya viongozi.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kuliongeza ni kwamba, tuna Watanzania wenzetu ambao wapo nje ya nchi ambao wameleta maombi kwamba kule wapo kwa muda wanafanya kazi nchi za nje, ndiyo hao tunawaita *diaspora*, lakini wangetamani na wao wapate ardhi wajenge, nyumba za maana na hawa wana uwezo.

Mheshimiwa Spika, baadhi yao kwa kutumia jamaa zao wametapeliwa, wametuma pesa mara chungu nzima, wamekuja, hakuna kitu! Wanaomba Wizara, nina ushahidi wa baadhi ya wenzetu ambao wameandika barua miaka mitano iliyopita kuiomba Wizara ya Ardhi, wapo wanaishi nchi za nje. Kwa mfano, yupo Dkt. Ruta na Dkt. Zamu wanatamani na wao waweze kuwa na nyumba, tumewasilisha na tumeleta barua zinazohusika, mpaka leo Wizara haijafanya chochote. Kwa hiyo, wenzetu ambao wanaishi nchi za nje kwa shughuli maalum kwa muda huu, wanatamani wakirudi nyumbani na wao wawe na ardhi waweze kujenga nyumba za maana, ambapo mpaka sasa hivi Wizara haijawafikiria.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia hotuba yangu hii ya leo au kupitia mchango wangu huu wa leo, Mheshimiwa Waziri alichukue hili kwa umuhimu mkubwa ili na hawa wenzetu na wao wafarijike na nchi yao, ambapo huko wapo kwa muda tu, makazi yao ya kudumu yapo hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru pia migogoro mingi ya ardhi imetatuliwa, lakini bado kuna migogoro sugu ambayo mingine toka enzi ya Waziri Mkuu Malecela ipo. Imewahi kuundiwa Kamati ya Bunge, migogoro hiyo ipo hadi hivi leo. Mgogoro wa Pori la Akiba la Swaga Swaga mpaka Hanang, huu mgogoro ni wa zamani mno! Toka enzi ya Waziri Mkuu Malecela na wakati huo iliamuliwa mipaka isibadilishwe, lakini mpaka leo bado.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kusogeza mipaka kwa kuwasogeza wananchi, hamuwatendei haki, hii siyo sahihi. Kwa hiyo, ifike muda basi kwamba miaka yote hiyo hadi leo mgogoro huo wa Pori la Akiba la Swaga Swaga haujapatiwa ufumbuzi, nafikiri Mheshimiwa Waziri pamoja na sifa alizosifiwa, sasa nataka aelekeze nguvu zake huko ili tuone hawa wananchi na wao wanapata faraja.

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro wa Mkungunero, vijiji kama 11 ardhi imeporwa na haujatatuliwa mpaka leo, hapa wahusika wa Wilaya wanahusika. kwa hivyo hili ni jambo ambalo Mheshimiwa Waziri tunaomba alipatie ufumbuzi, uelekeze nguvu zake huko.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa ardhi wa Pori la Malisho ya Ata, nalo ni eneo lingine kubwa ambalo mpaka leo linaleta matatizo.

Kwa hiyo, pamoja na juhudi alizozifanya Mheshimiwa Waziri ambazo kwa uhakika tunazithamini na tumezipongeza, lakini bado kuna maeneo ndani ya Wizara, kuna matapeli ambao wanatumwa na viongozi wa Wizara yake! Mambo hayo Mheshimiwa Waziri tunaomba ayapatie ufumbuzi wa haraka, vinginevyo sifa nzuri yote anayosifiwa itaharibiwa na matapeli hawa. Naomba asiwavumilie watu walioko Wizarani ambao wanaharibu taswira nzima ya Wizara hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nashukuru sana. (Makofi)

SPIKA: Ndiyo uzuri wa kuwa na Muungano, watu wanazungumza wote tu kila mahali, makini kweli kweli. Faida ya Muungano hiyo! (Kicheko/Makofi)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI: Mheshimiwa Spika, napenda niungane na wenzangu kuipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, nikianza na Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wao kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini pia, kwa ushirikiano wanaotoa katika Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, nimesimama ili nichangie katika moja ya hoja ambayo imezungumzwa hapa inayohusu Kata yangu ya Naumbu katika Kijiji changu cha Mgau. Naomba ku-*declare interest* kwamba, hiyo ni kata ambayo nilizaliwa, ambapo anatuhumiwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mgau kutoa ardhi hekta 2,500 kwa Alhaji Aliko Dangote.

Mheshimiwa Spika, nadhani ni vizuri mtu unavyotaka kuandika hotuba ambayo inasikika Kimataifa kuwa na uhakika wa yale unayoyasema ikiwa ni pamoja na takwimu na majina ya watu na majina ya miji. Katika hii Taarifa Naumbu imeandikwa Maumba, hiyo ni kuonyesha kwamba, hiyo hoja ni ya kuifikia tu njiani.

Mheshimiwa Spika, eneo lote ambalo lipo katika ghuba hiyo ya Sudi ni hekta 867 na eneo ambalo Alhaji Aliko Dangote ameomba ni hekta 25 tu kwa sababu, anachotaka kukijenga pale katika maneno halisi sio bandari ni *berth*, ni bandari ndogo, ambapo atakuwa anapakia hiyo saruji kwa kutumia *conveyor belt*, kwa hiyo, siyo eneo kubwa kama ambavyo tunataka kuaminishwa. Siyo hivyo tu, Alhaji Aliko Dangote ni mwelewa, ni mtu makini na anayefuata sheria za nchi; maombi yake yote kuanzia kule alikojenga kiwanda cha saruji ameyapitishia katika taasisi husika, ikiwemo pamoja na TIC.

Mheshimiwa Spika, alienda kutembelea Kijiji cha Mgau kutaka kujiridhisha na kupata uhakika kama kweli wananchi wa eneo husika wamehusishwa na wameridhia katika eneo lao kutwaliwa na Serikali, kwa sababu, ardhi yote kama tunavyofahamu ni mali ya Serikali, kwa hiyo, yeye alienda kuwasikia

wenyewe, je, hilo suala ambalo anaambiwa na Serikali wananchi wanalifahamu? Kwa hiyo, wananchi na wenyewe waliridhia kwamba, wako tayari aende akajenge hiyo *berth* katika kijiji chao na ardhi ambayo yeye ameomba ni hekta 25.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunavyozungumza, Serikali inafanya uthamini wa mali na ardhi ya wanavijiji iliyopo, ili wananchi wenyewe waweze kulipwa na Alhaji Dangote amilikishwe kwa utaratibu wa Serikali zilizopo. Mpaka sasa hivi alichoridhiwa yeye ni kufanya tu utafiti kule ndani ya bahari kujua suala la kina, upepo ukoje, hiyo *berth* itajengwa kwa kiasi gani, kuangalia mlango wa hiyo ghuba yenyewe inayozungumzwa kama kweli inaweza ikamudu kujenga hicho kitu, lakini, kwamba wanakijiji wa Mgau wanafikiriwa kwamba hawana uwezo wa kujua thamani ya ardhi, eti wabadilishe ardhi na kipande cha kanga na kuwakejeli kiasi hicho, kwa kweli nimesikitika, lakini nina imani kabisa wananchi wa Jimbo langu wamesikia kashfa walizopewa na wananchi wa Mgau wamesikia.

Mheshimiwa Spika, napenda niwahakikishie kwamba wananchi wa Mgau ni wananchi makini, wanajua taratibu zote za ardhi na wanajua thamani ya ardhi kwa sababu naweza nikasema katika Tanzania hii miongoni mwa Mikoa ambayo ardhi ina thamani ni pamoja na Mkoa wa Mtwara, hawawezi wakafanya hayo mnayowafikiria hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Alhaji Aliko Dangote aliahidi kuchangia maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, haswa kwa wananchi wanaozunguka katika eneo lile kama ambavyo wawekezaji wengine wanavyofanya. Kwa hiyo, aliahidi kuwajengea shule mbili za kisasa na kujenga kituo cha afya cha kisasa. Pia, ameahidi kuchangia milioni 450 na tayari anapitishia pesa kupitia CRDB ambazo zitawasaidia wananchi wanaozunguka katika maeneo yale na vijana katika kujianzishia miradi yao. Hizi shule na zahanati ameahidi mara tu ardhi itakapopatikana, ataanza kujenga kabla kiwanda hakijaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, makubaliano hayo hayana uhusiano wowote na ardhi ile ya kujenga *berth*, ahadi hiyo aliitoa kama sehemu ya kuchangia huduma kutokana na kiwanda ambacho anakijenga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina imani kabisa wapiga kura wangu wamesikia na wamesikia UKAWA ilivyowakashifu na mwezi wa Oktoba nadhani wanajua cha kufanya. Mchawi wa maendeleo yao wananchi wa Mtwara ambao hawataki wawekezaji nadhani wamemwona!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe wananchi wa Mtwara habari ya mtu kutoka huku akaja kuwaambia muandamane kwa sababu viwanda vinaenda Dar es Salaam, mkaandamana, mkachoma mali za watu, leo watu wanakuja kuwekeza, hao hao wanaanza kuwapiga vita wawekezaji ambao wamejitokeza! Nadhani wananchi wangu, Waswahili wanasema akili za kuambiwa mchanganye na za kwenu. Nadhani hii ni fursa nzuri sana ya wananchi wa Mtwara kuchanganya na akili zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnaona jinsi mwekezaji mkubwa, mahiri, ambaye anapiganwa na nchi nyingi, lakini sisi Tanzania, UKAWAwanamponda na kumfananisha na wakoloni ambao walibadilishana mali na kipande cha kaniki na kwamba, wanatufanya sisi wananchi wa Mtwara hatujui thamani ya ardhi ndiyo maana tunakubali kumpa Alhaji Aliko Dangote ardhi na kipande cha kanga! Nina imani kabisa mmesikia na mimi mmenisikia na mmenielewa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Naomba nitambue baadhi ya wageni!

Mmemsifia bibie mpendwa kabisa wa Mheshimiwa Lukuvi ambaye alikuwa hapa. Sasa yupo Mheshimiwa Balozi Mbelwa Kairuki, mume wa Naibu Waziri! Ahsante sana. Wabunge wanasema ahsante kwa kumtunza na kumruhusu afanye kazi. Maana ungeweza kumrudisha nyuma kama kawaida ya akinababa kuwarudisha akinamama nyuma, lakini wewe umefanya kazi kubwa sana ya kumpa nafasi ya kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Halafu, nina wageni wa Mheshimiwa Godbless Lema, ambao ni wanafunzi 56 na Walimu sita kutoka Shule ya Msingi ya *Saint Thomas* Arusha, wakiongozwa na Mwalimu Samson Mbwambo! Naomba wanafunzi hawa wasimame kama wapo humu ndani! Ahaa, ahsante sana! Karibuni sana! Tunawashukuru Walimu na tunawatakia heri watoto. *(Makofi)*

Pia, tuna wanafunzi 20 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Dodoma na hawa pia wasimame kama wapo ndani! Ahaa, ahsanteni sana! Karibuni sana na msome kwa bidii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, namwita Naibu Waziri, nampa dakika 50. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyeniwezesha kusimama hapa mbele ili niweze kuchangia hoja hii iliyowasilishwa na Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa napenda kuanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani yake kubwa aliyoonyesha kwangu na kupendezwa kwake kunitiua kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria na sasa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Napenda kumshukuru sana na tumekuwa kwa kweli tukiitendea haki nafasi hii na tunaamini hatujamwangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kipekee pia Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na viongozi wote, Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Makamu wote wa Rais wa SMZ kwa namna ambavyo wamekuwa wakitekeleza majukumu yao vizuri, lakini vilevile kwa namna ambavyo tumekuwa tukishirikiana na wakitupa miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda pia, kutoa shukrani za pekee kabisa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, Mbunge wa Jimbo la Isimani, kwa ushirikiano mkubwa ambao amenipatia katika kutekeleza majukumu yangu, hususan katika kumsaidia ndani ya muda mfupi ambao tumekuwepo katika Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Tumekuwepo kwa miezi minne tu, kwa kweli miezi minne ni muda mfupi mno kuweza kutatua changamoto zote katika Wizara yetu. Muda huu umetutosha kuweka misingi ya kutatua changamoto nyingi za Wizara za muda wa kati na muda mrefu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wakati akiwasilisha hotuba yake yameeleza kwa kina mafanikio ambayo tumeyapata kwa muda huo wa miezi minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kipekee kumshukuru Katibu Mkuu, Bwana Kidata pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Mayunga, watendaji wote wa idara mbalimbali, vitengo, mashirika yaliyoko chini ya Wizara kwa mshikamano na ushirikiano mkubwa mliotupatia. Kwa kweli, kazi yetu isingekuwa rahisi bila ushirikiano wenu na mafanikio ya Wizara yetu yanatokana kabisa na juhudi zenu ninyi wote. Tunawatambua na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa shukrani endapo sitachukua fursa hii kumshukuru sana mume wangu mpenzi, Balozi Mbelwa Kairuki. Kwa kweli, nakushukuru, umekuwa ni chachu kubwa ya maendeleo na uongozi wangu na naamini utaendelea kuniunga mkono, hususan mwaka huu katika harakati za uchaguzi mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda sana sana kuwashukuru wanangu wapenzi, Precious Kemilembe pamoja na Esther Kokubelwa kwa upendo wao, lakini pia kwa kunivumilia nyakati zote ambazo nimekuwa sipo nyumbani kutekeleza majukumu yangu kama mama.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda sana kumshukuru mama yangu mzazi na baba yangu, lakini vilevile mama mkwe wangu pamoja na wakwe zangu wote na ndugu zangu wote ambao wamekuwa wakinitia nguvu na kunitia moyo wakati wote. Upendo wao daima umenipa utulivu wa moyo wa kuwatumikia Watanzania bila kuchoka wala kukata tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki endapo sitaishukuru UWT – Dar es Salaam pamoja na UWT – Taifa na kuwashukuru sana kwa namna ambavyo tumekuwa tukishirikiana. Wamenichagua kuwa Mbunge wao na naamini nimetenda haki katika kutetea nafasi hii ya Ubunge wa Viti Maalum kuwakilisha kundi la Vyama vya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, lakini, napenda pia kutumia fursa hii kuwashukuru sana Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (*TUCTA*) na kupitia kwa *TUCTA* kwa wafanyakazi wote kwa mshikamano tuliouonyesha na mafanikio tuliyoapata. Tunapomaliza Awamu hii ya Nne tumepiga hatua kubwa kwa pamoja katika kuweka mazingira mazuri ya kisheria na kimfumo yaliyoboresha maslahi ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho na siyo mwisho kwa umuhimu, naomba nitangulize dua zangu kwa Mwenyezi Mungu na kumuomba azipokee na kuzilaza mahali pema roho za Marehemu Mheshimiwa Kapteni John Komba aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi na Mheshimiwa Eugen Mwaiposa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ukonga. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue fursa hii ili niweze kuchangia na kujibu hoja mbalimbali zilizochangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Pia, naomba nichukue fursa hii kuanza kujibu Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza iliyowasilishwa ilikuwa ni kuhusiana na ongezeko la gharama ya kuandaa Mpango Kabambe kwa Majiji ya Arusha na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, kabla ya kufikia makubaliano na hatimaye kuingia mkataba katika maandalizi ya mpango huu kabambe wa Arusha na Mwanza kulikuwa na majadiliano na katika majadiliano haya yalijumuisha tathmini, yalitathmini gharama katika kila kipengele ambacho kilikuwa kinajadiliwa.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za mwisho za majadiliano Serikali iliamua kuwa na mkutano muhimu wa wadau (*stake holders consultation meetings*) ili kujadiliana kuhusu uandaaji wa mpango kabambe kama sheria inavyohitaji. Vilevile, Serikali iliongeza mahitaji ya kutengeneza taswira za majiji (*models*) ya mpango kabambe kwa majiji hayo na pia iliweka kipengele cha kuwajengea uwezo wataalamu wa hapa nchini na kuandaa mpango kabambe kwa miji mingine huko mbeleni.

Mheshimiwa Spika, gharama zote hizo zimejumuishwa kwenye *reimbursable expenses* ambazo zitalipwa kulingana na matumizi halisi na siyo kwenye ada ya ushauri (*consultancy fee*). Mabadiliko haya yalipunguza gharama ya ada ya ushauri ambayo mwanzoni ilikuwa ni kubwa, maafikiano yakafanyika na kuingia mkataba na gharama zake kuwa Dola 4,483,000.95 kwa Jiji la Mwanza na Dola milioni 4.9 kwa Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Spika, baada ya mabadiliko haya gharama za ada ya ushauri kwa ajili ya kumlipa mtaalamu mshauri zilipungua, ambapo kwa upande wa Mwanza zilishuka kutoka Dola 3,179,560 hadi Dola 2,818,525, wakati kwa upande wa Arusha zilishuka kutoa Dola 3,549,760 hadi Dola 3,212,845.

Mheshimiwa Spika, ningedhani Kambi ya Upinzani ingetakiwa iipongeze Serikali kwa jitihada ilizozichukua katika kuhakikisha kwamba gharama hizi zinapungua, lakini badala yake imekuwa ni tofauti. Kwa hiyo, tuombe sana wananchi wanaotusikiliza, msikilize maneno haya ya upotoshaji, gharama zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge, Msemaji wa Kambi Rasmi Bungeni anajua hili na ndiyo maana hata pale kidogo anatabasamu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya pili kuhusiana na Serikali kupewa jukumu la kulipa kodi hizi za Mtaalamu Mshauri katika kuandaa mpango kabambe kwamba, Serikali sasa badala ya mtaalamu mashauri kulipia kodi, Serikali inalipa kwa niaba yake na kwamba haijamkata kodi hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kutoa taarifa kwamba, malipo yaliyofanywa kwa hati za madai zilizowasilishwa na mtaalamu mshauri yalikatwa kodi kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004 na jumla ya shilingi 192,219,274.62 zilikatwa Kodi ya Zuo (*Withholding Tax*) kwa malipo yaliyotokana na ada ya ushauri (*consultancy fee*) kupitia Hati za Malipo Namba 048VC14003642, lakini vilevile kupitia Hati ya Malipo Namba 048VC14003641 za tarehe 27 Machi, 2015.

Mheshimiwa Spika, hivyo siyo kweli na wala siyo sahihi kusema kwamba, jukumu la kulipa kodi limehamia kwa Serikali ya Tanzania, mtaalamu mshauri ataendelea kulipa kodi kama ambavyo anahitajika katika mkataba, kulipa kodi, kulipa ada na tozo nyingine zote ambazo zimeelekezwa katika mkataba huo. Kwa hiyo, niombe sana wananchi waweze kusikiliza hiki tunachokieleza na siyo kile ambacho kilikuwa kimeelezwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, pia, kulikuwa kuna hoja kwamba, mtaalamu mshauri alilipwa malipo ya 15% kabla ya kufanya kazi na kwamba mkataba ulieleza alipwe baada ya hatua ya kwanza kukamilika katika maandalizi ya mpango kabambe.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kutoa taarifa kwamba, hatua za uanzishwaji na uandaaji wa ramani za msingi (*inception and base mapping*) ilikamilika na taarifa yake iliwasilishwa Wizarani tarehe 3 Februari, 2015. Kamati ya Wataalamu (*Technical Review Cimmittee*) ilikamilisha kazi ya kuchambua na kutoa mapendekezo yao tarehe 8 Februari, 2015.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo yalipelekwa kwa mtaalam mshauri ambaye naye aliwasilisha *inception* ripoti hiyo na *BaseMapping* tarehe 16 Februari, 2015. Kamati ya wataalam ilikamilisha kazi ya kupitia taarifa ya mwisho tarehe 25 Februari, 2015 na baada ya hapo taarifa iliridhiwa na ndipo malipo yakafanyika tarehe 27 Machi, 2015.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine ya Kambi ya Upinzani kwamba mradi wa upimaji wa viwanja 20,000 ulitawaliwa na wizi, rushwa na ufisadi na kambi hii ilitaka ukaguzi maalum ufanyike ili kuweza kufahamu dosari zinazojitokeza katika utekeleza wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa upimaji wa viwanja 20,000 ni mradi uliotekelwa mwaka 2001/2002 na ni mradi mkubwa kwa kweli ambao umewahi kutekelezwa na Serikali yetu. Serikali kupitia Wizaru ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilifanya tathmini na kubaini dosari za kiutendaji na hatua stahiki zilichukuliwa kwa kuondoa watumishi nane waliohusika na dosari hizo. Mfano, wamiliki wa asili waliokutwa hawakumilikishwa viwanja kinyume na lengo la mradi.

Pamoja na dosari hizo, lengo la kupima viwanja lilifikiwa kwani lengo lilikuwa ni kupima viwanja 20,000 lakini mwisho wa mradi viwanja 53,000 vilipimwa. Hivyo malengo makubwa ya mradi yalitimizwa na manufaa kwa makundi yote ya jamii yalifikiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia kwamba taarifa ya Kamati ya Lukuvi alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambayo iliundwa mwezi Juni, 2010 kwa ajili ya kuchunguza maeneo ya wazi yaliyomo katika Jiji ambayo yalivamiwa na kuendelezwa, ilitaka kujua ni kwa namna gani taarifa hii ya Mheshimiwa Lukuvi imetokeleza.

Napenda tu kumwarifu Mheshimiwa Mbunge na Kambi nzima ya Upinzani kwamba hatua mbalimbali zimechukuliwa katika kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya Lukuvi alipokuwa Mkuu wa Mkoa ikiwa moja ni kuvunja nyumba Sinza, Masaki, Samora, Mbezi na maeneo mengine. Napenda tu kuliarifu Bunge lako kwamba hatua zinaendelea kuchukuliwa katika baadhi ya maeneo ya wazi yaliyovamiwa na kuna baadhi ya maeneo ambayo hayajavunjwa kutokana na wahusika kupeleka zuio Mahakamani na zoezi la uvunjaji litaendelea mara moja baada ya Mahakama kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile watumishi waliobainika kuhusika na uuzaji wa maeneo ya wazi walichukuliwa hatua za kinidhamu na za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa Mahakamani. Mfano, mtumishi mmoja wa Manispaa ya Kinondoni alifikishwa Mahakamani kwa upande wa Manispaa ya Ilala, amesimamishwa kazi na wengineo wamehamishwa kwenda kwenye vituo vingine.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imekuwa ikifanya ukaguzi ili kubaini ujenzi unaofanyika bila vibali kwa kutumia Wakaguzi wa majengo, pamoja na Askari Ardhi (*LandRangers*) ili kuhakikisha kwamba maeneo ya wazi hayavamiwi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilijitokeza ni kwamba mashamba yaliyotwaliwa yagawiwe kwa usimamizi wa Wizara ili wananchi waweze kupata ardhi badala ya viongozi wachache tu. Wizara inapokea ushauri huu, lakini napenda tu kuarifu Kambi ya Upinzani kwamba, tumeshaanza kuitekeleza katika kushughulikia ugawaji wa mashamba yanayokusudiwa kubatilishwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

Hivi sasa timu ya wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, wameshirikiana katika kufanya tathmini ya mahitaji ya ardhi kwa wanavijiji wanaoishi jirani na mashamba hayo baada ya umiliki wa mashamba kubatilishwa.

Wizara itakamilisha zoezi hili kabla ya tarehe 30 Juni ili wananchi wenye mahitaji wagawiwe.

Kwa kweli kipekee tumshukuru sana Mheshimiwa Herbert Mntangi, kwa kweli toka miaka hii mitano tumeanza Bunge hili amekuwa akifuatilia sana suala zima la umiliki wa mashamba haya, suala zima la ufutaji wa miliki lakini kikubwa ni kwa namna gani sasa wananchi wenyewe wazawa wa Muheza waweze kunufaika pindi mashamba haya yatakapogawiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine kwamba Serikali haijachukua hatua dhidi ya wananchi wachache kumiliki ardhi kubwa huku wananchi wengi wakiwa na mahitaji ya ardhi. Serikali inaendelea kuchukua hatua dhidi ya wananchi wanaohodhi ardhi bila kuiendeleza kwa kubatilisha miliki ya mashamba haya.

Hivi karibuni Serikali imebatilisha miliki za mashamba 18 yaliyopo katika Halmashauri za Wilaya za Kibaha na Mafia, vilevile tunaendelea kukamilisha taratibu nyingine ili mashamba mengine sita ambayo hayatumiwi katika Halmashauri ya Wilaya Mvomero na Halmashauri nyingine nchini yaweze kubatilishwa na kugawiwa kwa wananchi wenye mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hatutakuwa na haya na siyo kwa viongozi tu, tutoe pia rai kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wanamiliki pia ardhi kubwa ambazo hawajaziendeleza na viongozi wengine wote; mjitahidi mwendeele kama sheria inavyotaka. Hatutakuwa na husuda, mtu yeyote atakayekiuka, panga letu litakata kote kote.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja pia kwamba Serikali iweke ukomo wa kumiliki ardhi kwa ajili ya kilimo. Napenda tu kuliarifu Bunge lako kwamba, Serikali inakamilisha utafiti wa kubaini mahitaji ya ardhi katika Halmashauri mbalimbali nchini ili matokeo ya utafiti huo yaweze kutumika kama msingi wa kuweka ukomo wa kiasi cha mtu mmoja kumiliki ardhi. Zoezi hili tayari Wizara imeshaanza tangu Mei mwaka huu na tunatarajia kwamba itakamilika katika robo hii ya kwanza ya mwaka huu wa fedha yaani ifikapo Septemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hoja kuhusiana na mradi unaotekelezwa na Alhaj Dangote; na napenda kumshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia ambaye ni Mbunge wa Jimbo hilo ambapo mradi huu unatekelezwa na kwa kweli ameeleza kwa kina, lakini nitaomba pia kwa upande wa Wizara niweze kuongezea mengine machache.

Mheshimiwa Spika, Alhaj Dangote ni *strategic investor*. Tunapokuwa humu ndani tunaanza kubeza wawekezaji ambao kwa kweli wako kimkakati na wawekezaji mahiri, kwa kweli tutafanya hata wawekezaji wengine wanaotaka kuja kuwekeza katika nchi yetu wasite na kuona kwamba siasa zinatamalaki kuliko hati zao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika mradi huu wa Dangote, unatarajiwa utazalisha ajira mpya takribani 7,000 na mradi huu utakapokamilika mwaka huu 2015 takribani tani milioni tatu za *cement* zitaweza kuzalishwa. Vile vile kwa mwaka 2019 takribani tani milioni tano zitaweza kuzalishwa.

Mheshimiwa Spika, tunaamini uzalishaji huu utakapoanza kutekelezwa, italeta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Ujenzi, italeta mapinduzi makubwa na kichocheo katika ajira lakini vilevile katika mapato kwa Serikali na itawezesha huduma mbalimbali za kijamii kutekelezwa kuhusiana na kodi hizi tunazozipata.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa ujenzi wa kiwanda hiki cha Dangote ulipata hadhi ya uwekezaji mahiri na Wajumbe wa Kamati ya NISC waliridhia mwekezaji huyu kuweza kupewa vivutio mbalimbali ili aweze kutekeleza mradi wake kwa ufanisi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, taarifa! Mheshimiwa Spika, taarifa!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika eneo ambalo Dangote ameliomba kwa ajili ya ujenzi...

SPIKA: Mheshimiwa Halima, mlisema; naye mwache aseme na sisi tuendeleo.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Wewe, tulia dozi inaingia, tulia!

SPIKA: Mheshimiwa Waziri na wewe tulia!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika ujenzi wa Bandari ndogo, hivi sasa kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza bado hajamilikishwa, Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji ndiyo tuko katika mchakato wa kuhakikisha ni kwa namna gani sasa Dangote anaweza kupata eneo hili kwa ajili ya kujenga bandari hii ndogo katika Kijiji cha Mgao ambacho kwa kweli ni eneo muhimu sana katika kufanikisha mradi wake.

Kwa hiyo, napenda tu kusema kwamba maelezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba tayari ameshapewa, siyo kweli; na kwamba Serikali ya Kijiji ilikiuka sheria, siyo kweli, bado hajakabidhiwa. Viwanja vyote ambavyo anamiliki hivi sasa, anavimiliki kwa mujibu wa Kifungu cha 20 cha Sheria ya Ardhi ambayo inaelekeza kabisa mwekezaji ambaye ni raia wa kigeni atapata ardhi kwa ajili ya uwekezaji na ndivyo kinachofanyika hivi sasa. Dangote hana ardhi anayoimiliki yeye binafsi, ardhi yote inamilikiwa kupitia *derivative right* iliyotolewa na TIC. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusiana na uanzishwaji wa *Real Estate Regulatory Authority*. Napenda tu kuliarifu Bunge lako kwamba, tayari Serikali imeshampata Mshauri Mwelekezi, atakayeandaa utaratibu wa kuanzisha *Regulatory Authority* pamoja na masuala mengine inayohusiana na uendelezaji na udhibiti wa miliki nchini. Tunatarajia kwamba mamlaka hii itanzishwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 na ni imani yetu kwamba chombo hiki kitakuwa ni mkombozi wa kulinda maslahi ya watumiaji wa miliki.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine kuhusiana na mgogoro wa ardhi ulioko katika Kijiji cha Kifanya katika Mji wa Njombe na Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani alitaka Serikali itoe majibu kuhusu hatima ya ardhi iliyogawiwa kwa wakulima wa chai.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna mgogoro wa mashamba ya chai katika Kijiji cha Kifanya. Eneo la mashamba hayo awali lilitengwa kwa ajili ya kijiji kwa ajili ya malisho ya mifugo. Hamasa ya kilimo cha chai iliwafanya wananchi wenyewe kupitia Serikali yao ya Kijiji kubadilisha matumizi kutoka malisho na kuwa kilimo.

Katika ugawaji wa mashamba baadhi ya wanakijiji walikosa na baadhi ya mashamba yaligawiwa kwa watu ambao sio wanakijiji. Mgogoro huu hivi sasa umeshaanza kufanyiwa kazi kupitia Uongozi wa Wilaya na tayari wataalam wetu wa ardhi wameshajipanga na tarehe 11 Juni, watakuwa na kikao na Kamati iliyoundwa na kijiji ili kushughulikia suala hili kwa ajili ya kupata suluhu ya kudumu katika mgogoro huu ikiwemo kutenga eneo la malisho ya mifugo. Aidha, Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa Kanda husika anafuatilia utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine kuitaka Serikali kuanzisha Kitengo cha Kuratibu Uwekezaji katika Ardhi na Miliki. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, ili kukabiliana na watu wanaohodhi ardhi kubwa na kuhakikisha kwamba ardhi inatumika kwa matumizi yenye faida, katika mwaka huu wa fedha tunatarajia kuanzisha Kitengo cha Kuratibu Uwekezaji katika Ardhi, Mashamba na Majengo na ni imani yetu kwamba hatua hii italenga kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu kuhusu uwekezaji katika ardhi nchini kote.

Vilevile uanzishwaji wa kitengo hiki unaendana na utekelezaji wa mpango wa Matokeo Makubwa Sasa katika kipengele ambacho Wizara ya Ardhi inatekeleza katika kuboresha mazingira ya biashara.

Pia inaendana na muundo mpya wa Wizara ambao umeshapitishwa na Menejimenti na tunaamini utakapokuwa tayari, basi Kitengo hiki cha Kuratibu Uwekezaji kitaweza kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine ya kuanzisha *Land Bank* na hoja ni kwamba *Land Bank* hii iharakishwe. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, katika mwaka huu wa fedha 2015/2016, tumetenga jumla ya Shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuanzisha Mfuko wa Fidia (*Land Compensation Fund*) na tunatarajia kutumia fedha hizo kulipa fidia ya ardhi itakayotwaliwa kwa ajili ya kuanzisha hazina ya ardhi na mpaka hivi sasa tumejiwekea lengo kama Wizara kutambua eneo lenye ekari 200,000 ambazo zitakuwa hazijaendelezwa kwa ajili ya kuingizwa katika hazina ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia pia fedha za malipo ya *premium* ambazo sasa wamiliki wa viwanja watatozwa kuanzia tarehe 1 Julai, zitasaidia pia katika kutunisha Mfuko wa Fidia ya Ardhi. Wizara pia inaendelea na hatua za kufuta mashamba pori yaliyotekelezwa ili ardhi hiyo tuweze kuitumia kama hazina ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusiana na migogoro isiyoisha ya wakulima na wafugaji. Napenda tu kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, tatizo kubwa linalosababisha migogoro ni uwiano usio sahihi wa idadi ya mifugo na kiasi cha ardhi ya malisho iliyopo. *Livestock Unit* moja inahitaji hekta mbili za malisho kwa mwaka. Tanzania inazo *Livestock Unit* milioni 58 na kufanya eneo la ufugaji la kutosha linalotakiwa kuwa hekta milioni 56 kwa ufugaji pekee. Eneo la ardhi yote nchini tuliyonayo ni hekta milioni 96 huku asilimia hiyo 28 ya ardhi sawa na hekta milioni 27 ni ardhi ya hifadhi. Hii ina maana kwamba ardhi inayobakia kwa kilimo na makazi mijini na vijijini ni hekta milioni 12 pekee.

Kwa hiyo, mtaweza kuona kabisa ni dhahiri kwamba migogoro haiwezi kwisha na ardhi haiongezeki. Sisi kama Serikali tumekuwa tukichukua hatua kuhakikisha kwamba tunatayarisha mipango ili kuweza kutenga maeneo ya kilimo na ufugaji, vilevile kuhakikisha kwamba tunaendelea kutayarisha mipango ya matumizi ya ardhi. Niseme tu kwamba wakati umefika sasa Serikali za vijiji pamoja na Halmashauri zote ziandae sheria ndogo ndogo za kudhibiti migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, naziagiza Halmashauri zote nchini kutenga fedha za kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Kwa zile fedha za makusanyo ambazo Wizara inazirudishia Halmashauri takriban asilimia 30, basi zitumike kwa ajili ya mipango ya matumizi ya ardhi pamoja usimamizi wa Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja kuhusiana na Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi kushindwa kuleta mabadiliko kutokana na kuongezeka kwa nyumba zisizo bora. Wakala wa NHBRA umeendelea kufanya utafiti pamoja na kusambaza matokeo ya utafiti huo ili kuleta mabadiliko katika ujenzi wa nyumba bora.

Mheshimiwa Spika, ili kusambaza matokeo ya utafiti na kuhamasisha wananchi kutumia tafiti hizo, Wakala huu umeendesha semina mbalimbali kuhusu ujenzi wa nyumba bora ambazo zimefanyika katika Mkoa wa Mtwara, katika Wilaya ya Tandahimba katika Kata za Chaume, Lukokoda na Lihenje pamoja na Wilaya ya Mtwara Mjini. Pia imeendesha Semina ya Uhamishaji wa Ujenzi wa Nyumba Bora katika vikundi mbalimbali, imetoa mafunzo katika maeneo mbalimbali na imeweza kusaidia kutoa mafunzo ya vitendo kuhusiana na teknolojia rahisi ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa wateja takriban 67 walionunua mashine katika karakana ya Wakala.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia kuhusiana na CDA kwamba hawajalipa fidia ya takriban Shilingi bilioni tatu. Napenda tu kueleza kwamba kama ambavyo tumeeleza kupitia Waraka wetu Na. 1 wa mwaka huu tarehe 21 Mei, pale ardhi inapotwaliwa, mnufaika wa utwaaji wa ardhi hiyo atapaswa kuwasilisha uthibitisho wa uwepo wa fedha za kulipa fidia kwa mamlaka ya Halmashauri ambapo ardhi inatwaliwa na pia uthibitisho utawasilishwa kwa Mthamini Mkuu.

Napenda tu kueleza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba tutalifuatilia suala hili na kuona tatizo ni nini ili liweze kufanyiwa kazi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine zilizotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na kueleza kwamba Chama cha Mapinduzi tunamaliza mwaka huu tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu, tuliahidi Ilani ya Uchaguzi ya miaka mitano na kwamba tumekuwa matapeli na kwamba hatujatekeleza chochote.

Mheshimiwa Spika, yametekelezwa mengi. Nikiamua kuanza kusoma nyaraka nzima hii kwa ufupi sana ya page zaidi ya 35 muda hautakuwa rafiki kwangu, naomba tu nijaribu kugusia maeneo machache kwa faida ya wananchi wa Tanzania wenye kukitakia mema Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi, Chama kikubwa, Chama ambacho kimefanya mengi na yeye mwenyewe anatambua hata huo mgogoro wa Chasimba na Makongo

isingelikuwa yamewekwa katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, basi huenda na yenyewe yasingetekelezwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tulitoa ahadi kuhusiana na suala la utawala wa ardhi, tuliahidi kwamba Halmashauri za Miji na Vijiji zitakamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji vipya na kupanga mipango bora ya matumizi ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijiji zaidi 5,558 vilipatiwa Vyeti vya Vijiji. Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya, ilipima zaidi ya vijiji 1,619 katika Wilaya 37, lakini vilevile vijiji 499 viliandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika Wilaya 69. Kwa kweli haya ni mafanikio makubwa japo changamoto hazikosekani na ndiyo maana tunazitaka sasa Halmashauri mbalimbali ziweze kuweka vipaumbele kutenga bajeti ili kuharakisha shughuli za upimaji na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la upimaji wa mashamba na kuwapatia wananchi hati za kimila pamoja na kujenga Masjala za Ardhi, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imetekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kutoa hati za hati miliki ya kimila takribani 348,000. Serikali pia imejenga takriban Masjala za Ardhi za Vijiji 385 ambazo hivi sasa zinawahudumia wananchi ambako huko nyuma kabla ya utekelezaji wa ilani hii Masjala hizo hazikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani pia ilielezea programu 12 za utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tumeshaandaa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi wa miaka 20 (mwaka 2013 – 2033) na vijiji 499 vimeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine katika ilani kuhusiana na kurasimisha makazi nchini. Serikali imetoa elimu kwa wataalam katika Halmashauri mbalimbali 52 katika mikoa mbalimbali ili kuhakikisha kwamba tunarasimisha na kuzuia makazi holela nchini.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea hapa, kama nilivyoeleza, nina zaidi ya page 35. Naomba tu Mheshimiwa Halima tuweze kuonana baadaye ili nimwonyeshe mafanikio na namna tulivyotekeleza ilani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Katika Kamati hii walitoa hoja kwamba migogoro mingi ya ardhi imechangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kutokupimwa kwa maeneo mengi ya makazi ya wananchi, lakini vilevile suala zima la upatikanaji mgumu wa hatimiliki za kimila na ucholeweshaji wa kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kutoa taarifa kwamba hati za Hakimiliki za Kimila zinatolewa na Halmashauri ya Kijiji na usajili wake unaishia katika ngazi ya Wilaya chini ya utaratibu uliowekwa na Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka, 1999. Hata hivyo, Sheria hii ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 inatoa fursa ya kuandaa Hatimiliki kwa kutumia njia rahisi kabisa katika kuhakiki vipande vya ardhi bila kulazimika kutumia teknolojia ya hali ya juu ya upimaji. Ni wajibu sasa wa Halmashauri zote za Wilaya nchini kuhakikisha kwamba Vijiji vyote vinatoa Hati za Kimila kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi kwa upande wetu tumeweza kufanya miradi ya mfano ya utoaji Hatimiliki za Kimila katika maeneo mbalimbali na kutoa mafunzo katika Halmashauri za Wilaya ya Namtumbo, Manyoni, Bariadi, Mvomero, Iringa, Kilolo, Bunda, Maswa, Mbarali pamoja na Mbozi. Kwa hiyo, ni jukumu sasa la TAMISEMI na Halmashauri zetu kuhakikisha kwamba inaendelea kazi hii nzuri na kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana. Tunaomba tu tujitahidi iwe endelevu ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na Hati hizi za Kimila ambapo wataweza kupata usalama wa miliki zao lakini vilevile wanaweza wakazitumia kama dhamana kupata mitaji.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwamba Kamati imetupa pongezi kwa kuongeza bajeti ya Tume ya Matumizi ya Ardhi, kutoka Shilingi bilioni 1.9 hadi Shilingi bilioni 3.1. Niendeleo tu kuomba Halmashauri mbalimbali ziweze kuongeza bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunatenga fedha hizo katika mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeishauri Serikali kwamba inapotwaa maeneo ya wananchi ihakikishe kwamba inawapa fidia stahiki kulingana na bei ya soko la wakati huo. Kuanzia mwaka huu wa fedha kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alieleza, tumetoa Waraka Na. 1 wa mwaka huu 2015/2016 na tunatarajia kwamba hakuna uthamini wowote utakaoidhinishwa na Mthamini Mkuu kabla Halmashauri au mtu anayelipa fidia hajathibitisha uwepo wa fedha za kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa muda mrefu ilikuwa haina Mfuko wa kulipa fidia na tumeeleza kwamba tumeanzisha Mfuko wa Fidia mwaka 2014, tulianza na Shilingi bilioni moja na mwaka huu tumewatengea Shilingi bilioni tano na tunaamini basi Serikali itaweza kupata fedha ya kulipa fidia pale itakapokuwa ikitwaa ardhi kwa manufaa ya umma.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kuangalia utaratibu wa makusanyo ya maduhili ili Wizara iweze kubaki na makusanyo yake yaani *retentionat source*. Kwa mujibu wa Sheria za Fedha za Umma ya mwaka 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004, maduhili yoyote yanayokusanywa na Afisa Masuuli yanapaswa kuwasilishwa kwanza Hazina kwenye Mfuko Mkuu wa

Serikali. Hivyo, kisheria Afisa Masuuli hapaswi kutumia maduhuli anayokusanya kabla hajawasilisha Hazina. Kwa hiyo, hoja hii itakuwa ni ngumu kwa sasa kwa mujibu wa Sheria iliyopo kuweza kubaki na makusanyo hayo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Serikali iipe kipaumbele Sekta ya Nyumba katika mipango yake kwani sekta hii ni moja ya vichocheo vikuu vya kukuza uchumi wa nchi kama ambavyo nchi nyingine zinafanya. Serikali kwa upande wetu tumeandaa Rasimu ya Sera ya Nyumba ya Taifa, vilevile kama nilivyoeleza pale awali, tumeshapata Mshauri Mwelekezi atakayefanya pamoja na mambo mengine kuandaa andiko maalum kwa ajili ya kuanzisha *Real Estate Regulatory Authority* ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia uendelezaji miliki.

Vilevile Serikali imekuwa ikiwezesha Wakala wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (*HBRA*) kwa kuitengea bajeti kila mwaka ili iweze kuendelea na utafiti na usambazaji wa matokeo yake kwenye sehemu mbalimbali. Vilevile Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa taasisi mbalimbali za umma na za binafsi ili waweze kushiriki katika ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sheria ya *Mortgage Financing Special Provisions Act* ya mwaka 2008, Benki 20 tayari zimeshajitikoza kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba (*Housing Micro Finance*) utakaowezesha wananchi wa kipato cha chini kukopa kwa masharti nafuu kupitia vikundi vidogo vya wajasiriamali umeshaanzishwa.

Hivi sasa Benki Kuu inachokifanya ni kuandaa mwongozo ambao pindi utakapokamilika tunapoanza mwaka huu wa fedha, basi taasisi hizi za *Micro-finance* zitaweza kupata fedha kwa ajili ya kukopesha wananchi mbalimbali wanaotaka mikopo midogo midogo ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja kutoka kwa Mheshimiwa Moza Saidy ambayo ilichangiwa na Mheshimiwa Mnyaa kuhusiana na mgogoro kati ya wananchi walioko kwenye Pori la Akiba la Swagaswaga Wilaya ya Nchemba. Napenda tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba tulikwenda wote Kondo, hoja hii amekuwa akiifuatilia sana pamoja na Mheshimiwa Zabein Mhita, ni lazima nimtaje. Tulikwenda Mkungunero na tulieleza kwamba baada ya kumaliza Mkungunero tutakwenda katika Pori hili la Swagaswaga.

Mheshimiwa Spika, napenda kumweleza kwamba hivi sasa kinachoangaliwa ni uwezekano wa kufufua mipaka hii ya Pori la Akiba, lakini vilevile tunafanya sensa ili kutambua wananchi walioingia katika pori hili; waliokutwa na waliovamia.

Sensa hii tayari imeshaanza tangu mwezi Mei na hivi sasa bado inaendelea na tunajitahidi iweze kukamilika mapema ili tuweze kufufua mipaka hii. Baada ya sensa hii kufanyika, tutaweza kufahamu hali halisi lakini vilevile kujua ni hatua gani stahiki tuweze kuchukua.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la Pori la Mkungunero vilevile anajua kazi ambayo tumeifanya katika Pori hili kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma pamoja na Naibu Waziri wa Maliasili, tulitembelea eneo hilo Januari 27, ili kubaini mipaka ya eneo la Akiba pamoja na mipaka inayozunguka.

Napenda tu kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba Kikao cha RCC kiliamua kwamba wananchi wote ambao walikutwa kwenye pori hilo kabla ya kutangazwa Wizara ya Maliasili ili kulipwa fidia. Wananchi waliovamia iliamuliwa waondolewe. Pia iliamuliwa kwamba ni vyema turudishe mipaka ya Pori la Akiba kwa mujibu wa GN No. 307 ya mwaka 1996 na vile vile sensa ya nyumba pamoja na wananchi wanaolima kwenye eneo hili iweze kufanyika. Iliamuliwa pia kwamba, kufanyike au uandaliwe mpango wa matumizi bora ya ardhi wa vijiji vinavyozunguka pori hili la Mkungunero.

Mheshimiwa Spika, ilikadiriwa kwamba bajeti ya Shilingi milioni 84 kwa ajili ya kutekeleza mpango huu inahitajika. Napenda kufahamisha Bunge lako kwamba bajeti hii au makisio haya yameshawasilishwa katika Wizara yetu pamoja na Wizara ya Maliasili kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine kuhusiana na wananchi wa Ilemela, hoja hii iliwasilishwa na Mheshimiwa Amina Clement, kwamba wako wananchi wa Kata ya Nsumba ambao wamekuwa wakilalamikia kutoshirikishwa kwenye utoaji wa ardhi, fidia ambayo imekuwa ikitolewa ni ndogo kulingana na ardhi inayochukuliwa na wamekuwa hawajaridhishwa na uamuzi wa fidia hiyo.

Mheshimiwa Clement ameteka kujua ni lini sasa suala hili litaweza kufikia mwisho ili wananchi hao waweze kuendelea na shughuli zao?

Mheshimiwa Spika, napenda tu kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, bahati nzuri wananchi hawa walifika, niliwaona, lakini Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mheshimiwa Waziri alishawasikiliza alipokwenda Mwanza na tayari Mheshimiwa Waziri ameshaunda Tume au Kamati inayoongozwa na Kamishna wa Kanda ya Ziwa. Kamati hii hivi sasa inalifanyia kazi suala hili na itatoa mapendekezo ya namna bora ya kuhitimisha ndani ya mwezi huu wa Sita.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia kuna hoja ya Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mbunge wa Viti Maalum ambaye alitaka kujua migogoro ya fidia katika Wilaya ya Kondoa japo ni midogo, lakini imekuwa ikileta uvunjifu wa amani na amekuwa akitaka kujua kama endapo tutapeleka wataalam ili waweze kuangalia eneo hili la Kondoa. Tayari Wizara kama nilivyoeleza imeshatoa mwongozo wa ulipaji wa fidia. Tutafuatilia malalamiko haya ili kuona ni wananchi gani ambao wamekuwa wakilalamikia fidia hii na endapo hawajalipwa fidia stahiki ili tuweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Betty Machangu ambaye alitaka Serikali isimamie Halmashauri za Wilaya kutoa Hatimiliki za Kimila kwa kuwapa wanavijiji faida ya ardhi yao kuwa na thamani zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi inaendelea na jitihada za kuzisimamia Halmashauri ziweze kutekeleza Sheria ya Ardhi ya Vijiji; tunatoa miongozo mbalimbali pamoja na mafunzo kwa Halmashauri na Watendaji wetu katika ngazi ya Wilaya na Vijiji; na tumekuwa tukitoa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kutoa Hatimiliki za Kimila kulingana na uwezo wa Wizara.

Hata hivyo, bado tunapenda kusisitiza kwamba ni jukumu la kila Halmashauri kuipa kipaumbele Sekta ya Ardhi ili kuiwezesha kutekeleza majukumu ya Idara za Ardhi zilizoko katika Halmashauri ikiwa ni pamoja na utoaji Hatimiliki za Kimila kwa wananchi vijijini.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Anastazia Wambura kuhusiana na wananchi wa Manispaa ya Mtwara Mikindani eneo lile ambalo UTT walikuwa wamelichukua na kwamba ilikuwa vipimwe viwanja 10,000, lakini mpaka hivi sasa wananchi hawajui kinachoendelea na kwamba wamezuiliwa kufanya maendeleo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ambao ulikuwa utekelezwe kati ya ubia wa UTT na Halmashauri ya Manispaa ya Mikindani, kwa sasa mradi unatekeleza awamu ya kwanza kwa matarajio ya kupima viwanja 2,500. Kazi iliyofanyika hadi sasa ni kuandaa michoro ya mipango miji yenye viwanja takribani 3,000 na kazi ya kuthamini mali tayari ilikwishafanyika na wananchi 2,220 walikuwa wanategemewa kulipwa jumla ya Shilingi bilioni 75.

Hivi sasa ulipaji wa fidia na upimaji umesimama kusubiri maelekezo ya jumla kutoka TAMISEMI kwa Halmashauri zote nchini ya namna ya kutekeleza mradi ya aina hii kwa njia ya ubia baina ya Halmashauri na UTT. Wizara inafuatilia kwa ukaribu suala hili ili kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa mapema iwezekano kwa maslahi ya wananchi wa Mtwara na Taifa kwa ujumla kwa kutegemea maelekezo yatakayotolewa na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine ya Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ambaye alikuwa akitoa msisitizo kwamba Hatimiliki za Kimila wanawake waweze kupata tuongeze kasi. Napenda tu kumwarifu kwamba mipango na jitihada za kuhakikisha wananchi wanaendelea kumilikishwa maeneo yao, hususan wanawake na wanandoa inaendelea kutekelezwa.

Vilevile kama Wizara na pamoja na TAMISEMI tunaendelea kutoa elimu na kwa upande wa Jimbo la Iringa au Mkoa wa Iringa, jumla ya Hati za Kimila 11013 zilitolewa ambapo Hati 2,897 ni wanawake na wanaume ni 5,630 na umiliki wa pamoja, yaani *joint ownership* ya wanandoa ni 2,756.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ambaye alitaka kujua ni wateja kiasi gani au wananchi kiasi gani ambao wameweza kupata mikopo kwa kutumia dhamana ya Hatimiliki za Kimila. Napenda kiliarifu Bunge lako kwamba kwa kutumia Hatimiliki za Kimila kwa upande wa Iringa, CRDB imetoa mikopo ya takribani Sh. 178,140,000/=; kwa upande wa Benki ya Posta, imetoa mikopo ya takribani Shilingi milioni 30 na kwa SACCOS Sh. 407,500/=.

Napenda tu kutoa rai kwa benki mbalimbali kuhakikisha kwamba wanatoa mikopo hii kwa sababu Hatimiliki hizi za Kimila zinayo hadhi sawa kama ilivyo Hatimiliki za kawaida.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Betty Machangu kuitaka Serikali iweke mpango mzuri wa matumizi ya ardhi nchini ili kuwezesha ardhi kupangwa vizuri. Tayari kwa upande wetu kama Serikali na kama nilivyoeleza awali, tumeandaa Mpango wa Taifa wa Matumizi Ardhi, yaani *The National Land Use Framework Plan* ambao unaonyesha na kuongoza mpangilio wa matumizi ya ardhi nchini. Mpango huu unatekelezwa katika kipindi cha miaka 20 kuanzia mwaka 2013 hadi mwaka 2033.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia ya Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ambaye alitoa ushauri kwamba wananchi vijijini wapimiwe ardhi ili waweze kumilikishwa. Napenda kuchukua fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Sera na Sheria za Ardhi zimerekebishwa na hivi sasa mwanamke anayo haki sawa za kumiliki ardhi; za kupata, kuhamisha, kuendeleza na kutumia kwa masharti yaleyale kama ilivyo kwa wanaume. Hivyo basi, napenda kuchukua fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o kila mwanamke mwenye ardhi yake kijijini atapimiwa na kumilikishwa kwa kuzingatia taratibu sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba tu hapa kutoa angalizo kwa Halmashauri zetu na kutoa rai; wako wanawake wengine wa vipato mbalimbali.

Wengine bado wanakuwa hawapati taarifa na matangazo mbalimbali ya fursa hizi yanapotolewa. Tutoe tu rai kwamba wajitahidi kupitia matangazo mbalimbali kupitia redio za kijamii na fursa nyingine kupitia Wenyeviti wa Serikali za Vitongoji waweze kutoa matangazo ya fursa mbalimbali za viwanja na mashamba zinazojitokeza ili wanawake wengi zaidi waweze kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja pia ya Mheshimiwa Moza kuhusiana na mgogoro wa mpaka Wilaya ya Hanang'. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Moza kwamba Wizara yangu itatuma wataalam kwenda Hanang' ili mpaka wa Wilaya kwa mujibu wa GN zinazohusika iweze kuwekwa bayana.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Moza alimtaka Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake awaambie wananchi wa Kondo wanaozunguka Pori la Mkungunero watakwenda wapi? Tayari tumeshalieleza na naamini atakuwa tayari ameridhika.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kuhusiana na hoja ya hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi. Niseme tu kwamba tumelipokea na Wizara ya Ardhi imekuwa ikilifanyia kazi pamoja na Wizara ya Maliasili.

Naomba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pamoja na wananchi wote wanaozunguka msitu huu wa Kazimzumbwi, wawe na subira kidogo. Kupitia Wizara yetu na Wizara ya Maliasili tunashirikiana ili kuupitia mpaka huu kwa pamoja ili suala hili tuweze kulikamilisha kwa faida ya wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, naomba kabla sijamaliza nitambue pia hoja ya Mheshimiwa Lucy Mayenga ambaye kwa kweli kimsingi alitoa pongezi za dhati na ushauri mbalimbali kuhusiana na namna ya kuboresha Ofisi ya Msajili wa Hati pale Makao Makuu, lakini vilevile kuhusiana na namna gani tutaweza kutoa huduma nyingine zinazopatikana Wizarani katika Kanda zetu. Napenda kumhakikishia kwamba katika mipango ya mwaka huu hili tumeweza kulizingatia.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Mheshimiwa Hamoud Jumaa kupitia swali lake hapa Wizarani ambapo alielezea kwamba kulikuwa na Pori Mkoa Pwani takriban ekari 83,000 na kwa kweli aliongea kwa uchungu mkubwa na angalau alivyongelea sasa hivi ameona matokeo, Mheshimiwa Waziri amechukua hatua na tayari Mheshimiwa Rais ameshafuta takriban mashamba 18 katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunipa fursa hii kwa kunipa dakika hizi 50 kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba nami naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja, dakika 30!

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, asubuhi niliwaambieni kwamba Angella ni nguo ya chini ya kabati, ndiyo maana nimempa dakika 50 halafu mimi dakika 30. Maana hawa ndio Marais wa miaka kumi ijayo. Sisi tutakuwa Wazee wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie machache, naona mengi amejibu lakini sikujua kumbe watu wengi wameandika kwa maandishi, kwa hiyo, hata ningesoma hili jedwali nisingemaliza, lakini kwa utamaduni wetu, tutawagusa wengine tu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naanza na rafiki yangu Mheshimiwa Mnyaa. Najua kiwanja chako ulitapeliwa, watu wamejifanya Mnyaa ila sura tofauti, hawana sharubu kama wewe.

Kwa hiyo, niliyempa kazi, yuko hapa, leo jioni tutaonana, lazima urudishiwe kiwanja chako; na ushuri mwingine tumeupokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Kafumu nakuahidi kwamba tutakuja Igunga ili kuona hao matapeli wa Halmashauri. Kama wananisikia, waanze kujirekebisha huko huko, kwa sababu tukija hatuna msalie Mtume.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Shah, Mbunge wa Mafia kwa pongezi zako na shukrani, maana Waswahili wanasema usiposhukuru kwa kidogo hata kikubwa hupati. Sasa nashukuru lakini nataka nikuhakikishie kwamba, shamba hili limefutwa. Baada ya muda mfupi sana wathamini wangu watakuwa pale kuja kujiridhisha kama kuna chochote huyo mwekezaji aliweka juu kinahitaji fidia, tutamlipa. Pia tunakuja kufanya utaratibu wa kuhakikisha namna ya kugawia wananchi na tukiona wananchi wametoshaka, ardhi tunayo, tutaweka akiba ya Serikali pale pale Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwa haraka kidogo. Mheshimiwa Mntangi umetoa ushuri mwingi lakini mambo yako ya Muheza, watu wangu wameshakuja na wameongeza kasi kidogo ili kuhakikisha wanaainisha watu kule wenye shida ili tuweze kutekeleza kazi ile, kwa sababu hata Mheshimiwa Rais ametuagiza kwamba tuhakikishe kwamba tunawapa watu wenye shida na utaratibu huo tumpelekee yeye. Kwa hiyo, hilo jambo tutalifanya.

Mheshimiwa Spika, yako mengi. Nawashukuru vilevile Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam; Mheshimiwa Madabida na Mheshimiwa Zungu ameondoka lakini pia ameacha maandishi yake. Hoja nyingine ya Mheshimiwa Zungu inafanana sana na Mzee wa Temeke juu ya nyumba za *National Housing* na kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoelewana, ni kweli kwamba kuna kodi zimepandishwa sana, lakini nimeamua kama tulivyozungumza na Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Mzee wa Temeke, tutapanga tarehe wale wazee tuonane nao ingawa kwa sasa hawatafukuzwa kwenye nyumba zile; tuzungumze, tuweke msingi wa kudumu juu ya jambo hili. Msingi huo tukishauweka, basi kila Mtanzania atakayeathirika atajua utaratibu upi wa kufuata kama jambo hili limetokea tena. Kwa hiyo, naomba Mzee wa Temeke usiwe na wasiwasi, tutakutafuta ili tukae na wale wazee tuweke msingi wa kudumu juu ya eneo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Ndugulile, kuhusu barabara, kama nilivyosema, tunazo fedha tayari shilingi bilioni tatu. Asubuhi niliposema hatujapata fedha za maendeleo, mlitishika kidogo, lakini niliwaambia kazi hazilali. Hatujapata, lakini kazi zinakwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeshatenga za kuanzia Shilingi bilioni tatu katika vile viwanja vya Kibada 20,000 na kazi na kazi inanza *any time*. Pia kwenye mradi ule kwa Kigamboni, nimesema asubuhi kwamba tunakuja kuainisha barabara, kufanya uthamini, fedha za kulipa wale waliopo kwenye barabara tunazo, za kulipa tathmini, lakini na za kupasua barabara kwenye mradi. Tutaanza na ile barabara inayoishia kwenye daraja, tuifikishe mpaka mwisho, maana pale ilipoanzia hata daraja lenyewe halionekani thamani yake. Kwa hiyo, mambo yote haya tutayafanya. Mambo mengine yote tutaendelea kuwasiliana kwa kadri tunavyokuwa hapa.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema Mheshimiwa Mtemvu tutaongea, mambo yako yote yanajulikana pamoja na yale maghorofa tumezungumza yale ya Jeshi, tutaongea. (Makofi)

Mheshimiwa Bulaya, nimesikia migogoro yako yote ya Bunda, tuwasiliane zaidi na tutapeleka taarifa. Kamishna wangu wa upande ule yuko hapa, amesikia. Tutafuatilia wenyewe ili kuhakikisha migogoro yote ile ya Kawangwa, sijui Unyali na yote yale tunayafuatilia kwa kasi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Bulaya amezungumzia habari ya bomoa bomoa na wale waliozungumzia ile nyumba ya ghorofa iliyopo Nkhuruma. Halmashauri ya Ilala kwa sheria ndiyo wanaopaswa kuvunja.

Wao ndio watasimamia uvunjaji, lakini hawana fedha. Sisi tutalipa Shilingi bilioni moja kwa ajili ya uvunjaji wa lile jengo, lakini kwa amri ya Ilala. Maana wanaosimamia ubora na udhibiti wa majengo ni Manispa. Sasa sisi tutasimamia na nimeshazungumza na Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, narudia, nimemwomba kwa kushirikiana na Msikiti pale wa *Shia*, wazungumze na wapangaji wa jirani waondoke pale kwa muda na wakati tunaanza hilo zoezi, barabara zitafungwa, lakini jengo hilo ni lazima livunjwe. Lina ghorofa nyingi lakini lazima zivunjwe. Sasa kutokana na kuwa karibu na majengo matatu pale, ndiyo maana inahitaji *technology* maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huyo *contractor* ameagiza watalaam na mtambo kutoka China, kwa ajili ya kuvunja hilo jengo na jengo hilo litavunjwa katika muda mfupi ujao. Kwa hiyo, wananchi kama wanasisikia pale, waanze kujiandaa kusogea mbele, kwa sababu siyo hiari yao kuhama, lakini ni lazima wahame ili wapishe jambo hilo lifanyike.

Mheshimiwa Spika, kituo cha *satellite* Mungu akipenda tutajenga ingawa hatukukiingiza kwenye bajeti, lakini tunaendelea kuzungumza na wahisani fulani fulani ili watupe fedha tuweze kufanya jambo hili.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Chomboh, kwa ushiriki wako mkubwa kwenye Kamati. Nakushukuru sana Mheshimiwa Shekifu kwa maoni yako yote, tumeyasikia, najua wewe ni Mzee wa Kamati, maoni yako kila mara huwa tunayafanyia kazi na maono na ushauri wako wote uliosema kwenye Kamati yetu, tutaufanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Bwana Abuu Jumaa na wewe ni Mjumbe wa Kamati, tutafuatilia haya yote, lakini ujue tu kwamba mwezi uliopita tu uliniambia habari ya mashambapori ya Kibaha, lakini katika mwezi huu huu, Mheshimiwa Rais ameshafuta mashamba 16 na ni makubwa na yana majina makubwa humo ndani na mashamba mengine zaidi ya 100 yako kwenye *pipeline*. Ardhi hii tutaipima; sehemu kubwa ya ardhi hii tutaiweka akiba ya Serikali pale Kibaha, lakini nyingine tutawapa wananchi wenye uwezo wa kuendeleza hivi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mzee Laizer, juu ya mgogoro wako wa Longido, Arumeru na Monduli, nilishafika kwenye *site* pale mnapogombania malisho. Mgogoro ule utaondoka tu wewe na Mzee wa Monduli na Mzee wa Arumeru, Ole huyu hapa; tukae pamoja. Ndivyo nilivyoahidi. Tukikaa na ninyi watatu wakubwa, tutamaliza ule mgogoro, kwa sababu majibu nayajua, lakini nikisema hapa mtanipinga. Najua nani anayesababisha vurugu katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, kuna watu hawana haki pale, lakini yale maeneo ya malisho, ninazo ramani zote na kila kitu na mimefika kwenye *site*. Najua mwenye haki. Nilihidi nitakaa na ninyi wakubwa watatu, maana ninyi ndiyo vinara ili tumalize. Tukimalizana na ninyi, basi mgogoro utakuwa umekwisha. Kwa hiyo, nipe subira kidogo, tutazungumza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ile ya kule Kilimanjaro, nitamwarifu Mheshimiwa Mbunge *time* twende kuzungumza na yule mwekezaji, ili tuhakikishe kwamba hata kama yeye anabaki, lakini mifugo aliyoikuta pale iendelee kupata huduma kama kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru Mheshimiwa Halima kwa pongezi zake za Chasimba, nashukuru kwa kelele zako za muda mrefu, lakini kelele wakati mwingine zina matunda. Kwa hiyo, tutashirikiana; ilikuwa ni ndoto yangu muda mrefu. Siku ile walivyokuja kwangu wale vijana walimkuta Mwenyekiti wa Chama, Mzee Madabida Ofisini kwangu, kwa sababu nilipofika tu Chama cha Mapinduzi Mkoa wameniandikia barua. Moja ya jambo wameniambia, lazima umalize Chasimba, Makongo na Kigamboni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nami nimeamua huko huko. Sasa bahati nzuri huku nyuma kuna Mheshimiwa Halima. Sasa twende pamoja tu. Hata hivyo, i ninalo agizo maalum kwa Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa wa Dar es Salaam. Ndiyo maana kila ninapokwenda; Kigamboni nakwenda naye, Chasimba nitaenda naye na Makongo nitaenda naye. Nami ni Mjumbe wa Kamati Kuu, lazima nitekeleze maagizo ya Chama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la kuzingatia watu wa vipato, nimeshazungumza na ile Kamati, watu wote watakaopewa ardhi pale watamilikishwa kisheria. Anayetaka kuishi Mjini, ni lazima alipe ada za Mjini kisheria. Kwa hiyo, tutamkadiria kila mtu kutokana na *square meters* za ardhi yake atakayokuwa. Hatuangalii sura ya mtu! Sheria ya Ardhi haitazami sura ya mtu. Sasa kama ana *square meters* mbili, atachajiwa mita mbili; kama 10 mita 10. Wale wasio na uwezo nilishawaambia kwamba niko tayari kuwapa *grace period* ya kipindi fulani, mpaka watakapogomboa hati zao. Siyo lazima tuwa-charge mara moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hayo yote yako kwenye sura yangu kwa sababu sura yangu imeumbwa kuwa ya huruma. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Halima, tumeamua kwa makusudi kuwapunguzia Kodi ya Ardhi wananchi wenye mashamba moja moja. Tunataka wale wananchi wa vijijini nao wamilikishwe wapate hati.

Badala ya kulimalima tu mtu ana ekati mbili, analima ardhi haina thamani yoyote, sasa ukimwambia mama yangu yule wa Kijijini Idodi, amilikishwe ardhi kila mwaka achajiwe Sh. 1,000/= kwa ardhi yake, hataki! Ndiyo nasema, kwa sababu upunguzaji wa kodi hii ungenisikiliza vizuri ina mafungu mawili.

Mheshimiwa Spika, nimepunguza sana kodi za wananchi maskini wa vijijini, ambao walikuwa wanatozwa Sh.1,000/= kwa ekari moja na kuwarudishia kufanya Sh. 400/=. Mjue kwamba hii mwanzo ilikuwa Sh. 200/=. Ikapandishwa mara moja Sh. 1,000/=. Sasa imerudidhwa ni Sh. 400/=. Wale wananchi wa vijijini tunawapa hamasa ili wahalalishe mashamba yao, wapae hati, tupate mapato. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kuwa na Sh. 1,000/=, hawatalipa, hawatamilikishwa, thamani ya ardhi hawatakuwa nayo, lakini wale wa biashara, siyo Sh. 400/=. ni Sh. 5,000/= kwa ekari moja. Kwa hiyo, kuna tofauti hapo. Wale wanaofanya biashara tumewapunguzia kwa asilimia 50. Wao wanalipa Sh. 5,000/=, wale mama zetu wanaolima vijiji wanalipa Sh. 400/=.

Kwa hiyo, ningefurahi Mheshimiwa Halima ukubali hili, kwa sababu kwenye sera yetu sisi ya Chama cha Mapinduzi, kazi yetu ni kuwajali wanyonge. Sasa wanyonge wetu sisi ni wale wanaoishi vijijini. Kwa hiyo, hili ungelipenda, kwamba tumewapunguzia mzigo kutoka Sh. 1,000/= mpaka Sh. 400/=. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wale wa biashara tunawatoza ekari hiyo hiyo Sh. 5,000/=, maskini Sh. 400/=. Kupima mashamba; maskini kutoka Sh. 800,000/= kwenda Sh.300,000/=. Kwa hiyo, hivyo ndivyo tunavyokwenda. Bahati mbaya sana Mheshimiwa Halima nimeshasaini na nimeshaamua. (Makofi)

Mheshimiwa Halima, wewe ni Mjumbe wa Kamati yangu ingawa ni Waziri Kivuli. Nataka nikuahidi, kama Mungu akipenda mwaka mmoja ujao utaona kodi zimekusanywa sana katika eneo hili na umilikaji unaweza kukuta umekuwa mkubwa kwa sababu hii inashawishi watu wamiliki, wachukue hati.

Mheshimiwa Spika, yale mashamba yote yanayolimwa vijijini huko hawahalalishi, kwa sababu wanaogopa, ukishahalalisha tu, umeonwa kwenye mtandao, kila mwaka watakudai, kwa hiyo, wanalima kienyeji tu.

Mheshimiwa Spika, lakini hii inaweza ikawarahisishia kwa sababu upimaji umepungua kutoka Sh. 800,000/= kwenda Sh. 300,000/= na ada ya kila mwaka imepungua kutoka Sh. 1,000/= kwenda Sh. 400/=. Wanaweza wakashawishika kupima walio wengi ili angalau mashamba yao yaingie kwenye mtandao tupate fedha za kutosha.

Hebu tu-*bet* mimi na wewe mwakani unaweza kukuta takwimu hii, wanaolipa Sh. 400/= imekuwa kubwa kuliko ya mwaka huu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, *Audit* ya miradi ya viwanja 20,000 ilishafanyika, na nadhani taarifa hii ipo tayari na Kamati walishaiona nadhani. Kwa hiyo, tutaendelea kuwasiliana tuone kitu gani ambacho hakijulikani mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, masuala ya CDA tulishayatolea uamuzi hapa Mjini. Kuanzia sasa upo utaratibu mpya wa ushirikiano kati ya CDA na Halmashauri. Hakuna jambo linafanyika bila kuwasiliana na Manispaa ya Dodoma; wanaelewana wanafanya pamoja.

Mheshimiwa Mnyaa, ni kweli, sasa Serikali tunaongea wenyewe na nilisema asubuhi, kwamba tungependa taasisi za Serikali zinazojenga nyumba za gharama nafuu, *at least* zile nyumba za gharama nafuu ziondolewe VAT, siyo *National Housing* peke yake. Tunaomba waondolewe VAT, siyo *National Housing* au Taasisi, ila yule mnunuzi anayenunua nyumba zilizojengwa na taasisi za Umma.

Kwa hiyo, hili tunalizungumza na nilisema asubuhi nafikiri katika muda mfupi ujao linaweza kuwa limetolewa uamuzi na tutaweka kiwango, siyo kila nyumba. Zile nyumba za kununua Mheshimiwa Mnyaa na Lukuvi za Shilingi milioni 100, zile hatutagusa, lakini tunajua kiwango ambacho mwananchi wa kawaida anahitaji kununua na tafsiri halisi ya gharama nafuu. Ila ndiyo tunauzungumza ndani ya Serikali ili atakayenunua nyumba za taasisi za Umma, aondolewe hiyo VAT.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, uporaji unafanywa, hata kwangu pale wanajua nimeshawaambia hata juzi; wapimaji wote wanapopima *site* yoyote, lazima waweke kaporu kidogo. Viwanja vitano, sita, saba lazima waweke. Huo wizi upo tu. Hakuna mpima aliyefuzu, ambaye hawezi kufanya jambo hilo, labda wale wachache ambao ni malaika.

Kwa hiyo, tuendeleo kushirikiana huko kwenye Halmashauri, lakini na sisi tutaendelea kupiga kelele. Wapimaji walio wengi na sasa hivi tumeruhusu hata wapimaji binafsi na wafanya tathmini binafsi. Upimaji huu wa viwanja vingi huu, kwa vovyote vile wakikuletea mezani kama hujui kusoma ramani unaweza kukuta sehemu nyingine wameandika mabonde na nini, lakini humo ndiyo ukienda kule hakuna mabonde kwenye *site*; ila kwenye ramani utaona mabonde. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni kweli, lakini kwa kelele kelele hizi zinasaidia na wenyewe huko kuwashtua kwamba kumbe hata watunga sheria wanajua kwamba huwa tunafanya utapeli kwenye upimaji. Kwa hiyo, tutaendelea kusisitiza ili angalau watumishi wetu waendeleo kuwa waaminifu zaidi na kutenda haki.

Mheshimiwa Spika, watumishi waliopo nje (*Diasporas*) wanaruhusiwa kumiliki nyumba ili mradi tu wawe Watanzania. Najua sasa hivi watu wengi wananunua nyumba. Kama wanashindwa, waunganishe na mimi, nitawapa nyumba wanunue za *National Housing* na tunawapa *title*. Siku hizi tumeshaanza kutoa *title* kwa sheria yenu, *Unit Title* tunatoa! Tunazo nyumba nyingi, kama una watu, wasiagize kwa mashangazi zao kujenga nyumba. Watawatapeli; waje *National Housing*; tunazo hizo nyumba tutawauzia hata kesho na tutawapa na *title*, watakaa nayo huko huko.

Mheshimiwa Spika, mapori ya Swagaswagwa ya rafiki yangu Mrangi kule, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshayatoelea uamuzi na bahati nzuri Mkuu wa Mkoa wa Dodoma hapa tumempa hiyo kazi, anafuatilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juu ya *National Housing*, nyumba; Chama cha Wapangaji wameliletea barua, wao wanapendekeza kwamba wapangaji wa *National Housing* wasikae sana kwenye nyumba zile na hasa za Mijini, tuweke ukomo. Hili jambo kama linaniingiaingia hivi, kwamba watu waliopo katikati ya Miji katika mikoa yetu, ni wale wale walioingia tangu vijana mpaka wanazeeke wanastafu humo. Kwa hiyo, vijana wa sasa wanaopata ajira leo mpaka wanastaafu na wao hawatapata nafasi wala *chance* ya kupanga nyumba kwenye nyumba za Shirika la Nyumba. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Chama cha Wapangaji wanapendekeza tuweke ukomo ili angalau vijana hawa wafanyakazi katika miji nao wapate nafasi na fursa ya kupanga kwenye nyumba hizo. Wanasema hasa, tufanye utaratibu wa kuwatambua watu ambao wameshajenga nyumba zao mbili, tatu, nne, lakini bado wanaishi nyumba za *National Housing*, hawataki kukaa kwenye nyumba zao. Wanakaa katikati ya mji ambayo ni fursa ya wafanyakazi wanaotakiwa kufanya kazi mjini. Tutaliangalia. Mheshimiwa Rukia hupendi, lakini tutaliangalia. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema tutaliangalia. Mimi sisemi habari ya Wahindi! Ninyi msizungumze habari ya Wahindi hapa, mtaanza mambo ya rangi hapa. Sizungumzii habari ya rangi. Nasema, wale wote ambao wana nyumba nyingi tu wameshajenga, lakini wanang'ang'ania kukaa katikati ya mji, eti kwa sababu wamezoea pale ni mjini, karibu na mabenki na nini; nalo tunaliangalia ili angalau tuwape fursa na vijana wa leo kuonja fursa za Serikali kukaa pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilipotoa taarifa kwenye kitabu, kuonyesha ikama na upungufu wa Maafisa Ardhi wengi mmeshtuka, lakini nilitaka kuwapa taarifa kwamba baada ya kugundua hilo na kwa sababu ikama hii Halmashauri nyingi hawawezi kujijaza, tumefanya uamuzi sasa, tunazungumza na TAMISEMI; kwa sababu kanda mbili zinatakiwa sana na sisi tuna kanda nane, kwa hiyo, tunataka kuanzia mwaka huu wa fedha, wapima wote tunawaweka kwenye Kanda na wafanya tathmini wote tunawaweka kwenye Kanda.

Mheshimiwa Spika, au tunaweka utaratibu na TAMISEMI, yule Kamishna wa Kanda anawadhibiti yeye ili kazi ikitokea kwenye Kanda husika, wote wafanye. Kwa sababu tumeamua mwezi wa Saba kununua vifaa vyote vya kisasa vya upimaji na kuviweka chini ya *Assistant Commissioners* wa Kanda. Vifaa vya upimaji vyote vinavyotakiwa, iwe ni *Total Stations*, sijui *GPS*, zote zitakuwa kwenye Ofisi zetu za Kanda ili angalau kila Kanda iwe na vifaa vyote vizuri vya upimaji vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu katika kanda utakuta wapima wachache, ndiyo maana tunataka tuwa-*pool* wawe pamoja ili waweze kushughulika na Kanda nzima, pamoja na wafanya tathimini. Tunataka tuwakusanye ili angalau washughulikie kanda nzima.

Kwa hiyo, tutashughulika na wenzetu wa TAMISEMI ili tuone uwiano kila Kanda iwe na Wathamini na Wapima katika Kanda zote waweze kuenea na waweze kutumia vifaa vile vya Kanda. Siyo rahisi kwa Halmashauri moja moja kununua hivi vifaa vya upimaji, ni gharama kubwa, lakini sisi kama Wizara, tumeamua kununua kwa sababu ni jukumu letu, lakini watalaam wa Halmashauri tutawaunganisha pamoja ili waweze kutumia hivi vifaa kwenye Kanda inayohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, huu upungufu mliouna kwenye kitabu utakuwa hauna maana kwa sababu kazi zote zitakuwa zinafanywa kwa pamoja kwa kusimamiwa na Kanda husika.

Mheshimiwa Spika, kuna *issues* zimezungumzwa hapa kwenye taarifa ya Mheshimiwa Halima, *issue* ya *Mawenzi Sports Club*. Nimemwagiza Kamishna wangu aijibu kwa maandishi ili afafanue ukweli, kwa sababu yanayozungumzwa ni tofauti na yaliyoandikwa kwa tathmini. Ninayo taarifa hapa, ni ndefu, sitaki kuisema hapa, lakini tutaiandikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile *issue* ya Himo ya Mheshimiwa Mrema, *Doctor* yuko wapi? Tutamwandikia yeye na yule mwenzake ambaye wanalalamikiana siku zote, tutampa majibu. Naye anayozungumza (bahati nzuri anakuja) na yenyewe yana utata. Kwa hiyo, tutazungumza tuwaambie ukweli ni nini. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mrema na wote wanaohusika na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, tutawaambia majibu yetu ya kitalaam ili kila mtu ajue ukweli juu ya masuala ya Himo na yale ya *Moshi Sports Club*, ijulikane. Siyo vizuri kuzungumza masuala ya miliki za watu hadharani hapa, lakini tutawaandikia kwa sababu...

MBUNGE FULANI: *(Aliongea nje ya microphone)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Eeeh!

SPIKA: Naomba usiwasikilize hawa ndugu huku! *(Kicheko/Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, nasema kama nilivyopanga kuzungumza. Kwa hiyo, *issue* ya *Mawenzi Sports Club*, tutawaandikia majibu yake na *issue* ya Himo, Mheshimiwa Dkt. Mrema tutakuandikia; na wengine wote. Unajua lile eneo linamilikiwa na watu wengi sana. Siyo huyo tu unayemtaja, wako wengi. Kwa hiyo, tutakuandikia wewe majibu na huyo mwingine unayemsema na Halmashauri ya Moshi na maoni yetu. Tutawaandikieni rasmi ili mjue wazi kwamba maoni ya kitaalam yakoje. Hayo ndiyo yatakuwa maoni ya Serikali. Sasa mtu yeyote atayekuwa haridhiki na maoni ya Serikali, mlango upo, anakwenda Mahakamani au anatafuta rufaa mahali pengine.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Kamati yangu. Maneno mengine waliyozungumza katika mchango wao kwa kweli ni mawazo mazuri. Nataka kuwahakikishia haya ingawa muundo wenyewe wa Kamati unaishia ukingoni lakini sisi kama Serikali tunakwenda kuyafanyia kazi, maana tunaondoka sisi tu lakini Serikali ipo. Kwa hiyo, watakaokuja baadaye watafuatilia na kuona kwamba haya yamefuatiliwa na tutafanya.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Kamati tumekuwa pamoja kwa muda wote, na mawazo yenu mmekuwa mnatoa ni ya kiungwana sana, ya kujenga, hayana kutafuta mchawi bila kujali itikadi. Kwa hiyo, nawashukuru sana. Nataka mwamini tu maoni yenu yote haya tutayatolea maelezo.

Pia limezungumzwa hapa suala la mgogoro wa Magereza na Mheshimiwa Aeshi. Tutafuatilia. Nimeona Mkoa umeshaanza kuchukua hatua ya kuzungumza na Magereza ili angalau Magereza wawaachie ardhi kidogo. Tutawasaidia ili kuona kwamba Magereza na kuzungumza na Wizara ya Mambo ya Ndani ili kuona kwamba Magereza wanaelewa jambo hili ili kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo ametoa ushauri mwingi, nimeona ushauri mwingi sana lakini ushauri huu naomba uniruhusu nikuandikie kwa sababu wewe umetoa ushauri katika maeneo mengi sana. Nitakuandikia majibu yote ya ushauri wako ulioutoa. Naheshimu sana ushauri wako, umechangia katika maeneo mengi sana.

Mheshimiwa Cecilia Paresso umezungumzia habari ya wananchi wa Kijiji cha Mang'ola ambayo majibu yake ninayo, bahati mbaya naye hayupo. Kwa hiyo, naomba nikuandikie majibu yako, kwa sababu ninayo majibu marefu hapa.

Mheshimiwa Gekul amezungumzia habari ya eneo ambalo lilikuwa la *National Housing*. Ukweli eneo hili limepata baraka ya kikao kilichokaa tarehe 12 na 13 Mei, 2015. Sasa kwa mujibu wa utaratibu wangu kama Waziri wa Ardhi, Madiwani wakishafungamana pale, wamechukua na rungu kama hili wakaamua, Waziri wa Ardhi ngumu kweli. Kama wamegawa kiwanja hicho kiwanja kwa mtu, mimi kukiondoa inakuwa ngumu. Kwa hiyo, jambo hili limekwisha. Baraza la Madiwani wameshaamua kufanya hivyo walivyofanya

Mheshimiwa Spika, hata eneo lile la shamba la Singu naona wenye shamba nao wamekubali kuleta michoro. Wataleta michoro ile Mipango Miji, tutaiangalia na tutawarudishia ili wafanye. Hata hivyo, kwa ujumla, kama nilivyosema, nitapitia maeneo yote nilikopita ili kuhakikisha nafanya tathmini ya utekelezaji wa kero zangu, zile ambazo wananchi walitoa mbele yangu.

Mheshimiwa Makalla naye ametoa maelezo mengi, tutamjibu. Ameainisha kero zake nyingi sana za Mvomero, najua siku nyingi sana Mheshimiwa Makalla amefuatilia sana kero zinazomgusa kule Mvomero mpaka wakati mwingine tunamwona anapanda na pikipiki anakwenda kuzifukuzia hizo. Nitamjibu mdogo wangu ili angalau wananchi wajue kwamba anafuatili.

Mheshimiwa Rajab umetoa ushauri na ninataka nikuhakikishie kwamba ushauri wako ulioutoa, Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI, itaweka utaratibu wa kushughulikia mikataba ya uwekezaji katika nchi nzima. Unajua ulichokisema na sisi tumeafiki.

Kwa hiyo, tutaweka utaratibu. Halafu pia umezungumzia habari ya fidia inayolipwa kwa wananchi wa Katosho. Tumesema tulishasikia, hata mimi watu wananiitea simu nyingi sana. Tunapeleka timu ya wathamini kwenda kujua kilichotokea ni nini Katosho. Wenyewe Kigoma wananiandikia sana. Lakini eneo hili la Katosho limetengwa kwa ajili ya Bandari Kavuu, ila masuala ya fidia tutatuma watu wetu waende wakaangalie yanavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ritta Kabati umetoa ushauri kwamba Halmashauri zipewe wataalam. Ni kweli hatuna wataalam wa kutosha, lakini kama unazungumzia Mjini Iringa, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa nimeshasaini ile GN. Nilikuja pale, nafikiri mliokuwepo mnakumbuka, nafikiri hata Mheshimiwa Mchungaji Msigwa alikuwepo. Nimeshasaini GN ya kuwaruhusu watengeneze *Master Plan* mpya ya Manispaa ya Iringa.

Kwa hiyo, hiyo *Master Plan* sasa wajidai wenyewe kuangalia Iringa ya miaka kumi ijayo wanataka iende namna gani. Sisi Wizara tutatuma washauri tu wa kuwashauri, lakini wenye kuamua Iringa wanayoitaka, itakuwa ni watu wa Iringa wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingi umetolewa na Mheshimiwa Rebecca na Mheshimiwa Naomi. Nataka niseme tu kwamba ushauri wenu mbalimbali mlioutoa tumeuchukua na tutaufanyia kazi. Mheshimiwa Clara Mwituka vile vile umetoa ushauri wako tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa, nakushukuru sana kwa pongezi zako, lakini pia kwa kusisitiza haki za wanawake ambazo tunaamini kwamba zipo kikatiba. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Betty Machangu ametoa ushauri mwingi sana. Nakuunga mkono katika mambo mengi uliyosema Mheshimiwa Betty Machangu. Nataka nikuhakikishie kwamba ushauri mwingi ambao umeutoa katika maandishi yako yaliyo mengi, maana wewe hukusema, tutayafanyia kazi, tunayo. Najua umetoa kwa sababu ya uzoefu, umefanya kazi kwenye *field*, haya mambo yote unayajua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, ushauri wako tutauchukulia maanani kama ulivyoshauri; lakini pia Mheshimiwa Herbert Mtangi nilishasema yako mambo *specific* ya kule kwako tutakuja kufanya, lakini yale mengine ya ushauri tutayachukulia maanani katika kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, pia narudia, Mheshimiwa Shekifu tunajitahidi kutekeleza ushauri uliotupatia kama nilivyosema. Najua iko hamu kubwa ya kuhakikisha kwamba yale mashamba ambayo Rais ameonesha nia ya kuyafuta na ameyafuta, yaweze kupangwa na kutumika na wananchi, tutafanya hilo. Wewe ndio Mzee wa Tanga, lazima tuharakishe ili usije ukaulizwa keshokutwa juu ya meza ukipanda pale, ahadi zako umefanya nini. Kwa hiyo, tutashirikiana kuhakikisha kero hizo tunaziondoa.

Mheshimiwa Laizer nimeshasema. Mheshimiwa Ndugulile umezungumza juu ya vibao vile, tutaelekezana baadaye, lakini eneo lile ni la Serikali, lilikuwa la *TIPPER*. Unakumbuka lile ndilo lililowafukuza Wakurugenzi fulani kazi.

Sasa tumelihalalisha, tumelipima pale ili kuzuia upoteaji wa rasilimali kwa wakati ule, kwa sababu wakati ule lilishakuwa limeondolewa, limeshauzwa, ni mali ya Serikali kwa sababu hii ni mali ya TIPPER. Kwa hiyo, baadhi ya maeneo tumewapa TIPPER wenyewe na mengine tumewapa TAZAMA na maeneo mengine tume-reserve kwa ajili ya wananchi. Kilichobaki sasa ni kwenda kuangalia wananchi wanaoishi pale ili tuelewane nao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rachel, mwanangu Mashishanga ametoa ushauri mwingi naye, ametoa maoni yake juu ya maeneo mbalimbali ya Kizumbi, Nyahenda, nimeyasikia. Naomba tu unipe nafasi kwa sababu mkeka huu ni mkubwa, mimi nitakuandikia majibu haya kwa Serikali, lakini tumefurahi na tumesikia ushauri wako. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ujumla naomba nirudie tena kuwashukuru wote waliosema maneno mengi hapa. Naomba tu niseme kwamba jambo moja sijalijibu kwa sababu bado halijanijia kichwani vizuri. Yamezungumzwa mengi juu ya Mheshimiwa Gama hapa, RC wa Kilimanjaro. Sasa kichwa changu hakiamini kama mambo yale yanaweza kufanyika. Hakiamini bado. Kwa tabia, huwa sijitumbukizi kwenye jambo ambalo siamini. Sasa na Askofu wa Rombo niliona anashangilia sana. Mzee, naomba mnipe muda tuyachunguze haya mambo, tuyafanyie kazi ili tusije tukamwonea mtu.

MBUNGE FULANI: Bunge linakwisha!

WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Hapana, Bunge haliishi kwa sababu haya maneno hamkufanya kwa sababu ya Bunge, ni kwa sababu ya wananchi. Wananchi hawaishi, tunaisha sisi tu. Ninyi msifanye hapa kwa sababu ya kura zenu, tunafanya kwa ajili ya wananchi. Wananchi wapo! Bunge hata kama linaisha, lakini kazi hii tutaifuatilia ili tuone kwamba haya yaliyosemwa dhidi ya Gama ni kweli? Kweli haya maneno yanaweza yakafanyika na kiongozi kama yule? Kama kweli yamefanyika, basi sisi tutayarekebisha. Kwa sababu unajua sisi kwenye Wizara ya Ardhi yaliyo mengi yanafanywa kwa mujibu wa sheria, siyo kwa utashi wa mtu yeyote. Kwa hiyo, kama kweli kuna mtu amefanya kinyume cha sheria, jibu lipo tu.

Kwa hiyo, naomba Mzee wa Rombo, tumesikia maneno yako, lakini niacheneni nipate muda kidogo na mwenzangu wa TAMISEMI yupo hapa, Mheshimiwa Waziri. Tutayafanyika kazi, tunayafuatilia ili tujue ukweli uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kebwe, Mbunge wa Serengeti ameeleza mengi sana. Mzee wa Serengeti nimekusikia, najua umeeleza vitu vingi sana ambavyo una uchungu na Serengeti.

Sasa mimi na wewe tutakaa nitakupa haya majibu na kama ikibidi una mashaka, naweza nikatuma hata mtu wangu aje mpaka Serengeti ili tufuatilie haya uliyoyasema kwa maslahi ya Wilaya yetu ya Serengeti. Nataka kukwambia kwamba ushauri wako na mashaka haya tutashirikiana ili kuhakikisha kwamba yanaondolewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa kuwa kengele nyingine inakuja nataka nirudie kumshukuru sana Mheshimiwa Angela Kairuki kwa sababu maeneo mengi ameyagusa gusa hapa. Kama ilivyo ada, isingekuwa rahisi kujibu maneno yote lakini majibu tunayo, lakini tutajitahidi yale ambayo yatasaidia Bunge na yatamsaidia Mbunge mmoja mmoja, tutamwandikia ili angalau apate ushahidi huko walikomtuma aweze kuwasomea majibu yetu yaweze kumsaidia yeye na wananchi waliomtuma.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, hata yale ya Tondoroni ninayo, lakini tutawajibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIB NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono, Katibu!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt ... Shs. 9,529,648,283/=*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimwa Barwany!

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja yangu hapa ni kwamba, kwa muda mrefu ndani ya Bunge hili tulikuwa tunazungumzia suala zima la mashamba pori ambayo kwa muda mrefu yametelekezwa katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi yetu, lakini kauli ya Serikali mara zote ni kwamba hati hizo zitafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara, maeneo yote yenye rutuba na ardhi nzuri ambayo ingewasaidia wananchi katika kilimo chao, wakati ule wa Serikali za Kikoloni maeneo yale yalitwaliwa kwa mujibu wa sera ya uwekezaji wa wakati ule, lakini bado wananchi wana hitaji kubwa la ardhi na mpaka sasa bado ardhi hiyo haijarejeshwa kwa wananchi. Kauli ya Serikali kupitia Mheshimiwa Rais alishasema kwamba hati zote kwa mashamba yale ambayo yametelekezwa zitarejeshwa ili wananchi waweze kupatiwa.

Katika kipindi chako cha miezi sita Mheshimiwa Waziri tulitegemea kelele na vilio vya wananchi wa Mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara ungekuja kuangalia hali halisi ya maeneo yale ili Serikali ikatekeleza agizo lake, lakini bado mashamba yale ya Mkwaya, Kitunda na maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Lindi bado yametelekezwa na mashamba pori na inafikia mahali wenye ardhi ile ambao wamewekeza, wanatumia mashamba yale kuchukulia mikopo benki na kufanya miradi mingine zaidi ya kuendeleza maeneo yale kiasi kwamba mahitaji ya wananchi yamebaki pale pale.

Hivyo, naomba kauli ya Serikali. Sina haja ya kuchukua mshahara wako Mheshimiwa Waziri, nataka kauli ya Serikali sasa kabla hujaondoka katika nafasi ya miezi minne iliyobakia. Serikali inatoa tamko gani juu ya mashamba pori ambayo hayajarejeshwa kwa wananchi mpaka sasa? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, maelezo!

WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumechukua hatua na tutaendelea kuchukua hatua kwa mashamba pori, pamoja na mashamba mengi ambayo yametelekezwa. Mwezi uliopita nimekaa Arusha siku kumi, nimeshughulikia na ndiyo maana tumeweza kupata ekari 7,000 kwa mashamba kama tisa ya wawekezaji yaliyofutwa kama unayoyasema wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefuta shamba 304, 305 na tumepata ekari 4,000 ambazo tunawapa *ArushaDC*; lakini tumefuta mashamba mengine zaidi ya ekari 900 kwenye eneo la Arumeru; na shamba maarufu sana watu wa Arumeru wanalijua 371. Ingawa halijafutwa, lakini mwekezaji tumeelewana ametupa na ekari nyingine 100 katika shamba lililobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shamba lingine la mwekezaji ambalo halijafutwa vile vile lakini wananchi wana shida. Nimebanana naye mpaka amenipa ekari 696 ili niwape wananchi wale watu 35 ambao walikuwa ndani kwenye shamba lake. *(Makofi)*

Sasa utaratibu ni huu Mheshimiwa Bwana Barwany, kwamba mashamba yale hayamilikiwi na Serikali kwa maana ya Wizara, mashamba haya kwa sheria zote za ardhi yako chini ya himaya ya Halmashauri.

Kwa hiyo, wa kwanza kuonyesha nia ya kufuta, ni lazima iwe Halmashauri yenyewe. Kama ulivyoona Malonje, Halmashauri imeshatoa *notice* ya siku 90. Kwa hiyo, nataka unisaidie kwa Mkwaya na Kitunda, Halmashauri mlishachukua hatua hiyo ya kutoa *notice*? Usiseme tu yalikuwa ya kikoloni, lakini yana hati. Kama wameshawahi kuchukua hatua, nijulishe hata kesho, au kama wana-*copynotice* ilishafikia ukomo, imekuja Wizarani, nitachukua hatua kabla sijaondoka, lakini utaratibu unaanza kwenye Halmashauri, hatuanzii juu. Mashamba ya Kibaha 16 wameleta mwezi uliopita, tumefuta. Shamba la Mafia tulizungumza Bunge lililopita limeshafutwa, lakini watu wa Mafya wametimiza masharti.

Kwa hiyo, kama Mkwaya na Kitunda sina kumbukumbu nzuri. Lakini tushirikiane na wewe, hebu waulize watu wa *Lindi status* ya hili jambo. Kama kweli walishatoa *notice* na wakaonyesha nia ya kuyafuta haya mashamba wakaleta kwetu, tutashughulikia haraka iwekanavyo, lakini utaratibu ni lazima uanzie kwenye Halmashauri. Sijui kama nimekujibu vizuri.

MWENYEKITI: Umemjibu vizuri. Mheshimiwa Diana Chilolo!

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutambua mchango wangu na amekiri kwamba atanjibu kwa maandishi. Hata hivyo, nina hoja moja tu ambayo ninahitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi ya wafugaji na wakulima inatokea Tanzania kwa sababu ya kugombea ardhi. Mkoa wa Singida kwa kutambua hilo walipokea mapendekezo kupitia Halmashauri zote ikakubali kabisa kwamba vijiji 37 maeneo yapimwe kwa ajili ya wafugaji pamoja na malisho, lakini zoezi hilo mpaka sasa hivi halijafanyika kwa sababu ya Halmashauri zote kutokuwa na fedha, vifaa na uhaba wa watumishi. Niliona nipate ufafanuzi kwa ajili ya wafugaji wanaonisikiliza pamoja na Uongozi mzima wa Mkoa wa Singida. Kupitia Bajeti hii, Serikali imejipanga vipi kusaidia Mkoa wa Singida kuweza kupima maeneo haya niliyoyataja?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye Bajeti mwaka huu, tuna vijiji 200 tutavipima. Tutaangalia uwezekano wa vijiji vya Singida kuwemo katika orodha hiyo ya vijiji 200, lakini kwenye maelezo kwenye hotuba yangu nimetoa suluhisho, kwamba tunaanzisha Vikosi vya Upimaji kwenye Kanda; na Kanda yako wewe ni Tabora...

MWENYEKITI: Naomba *microphone*...

WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Tutaangalia wapimaji waliopo kwenye Kanda ile ili waweze kutumika ingawa wataendelea kuwa watumishi wa Halmashauri, lakini waweze kutumika kikanda kwa sababu sisi tutanunua vifaa tutaweka kwenye Kanda. Vilevile mjue kwamba hii kazi ya upimaji wa vijiji sio kubwa kiasi hicho. Ni Shilingi milioni sita tu. Halmashauri yoyote ambayo ina Shilingi milioni sita leo, sisi kesho tunakwenda na vifaa vyetu vyote, tunawawekea mpango wa matumizi ya ardhi Kijiji kizima. Siyo fedha nyingi sana, Shilingi milioni sita. Hata wananchi wenyewe ndani ya kijiji wanaweza wakashirikishwa wakachanga Shilingi milioni sita, sisi tukawapelekea wataalamu kwa posho zetu na vifaa vyetu tukafanya hivyo mpaka tukawapa na makaratasi yote.

Kwa hiyo, ipo njia. Mkiwa na haraka sana, toeni Shilingi milioni sita tuje, vinginevyo msubiri mpaka bajeti hii ambayo ukisoma kuna vijiji 200 ambavyo *inshaallah* tukipata bajeti, tutakufikiria na wewe Singida. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kitandula!

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilizungumzia juu ya mgogoro wa Segoma; umiliki wa msitu ule kwa Kijiji ambapo Baraza la Madiwani liliridhia kwamba msitu ule umilikiwe na Kijiji, lakini hapa katikati kumekuwa na sintofahamu ya maamuzi mengine kutoka Mkoani kwamba zoezi lile lisitishwe na zoezi hili linasitishwa bila kufuata utaratibu.

Sasa nafahamu nia njema ya Wizara katika kutatua tatizo hili, lakini ninachoomba tu ni kauli ya Wizara kwamba ni lini Waziri atakuja Mkinga twende Segoma ili tuondoe kero hii ambayo inawafanya wananchi wajisikie wanyonge kwa kupoteza haki yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru!

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Kitandula kwa kufuatilia suala la eneo la Sigi Segoma Wilaya ya Mkinga; na wananchi wake walishakuja na tulishafanya kikao na Wizara na kwa kweli inashangaza. Ukiangalia barua ya Halmashauri ya Wilaya ilikuwa ni bayana kabisa kwamba Kijiji cha Sigi Segoma kitoe gharama za kesi na baadaye wakabidhiwe eneo hilo. Lakini baadaye cha kushangaza mambo yamekuwa siyo na kumekuwa na kutishiana maisha katika Wilaya hiyo.

Napenda kumwarifu kwamba tayari Mheshimiwa Waziri amenielekeza nifike huko na tutapanga na Mheshimiwa Mbunge kuona ni lini tutakwenda kulitatua suala hilo maana yake ni lazima lirudi kwa wananchi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mrema!

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Waziri ni kuhusu shamba la Lokolova, Mheshimiwa Rais alipoomba...

MWENYEKITI: Sasa unaongea na nani? Mimi au Waziri?

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Naomba niongee na wewe!

SPIKA: *Okay! (Kicheko)*

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Rais alipokubaliana na wazo la kujenga Soko la Kimataifa Himo Lokolova, wale wanaushirika ambao waliunda ushirika wao kwa ajili ya ufugaji na kilimo, walikubali kwa moyo mweupe kutoa ekari 140 kwa ajili ya kuanzisha hilo soko. Baada ya kutoa eneo hilo, Uongozi wa Mkoa ukaenda ukafuta ule ushirika na ili waweze kumiliki ekari 2,600 za wanakijiji, imetuletea mgogoro mkubwa sana baada ya ushirika ule kufutwa tumekwenda kwa Rais, tumekwenda kwa Waziri Mkuu; namshukuru sana Waziri Mkuu hayupo hapa; nami sijui kwa nini hajachukua fomu ya Urais. Aliagiza ushirika ule urejeshwe.

Sasa Mkoa ulikwishajipanga na watu wao kuunda kampuni; eti wenye ardhi ni watu wa Lokolova, wao waunde kampuni ya kuendesha Lokolova. Wakaenda China, wamejipanga, Mbunge mwenyewe wala hana taarifa, wamekuja na watu wao. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa wananchi wanachosema, ile kazi nzuri Mheshimiwa Waziri uliofanya Kigamboni, ardhi ile umerejesha kwa wananchi wamiliki ile ardhi, wanunue hisa kwenye kampuni yoyote wanayotaka, kama ni kujenga waelewane na kama ni kuuza waelewane, lakini siyo Mkoa kujichukulia madaraka ya kuendesha huo Ushirika wa Lokolova kama wanavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Himo na watu wa Lokolova wanasema wapo tayari kushirikiana na Serikali, kama walivyotoa kwa ajili ya Soko la Kimataifa, wako tayari kuwa na hisa kwenye huo mji wa kisasa, lakini wanachotaka, wana vijana wao wa Chuo Kikuu wameshaandika *write-up* nzuri sana. Wanachotaka, ile biashara wafanye wao, siyo wafanyiwe na wajanja wa Mkoani Moshi wakiongozwa na Gama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nauliza kama Mheshimiwa Waziri yuko tayari, kazi nzuri takatifu ya Mungu aliyoifanya Kigamboni na yenyewe iende mpaka Lokolova Himo. Huo ndiyo ufafanuzi ninaouomba tu!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, maelezo!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la Lokolova wanaushirika hawa, wao wenyewe waliridhia kutoa kipande hicho kwa ajili ya kujenga Soko la Kimataifa.

Halmashauri ilichokuwa inakifanya au kupitia Wizara yetu ilikuwa ni suala la umilikishaji tu na tayari tumeshaandaa mchoro wa Mipango Miji, lakini pia upimaji na umilikishaji utafanyika tu baada ya wahusika hawa kuelewana. Maana baada ya eneo hili kugaiwa sasa kwa Halmashauri ili kuweka Soko la Kimataifa, baadaye ushirika huu na wenyewe pia ulionekana unataka kuwa ni wamiliki wa soko hili.

Kwa hiyo, tunaomba sana wao wenyewe wamalizane huko ili tuweze kukamilisha suala zima la umilikishaji kwamba ni ushirika au ni Halmashauri, lakini kwa upande wetu, sisi tumeshaandaa michoro ya Mipango Miji na tupo tayari wakati wowote kulimilikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ester Bulaya!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Wakati nikichangia kwa maandishi na kama ambavyo pia kwenye taarifa yetu ya Kamati imeonyesha, tumezungumzia kwa kina kuhusiana na Serikali kuchelewa kubomoa jengo ambalo lilileta maafa miaka miwili iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kulisisitiza hili kwa sababu agizo hili lilikuwa la muda mrefu na limekwenda likisuasua, lakini eneo lile bado wananchi wanaishi kwa hofu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu peke yake, kuendelea kuwepo kwa jengo lile kunafanya watu wengine au Halmashauri nyingine zisizingatie kutoa vibali vya ujenzi kwa mujibu wa sheria na yapo majengo mengi sana ambayo yanaendelea kujengwa kwa sababu tu kuona kuna jengo limejengwa, tumezungumzia kwamba linapaswa kubomolewa lakini bado mpaka sasa hivi halijabomolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri, amesema watashirikiana na Wizara iliyokuwa kwa Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwa maana ya Halmashauri. Tunachohitaji ni kwamba lazima kuwe na *time frame*. Umesema mtabomoa hivi karibuni. Hivi karibuni inaweza kuwa miezi mitatu ijayo, miezi sita ijayo na kadhalika.

Ninachohitaji Mheshimiwa Lukuvi, ni *commitment* ya Serikali hapa. Ni mpaka muda gani jengo hili litakuwa limebomolewa? Maana tunakwenda kumaliza uhai wa Bunge na hii ni takriban miaka miwili Kamati tumekuwa tukisisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya, kuna Misikiti pale, kuna Madrasa na Hospitali. Mpaka ile Hospitali sasa hivi wameamua kuondoka kwa sababu tu ya hofu kwa jengo ambalo limebaki. Kwa hiyo, naomba *commitment* ya Serikali mpaka kufikia lini mtakuwa mmebomoa siyo tu hivyo ilivyokuwa *vague* kwamba hivi karibuni.

MWENYEKITI: Haya. Mnapompongeza mmwite Lukuvi. Mnapozungumzia kazi yake, mwiteni Waziri wa Ardhi. Ndiyo kanuni. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nafikiri Mheshimiwa Ester anajua jambo lenyewe lilikuwa Mahakamani. Nakumbuka kuna watu walishtakiwa kwa kuua kwa kutokukusudia na watu wengi hata wataalam wa Manispaa pale wameshtakiwa na kadhalika. Baada ya mambo yote hayo kwisha sasa, Mheshimiwa Ester atakumbuka kwamba tulipokaa hapa kwenye Kamati wiki mbili zilizopita ndipo nikaahidi kwamba nitalisimamia na kuhakikisha haya yanafanyika.

Mheshimiwa Spika, haya yote niliyoyasema, nimeyafanya kwa kipindi cha wiki mbili; kutafuta *contractor*, kutafuta pesa na kusaini mkataba. Kwa hiyo, mkataba wa mbomoaji tumeshausaini, pesa tutalipa sisi, lakini mjue kwa usimamizi hasa, wanaopaswa kusimamia ubora wa majengo katika miji ya ujenzi, siyo Wizara ya Ardhi, ni Manispaa. Kwa hiyo, Manispaa ndiyo wanaotoa *demolition order* ya kuvunja na ndiyo watakaosimamia uvunjaji. Sasa tunashirikiana tu kwa sababu kiwanja chenyewe ni cha *National Housing*, ndiyo maana na sisi tunatoa pesa ili kuharakisha hilo kwa sababu likibaki lile jengo bovu, kile kiwanja chetu hakina maana. Bora livunjwe ili kiwanja chetu kibaki, tuingie na mbia mwingine.

Kwa hiyo, sisi Wizara ya Ardhi tunaingia tu kwa sababu ya mgongo wa *National Housing*, otherwise Wizara ya Ardhi tungekuwa hatuna chetu, kwa sababu wanaopaswa kusimamia ubora wa majengo ni Halmashauri za Miji.

Kwa hiyo, Ilala wameshatekeleza wajibu wao kwani wameshatoa kibali, sisi tumeshatafuta *contractor*, lakini huyo *contractor* katuambia. Maana mwanzo tulitafuta taasisi zote za ndani ikashindikana, hakuna hata mmoja mwenye uwezo wa kufanya kazi hiyo. Kampuni hii ya *CRJE* ndiyo imekubali kubeba huo mzigo na gharama zake tunalipa sisi, nimewaambia Shilingi bilioni moja; na hivi sasa na wenyewe kwa sababu jambo hili hawajalifanya kuvunja maghorofa kumi na ngapi yale, wameagiza hicho kifaa na wataalam wengine *extra* waje kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Ester, mkataba tumeshasaini na pesa tayari; na mmeniagiza wiki mbili zilizopita. Sasa haya niliyoyafanya katika wiki mbili, kwanza ungeshukuru tena kwamba angalau una masikio umesikia, lakini sisi tusingeweza kusaini mkataba na kulipa pesa kama jambo halifanyiki.

Kwa hiyo, ndiyo maana nimesema katika muda mfupi ujao, jambo hili litatekelezwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam tumeshazungumza naye na wenzetu wa Shia pale jirani wenye Msikiti tumeshazungumza nao. Akisharudi yule Mchina na vifaa tutawaarifu wenzetu na *RC* amesema hata barabara atafunga, wale majirani kumbe wameshakubali kuondoka kwenda kuhamia mahali pengine ili tufanye ubomoaji.

Kwa hiyo, sina tarehe kama anafikiri ni tarehe, lakini nataka kukuhakikishia kwamba ni hivi karibuni kwa sababu hata sisi tungekuwa ni watu wa ajabu *kuji-commit* Shilingi bilioni moja na kulipa kwa kazi ambayo tunafikiri haitafanyika. Kwa hiyo, tumeshaamua tutafanya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika hotuba ya Kambi ya Upinzani, tulihoji juu ya gharama za uendelezaji wa Jiji la Mwanza na Arusha.

MBUNGE FULANI: *(Aliongea nje ya microphone)*

MHE. HALIMA J. MDEE: Mh!Hii ndiyo sauti ya zege wewe ichukulie hivyo hivyo tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulihoji juu ya gharama ambazo amelipwa mtaalam mwelekezi kwa *Master Plan* za Arusha na Mwanza na nilijibiwa kidogo kwa mbwembwe. Arusha Shilingi bilioni 9.8 na Mwanza Shilingi bilioni 8.8. Ni fedha tu za mtaalam mshauri ama *consultant*. Nafahamu vilevile kwamba kwa Dar es Salaam kulikuwa na kitu kama hicho kilichofanyika, lakini kilifanyika kwa Shilingi bilioni 3.6.

Sasa nataka Mheshimiwa Waziri anisaidie, hatutafutani uchawi, tunajenga nyumba moja; kwa hiyo, tunatakiwa tukijibiana, tujibiane tu Kitaifa. Ni utaratibu gani ambao ulitumika kumpata huyu mtaalam mwelekezi wa sasa na kama walishindanishwa na walishindanishwa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu. Sitaki hata kuchukua Shilingi ya mtu, nataka tu anipe majibu kwa sababu kuna miji mitatu; Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Tunajua sasa hivi kwenye randama mmetenga Shilingi bilioni 13 kwa ajili ya kumlipa Mtaalam Mshauri kwa hayo maeneo mawili. Kwa hiyo, nataka nipate hiyo taarifa kama kulikuwa na ushindani ili twende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu!

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri! Mnasubiri nini?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Maana Mheshimiwa Halima hapa anataka ulaji, sasa lazima tuwe na uhakika kama kuna ulaji au hakuna. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba ile gharama ya *Master Plan* ya Dar es Salaam ilikuwa zaidi ya hii, *of course* tulisaidiwa kidogo, lakini gharama za *Master Plan* ya Arusha na Mwanza tunazitoa sisi Wizara ya Ardhi kutokana na umuhimu wa kupanga Mji wa Arusha na Mwanza. Ni kweli kwamba tuna mshauri mwelekezi kampuni moja ya Subana ya Singapore na mnaojua Subana ni miongoni mwa mabingwa wa upangaji wa miji yao kama walivyofanya Singapore.

Kwa hiyo, tuliwachukua hawa kwa sheria na PPRA waliridhia tuchukue *under singlesourcing*, tuliwachukua wao kutokana na uzoefu waliokuwa nao baada ya kushirikiana ndani ya Serikali tuliruhusiwa tuwachukue hawa. Ingawa ni mtaalamu mwelekezi Subana, lakini asilimia 90 ya wataalamu ambao amewaajiri, anawalipa pesa hizi, ni Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Arusha utamkuta huyo Subana ni mmoja; ukienda Mwanza unaweza kumkuta mmoja au wawili lakini ame-*pool* wataalamu kama 40 hivi Watanzania ambao ndio anawalipa kutokana na hizi fedha. Sisi hatutoi fedha nyingine. Kama ni gharama za posho za kila siku, analipa mwenyewe Subana kutokana na kazi yake ya *consultancy*.

Kwa hiyo, hawa wanatengeneza hiyo *concept plan*, watakamilisha kama *lead consultant* lakini kama nilivyosema, kiasi kikubwa cha wasaidizi wao, ni wa ndani. Kwa hiyo, hizi fedha wanazozipata siyo kwamba anazihamisha, ila anazitumia pamoja na Watanzania waliopo kufanya hii kazi.

Kwa hiyo, tulitumia *single sourcing* lakini ilikubaliwa na PPRA na ndani ya Serikali tulikubaliana kwamba tufanye hivyo kwa nia njema ya kufanya jambo hili. Nami mwenyewe nimekwenda Arusha nikagundua kwamba baadhi ya mambo yalikuwa hayajakaa vizuri kwa sababu Waheshimiwa Madiwani pamoja na kwamba walikuwa na hamu sana ya kuanza lile jambo kwa kasi, wakaanza bila hata kupitisha kwenye *Council*, hata walikuwa hawa fedha, nikatoa fedha zangu wakapitisha kwenye *Council*. Nikatangaza kwenye *GN*.

Kwa hiyo, mambo yote yapo kisheria na yanaendelea vizuri. Nawashukuru sana Madiwani wa Arusha Jiji, *ArushaDC* na Meru ambao wamekubali kutoa hata maeneo yao pembeni ili yawekewe pamoja kwenye mpango wa Jiji na viongozi wa Mwanza Jiji wanasaidia sana. Wako so *supportive* kwa sababu ndiyo wametupa ofisi pale ingawa tuna mpango wa kutoka nje pale Arusha kwa sababu nafasi ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukwambia kwamba hizi fedha ingawa anaonekana mgeni ndiye anayepewa, lakini kikubwa ndiyo zinatumika na Watanzania wote katika kukamilisha hii kazi na utaratibu tulioupata ndiyo huu ambao kwa kweli hauna mgogoro ndani ya Serikali, unatumika mahali pengi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Medeye!

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa fursa hii. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi niliandikisha jina kwamba ningechangia wakati wa mshahara wa Mheshimiwa Waziri lakini tumeshazungumza na Mheshimiwa Waziri, tumekubaliana kwamba tukutane mezani tumalize mgogoro ambao tulitaka kuujadili hapa lakini namheshimu sana na tumekubaliana hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* Shs. 9,714,282,624/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 - *Policy and Planning* Shs. 1,167,264,883/=

MWENYEKITI: Unaposimama, unamwangalia na Spika ajue kama unamtaka. Haya, Mheshimiwa Ester Bulaya!

MHE. ESTER A. BULAYA: Najua unanijua, umesahau tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi katika *subvote 1003* kasma ya 220700 - *Rental Expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mwaka juu ilikuwa Shilingi milioni 33, mwaka 2014 Shilingi milioni 17, mwaka huu ime-shoot tena mpaka Shilingi milioni 32. Tunataka kujua kwa nini ongezeko limekuwa kubwa kuzidi mwaka 2013 wakati mwaka 2014 lilipungua?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Esther Bulaya kuhusiana na ongezeko hili kwenye kasma ya *Rental Expenses*.

Kwanza kabisa, Idara hii ya Mipango ndiyo itakayokuwa ikiratibu suala zima la maandalizi ya sera ya nyumba, lakini vilevile suala zima la maandalizi ya *Real Estate Regulatory Authority Regulation and Development Act* pamoja na masuala mengine. Kwa hiyo, fedha hii ukiangalia kwanza gharama za kukodi kumbi mbalimbali za mikutano kidogo imeongezekana na tutahitajika kuita wadau mbalimbali katika kujadili maandalizi ya sera hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 – Mgnt Information System... ..Shs. 751,255, 282/=

Kif. 1005 – Internal Audit Unit Shs. 845,745,032/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo, anza.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko katika kifungu kidogo cha 221000 – Travel-in-country. Nataka maelezo kidogo, ni kwa nini kifungu hiki ambacho kiko Internal Audit kimeendelea ku-shoot kwa hali ya juu sana kutoka Shilingi milioni 138 mwaka 2014 mpaka Shilingi milioni 304? Naomba maelezo hasa ukizingatia ni Kitengo cha Ukaguzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, hawa Wakaguzi watakuwa wakienda kukagua kodi mbalimbali za ardhi na imeongezeka kwasababu tumeongeza vituo mbalimbali vipya vya makusanyo, lakini pia vilevile kama ambavyo umeona katika maeneo mbalimbali ya ukaguzi, lakini viwango vya posho kwa mwaka huu wa fedha vimeongezeka across Serikali nzima.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rajab Mbarouk!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko katika item 230400 - Routine Maintenance Repair of Vehicle and Transport Equipment. Tumeona hapa, mwaka 2014 mlikuwa na Shilingi milioni 20,500 na sasa hivi ni Shilingi milioni 28 kamili; na nimepitia Randama nikaona kwamba matengenezo haya ya gari ni gari moja tu ambalo ni la Idara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua, gari hili moja ambalo ni la idara mwaka 2014 limetengenezwa kwa Shilingi milioni 20 na mwaka huu linatengenezwa kwa Shilingi milioni 28. Naomba kupata maelezo.

NAIBU WAZIRI WA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza gharama za matengenezo zimepanda...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, mpaka uitwe!

NAIBU WAZIRI WA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Samahani Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwanza kabisa, ukiangalia gharama za matengenezo zimepanda, lakini vilevile gari hili limechoka sana, kwa hiyo, vipuri vyake kidogo vitakuwa ni gharama. Naomba aridhie hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bulaya, yaani liko moja tu?

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, napenda kupata ufafanuzi katika kasma 221100 - Travel Out of Country, tumeona ime-shoot kutoka Shilingi milioni 26 mpaka Shilingi milioni 51.

MWENYEKITI: Ehee, umeiona? Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Bulaya. Gharama hizi zimeongezeka. Ukiangalia katika mwaka huu wa Fedha tunatarajia kupeleka watumishi watatu wa kitengo hiki cha ukaguzi nje ya nchi kupata mafunzo mbalimbali lakini vile vile iko mikutano mbalimbali ya Uanachama kuhusiana na Ukaguzi.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiiko yoyote)

Kif. 1006 – Procurement Mgnt Shs. 639852,450/=
Kif. 1007 – Government Comm. Unit... .. Shs. 430,860,789/=
Kif. 1008 – Legal Services Unit Shs. 498,704,205/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiiko yoyote)

Kif. 2001 - Land Admin. Division... .. Shs. 3,636,242,719/=

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa nia njema tu, nilikuwa nataka kupata maelezo ya ufafanuzi; kwenye Kasma 229900 - Other Operating Expenses imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 100 kutoka Shilingi milioni 10 mpaka Shilingi milioni 21. Tatizo ni nini hapa?

SPIKA: Kwani ni tatizo? Ni kitu gani. Siyo lazima iwe ni tatizo. Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Bulaya. Katika milioni hizi 21.9 zitatumika kulipia gharama za mshauri mwelekezi atakayeandaa Land Office Operational Manual Shilingi milioni 6.9 lakini pia vilevile Shilingi milioni 15 zimetengwa kwa ajili ya gharama ya mazishi endapo kuna mtumishi atafariki.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 – Survey and Mapping Div.Shs. 5,764,328,205/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan! Haiwaki?

MHE. SUZAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, inawaka ila ulikuwa hujanitaja jina, usije ukanishushua.

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Susan Kiwanga! (Kicheko)

MHE. SUZAN L. A. KIWANGA: Ahsante. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa kifungu cha 220700 - Rental Expenses. Nimeona katika bajeti mbili mfululizo kwanza ilikuwa ni milioni 14, ikaja milioni 65 lakini sasa hivi wanaomba milioni 240. Kwa nini ongezeko limekuwa kubwa? Ukiangalia bajeti nzima, karibu bilioni ni upangaji. Kwa nini msijenge?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Kiwanga kwamba gharama hizi zimeongezeka kwanza kwa ajili ya kumbi mbalimbali za mikutano, lakini pili kama unavyofahamu, Idara yetu ya Ramani iko pale pembeni ya Wizara ya Ardhi. Pia tunatarajia watahamia katika jengo la National Housing.

Kwa hiyo, gharama kidogo zitapanda ili kuweza kufanya marekebisho. Mikakati tuliyonayo ni kwamba tutashirikiana na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kujenga jengo la ramani karibu na pale lilipo sasa hivi la Mapping Section

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rukia!

MHE. RUKIA KASSM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika kifungu kidogo cha 220800 - Training Domestic. Hiki kifungu kinaonekana kwenye mwaka 2014/2015 kulikuwa kuna Shilingi milioni 95, lakini ime-shoot kutoka Shilingi milioni 95 mpaka Shilingi milioni miaka 118. Naomba ufafanuzi.

NAIBU WAZIRI WA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Kassim kama ifuatavyo:

kwanza, ukiangalia katika hoja hii kifungu kimepanda kwa sababu gharama za mafunzo especially gharama za kujikimu na posho mbalimbali zimepanda.

Pili, tunatarajia kupeleka watumishi wengi zaidi kutoka katika Idara hii ya Upimaji na Ramani takriban watumishi 19 katika ngazi ya degree, ngazi ya Diploma katika Vyuu vyetu vya Tabora na Morogoro. Kwa hiyo, idadi imeongezeka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndugulile!

MHE. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza katika kifungu namba 229900 - *Other Operating Expenses*.

MWENYEKITI: Kimeshasemewa hicho.

MHE. FAUSTINE E. NDUGULILE: **Bado hakijasemewa.**

MWENYEKITI: **Hakijasemewa? Okay!**

MHE. FAUSTINE E. NDUGULILE: **Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza katika kifungu cha *Other Operating* kama nilivyosema awali 229900 katika Idara ya *Service and Mapping Division* ambayo inafanya kazi kubwa sana. Sasa nikiangalia katika kifungu hiki wametenga Shilingi milioni 73 na sasa hivi Wizara ina mipango mikubwa tu ya kutengeneza na *develop master plans* na upimaji pamoja Mji wa Kigamboni.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua: Je, kifungu hiki kinaweza kutosheleza kazi yote kubwa ambayo mnataka kuifanya nchi nzima?

NAIBU WAZIRI WA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Ndugulile kuhusiana na kifungu hiki cha 229900. Gharama hizi zimeongezeka kwanza tunatarajia kuweka Mshauri Mwelekezi atakayetusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kutokana na tengeo tulilolipata lakini vile vile uki-*compare* na mwaka 2014, tunatarajia gharama hizi ziwe hizo Shilingi milioni 73 kwa ajili ya kumgharamia Mshauri Mwelekezi ambaye ataandaa Sera ya Upimaji na ramani, lakini pia vilevile katika Kanda yetu mpya ya Mashariki tunatarajia kutumia gharama hizi kununua vifaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Eng. Mnyaa nilikuona.

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kupata ufafanuzi kidogo kuhusu kifungu 230300 cha *Routine Maintenance ya Waterand Electricity Installation*. Sasa sijui inawezekanaje ikiwa kifungu hiki hakijatengewa hata Shilingi moja toka mwaka 2014 na mwaka huu? Ni kwamba hakuna *routine maintenance* tena au vipi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, umekiona? Ni 230300.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama hizo za matengenezo zitagharamiwa na idara ya Utawala.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya, nilikuona? Hapana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamatiya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2003 – *Registration of Titles Unit* Shs.1,184,349,407/=

Kif. 2004 – *Valuation Unit*... .. Shs. 894,015,570/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rukia!

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika kifungu kidogo 210100 -*Basic Salary – Pensionable Post*. Hiki kifungu kinaonekana mwaka 2014/2015, kilikuwa na Shilingi milioni 392, lakini sasa hivi kuna Shilingi milioni 274. Nilitaka tu ufafanuzi kujua: Je, kuna wafanyakazi hapa wamepunguzwa au imekuwaje? Naona kimeshuka badala ya kuongezeka.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hiki kimepungua. Kwanza kuna watumishi watano wa Idara hii ya uthamini, wamestaafu. Vilevile Masekretari na watunza kumbukumbu watagharamiwa na Idara ya Utawala na ndiyo maana kuna punguzo hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Medeye!

MHE. GOODLUCKY J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kasma 220200 – *Utility, Supply And Services*, kwa mwaka huu kuna sifuri. Sasa nataka kujua kama ni *omission* au hawahitaji fedha kabisa kwa mwaka huu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wanakaa kwenye jengo moja, utawala ndiyo watakaogharamia gharama hizo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2005 – *Dar es Salaam Zone* Shs. 785,900,000/=
Kif. 2006 – *Eastern Zone* Shs. 841,260,000/=
Kif. 2007 – *Central Zone* Shs. 863,470,000/=
Kif. 2008 – *Western Zone* Shs. 936,350,000/=
Kif. 2009 – *Lake Zone* Shs. 1,120,540,000/=
Kif. 2010 – *Northern Zone*... .. Shs. 808,460,000/=
Kif. 2011 – *Southern Zone*... .. Shs. 601,260,000/=
Kif. 2012 – *Southern Highlands Zone* Shs. 986,010,000/=

(Vifungu vilivyochotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 – *Rural & Town Planning Div.* ... Shs. 20,311,012,244/=

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kifungu kidogo 22900 - *Other Operating Expenses*. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri alilijibia, nataka kujua, hii ni ile *master plan* ya Arusha na Mwanza. Ukiangalia hii *document* yao inaonyesha kwamba kila *stage* kunakuwa na malipo.

Sasa nataka kujua kwamba sasa hivi imeshalipwa kiasi gani na mgawanyo ukoje mpaka sasa hivi? Huyu Mwelekezi ameshalipwa kiasi gani, kwa sababu kuna *stages*, mmesema asilimia 15.

Sasa tunataka kujua mpaka sasa hivi atakuwa amelipwa kiasi gani? Kwa sababu mwaka 2014 kulikuwa kuna hili tengeo la Shilingi bilioni nne: Je, mpaka sasa hivi mmeshamlipa kiasi gani?

MWENYEKITI: Ndiyo tunafikiria Bajeti hii. Tuko kwenye Bajeti ya mwaka huu, siyo ya mwaka 2014. Siyo sahihi kwasababu *we are estimating*. Sasa mkikubali nyie, ndiyo hela. Mpaka tupitishie ile *vote* ndiyo itakubalika. Kwa hiyo, mpaka hii. Huwezi kusema katika hii imelipwa ngapi? Maana yake ni hii.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3002 – *Housing Division*... .. Shs. 2,912,220,097/=

Kif. 3003 – District Land & Housing Tribunal... Shs. 4,361,315,210/=

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kif. 1001 – Administration & HR Mgnt ... Shs.1,000,000,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rajabu!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka *clarification* tu ya hii Shilingi bilioni moja katika *item 6327 - Construction and Rehabilitation of Building*. Nimejaribu kuangalia, katika matumizi ya kawaida kuna zaidi ya Shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya matengenezo ya ofisi na ujenzi mdogo mdogo. Sasa hapa *still* katika miradi ya maendeleo kuna Shilingi bilioni moja. Naomba *clarification*, hizi hasa zinataka kutumika katika maeneo gani?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hoja ya Mheshimiwa Mbarouk. Hapa ni kwa ajili ya ujenzi wa maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora, Shilingi bilioni moja.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 – Land Administration Div. ... Shs. 3,858,996,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 – Surveys & Mapping Div. ... Shs. 7,100,000,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika *sub-vote 2324*. Utakumbuka kwamba Wizara hii kupitia Mashirika ya Kimataifa yalikuwa na mpango wa kuweka mipaka au kuongeza mpaka katika Bahari Kuu. Sasa nataka kujua: Je, fedha hizi ambazo ni Shilingi bilioni 1,100 ndizo hizo zitatumika katika kuendeleza au kuweka mpaka ule wa bahari kuu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, maelezo!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli. Hiyo itasaidia katika kutetea andiko letu kwa ajili ya kuongezewa ardhi katika bahari na yenyewe itatumika katika shughuli hiyo. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami napenda kupata ufafanuzi kwenye kasma 2326. Najua kinahusiana na masuala ya upimaji wa mipaka vijijini na Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake alizungumzia kwamba kuna baadhi ya Wilaya zitaanza. Sasa katika mchango wangu pia nilizungumzia kwa upande wa Bunda, kuna matatizo makubwa sana ya mipaka ya vijiji na kuleta mgogoro mkubwa kati ya Wilaya na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hapa zimetengwa Shilingi bilioni sita; nataka kujua: Je, Bunda ni eneo mojawapo ambalo litanufaika na huu mpango?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, maelezo!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwambia Mheshimiwa Ester kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alieleza, tutatuma watu kuangalia ukubwa wa migogoro hii na endapo kutakuwa na uhitaji, basi fedha hizi pia zitatumika katika kupima mipaka hiyo.

(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 – *Rural & Town Planning Div.* ... Shs. 1,000,000,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndugulile, nilisema ukae, siyo utaratibu. Katibu!

Kif. 3001 – *Rural and Town Planning Div.*... Shs. 1,000,000,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndugulile!

MHE. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Hapa zimetengwa Shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuendeleza Mji Mpya wa Kigamboni. Kwa mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, wamesema kwamba pamoja na yale maafikiano tuliyokuwa tumefikia wana kazi ya kukamilisha *Master Plan* na kufanya upimaji wa miundombinu kwa ajili ya eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa wametenga Shilingi bilioni moja, lakini kwa ufahamu wangu wa haraka haraka, gharama zote hizo ni kubwa kuliko hizi. Sasa sizioni hapa katika bajeti. Je, hii bajeti iliyoko hapa ni kwa malengo gani na hizo fedha za ziada watazipata wapi?

MWENYEKITI: Yaani hii Shilingi bilioni moja ni ya kazi gani? Ndiyo suala hilo. Hizi habari ya “mnazipata wapi nyingine hizo,” sijui. Tunazungumzia hizi hapa!

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kazi nyingi nilizosisema, nyingi tumeshazi-*commit* pesa zake katika bajeti tunayoendelea nayo hivi sasa.

MWENYEKITI: *Microphone!*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Hizo barabara za Kibada, Shilingi bilioni tatu tunazitoa sasa kabla ya mwezi wa Saba na hiyo kazi niliyosema ya kwenda kufanya *dermacation* kuhakikisha barabara zile zinawekwa, wadhamini pamoja na wapima wanakwenda wiki ijayo, fedha tunazo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukimaliza hiyo kazi, tutaanza kuonyesha *alignment* ya barabara kwa fedha za mwaka huu, lakini kiasi kikubwa cha fedha tunazotumia sisi ni za *retention* siyo hizi za maendeleo.

Kwa hiyo, hata hizi Shilingi bilioni tatu, tuna mfuko wetu wa *retention* ambao tunatumia kwa kazi mbalimbali. Sasa tunaipa kipaumbele Kigamboni kutokana na *retention*. Badala ya kutumia kazi nyingi, huwa tunapendelea zaidi Kigamboni. Huwezi kuzipata hapa kwenye kitabu cha maendeleo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3002 – *Housing Division* Shs. 500,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)
(Bunge lilirudia)

TAARIFA

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwa ushirikiano mliotuonyesha wote leo na shukrani zote, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu likubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja (*Makofi*)

WAZIRI WA ELIMU: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2015/2016 –
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya
Makazi yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Napenda kuchukua nafasi niseme kwamba, hii kufuatana na Wizara za Kisekta ndiyo Wizara yetu ya mwisho katika zile za Kisekta.

Sasa tunasubiri Bajeti tarehe 11. Safari hii kidogo utaratibu wetu haukwenda vile tulivyopanga kutokana na kwanza kuwa na muda finyu, lakini pia baada ya kupata mkasa tuliokuwanao, ukavuruga kidogo.

Kwa hiyo, ilikuwa tuwe tumemaliza Wizara zote Jumamosi. Kwa kawaida huwa tunamaliza na Wizara ya Fedha, lakini kwa kuwa Wizara ya Fedha ilikuwa lazima iwe tayari kufanya kazi leo ya kupitia ile bajeti pamoja na Kamati, kwa hiyo, ikabidi tu-swap na hawa ili tumalize leo.

Waheshimiwa Wabunge, lakini bado Kamati ya Bajeti hamzuiwi kwenda kusikiliza, ingawa maamuzi ya Kamati ya Bajeti ndiyo yanakuwa ya kwao. Kama kawaida, mnajua mnaweza kutoa mawazo lakini hamwezi kupiga kura nyie wengine, ndiyo kawaida.

Kwa hiyo, nawashukuruni sana kwamba tumemaliza *Sectoral Ministries*. Inawezekana kabisa pale tulipitisha ikatokea *some addendum* au mabadiliko katika baadhi ya vifungu kwa sababu mara zote tunapofanya zile Wizara ikifika kwenye Kamati ya Bajeti, unaweza kuona uko umuhimu mahali fulani zaidi, kwa hiyo, mkashangaa hata zile mlizopitisha zinaweza kubadilishwa kwenye *addendum*. Inawezekana! Sisemi itafanyika hivyo, lakini inawezekana. Kwa sababu cha mwisho kabisa, ni ile ya mwisho kabisa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kesho wataendelea na ile Kamati ya Bajeti na keshokutwa. Kwa hiyo, kwa siku ya leo nawashukuru, nawatakia jioni njema, naahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.21 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 9 Juni, 2015 Saa Tatu Asubuhi)